

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 17 Aprili, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

MHE. MOHAMMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Maoni ya Kamati hiyo juu ya utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

MHE. SALOME W. MAKAMBA K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

MWENYEKITI: Ahsante. Katibu.

KATIBU MEZANI – BAKARI KISHOMA:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Maswali, swali letu la kwanza linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na linaulizwa na Mheshimiwa Aisharose Ndoghoi Matembe, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 98

Changamoto Zinazoikabili Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Singida

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE aliuliza:-

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida inakabiliwa na uhaba mkubwa wa Watumishi, uchakavu wa majengo, mifumo mibovu ya maji safi na maji takatiki ikiwemo na ukosefu wa gari la wagonjwa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuipatia hospitali hiyo watumishi wa kutosha hasa ikizingatiwa kuwa hospitali hii ni tegemeo la watu wengi hasa akinamama wajawazito?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuipatia hospitali hiyo vifaa tiba na vitendea kazi vingine ikiwemo *CT Scan* na *MRI*?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aisharose Ndogholi Matembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2018/2019, imeajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya 52, katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida hivyo kupunguza tatizo la upungufu wa watumishi na kufikia asilimia 45. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara inategemea kuomba kibali cha kuajiri watumishi 197 wa kada mbalimbali za afya kwa ajili ya hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiendelea kuboresha huduma za uchunguzi katika hospitali zote za Rufaa za Mikoa ikiwemo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida. Mpaka sasa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida imeshapelekewa mashine mpya ya kisasa ya *X-ray (digital x-ray)* na imeanza kufanya kazi. Sanjari na hilo, hospitali mpya, itakapokamilika itasimikwa vifaa vya kisasa ikiwemo *CT Scan* ili kuiwezesha kufanya kazi kwa hadhi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa magodoro, vitanda na vifaa tiba Wizara itaendelea kuhakikisha Hospitali inatenga bajeti kupitia mpango kabambe wa Hospitali *Comprehensive Hospital Operational Plan (CHOP)* kwa ajili

ya ununuzi wa vitanda, magodoro na vifaa tiba ambapo kwa mwaka huu wa fedha 2018/2019, tayari imetumia kiasi cha Sh.673,575,168.58/= kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba na vitendea kazi kama magodoro, mashuka, vitanda, mashine ya kufulia, *ultra sound* pamoja na vifaa kwa ajili ya chumba cha wagonjwa mahututi (*ICU*).

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Matembe.

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa hospitali yangu ya Rufaa ya Mkoa wa Singida inahudumia zaidi ya wagonjwa 300 kwa siku na inatoa huduma katika maeneo mawili tofauti, ipo hospitali ya zamani, ambayo ipo katika Kata ya Ipembe na hospitali mpya ya Rufaa iliyopo katika Kata ya Mandewa. Je, Serikali inampango gani wa kuhakikisha inapeleka fedha za kutosha ili kumaliza ujenzi katika hospitali mpya ya Rufaa ya Mandewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, kwa kuwa hospitali hii inakabiliwa na uhaba mkubwa wa Madaktari Bingwa wakiwemo wa wanawake na watoto pia ina uhaba wa vifaa tiba kama *Oxygen Concentrator, baby warmer na phototherapy machine*. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka mahitaji haya muhimu katika hospitali yangu ya Rufaa ya Mkoa wa Singida? Nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo mawili Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Ndungulile

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Aisharose Ndoghoi Matembe, amekuwa ni mfuatiliaji mkubwa sana wa maendeleo ya hospitali hii ya Rufaa ya Mkoa wa Singida na amekuwa ni mdau mkubwa sana kwetu sisi Wizara ya Afya kufuatilia masuala mbalimbali, nataka kumpa pongezi hizo.

Naomba sasa nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aisharose Matembe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tumezipokea hizo hospitali za Rufaa za Mikoa na kusudio letu ni kuhakikisha kwamba tunaziboresha ili ziweze kutoa huduma za kibingwa kama zilivyokusudiwa na ni kweli kwa sasa Mkao wa Singida una hospitali ya zamani ambayo inatumika kama hospitali ya Rufaa ya Mikoa, lakini kuna ujenzi wa hospitali mpya ambao unaendelea pale Mandawe na nilishaitembelea na kusudio la Serikali ni kuhakikisha kwamba sasa tunaikamilisha ile hospitali. Baada ya hapo ile hospitali ya zamani tuirudishe katika ngazi ya halmashauri iweze kutumika kama hospitali ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pilii kama nillivyojibu katika swali langu la msingi, tutaendelea kuboresha na kuongeza Madaktari kadri tutakavyokuwa tunaendelea kuzalisha. Mwaka jana timesomesha Madaktari takriban 125, mwaka huu tena tumeshasomesha Madaktari Bingwa zaidi ya 100. Kwa hiyo, kadri wanapokuwa wanamaliza na sisi tutakuwa tunawapangia katika hospitali zetu za Rufaa za Mikoa. Lengo letu kama Serikali ni kuhakikisha kwamba zile huduma za msingi za magonjwa ya ndani, magonjwa ya watoto, magonjwa ya mifupa, magonjwa ya akinamama, wataalam wa radiolojia, wataalam wa magonjwa ya dharura, kila hospitali ya Rufaa za Mikoa iweze kuwa nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na masuala ya vifaa tutaendelea kuongeza vifaa hivi kadri tutakavyoweza lakini nitoe msisitizo kwa waganga Wakuu wote wa hospitali za Rufaa wote wa hospitali za mikoa, masuala mengine wala siyo kuhitaji kusubiri Serikali, fedha wanazo waweze kuagiza vile vifaa ambavyo wanaviona ni muhimu katika utoaji wa huduma zao za afya.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Musukuma na Mheshimiwa Japhary Michael ajiandae.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru matatizo yaliyoko Singida ni sawa kabisa na matatizo yaliyoko Geita DC, Hospitali ya Wilaya ya Geita imepandishwa hadhi takriban miezi sita na tunaishukuru sana Serikali kwa sababu imetuletea vifaa vingi *x-ray machine, Ultra sound, machineza* meno, vitu vya *theatre*, lakini vitu hivi vyote viko *store* kwa sababu hatuna wataalam na hospitali ile inaendeshwa na AMO na Madaktari wetu wengi bado wako Geita Mjini wamekaa tu ofisini. Je, ni nini kauli ya Serikali kumwelekeza Mganga Mkoo wa Mkoa apeleke watu wenye hadhi ya kuendesha Hospitali ya Wilaya?

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Joseph Musukuma kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya kufuatilia Hospitali hii ya Nzela katika Wilaya ya Geita na nilipata fursa ya kutembelea hospitali hii na ni hospitali kubwa na ilijoengwa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelekezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhambi kubwa sana kama hospitali imekamilika na vifaa vipo na haitoi huduma zile zilizokusudiwa wakati sisi kama Serikali tulishapeleka wataalam. Nitumie fursa hii kumkumbusha Mganga Mkoo na kumwelekeza Mganga Mkoo wa Mkoa kuhakikisha kwamba wale wataalam wote amba Serikali imewapatia na wapo mjini hawako katika kituo cha kazi kuhakikisha kwamba mara moja wanafika kule na wanatoa huduma kwa wananchi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Japhary Michel.

MHE. JAPHARY R. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Singida halitofautiani sana na tatizo la hospitali ya

Mawenzi ya Mkoa wa Kilimanjaro, ambapo hospitali ile imezidiwa sana na wagonjwa.

Sasa swali langu kwa Serikali, wako tayari kusaidia kuongeza Madaktari katika hospitali ile ya Mawenzi ili iweze kutoa huduma inayoridhisha kwa wagonjwa katika hospitali ile?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Japhary Michael, Mbunge wa Moshi, kama ifuatavyo:-

Hospitali ya Rufaa ya Mawenzi ni hospitali ya Mkoa katika Mkoa wa Kilimanjaro na bahati nzuri nimepata fursa ya kutembelea ile hospitali. Kwa maana ya kuwa na Madaktari tunao Madaktari wa kutosha, changamoto ambayo tunayo pale ni Madaktari Bingwa na hili tumeshalionwa Mheshimiwa Mbunge. Juhudi ambazo tunazifanya sasa hivi ni kusomesha Madaktari wengi zaidi na kuanza kuwapanga katika idara mbalimbali ambazo nimezisema katika swali la msingi, kuhakikisha kwamba sasa zile huduma za kibingwa zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tunaboresha mnyororo wa rufaa kwa maana ya kuboresha vituo vya afya na ujenzi wa hospitali za wilaya mbili ambazo zinaendelea katika Mkoa wa Kilimanjaro kuhakikisha sasa ule mzigo ambao ulikuwa unakwenda pale katika hospitali ya mkoa, uweze sasa kuchukuliwa na hivi vituo vya afya pamoja na hospitali za wilaya.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, swali linalofuata linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na linaulizwa na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo.

Na. 99

Kupitia Upya Sera ya Elimu Nchini

MHE. RASHID A. SHANGAZI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapitia upya Sera ya Elimu kwa lengo la kuongeza tija na kuendana na mahitaji ya sasa?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Ole Nasha.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio au maboresho ya Sera hufanyika kwa vipindi tofauti kulingana na mahitaji ya wakati. Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 ni matokeo ya mapitio yia Sera ya Elimu ya mwaka 1995.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuanza utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Serikali imebaini changamoto katika baadhi ya maeneo na mengine kuwa na upungufu katika utekelezaji wake. Hivyo, Serikali imeanza mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 kwa kufanya majadiliano na wadau/wataalam mbalimbali kwa lengo la kupata maoni yao na kuhakikisha ushirikishwaji wa makundi yote muhimu unafanyika ili Sera hiyo iweze kuendana na mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato huu wa kupitia upya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 unaendelea na kwa wakati muafaka tutawashirikisha Waheshimiwa Wabunge.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Shangazi.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Serikali ninayo maswali mawili ya madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa Sera ya elimu ya mwaka 2014 imetamka wazi kwamba elimu ya msingi itaishia darasa la sita na hadi hivi tunavyozungumza Serikali bado haijatekeleza katika eneo hilo. Je, Serikali inatuambiaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni kwa kiasi gani Sera hii ya Elimu inazingatia ubora wa elimu, hasa ukizingatia kwamba mionganoni mwa mikoa ambayo huwa haifanyi vizuri katika mitihani mbalimbali ni Mkoa wa Tanga. Sasa nataka kujua ni kwa kiasi gani Sera hii ya elimu inazingatia suala zima la ubora wa elimu kwa maana ya *quality assurance*? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo kwa kifupi tu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rashid Shangaz, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu, naomba nitumie nafasi hii kusema kwamba Mheshimiwa Shangazi amekuwa akifuatilia suala hili na masuala yote yanayohusiana na elimu na kwa kweli kwa nafasi yake hakuna ubishi kwamba ni moja katika Wabunge bora kabisa ambao wame wahili kutokea katika Bunge hili. Swali lake la kwanza ni hilo kwamba kwa nini hatujatekeleza wazo lile la Sera la kuishia darasa la sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu letu ni kwamba Sera siyo Msahafu, kwa hiyo Serikali inabadilisha Sera kadiri inavyoona kwamba inafaa kulingana na mahitaji ya wakati huo. Kwa sasa busara imetujia upya kwamba elimu kuanzia darasa la kwanza mpaka la saba siyo kitu kibaya, kwa hiyo hatuna haja

ya kubadilisha na ndiyo maana tumbakia na mfumo wa zamani na hatujavunja sheria, Sera siyo lazima itekelezwe, Sera unatekeleza na unabadijisha kadiri unavyoona inafaa. Kwa sasa tuko kwenye mapitio na ni moja ya mambo ambayo tuliona kwamba hatutakeleza na tutaendelea na utaratibu wa zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuhusiana na ubora wa elimu ni kweli kwamba Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, imeweka msisitizo mkubwa katika masuala ya udhibiti ubora wa elimu na ndiyo maana kumetokea mabadiliko makubwa sana katika mfumo wetu wa udhibiti ubora. Zamani tulikuwa tunasema ni ukaguzi wa elimu lakini siku hizi tunadhibiti ubora, lakini vile vile mtindo mpya wa kudhibiti ubora ni wa kiushirikishwaji zaidi unawaleta wadau wote kushiriki katika kudhibiti ubora wa elimu, lakini vilevile kama wote mnavyojua sasa tuko katika mikakati mikubwa ya kuhakikisha kwamba Wadhibiti Ubora wanawezeshwa kwa kupata vifaa na ofisi. Kimsingi tumeweka mikakati mikubwa sana ya kuhakikisha kwamba elimu yetu inakuwa bora. Moja kati ya masuala ambayo tunayafanya kazi katika mapitio ya Sera ni kuendelea kuweka mifumo ambayo itawezesha kudhibiti ubora wa elimu.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Masoud

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mapitio ya Sera ya Elimu na kuweka mikakati ya ubora wa elimu, ni mara kadhaa hapa Bungeni Serikali imekuwa ikiahidi kuboresha maslahi ya walimu ikiwemo posho ya kufundishia (*teaching allowance*). Vilevile kwenye sherehe mbalimbali za walimu katika maeneo kadhaa Serikali wamekuwa wakiahidi kuboresha posho ya kufundishia (*teaching allowance*) lakini hadi sasa waliopata fedha hizo ni Wakuu wa Shule na Waratibu wa Elimu. Naomba kujua kama Serikali iliwardanganya walimu na lini fedha hizo zitatolewa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali na Mheshimiwa Masoud, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika azma ya kuboresha elimu maslahi ya walimu na wafanyakazi wengine katika sekta ya elimu ni kitu muhimu. Ndiyo maana kwa sasa Serikali inajaribu kupitia upya utaratibu mzima wa maslahi ya watumishi wa umma kwa jumla wakiwemo na walimu ili baada ya hapo tuweze kuwa na maslahi ya walimu ambayo yataenda na wakati wa sasa lakini vilevile ili waweze kufanya kazi yao vizuri katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu swali la madeni, naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ilijikita kwanza katika zoezi la kufanya uhakiki ili kubaini madeni ya kweli. Baada ya hapo tayari baadhi ya malipo yalishafinyika na mengine yataendelea kulipwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mwezi Januari, 2019, Wizara ya Elimu ilitoa Mwongozo juu ya Muundo wa Bodi za Shule kuanzia shule za msingi mpaka Serikali. Katika muundo ule, Wizara imeelekeza katika shule ya sekondari na shule za msingi muundo utoe nafasi kubwa sana kwa walimu ambapo watakuwa watano lakini pia wazazi au nje ya walimu wanakuwa watatu. Je, katika maana nzima ya makusudio ya Bodi kwenda kuangalia ufanisi wa taaluma na majengo na mambo yanayoendelea shulenii, Wizara haionti kwamba jambo hili limekosewa na kwamba linahitaji lirekebishwe haraka sana kabla hapajaharibika?

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu kwa swali hilo Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Olenasha.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba hivi karibu tumetoa Mwongozo mpya wa Bodi za Shule na lazima niseme kwamba baada ya kuutoa tumegundua kuna maeneo ambayo yangeweza kuwa bora zaidi na mojawapo ni hilo alilosema Mheshimiwa Kikwete. Naomba nimhakikishe kwamba tayari Wizara inaupita upya tena Mwongozo ule kwa kushirikiana na wadau ili tuwe na Mwongozo ambao utakotupeleka mbali zaidi.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, swali linalofuata bado linalekezwa kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na linaulizwa na Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 100

Ongezeko la Wasichana kwenye Masomo ya Sayansi

MHE. SUSAN A. J. LYIMO (K.n.y. MHE. CATHERINE N. RUGE) aliuza:-

Kumekuwa na idadi ndogo ya wasichana wanaodahiliwa katika vyuo vya elimu ya juu katika fani ya sayansi ikizingatiwa kuwa sasa tunaelekea katika uchumi wa viwanda:-

Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha inaongeza idadi ya wasichana katika masomo ya sayansi kuanzia ngazi ya chini mpaka vyuo vikuu?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Olenasha.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina dhamira ya kuhakiksha kuwa usawa wa kujinsia katika elimu na mafunzo unazingatiwa. Aidha, Serikali inatambua changamoto zinazosababisha wanafunzi wa kike kushindwa kumaliza mzunguko wa elimu na kupelekea kuwa na idadi ndogo ya wasichana wanaojunga na ngazi nyingine za elimu hasa katika masomo ya sayansi na hisabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na hali hii, Serikali inatoa fursa zaidi kwa wasichana kwa kuongeza nafasi za udahili kwa kidato cha V-VI katika tahasusi za sayansi ambapo katika shule 141 zinazochukua wasichana wanaosoma tahasusi za sayansi, shule 85 ni za wasichana tu na 56 za mchanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua hizo, Serikali imeendelea na ujenzi wa mbweni na hosteli katika shule na vyuo hasa katika mazingira yenye changamoto ambapo wanafunzi wa kike hupewa kipaumbele kwenye mabweni na hosteli hizo. Vilevile ununuzi na usambazaji wa vifaa vya maabara pamoja na vitabu vya masomo ya sayansi umefanyika ambapo shule za sekondari 1,696 zimepata vifaa vya maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuweka mazingira rafiki kwa wanafunzi wote ili wafikie malengo yao katika elimu. Aidha, nitumie fursa hii kuwataka wazazi na jamii kuachana na mila, desturi na mitazamo hasi dhidi ya watoto wa kike kwani ni kikwazo katika maendeleo yao na jamii kwa ujumla.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri

na mikakati yote ya Serikali bado idadi (*ratio*) ya wasichana kwa wavulana katika vyuo vyety vyelimu ya juu ni ndogo sana katika masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba baadhi ya vyuo, kwa mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam siku za nyuma kilikuwa na programu ambayo ilikuwa inawasaidia wasichana ambao wamepata *point chache* wanakuja kwenye hiyo programu walau miezi miwili ili waweze sasa kuijunga na vyuo lakini programu hiyo sasa haipo na bado tunahitaji sana wasichana kuendelea na masomo. Swali la kwanza, je, ni lini programu kama hizo zitarudishwa ili kusaidia wasichana kwa kuwa tunatambua mazingira magumu wanayowapata wasichana huku chini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, pamoja na kwamba wanajenga mabweni au hosteli katika vyuo na shule zetu lakini bado tuna tatizo kubwa sana la uhaba wa mabweni ambayo yangewasaidia wasichana hawa kuweza kuijunga na vyuo vyelimu ya juu kuweza kuweka uwiano wa kijinsia siyo tu katika vyuo lakini hata katika masuala mazima ya siasa maana tunapata wanawake wachache kwa sababu hiyo. Ni lini mtatekeleza hilo?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, kwa kifupi tu Mheshimiwa Olenasha.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Susan Lyimo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam siku za nyuma kilikuwa na mpango ambao ulifanikiwa sana wa kuwasaidia wanafunzi wengi wa kike kuweza kuijunga na masomo ya sayansi. Mpango ule muda wake ulishaisha lakini kwa sasa tayari kuna majadiliano ya kurudisha au kuanzisha programu inauhusiana na suala hilo na katika hali ambayo itawahusisha watoto wa kike wengi zaidi katika vyuo vingine, kwa hiyo, majadiliano yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi kama Serikali tunachofanya ni kuboresha elimu kwa ujumla wake pamoja na kutoa hamasa na kuomba wananchi na wadau wote washirikiane katika kuondoa mila na fikra potofu ambazo zinafanya watoto wa kike waogope kwenda kuchukua masomo ya sayansi. Nashukuru kwamba leo tumetembelewa na wanafunzi wa kike wa sekondari. Naomba nitumie nafasi hii kuwaeleza kwamba sayansi na hisabati ni ya kila mtu na siyo kwa ajili ya wanaume tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swalı lake la pili kuhusiana na ujenzi wa mabweni na hosteli, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara yangu mwezi Januari ilipeleka katika shule na vyuo tofauti 560 shilingi bilioni 56 ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kujenga miundombinu katika shule na vyuo vyetu na kati ya fedha hizo, nyingi zimeenda vilevile katika kujenga hosteli na mabweni. Yeye mwenyewe anajua baadhi ya vyuo kwa mfano Chuo cha Ardhi na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere tunajenga hosteli kwa ajili ya wanafunzi lakini maarufu kwa utetezi wake wa *Hall 2* na *Hall 5* katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa sasa vimetengewa shilingi bilioni nne. Kwa kweli katika vyuo vyetu tunajitahidi kujenga mabweni na hosteli za wanafunzi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwalongo na Mheshimiwa Yussuf Hussein.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Ili watoto wa kike waweze kufanikiwa katika masomo ya sayansi wanahitaji uwepo wa walimu. Tuna tatizo kubwa sana kama nchi ya walimu wa sayansi na hasa hasa *physics*. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakisha shule zetu zinapata walimu wa kutosha wa *physics*?

MWENYEKITI: Ahsante. Walimu wa *physics* wa kutosha, Mheshimiwa Olenasha, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwalongo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema kwamba ili watoto wa kike waweze kufanikiwa kuchukua masomo ya sayansi ni lazima kuwa na walimu na ndiyo maana Serikali imekuja na mikakati thabiti ya kuhakikisha kwamba walimu wanapatikana. Wote tunakumbuka kwamba Serikali ilipeleka wanafunzi wale waliokuwa *UDOM* kwenda kusoma masomo ya sayansi na tunategemea wataanza kuingia sokoni kwa ajira za hivi karibu. Pia katika vyuo 35 ambavyo tunavyo, Serikali imeamua sasa kutenga vyuo vichache kati ya hivyo vinakuwa ni vyuo vinavyofundisha sayansi. Kwa hiyo, tunaendelea kuongeza fursa na udahili katika vyuo vya elimu vinavyotoa walimu wa sayansi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Yussuf.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Napenda nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, kumekuwa na malalamiko mengi ya wanawake kwamba hawapati nafasi za kutosha katika shule kuanzia sekondari, vyuo na vyuo vikuu. Sasa ni mkakati wa Serikali kwamba wanawake wakiflikia hapo waanze kubinywa au wanawake wenyewe wamezoea kudekezwa tu?

WABUNGE FULANI: Aaaaaaa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yussuf.

MBUNGE FULANI: Wewe umezaliwa na nani?

MWENYEKITI: Hebu tusaidiane kidogo, unauliza vizuri lakini hilo neno kudekezwa linyooshe tu.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aseme kuna mkakati kwamba wanawake

wanabinywa au sasa wao wenyewe wanataka wasaidiwe tu kwenda vyuoni?

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti nilichokuwa nazungumzia katika maswali yangu yaliyopita ndiyo inajionyesha dhahiri hapa kwamba ni suala la mila, desturi na fikra potofu dhidi ya uwezo wa watoto wa kike kuweza kuendelea na kufanya vizuri kama watoto wa kiume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge kila mmoja katika nafasi yake ajielekeze kwenye ukweli kwamba mtoto wa kike ana uwezo sawa na mtoto wa kiume, kwa hiyo, tuwasaidie waweze kusonga mbele. *(Makof)*

MWENYEKITI: Ahsante kwa kuliweka vizuri hilo, tunataka hawa wasichana wasome na watasoma. *(Makof)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, swali linalofuata linalekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na linaulizwa na Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maaalum.

Na.101

Huduma kwa Akina Mama Wajawazito Gerezani

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA aliuliza:-

Baadhi ya wanawake huingia gerezani wakiwa na ujauzito na hivyo kujifungulia gerezani.

(a) Je, ni huduma gani wanazopata ili kuhakikisha wanajifungua salama?

(b) Je, ni jitihada gani zinafanywa ili kuwapatia akina mama hao vyakula vinavyopendwa na wajawazito?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kangi Lugola.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza limekuwa likihifadhi wafungwa wa alia zote wakiwemo wafungwa wa kike wajawazito. Katika kuhakikisha kwamba wafungwa wajawazito wanajifungua salama, Jeshi la Magereza limekuwa likitoa huduma za afya, chanjo na kuhakikisha wanahudhuria kliniki za mama wajawazito katika vituo vya afya vya magereza na pale inapobidi kuwapeleka hospitali za Serikali.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza limekuwa likiwapatia wafungwa wajawazito vyakula wanavyovihitaji kiafya kwa kuzingatia maelekezo na ushauri wa Daktari wa gereza ili kuhakikisha afya ya mama na mtoto inalindwa. Aidha, Serikali inazidi kuboresha bajeti ya huduma hizo ili kuhakisha kwamba wafungwa wajawazito wanapata huduma hizo inavyostahili.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Malembeka.

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Waziri na kumpa pongozi kwa majibu yake ambayo yanaonyesha nia ya dhati ya Serikali kuwasaidia wafungwa wanawake. Maswali yangu mawili yanyongeza ni kama ifuatavyo:-

(a) Je, Serikali inawasaidiaje watoto ambao wapo gerezani na mama zao kielimu na kisaikolojia kwa kuzingatia haki za watoto husasan wanapotumikia kifungo hicho ambacho watoto wao hawahusiki nacho?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa wanawake wafungwa ambao ni wajawazito wakatumikie kifungo hicho nje ili waweze kuwalea watoto wao katika familia huru badala ya kuwa gerezani? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Majibu kwa maswali hayo mawili, Waziri wa Mambo ya Ndani Nchi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Malembeka kwa jina maarufu Nyoka wa Kijani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wapo akina mama wafungwa ambao wanajifungua watoto wakiwa magerezani. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Nyoka wa Kijani, Nyara ya CCM kwamba utaratibu wa Jeshi la Magereza kuititia kanuni za Jeshi la Magereza watoto ambao wamekwishazaliwa magerezani wanopofikia umri wa kuanza awali wamekuwa wakisoma kwenye shule za awali zilizopo kwenye magereza zetu. Pia kwa kuititia watumishi wa magereza ambao wana utaalamu wa masuala ustawi wa jamii wamekuwa wakiwapa elimu pamoja na kuwafariji watoto hawa ili wajione wao siyo wafungwa ndani ya magereza isipokuwa wamezaliwa katika wakati ambao mama zao wapo magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kwamba kwa nini wafungwa ambao wanajifungua magerezani wasipate adhabu nyingine badala ya kuwafunga magerezani. Tunao utaratibu kuititia sheria yetu ambayo inaitwa *Probation for Offenders* pamoja na *Community Services*, wale ambao wana vifungo chini ya miaka mitatu tumekuwa tukiandaa utaratibu wa kuwaondoa magerezani ili wawe na vifungo mbadala. Hata hivyo, kuna utaratibu watoto wanaokuwa

magerezani wanapofikia umri ambao wanaweza wakaishi uraiani bila kuwa na mama zao ndugu zao wamekuwa wakishirikishwa ili waweze kutoa malezi kwa watoto ambao mama zao wapo magerezani. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimwia Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Katika Gereza la Morogoro Mjini kuna msongamano mkubwa sana wa mahabusu na wafungwa hasa kwa upande wa wanawake. Je, kuna mkakati gani wa kupunguza msongamano huu wa wafungwa na mahabusu hasa wanawake kwenye Gereza la Morogoro?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, kwa kifupi tu Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mkuu wa Mkoa Mstaifu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna msongamano kwa wafungwa na mahabusu katika magereza mbalimbali katika nchi yetu. Gereza alilolisema Morogoro ni mojawapo ya magereza yenye msongamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kupitia sheria mbalimbali tumekuwa tukijaribu kuzitumia ili kuwaondoa wafungwa ambao wana vifungo vifupi. Pia tumekuwa tukitumia Sheria yetu ya *Parole* kupunguza msongamano. Vilevile Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa akitoa msamaha kwa wafungwa ili kupunguza msongamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwataka Watanzania popote pale walipo wasijihushe katika uhalifu utakaowasababishia wawe wafungwa ama mahabusu.

Waelewe kwamba watakapofanya uhalifu wataenda kwenye magereza ambazo zina msongamo. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kuwasahi wasijjhuishe katika uhalifu. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Fakharia.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa ujauzito ni kawaida kwa mwanamke yeote kwa mfungwa au mtu aliyepo uraiani. Kwa hawa wafungwa ambao tayari ni wajawazito, kuna wakunga *standby* ili wawasaidie? Kwa sababu uchungu unakuja *time* yoyote na wapo ndani ya gereza, je, mnawawekea wazalishaji/wakunga *standby* wa kuwasaidia uchungu unapowajia? (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, kwamba kwenye Jeshi la Magereza, tunazo Zahanati na Vituo vya Afya ambapo wapo Madaktari wanaotoa uthalam wao kuhakikisha kwamba yale mahitaji yote ya akina mama katika kuhudhuria kliniki na kufuatilia siku za kujifungua wanazifanya kama kawaida. Pia tunao wakunga ambao siku zao zikifika wanawazalisha kama kawaida na hata vifaa vya kujifungulia wanavipata kama kawaida; na hata vile vyakula ambavyo akina mama, vinachochewa na mahitaji ya ujauzito; iwe ni udongo au chakula chochote kile wanaletewa kama kawaida. Ahsante sana. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Khatib Haji.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mwuliza swali alitaka kujua msaada unaopatikana kwa hawa mama zetu wanaokuwa wajawazito Magerezani na kujifungua. Zipo taarifa kwamba wako baadhi ya wanawake wanaoingia wakiwa sio wajawazito lakini wakapata ujauzito ndani ya Magereza. Inaeleweka kwamba

walinzi wa wafungwa wa kike ni wanawake, mimba hizi wanazipataje Mheshimiwa Waziri? (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Haya. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kangi Lugola.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa hakuna mimba ambazo zinatokea Magerezani. Hilo la kwanza. La pili, mimba tunazozzungumzia ni mimba ambazo mfungwa ama mahabusu anaingia gerezani akiwa tayari kule uraiani anakotoka ameshapata ujauzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana kulitokea jaribio hapa kwa Wabunge wakiwa wanataka tuweke sheria au utaratibu wa kuruhusu wenza wa mfungwa anayekuwa Gerezani ili waweze kupata fursa ya kwenda kufunguka wakiwa Gerezani, ya kwenda kujinifasi wakiwa Gerezani, lakini tulisema kwamba kwa sheria zetu na mila zetu, hatuwezi tukaruhusu hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante Waheshimiwa tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi na linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 102

Ahadi ya Ujenzi wa Minara ya Simu

MHE. JEROME D. BWANAUSI aliuliza:-

Serikali iliahidi kujenga minara ya simu katika Kata za Sindano, Lipumburu, Namtona, Mcharu, Chikolopola na Mkundi.

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ilivainisha Vijiji vya Kata za Sindano, Lipumburu, Namtona, Mchauru, Chikolopola na Mkundi kwa ajili ya tathmini kuangalia mahitaji halisi ya Mawasiliano kwenye eneo hilo. Baada ya tathmini husika kukamilika, Serikali kuitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote iliviingiza Vijiji vya Kata za Mchauru katika mradi wa mpakani na kanda maalum unaotekelezwa na Kampuni ya Simu ya Tigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari vibali vya ujenzi kutoka *NEMC* vimeshapatikana, hivyo Kampuni ya simu ya Tigo inategemea kuanza ujenzi wa mnara sambasamba na kufunga vifaa vya mawasiliano mara moja. Aidha, ujenzi wa mnara huu unatarajiwaka kukamilika mwezi Januari, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za Sindano na Lipumburu ziliingizwa katika mradi wa awamu ya tatu ambao ulitiwa saini tarehe 13 Desemba, mwaka 2018 na utekelezaji wake unategemewa kukamilika mnamo mwezi Septemba, 2019. Kata ya Sindano itafikishiwa huduma ya mawasiliano na Kampuni ya Vodacom na Kata ya Lipumburu itafikishiwa huduma ya mawasiliano na Kampuni ya *TTCL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya Kata za Namtona, Chikolopola na Mkundi vitaingizwa katika orodha ya miradi ya zabuni zinazotangazwa katika siku za usoni kulingana na upatikanaji wa fedha hususan katika mwaka huu wa fedha 2019/2020.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bwanausi. (*Makof*)

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Lulindi. Swali langu la kwanza; Serikali iliahidi miaka miwili iliyopita kwamba itahakikisha inajenga minara katika mipaka yetu yote ya nchi, ikiwemo mpaka wa Tanzania na Msumbiji, lakini vijiji ambavyo viko mpakani mwa Tanzania na Msumbiji ujenzi wake umekuwa ukisua sana, hivyo kuwafanya wananchi wa Jimbo la Lulindi kutumia minara iliyoko Msumbiji.

Je, Mheshimiwa Waziri atawaambia ni lini maeneo ya Namtona na Chikolopola yatawekewa minara?

Swali la pili; vibali vya ujenzi kutoka *NEMC* kuchukua muda mrefu sana kuvipata: Je, Wizara inashirikiana vipi na Wizara inayohusika na *NEMC* ili kuhakikisha *NEMC* hawakamishi ujenzi wa minara hapa nchini? (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Eng. Nditiye.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli kwamba tuna changamoto kubwa sana kwenye mipaka ya nchi yetu kutokana na mwingiliano wa mawasiliano kutoka nchi za jirani. Hivi karibuni kilifanyika kikao kikubwa sana cha *East African Communication (EACO)* pale Arusha, ambako wataalam wa Mamlaka za Mawasiliano za nchi za Afrika Mashariki walijadili kwa kina namna ya kuondoa changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mbunge kwamba changamoto hizo zinakwenda kutatuliwa na mpaka sasa hivi baadhi ya Makampuni ya simu tumeshaanza kuyaelekeza yaende yakafanye tathmini ya kiufundi namna ya kuondoa mwingiliano wa mawasiliano kutoka nchi nyingine. Kwamba ni lini tutapeleka mawasiliano; wakati wowote. Kama nilivyojibu katika swali langu la msingi

tayari mkandarasi yupo, ameshajulikana ni Tigo na atapeleka mawasiliano kabla ya mwezi Januari mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la pili, ameuliza kwa nini vibali vya ujenzi kutoka *NEMC* vinachelewa? Ukweli ni kwamba katika taratibu za ujenzi wowote lazima taratibu zifuatwe. Moja kati ya taratibu ni kupata kibali kutoka *NEMC*. Wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana ndugu zetu wa *NEMC* wa kuhakikisha kwamba minara inakopelekwa lazima kusiwe na madhara kwa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kushirikiana nao katika hali ambayo tunaamini kuwa hakuna ucheleweshaji mkubwa sana. Panapokuwa na ucheleweshaji mkubwa, huwa tunawashauri Wakandarasi wale au watoa huduma watafute eneo lingine ambalo haliwezi kuwa na changamoto kwa wananchi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chikota, Mheshimiwa Kadika.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Changamoto ya minara inayokabili Jimbo la Lulindi, inafanana na ile ya Jimbo la Nanyamba. Unapozungumzia mpaka wa Tanzania na Msumbiji ni pamoja na Kata ya Kitaya na Kilomba iliyopo katika Jimbo la Nanyamba; na Kampuni ya *TTCL* imepewa dhamana ya kujenga minara minane, katika Jimbo langu la Nanyamba; sasa nataka nipate kauli ya Serikali.

Je, ujenzi huo utakamilika lini? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri. Lini ujenzi utakamilika?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwenye Kata ya Kitaya na Kilomba Kampuni ya Mawasiliano Tanzania (*TTCL*) ilipewa tenda ya kufunga minara maeneo yale. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba

mkandarasi tayari ameshaanza kukusanya vifaa kwa ajili ya kuvipeleka pale na hivi karibuni kazi itaanza; na ametuhakikishia kwamba ndani ya miezi sita, pale minara itakuwa imeshawekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni sambasamba na kwa Mheshimiwa Nape Nnauye kule Chiuta ambako wanahitaji mnara ili wananchi wa kule na wenyewe wawekewe mawasiliano. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mgeni, halafu Mheshimiwa Mabula Stanslaus halafu Mheshimiwa Selasini.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi. Tatizo lililopo katika Mkoa wa Dodoma kama alivyouliza Mbunge aliyepita, nami tatizo hilo hilo katika Jimbo langu la Mgogoni. Jimbo hilo lina sekta muhimu sana kama Polisi na kadhalika, lakini bado mawasiliano ni tatizo:-

Je, ni lini, utajengwa mnara katika Jimbo hilo Kijiji cha Finya?

MWENYEKITI: Haya, sawa. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Lini mtasaidia ujenzi huo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli eneo alilolitaja lina changamoto ya mawasiliano. Nakiri kwamba nimeshawahi kutembelea eneo lile na tumeshachukua *coordinates* kwa ajili ya kutangaza tenda ambazo zinatangazwa mapema mwezi wa tano kwa ajili ya kusambaza mawasiliano katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba eneo hilo litazingatiwa kwa sababu kuna taasisi za kijamii ambazo ziko maeneo ya pale.

Itakapotangazwa tukapata mkandarasi kazi zitaanza na kumalizika mara moja. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mabula.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa matatizo yaliyoko Lulindi ni sawa kabisa na matatizo yaliyoko Jimbo la Ilemela, hasa kwenye Kata za Sangabuye ambapo kuna Kituo kikubwa cha Afya na upatikanaji wa mawasiliano umekuwa ni adimu sana, sambasamba na Kisiwa cha Bezi ambako hakuna kabisa mawasiliano na kuna wakazi wengi sana na Mheshimiwa Naibu Waziri ameshapata nafasi ya kutembelea kule; anawaambia nini wakazi wa Bezi na wakazi wa Sangabuye ni lini watapata mawasiliano ili na wao wawasiliane ukizingatia pale kuna Kituo cha Afya ambacho watu wengi wanaweza kupoteza maisha kwa kukosa mawasiliano?

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Eng. Nditiye.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli nilitembelea Kata ya Ilemela kwa Mheshimiwa Angelina Mabula, Naibu Waziri wa Ardhi na nilionyeshwa mpaka eneo la Bezi ambako kunahitaji mawasiliano. Nakiri kwamba kuna changamoto ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie tu kwamba maeneo mengi ya nchi yetu Waheshimiwa Wabunge wengi sana minara yao ya mawasiliano haifanyi kazi vizuri. Tunakwenda kutuma timu ya wataalamu kwa ajili ya kurekebisha minara hiyo ya mawasiliano ili iweze kutoa mawasiliano vizuri kwa wananchi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Bezi tumeshafanya tathmini, tumeshatuma mafundi na wataalam kwa ajili ya

ukaguzi. Hivi karibuni tutatangaza tenda na Kisiwa cha Bezi kitakuwemo kwa ajili ya kupelekewa mawasiliano. Ahsante. (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Kiswahili ni lugha pana sana, msiwe na wasiwasi. Mheshimiwa Selasini halafu Mheshimiwa Joseph Haule.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. Tatizo la mwingiliano wa mawasiliano ni kubwa sana katika Wilaya ya Rombo. Karibu nusu ya vijiji tunatumia *lines* za simu za *Safaricom*, tunasikiliza redio *KBC* na televisheni ya *KTN* ya Kenya. Hii ni hatari sana kwa usalama wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikiuliza hili swalii tangu Mheshimiwa Makamba akiwa Waziri mhusika.

MWENYEKITI: Swalii sasa Mheshimiwa.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii; Serikali ituambie sisi watu wa mpakani ni lini tatizo hili litatuliwa? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Ni lini? Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swalii la pili la nyongeza niloulizwa na Mheshimiwa Bwanausi, niliezea Bunge lako Tukufu kwamba tayari tumeshakaa vikao, wataalamu wa Mamlaka za Mawasiliano za nchi za Afrika Mashariki kutathmini na kuzungumzia kuhusu suala la mwingiliano wa mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote wanaokaa maeneo ya mipakani nikiwemo hata mimi mwenyewe kwamba suala hili la mwingiliano wa mawasiliano kutoka nchi jirani linashughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata juzi nimepitia pale Tarime, mwenyewe nikiwa pale pale Tarime, nilikaribishwa karibu Kenya *Safaricom* nikashangaa, lakini ndio hivyo mwingiliano wa mawasiliano upo na tumekwishakaa kuanzia mwezi wa Pili tulikaa; na juzi nimemtuma Naibu Katibu Mkuu wa Mawasiliano kwenda *ku-cement* kitu kilichoongeleta mwezi wa Pili na watu wa *EACO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote wa mipakani kwamba hili linashughulikiwa na tunahakika kabla ya mwezi wa Kumi litakuwa limeshafanyiwa kazi, kwa sababu maeneo mbalimbali tayari hatua mbalimbali zimeshaanza kufanyika.

MWENYEKITI: La mwisho, Mheshimiwa Haule.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Tatizo la Lulindi linafanana sana na Jimbo la Mikumi ambapo kwenye maeneo ya Vidunda, Uleli Ng'ombe, Kisanga, Tindiga na maeneo ya barabara ya kuu ya Tanzania; na Zambia maeneo ya Msimba, Mbamba pamoja na kwenye Hifadhi ya Mikumi, kuna tatizo kubwa sana la mawasiliano:-

Je, ni lini Serikali itawapatia mawasiliano wananchi wa Mikumi wa maeneo yao?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano: ni lini mtawapatia Mawasiliano eneo la Mikumi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mikumi lila changamoto moja ya kupeleka mawasiliano kwa uhakika, lile Jimbo liko linapakana sana na Hifadhi yetu ya Mikumi na utaratibu wa kuweka minara kule lazima upate kibali kutoka Wizara nyingine. Wasiwasi uliopo ni kwamba tukiweka mnara, watakaohudumia ule mnara watakuwa ni waaminifu wasiletie hujuma. Kwa hiyo, tumekuwa tukipata changamoto mbalimbali za namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa eneo kubwa sana, wananchi wa Mikumi wanapata mawasiliano. Vijiji alivyovitaja, kimojawapo kinapata mawasiliano ya Halotel, isipokuwa nilipotembelea pale wananchi walitaka wapate na vodacom, kwa maana ya M-pesa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashauri na kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge kwamba lengo la Serikali kwa hatua hii, ni kuhakikisha tunapeleka mawasiliano maeneo yale ambayo hakuna mawasiliano kabisa kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale maeneo ambayo tayari yana mawasiliano yanataka *option* nyingine, watusubiri kidogo na ndiyo maana tunapeleka mawasiliano kule ambako hakuna mawasiliano ili Makampuni mengine yavutike kwenda kuwekeza pale, kwa sababu mwisho wa siku ni makampuni ambayo yanakwenda kupata faida na wananchi vilevile. Kwa hiyo, nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge...

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Swalii linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Viti Maalum na linalekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

Na. 103

Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji

MHE. REHEMA J. MIGILLA aliuliza:-

Manispaa ya Tabora ipo kwenye mradi mkubwa wa maji toka Ziwa Victoria na Bwawa kubwa la Igombe linalotumika kuhudumia Wakazi wa Tabora Manispaa litakuwa halina matumizi tena.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuliweka Bwawa la Igombe kwenye scheme za umwagiliaji ili wakazi wa Tabora waendeshe Kilimo cha umwagiliaji?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Viti maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupanga matumizi ya maji kutoka katika chanzo, utunzaji wa mazingira na matumizi ya kijamii hupewa umuhimu zaidi kablo ya matumizi mengine. Ujenzi wa miundombinu ya kutoa maji kutoka Ziwa Victoria umelenga zaidi katika kupunguza upungufu wa maji uliopo kwenye Manispaa ya Tabora ambayo kwa sasa inahudumiwa na Bwawa la Igombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji hayo ni kwa ajili ya matumizi ya kijamii tu kwani hayatatosha kwa Kilimo cha umwagiliaji. Kwa kutambua umuhimu wa kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa tija na kukabiliana na mabadiliko tabianchi, Wizara yetu kuitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, ina mpango kabambe wa Taifa wa umwagiliaji unaotekelezwa kuanzia 2018/2019 hadi mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo katika Manispaa ya Tabora, mpango huu umejumuisha uboreshaji na ujenzi wa skimu za umwagiliaji za Imalamihayo, Inala, Magoweke na Bonde la Kakulungu.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Migilla Rehema.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nimponegeze Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo kwa majibu yake mazuri, lakini napenda niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tabora ni miongoni mwa mikoa ambayo imepata athari kubwa sana ya uharibifu wa mazingira kutokana na ukataji wa miti ambayo inatumika zaidi kwa ajili ya mkaa na kuni. Hali hiyo

imepelekeea Mkoa wa Tabora na maeneo ya jirani kupata mvua ya kusuasua ambayo ndio inatumika zaidi kwa kilimo. Sasa swali langu, je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kuhakikisha kwamba pamoja na athari zote hizo zilizopatikana wananchi wataendelea na shughuli za kilimo kama kawaida? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, pamoja na Serikali kuyaingiza maeneo ya Imlalamihayo, Inala, Bonde la Kakulungu na Magoweko katika mpango wa umwagiliaji, lakini mpaka leo maeneo haya bado hayajaanza kufanya kazi. Sasa tunataka tupate majibu ya Serikali ni lini maeneo haya na skimu hizi zitaanza kufanya kazi kwani mpango huu unaonesha umeanza kazi tangu mwaka 2018?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Omary Mgumba.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):
Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rehema Juma Migilla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza anataka kujua mikakati ya Serikali kwa ajili ya kuendeleza kilimokwa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi hapo Tabora. Sisi kama Serikali cha kwanza tulichokifanya, mkakati mkubwa tuliokuwa nao ambao badala ya kutegemea fedha za kibajeti, lakini pia badala ya kusubiri fedha za washirika wa maendeleo kutoka nje ya nchi tumeielekeza Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo kuja kwenye halmashauri mbalimbali nchini kukaa nao na kubainisha yale maeneo yanayofaa kwa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kubainisha kujua mahitaji yenu wataenda kuingia mikopo kwa dhamana ya halmashauri na sisi Serikali tutawadhamini zaidi ya asilimia 80 ili kujenga miundombinu ya umwagiliaji ikiwemo huu Mkoa

wa Tabora ili wakulima waendelee kulima cha kisasa cha uhakika na chenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili anasema, ni lini kwamba miradi hi tuliyotaja kwenye jibu letu la msingi kwamba itaanza kufanya kazi. Hii miradi itaanza kufanya kazi muda mfupi ujao baada ya upatikanaji wa fedha za kibajeti na kama nilivyo sema kwenye jibu la awali chanzo kingine cha pesa ni kupitia mikopo kupitia Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tuko nyuma sana ya muda, tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Edwin Amandus Ngonyani, Mbunge wa Namtumbo, bado linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

Na.104

Kutafuta Masoko ya Tumbaku Nchini Misri

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI aliuliza:-

Je, Wizara ya Kilimo inashirikianaje na Wizara nyingine zinazohusika na uwekezaji wa mambo ya nje kutafuta soko la tumbaku nchini Misri badala ya kulazimika kutumia nchi za Uganda na Kenya peke yake?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Innocent Bashungwa Waheshimiwa tuko nyuma

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Amandus Ngonyani, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014/2015, uzalishaji wa tumbaku ya moshi (*Dark Fire Cured Tobacco- DFC*) ulisimama Mkoani Ruvuma kutokana na kukosa soko. Jithada za Serikali zikawezesha kampuni ya *Premium Active Tanzania Limited* kuonesha nia ya kununua tumbaku hiyo ya *DFC* ambayo hapa nchini huzalishwa Namtumbo na Songea Vijijini, Mkoani Ruvuma. Kampuni hii ilieleza kuwa lipo soko kubwa la tumbaku aina ya *DFC* nchini Misri na Algeria, lakini tumbaku ya Tanzania inauzwa kwa bei ya juu kutokana na kodi inayotozwa ikilinganishwa na aina hiyo ya tumbaku kutoka nchi za Uganda na Kenya kwa kuwa nchi hizo Uganda, Kenya, Algeria na Misri ni wanachama wa Jumuiya ya *COMESA* na kwa hiyo kodi za kuingiza tumbaku, chai na bidhaa nchini Algeria na Misri kutoka Uganda na Kenya ni za chini ukilinganisha na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hilo, Wizara ya Kilimo inashirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuanzisha mazungumzo na Nchi Wanachama wa *COMESA* na nchi kama Misri na Algeria kupitia Balozi zetu ili kuandaa makubaliano maalum yaani *bilateral agreement* yatakayowezesha nchi yetu kupeleka tumbaku katika nchi hizo kwa kodi nafuu. Mazungumzo hayo yamefikia hatua nzuri na matarajio ni kufungua milango ya soko hilo na hivyo kuongeza kipato kwa wakulima na Taifa kwa ujumla. Aidha, makubaliano hayo yakikamilika Tanzania inaweza pia kuuza chai nchini Misri na Algeria kwa faida kuliko ilivyo hivi sasa au badala ya kuuza chai kupitia mnada wa Mombasa nchini Kenya.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ngonyani.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa. Niipongeze Serikali kwa hatua inazozichukua kuimarisha soko la tumbaku nchini. Njia mojawapo ya kuimarisha soko la tumbaku kwa upande wa sisi Wanaruvuma ni kufufua Kiwanda cha Kuchakata Tumbaku kilichoko Songea ambacho kinamiliikiwa na *SONAMKU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SONAMKU* kwa kushirikiana na mnunuzi wanakwamishwa na Serikali kwa kutoilipa VAT return ya jumla ya shilingi bilioni 12 Kampuni hiyo ya *Premium Active Tanzania Limited* na hivyo kampuni hiyo kushindwa kushirikiana na *SONAMKU* kuanzisha au kufufua kile kiwanda.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha hizi fedha zinalipwa ili sisi Wananamtumbo tuwe na uhakika na soko la tumbaku kwa kufufua hicho kiwanda? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalila pili, Wananamtumbo tunajihuisha vilevile na kilimo cha Korosho na Mazao mchanganyiko ya mahindi mbaazi, ufuta, alizeti na soya. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha masoko ya mazao haya ili Wananamatumbo tuendelee kupata nafuu lakini na suala la mbolea au pembejeo kwa ujumla?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu hayo Mheshimiwa Bashungwa, Naibu Waziri wa Kilimo.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Edwin Amandus Ngonyani, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Edwin Ngonyani kwa namna alivyoshirikiana na Serikali kupata soko la tumbaku kwa kampuni ya *Premium Active Tanzania Limited*. Nampongeza sana Mheshimiwa Ngonyani na kwa namna anavyohangaikia Wananamtumbo katika kuhakikisha wananaufaika na sekta ya kilimo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma ya Serikali ni kufufua viwanda vikiwemo viwanda ambavyo vinachakata mazao yanayotokana na kilimo likiwemo zao la tumbaku. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wizara ya Kilimo tutakaa na wenzetu upande wa Wizara ya Fedha kuangalia hili suala la VAT ambalo Mheshimiwa Ngonyani ameliuliza kama swalila lake la nyongeza namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia swalı lake la pili ni kuhusu mkakati wa Serikali katika uhakikisha tunapata masoko ya uhakika ya mazao mchanganyiko pamoja na zao la tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya Serikali ya kuhakikisha tunapata masoko ya uhakika kwa wakulima wetu kwanza tumeanza na mikakati ya kupata *institutional buyers* na Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, walishuhudia Serikali ikisaini mkataba na *World Food Programme* kwa upande wa zao la mahindi kwa wakulima wetu na tunaendelea kuongea na *institutional buyers* wengine ambao watasaidia wakulima wetu kupata masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara kwa kushirikiana na Balozi zetu nje ya nchi tunaendelea kuwasiliana nao na kuangalia mikakati ya kushirikiana ili tuweze kupata masoko zaidi katika mazao mchanganyiko na mazao ya kimkakati. Kwa mfano, mwezi Mei, kuna timu inaenda China hususan kwa ajili ya kutafuta soko la tumbaku pamoja na parachichi, karanga na mazao mengine.

Kwa hiyo napenda kumhakikisha Mheshimiwa Ngonyani pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali inaendelea kujipanga na tayari tumefanikiwa katika maeneo ya kupata masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Waheshimiwa Wabunge kama Mheshimiwa Ngonyani alivyoshirikiana na Serikali kupata soko la tumbaku kuptia kampuni ya *Premium Active Tanzania Limited*, basi na wao waendelee kushirikiana na sisi Wizara ya Kilimo kuwasaidia wakulima wetu kupata masoko ya uhakika. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swalı linalofuata, linaulizwa na Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi, Mbunge wa Karatu na linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji.

Na. 105

Vijiji vitakavyonufaika na Mpango wa WSDP I

MHE. QAMBALO W. QULWI aliuliza:-

Kijiji cha Makhoromba ni kati ya vijiji 10 vilivyopangwa kunufaika katika mpango wa *WSDP-I* Wilayani Karatu. Hadi hivi sasa Wilayani Karatu mradi wa maji katika kijiji hicho haujatekelezwa:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza mradi huo ili wananchi hao waondokane na tatizo kubwa la kukosa huduma ya maji?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Makhoromba kina vitongoji vinne na kwa sasa upo mradi uliotekelawa na Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro kwa kushirikiana na wananchi pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Karatu, ambao unatoa huduma katika vituo vitatu vyta kuchotea maji, lakini kutokana na ugumu wa kijilografia hakuweza kufika kila kitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuona umuhimu wa kutatua tatizo la uhaba wa maji katika maeneo mengi ya kijiji hicho, Serikali iliweka kijiji hicho kuwa miongoni mwa vijiji 10 vilivyopangwa kunufaika na programu ya *WSDP-I*. Aidha, mradi wa maji katika kijiji hicho haukutekelezwa kwa kuwa kipaumbele kiliwekwa katika ukamilishaji wa miradi mingine ya *WSDP-I*/iliyokuwa imeanza kutekelezwa kabla ya kluanzisha miradi mipyta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeelekeza Halmashauri ya Wilaya ya Karatu kutafuta vyanzo vya uhakika vyenye maji ya kutosha vitakavyoweza kuhudumia maeneo mengi ya kijiji hicho kulingana na jirografia yake na kufanya usanifu wa mradi huo utengewe fedha katika mwaka wa 2019/2020.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Qambalo.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hali ya upatikanaji wa maji katika kijiji hicho ni mbaya sana, ukiongea habari ya vituo vitatu kwa wananchi zaidi 5,000 ni chini kabisa ya kiwango ambacho kinaruhusiwa. Sasa nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Mheshimiwa Waziri anajua Halmashauri ya Wilaya ya Karatu ina idadi ndogo ya watumishi katika sekta ya maji na kazi za kitaalam alizozielekeza kwa idadi ya wataalam tullionao haitaweza kukamilika. Je, yuko tayari sasa kuongeza nguvu ya uhandisi na wataalam wa *survey* ili kazi hiyo aliyoelekeza ifanyike kwa muda unaotakiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, vyombo vya watumia maji, mfano, Bodi za Maji, Mamlaka Jumuiya za Watumia Maji na Kamati za Maji zinatambulika kisheria na vimetoa huduma za usimamizi na uendelezaji wa miradi ya maji. Hivi karibuni Serikali imesimamisha uchaguzi wa chombo cha maji kinachoitwa *KAVIWASU* pale Karatu ambacho kimetoa huduma hiyo kwa zaidi ya miaka 20. Je, ni halali Serikali kuingilia mchakato wa kupata viongozi wa wananchi ili waweze kusimamia chombo chao? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri, lakini kubwa sisi kama Wizara ya Maji tunatambua changamoto kubwa sana ya maji Karatu na ndio maana tuna mradi mkubwa sana wa *TOM* zaidi ya milioni 650 ambaao tunaukeleza. Kikubwa tunatambua utekelezaji wa miradi

ya maji unategemeana na watumishi wa kutosha wenye weledi na wenyewe uwezo na sisi kama Wizara ya Maji ndio maana tukaja na Wakala wa Maji. Nataka nimhakkishie uanzishwaji wa wakala ule tutahakkishie tunaweka wataalam wetu wa kutosha na katika eneo lake ili mwisho wa siku wananchi wa Karatu waweze kupata maji safi, salama na yenye kutosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu chombo cha watumiaji maji, nataka nimhakkishie Mheshimiwa Mbunge hilo nimelipokea hebu tulifuatilie kwa ukaribu ili tuweze kulitolea ufanuzi wa haraka. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, Mbunge wa Chemba na linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Na. 106

Ujenzi wa Mahakama Chemba

MHE. JUMA S. NKAMIA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya ya Chemba?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Balozi Mahiga, Waziri wa Sheria na Katiba.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Wilaya ya Chemba ni moja ya wilaya zinazokabiliwa na ukosefu wa huduma za mahakama ya wilaya. Kwa nyakati tofauti, nimekuwa nikilieleza Bunge lako Tukufu kwamba Mahakama

ya Tanzania inakabiliwa na changamoto kubwa ya miundombinu ya kutolea huduma za kimahakama katika ngazi zote. Kati ya Wilaya 139 zilizopo nchini, ni Wilaya 34 tu zenye majengo ya mahakama.

Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Mahakama ya Tanzania imekuwa ama ikiazima majengo kwenye Ofisi za Halmashauri, Mkuu wa Wilaya au kupanga pale yanapokosekana kabisa majengo hayo, ili kuendelea kutoa huduma za kimahakama. Katika maeneo ambayo Mahakama ya Tanzania haina kabisa majengo huduma hiyo imekuwa ikiendelea kutolewa na mahakama ya wilaya nyingine iliyopo jirani kwa utaratibu wa kitembelea kwa ratiba walizojipangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uhaba wa miundombinu takribani wilaya mpya 29, iklwemo ya Chemba mkoani Dodoma ambayo imetokana na Wilaya ya Kondoa bado haina Mahakama ya Wilaya. Hivyo, Wilaya hiyo kwa sasa inaendelea kuhudumiwa na Mahakama ya Wilaya ya Kondoa. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2019/2020, mpango wa Mahakama ya Tanzania ni kuhakikisha kuwa jengo la Mahakama ya Wilaya ya Chemba linajengwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa lengo la Serikali ni kusogeza huduma za mahakama karibu na wananchi, naomba kumthibitishia Mbunge kwamba tutafanya kila jithada ya kuendeleza ujenzi wa mahakama kila wilaya hapa nchini inapokuwa inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Mheshimiwa Nkamia.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza nishukuru kwa majibu ya historia ya Mheshimiwa Waziri. Halmashauri ya Wilaya ya

Chemba tayari tumeshatoa jengo kwa ajili ya Hakimu wa Wilaya na Hakimu wa Wilaya ya Chemba ameshateuliwa kama Waziri hana habari. Sasa swalilangu ni kwamba, kama majengo haya Waziri anasema inategemea na upatikanaji wa fedha ndio mahakama itajengwa, Hakimu ameteuliwa kuja kufanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mheshimiwa Waziri kwa taarifa tu ni kwamba, Wizara ya Mheshimiwa Waziri tayari imeshanunua kiwanja Chemba na wamekwenda kukikagua. Sasa anaponiambia hapa kwamba inategemea na upatikanaji wa fedha, naomba anihakikishie hizo fedha kwenye bajeti ya mwaka huu zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Chemba?

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa maswali hayo mawili Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Balozi Dkt. Mahiga.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba pesa hizo zimetengwa na ninaposema upatikanaji wa pesa ni kama fedha hizo tukiziomba zilizotengwa tutaweza kuzipata kutoka Hazina ili tuzielekeze katika kufanya shughuli za kazi na huduma katika Wilaya ya Chemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumhakikishia hilo. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, leo ndio siku yenyele ya hoja ya Wizara hii na muda wetu umeenda sana mnafahamu, kwa hiyo sitachukua tena maswali ya nyongeza.

MWENYEKITI: Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, leo ndiyo siku yenyele, leo ndiyo hoja ya Wizara hii na muda wetu umeenda sana mnafahamu, kwa hiyo, sitachukua tena maswali ya nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na matangazo. Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni waliopo Jukwaa la Spika, tuna wageni 17 wa Mheshimiwa Dkt. Augustine Mahiga, Waziri wa Katiba na Sheria ambao ni viongozi wa Wizara na Taassiszi zilizo chini ya Wizara hii ambao ni Prof. Sifuni Mchome - Katibu Mkuu; Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ndugu Amon Mpanju; Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu Tanzania, Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi; Kaimu Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu, Kanda ya Dodoma, Mheshimiwa Jaji Latifa Mansour; Kaimu Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Ndugu Solanus Nyimbi; Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dkt. Evaristo Longopa. Karibuni sana. (*Makof*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba mnisikilize. Tunaye Mkurugenzi wa Mashtaka (*DPP*) - Ndugu Biswalo Mganga; Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka - Ndugu Edson Makallo; Wakili Mkuu wa Serikali (*Solicitor General*) - Dkt. Clement Mashamba; Naibu Wakili Mkuu wa Serikali - Dkt. Ally Possi na Kabidhi Wasii Mkuu *RITA* -- Ndugu Emmy Hudson. (*Makof*)

Wageni wengine ni Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Mheshimiwa Jaji January Henry Msofe; Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Ndugu Casmir Kyuki; Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, Dkt. William Pallangyo; Kaimu Katibu Mtendaji Tume ya Hakiza Binadamu na Utawala Bora, Ndugu Fatuma Muya; Katibu Msaidizi, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Ndugu Enziel Mtei na Kaimu Naibu Mkuu wa Chuo, Taaluma, Tafiti na Ushauri, Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto, Ndugu Mwanabaraka Mnyukwa. Ahsante sana wageni wetu kwa shughuli yetu ya leo. (*Makof*)

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tuna mgeni wa Mheshimiwa Jumaa Aweso, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambaye ni ndugu yake kutoka Pangani,

Mkoani Tanga Ndugu Rahma Kilumanga. Karibu sana.
(Makofi)

Tuna wageni sita wa Mheshimiwa Japhary Michael, ambao ni familia yake kutoka Moshi, Mkoani Kilimanjaro wakiongozwa na shemeji yake Ndugu Hope Mushi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Neema Mgaya, ambao ni wafanyakazi kutoka DAR 24 Media, Mhariri Pius Yalula, Mtangazaji Ndugu Mercy Mbaya na Mpigapicha Ndugu Issa Ramadhani. Karibuni *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Mbunge wa Longido ambaye ni mpiga kura na mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido Ndugu Jacob Laiser. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Goodluck Mlinga ambaye ni Ndugu Getrude Ndibalema, huyu alikuwa Naibu Katibu Mkuu wa BAVICHA ambaye amehamia CCM. Karibu sana.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NWENYEKITI: Mheshimiwa Susan Lyimo, mimi nasoma kilichoandikwa hapa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NWENYEKITI: Imeandikwa aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa BAVICHA ambaye amehamia CCM jana tarehe 16/4/2019. *(Makofi)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MBUNGE FULANI: Asimame hatujamuona.

MWENYEKITI: *Order, order, order in the House. (Makof)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MBUNGE FULANI: Mwenyekiti asimame tumuone vizuri.
(Makof)

MWENYEKITI: Karibu sana Bungeni lakini karibu sana
CCM. *(Makof)*

Tunao wageni 19 wa Mheshimiwa Rashid Ajali Mbunge amba ni Walimu kutoka Newala, Mkoani Mtwara wakiongozwa na Mwalimu Musa Ngozi. Walimu wetu toka Mtwara, karibuni sana. *(Makof)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Salome Makamba, amba ni familia yake kutoka Jijini Dodoma, wakiongozwa na mama yake mzazi Ndugu Mary Makamba. Karibuni sana. *(Makof)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, amba ni wafugaji kutoka Hanang', Mkoani Manyara amba ni Ndugu Yohana Bilo na Ndugu Mathayo Darema. Karibuni sana wageni wetu. *(Makof)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria amba ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa, Wilaya ya Rufiji wakiongozwa na Ndugu Rajab Mbonde Kaswakala na Ndugu Omari Mtua, Katibu wa Wilaya ya Rufiji. Karibuni sana wageni wetu kutoka Rufiji. *(Makof)*

Katika orodha ya wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, tunaye pia Mheshimiwa Jaji George Masaju. Wengi mtamtambua alikuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Karibu sana. *(Makof)*

Ahsanteni sana kwa makofi hayo, wanasema wanam-*miss* sana, lakini tunaye Dkt. Kilangi kama AG. Ndiyo hivyo tunapokezana Waheshimiwa.

Kuna kundi la wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo, tuna wanafunzi 166 na walimu saba kutoka Shule ya Sekondari ya Msalato ambao wametembelea Bunge kujifunza jinsi linavyofanya kazi zake wakiongozwa na Mwalimu Abraham Danya. Karibuni sana. Tumieni muda huu vizuri muone yanayofanya Bungeni hapa lakini kubwa zaidi mkasome kwa bidii. (*Makofi*)

Matangazo mengine, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kutakuwa na mhadhara kwa umma kuhusu mwelekeo wa upatikanaji wa chakula, kukuza mnyororo wa thamani ya uzalishaji wa bidhaa zinazotokana na kilimo duniani. Mhadhara huo utafanyika Ukumbi wa Pius Msekwa, saa 8.00 mchana. Mgeni rasmi atakuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Job Ndugai. Wabunge wote mnakaribishwa.

Tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mwenyekiti wa Jumuiya ya *St. Thomas More* Bungeni hapa kwamba leo tarehe 17/04/2019 kutakuwa na Ibada ya Misa kwa Wakristu Wakatoliki mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa 7.00 mchana ambayo itafanyika katika ghorofa ya pili ya Ukumbi wa Msekwa. Wabunge wote mnaopenda kushiriki kwenye Ibada hiyo mnakaribishwa, Wakristu, mimi najumuisha Wakristu wote siyo wa *Roman Catholic* tu.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nisahihishe kidogo, wakati nikamtambulisha mgeni wa Mheshimiwa Salome Makamba, ni mama yake mzazi Mheshimiwa Salome Makamba ambaye ni Mwenyekiti wa Mtaa kuitia CCM kule Shinyanga. (*Makofi*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

NWENYEKITI: Mnaona mambo yalivyo matamu? Mama yuko huku CCM lakini binti yake yuko CHADEMA, ndiyo maisha hayo. karibu sana mama yetu. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Ndiyo muache ubaguzi.

NWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu ndiyo huo mnauna, matangazo yangu nimemaliza, kama nimeruka mengine tutatangaza baadaye. Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2010 - Wizara ya Katiba na Sheria

MWENYEKITI: Ahsante.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

MWENYEKITI: Haya, ngoja nichukue *notebook*, Mheshimiwa Sophia.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 68(7), kwa sababu ya muda sitaisoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge letu liko kwenye Jumuiya mbalimbali za Mabunge ya Afrika Mashariki na SADC. Sisi kama Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

kwenye Bunge letu kuna vyama mbalimbali ya Kibunge ambavyo vinawaweka Wabunge pamoja kuweza kueleza shida zao mbalimbali ili ziweze kutatuliwa au kueleweka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge letu la Tanzania lina Chama kinaitwa *TWPG* na chama kama hicho kipo Uganda, wenzetu wanaita *UWOPA*. Moja ya lengo la *TWPG* na *UWOPA* tukiweka vyama vyetu pembeni ni kuongeza idadi ya wanawake kwenye Bunge hili bila kuzingatia chama lakini kutetea haki za wanawake waliopo katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Mheshimiwa Masoud ambaye ni mwanaume hayuko kwenye chama chetu, alileta hoja ya kutetea watoto wa kike katika Bunge lako tukufu. Hoja hiyo iliungwa mkono na baadhi ya wanawake na wengi wakaipinga akiwemo Naibu Spika akaitolea ufanuzi kwamba mabweni siyo sababu pekee ya kuwafanya watoto wa kike wapate mimba. Katika mapambano haya sisi kama wanawake na katika Chama chetu cha *TWPG*, tunadhani tunapopeleka ajenda mbele, ni ili kuhakikisha Serikali na wadau ambao ni wanaume wajue umuhimu wa mtoto wa kike, lakini nashangaa kama wanawake hatufuati azimio hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, je, kuna umuhimu wa hiki Chama cha *TWPG* kutumia fedha za wahisani kutufanya mafunzo sisi kama Wabunge wanawake kwa umoja wetu au hawa wahisani wanapoteza hizo *resources* kutuletea sisi Wabunge tulioko katika Bunge lako? Je, naruhusiwa kama Mbunge binafsi kuwaandikia wahisani wasitupatie hizo fedha badala yake wapeleke kujenga hayo mabweni? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbarouk.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 47(1)(2) ambayo naomba niisome kutokana na umuhimu wake.

Kipengele cha (1) kinasema: "Baada ya muda wa maswali kuisha, Mbunge ye yote anaweza kutoa hoja kuwa Shughuli za Bunge kama zilivyoorodheshwa kwenye Orodha ya Shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma." Kipengele cha (2) kinasema: "Hoja ya namna hiyo itakuwa ni maalum na inaweza kutolewa wakati wowote hata kama majadiliano yanaendelea."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wangu kwako ni kwamba nchi yetu ya Tanzania ni mionganini mwa nchi zilizoridhia na kusaini Mkataba wa Kulinda Haki na Usalama wa Watoto Duniani. Pia katika siku za karibuni pametokea wimbi la mauaji ya watoto wadogo. Jambo hili lilianza mwaka jana katika Jiji la Dar es Salaam waliuawa karibu watoto wanne.

Vilevile likajitokeza katika Mkoa wa Njombe wakauliwa watoto saba kwa mara moja, lakini jana katika vyombo vyta habari wametangaza tena kwamba Tabora watoto sita wameuliwa kwa kupigwa mapanga na watoto wanne mpaka sasa hivi wako mahtuti hospitalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tabia tunapozungumza mambo tunasema jambo hili halijatokea hapa Bungeni, lakini kwa mujibu wa Kanuni hiyo hao watoto wanaouawa ni sehemu ya umma wa Tanzania. Mimi naomba kutoa hoja tuahirishe shughuli za Bunge tujadili hili suala la watoto kuendelea kuuawa na limeanza katika mikoa mitatu lakini ni kama tone la mafuta ya taa litaendelea kwenye mikoa mingine mpaka litakuwa sasa ni janga la kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja hiyo na naomba mwongozo wako.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MWENYEKITI: Ngoja nimalize hawa nilionao, Mheshimiwa Haonga.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) na kwa sababu ya muda tu kwamba hautoshi, sitaisoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati swali namba 104 linajibowi, Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa anajibu swali hilo alisema kwamba Wabunge tushirikiane na Wizara kutafuta masoko ya mazao na tuige mfano wa Mbunge *Engineer Ngonyani* kama alivyofanya kwenye zao la tumbaku.

Mheshimiwa Mweyekiti, tunafahamu wote kwamba mwaka 2018 wakati wakulima wa kahawa kule Bukoba waliposikia kwamba soko la kahawa ni zuri Uganda, wakapeleka kahawa yao, Serikali iliwazuia na wananchi wengine nasikia walikamatwa, kitu ambacho kwa kweli killitusikitisha sana. Kwa sababu mkulima anapokuwa analima, ananunua pembejeo kwa bei ya juu sana na wakati anahangaika Serikali imekaa pembedi, anapokuja kujitafutia masoko Serikali ndipo inapoingia na kusema kwamba usiuze kahawa yako au mazao yako sehemu fulani, uza kwa utaratibu huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako, je, Waziri alikuwa kweli *serious* kwenye hili jambo alilokuwa anazungumza? Yuko tayari sasa kuruhusu sisi Wabunge pamoja na wakulima wetu huko majimboni kutafuta masoko popote pale na Serikai haitatuingilia tena tukipeleka kahawa Uganda na maeneo mengine ya nchi? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Makilagi.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati unapokea miongozo tofauti tofauti, amesimama Mheshimiwa Mbunge Mama Mwakagenda ambaye kwa kweli huwa namheshimu sana na ninampenda sana; alizungumza jambo ambalo kwa kweli binafsi naona amepotosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo yake amesema, kuna hoja iliwasilishwa ikihusiana na masuala ya mimba za utotoni na kwamba Naibu Spika alipinga na baadhi ya Wabunge wanawake hatukuunga mkono na kwamba tuko kwenye kikundi cha wanawake cha *TWPG* lakini hatukuunga mkono. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niweke vizuri kumbukumbu kwamba Naibu Spika hakupinga na wala Wabunge wanawake hatukupinga, kilicholetwa hapa Bungeni ni takwimu zinazoonesha suala zima la watoto kutokuwepo shulenii na kiwango kikubwa kilioneshwa ni utoro na siyo mimba. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, kilichoonekana, suala zima la ujenzi wa mabweni siyo pekee la kumfanya mtoto apate mimba, ni pamoja na malezi na makuzi ya wazazi, ni pamoja na changamoto mbalimbali zinazowakabili watoto. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka niweke vizuri hizi taarifa, maana taarifa ililetwa hapa na Mheshimiwa Naibu Spika alitusomea na hakupinga na hakuna Mbunge ye yote aliyepinga. Kinachotakiwa kufanyika hapa ni sisi wazazi kwenda kulea watoto na suala la mabweni siyo kigezo peke yake cha kufanya watoto wapate mimba shulenii. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge.

Nianze na Mheshimiwa Haonga. Umeomba mwongozo wangu kutowana na majibu yaliyotolewa na Serikali kuititia Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo. Mwongozo wangu kwa suala hilo ni kwamba kwa mujibu wa kanuni zetu, lakini pia kwa mwongozo ambao umetolewa huko nyuma, naurudia; kama mwenye swali kajibowi na Serikali halafu kauliza maswali yake na akaridhika na maswali ambayo yamejibowi na Serikali kuititia Waziri aliyekuwa anajibu maswali hayo, wewe ambaye ni Mbunge unauliza swali la

nyongeza huwezi ukaomba Mwongozo kwamba majibu uliyopewa hayakukidhi kiwango cha majibu uliyotarajia. Unachoweza kufanya ni kuuliza swalii la msingi kwenye eneo ambalo unadhani halijakaa vizuri. Kwa hiyo, kwa maelezo uliyoyatoa, kama wewe unadhani majibu ambayo yametolewa kwa Mheshimiwa Ngonyani hayaendani na uhalisia, wewe una uwanja mzuri tu wa kuuliza swalii la msingi kwa Serikali na utapata sasa nafasi ya kujibiwa, nawe utayasema yale uliyonayo. Huo ndiyo mwongozo wangu kwako.

Mheshimiwa Sophia, nimshukuru tu Mheshimiwa Makilagi kwa hayo aliyojasema. Nadhani alikuwa anatoa taarifa zaidi kuliko mwongozo, nilivyomwelewa ili kuliweka suala hili sawa. Mheshimiwa Sophia una uzoefu wa Kanuni. Swalii hili liliulizwa juzi; majibu yalitolewa, nami nilikuwa humu. Halijatokea mapema leo humu.

Kwa hiyo, liko nje kabisa, sina kitu kinachowezesha mimi nikupe mwongozo kwa hilo. Kwa hiyo naliweka pembedi. Hayo mambo mwende mkakae kwenye vikao vyenu kule mkayazungumze, yatakuwa na tija na afya zaidi kule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mbarouk, umetumia kanuni ya 47 (1) na (2) kuhusu dharura. Kanuni zetu ziko wazi kabisa kwa masuala haya. Kanuni ya 47, usiishie tu hapo, nenda na kwenye 48 na hasa ile ya 48 (4): "jambo lolote litahesabiwa kuwa ni lenye maslahi kwa Umma iwapo utatuzi wake unategemea hatua zaidi kuliko zile za utekelezaji wa kawaida wa sheria peke yake." Sasa yote haya ambayo unayasema, tukio moja moja au matukio mawili katika eneo moja, lakini yote unaona ni kama uvunjifu wa sheria.

Hata ungesema Bunge lisitishe shughuli zake kuzungumza hilo, tutakuwa tunaongelea nini? Ndiyo maana nasema, hoja yako nilikuruhusu uielezee hatua ya kwanza, maana lazima uielezee nimekuruhusu, hatua ya pili ilikuwa nione kama linakaa vizuri sasa nikupe tena nafasi useme ili sasa uungwe mkono na Wabunge.

Mimi narinidhika kwamba hatuna jambo la dharura ambalo litafanya tusitishe kwa muda shughuli zetu. Kwa maoni yangu pia, mwongozo wangu, huo hautakuwa utaratibu mzuri wa kuendesha shughuli za Bunge. Huo ndiyo mwongozo wangu kwa hayo maeneo manne.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Kama nilivyosema, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria Dkt. Augustine Phillip Mahiga, uwasilishe hoja yako, una muda usiozidi saa moja. Karibu sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2010 - Wizara ya Katiba na Sheria

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani za pole. Awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa fadhila na rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana tena katika Bunge lako, kuwasilisha na kujadili mpango wa makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunitfea tena kuitumikia Serikali ya Awamu ya Tano katika nafasi nyingine ya Waziri wa Katiba na Sheria. Ninaahidi kuitumia nafasi hii kwa uadilifu, uaminifu na unyenyekevu mkubwa kwa maslahi mapana ya Taifa na wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majonzi makubwa nikupe pole wewe, Bunge lako, familia na wananchi wote wa Korogwe Vijijini kwa kuondokewa na mwenzetu Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijijini kupitia Chama cha Mapinduzi na Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria aliyefariki tarehe 2 Julai, 2018. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo mkunjufu, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri kwa niaba ya Spika, kwa kuliongoza na kulisimamia Bunge letu katika kuishauri Serikali. Pia nampongeza Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansansu na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kutekeleza majukumu yao kwa umahiri na kwa kuzingatia katiba, sheria, kanuni na taratibu zillizowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile natumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri ambayo imeweeka msingi wa mwelekeo wa kisera na kiutendaji katika utekelzaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2019/2020. Aidha, nampongeza kwa uongozi wake mahiri katika kusimamia shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako, naomba niwapongeze Wenyeviti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mohamed Omari Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene Mbunge wa Kibakwe kwa uongozi wao mahiri ikiwa ni pamoja na kuziwezesha Kamati wanazoziongoza kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inayo imani kubwa kwao na itaendelea kuwapatia ushirikiano unaostahili katika kipindi chote cha uongozi wao. Vile vile natoa

shukurani za dhati kwa Kamati hizo kwa kazi kubwa ya kuchambua Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilihakikishie Bunge lako kuwa Wizara yangu inatambua na kuthamini mchango wa Kamati hizi katika...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu Bungeni.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: ...kuhakikisha sheria na mchango wao kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu katika nyanja za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii, kitamaduni, mazingira na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika nitumie nafasi hii kuwapongeza kwa dhati Wabunge wenzangu waliochaguliwa hivi karibuni kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ambaye ni Mheshimiwa *Engineer Christopher Kajoro Chiza*, Mbunge wa Jimbo la Buyungu; Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Jimbo la Monduli; Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Jimbo la Ukonga; Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijiji; Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Jimbo la Liwale; Mheshimiwa James Kinyasi Millya, Mbunge wa Jimbo la Simanjiro; Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Jimbo la Ukerewe; Mheshimiwa Ryoba Chacha Marwa, Mbunge wa Jimbo la Serengeti; Mheshimiwa Pauline Philip Gekul, Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini; na Mheshimiwa Abdallah Ally Mtalea, Mbunge wa Jimbo la Temeke. Binafsi ninawatachia kila la heri na baraka za Mwenyezi Mungu katika kutekeleza majukumu yao ya Ubunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwapongeza Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika kipindi

cha mwaka 2018/2019 kuziongoza Wizara mbalimbali za Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongezo Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge na Waziri wa Viwanda na Biashara; Mheshimiwa Josephat Ngailonga Hasunga, Mbunge na Waziri wa Kilimo; Mheshimiwa Angella Jasmine Mbelwa Kairuki, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji; Mheshimiwa Dotto Biteko, Mbunge na Waziri wa Madini; na Mheshimiwa Profesa Palamagamba Johan Aidan Mwaluko Kabudi, Mbunge na Waziri wa Mambo ya Nje ya Nchi na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza Waheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mbunge na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii; Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge na Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na Mheshimiwa Innocent Lughu Bashungwa, Mbunge na Naibu Waziri wa Kilimo. Nawatakia wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nafasi mbalimbali katika utumishi wa Umma. Kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao mapya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria inaongozwa na dira isemayo, "Katiba na Sheria Wezeshi kwa Maendeleo ya Taifa; na dhima ya kuwa na "Mfumo Madhubuti wa Kikatiba na Kisheria Wenye Kufanikisha Utekelezaji wa Sera na Mipango kwa Maendeleo ya Taifa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu muundo na majukumu ya Wizara. Wizara ya Katiba na Sheria inajumuisha mhimili wa Mahakama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Wakala wa Usajili, Ufisili na Udhamini, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Kurekebisha Sheria, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika hati ya mgawanyo wa majukumu kwa Mawaziri kama ilivyoorodheshwa katika Ibara ya 10 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2018/2019. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara yangu ilipanga na kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maeneo mahsus ya kipaumbele kwa misingi ya kufanikisha Dira ya Wizara. Vipaumbele vilivyonetekelezwa katika kipindi hiki ni kama inavyoonekana katika Ibara 11 ya hotuba yangu. Aidha, hatua zilizochukuliwa ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maandalizi ya Sheria ya Taifa; Wizara yangu, kwa ushirikiano na wadau muhimu wa sekta ya sheria, imeendelea na utunzi wa Sheria ya Taifa ya Sheria kama moja ya mikakati ya Wizara kuimarishe sekta ya sheria ili iweze kutoa mchango stahiki kwa maendeleo ya Taifa na wananchi kwa ujumla, hususan katika kufikia maendeleo ya uchumi wa kati wenye kutegemea viwanda na kupunguza umaskini. Hatua iliyofikiwa ni kama inavyoilezwa katika Ibara ya 13 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio na maboresho ya sheria mbalimbali. Wizara yangu ilifanya uchambuzi wa kisera na kisheria wa mfumo wa sheria zinazosimamia utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala ya kuandaa mapendekezo ya kuwezesha kutungwa kwa sheria mahsus ya utatuzi wa migogoro kwa njia za majadiliano, upatanishi, maridhiano na usuluhishi kama njia mbadala ya utatuzi wa migogoro, kama ilivyofafanuliwa katika Ibara ya 14 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarishe utendaji wa Sekta ya Sheria na pia kuhakikisha kwamba sheria zilizopo zinaakisi hali halisi ya sasa na kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kiteknolojia na mazingira, Wizara iliwasilisha Bungeni mapendekezo ya marekebisho ya Sheria mbalimbali kama zilivyobainishwa katika Ibara 15 hadi 17 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkakati wa kusimamia masuala ya Utajiriasilia na Rasilimaliasilia; katika kuhakikisha kuwa kunakuwa na ufanisi katika utekelezaji wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Umiliki na Usimamizi wa Utajiriasilia na Maliasilia za Nchi ya mwaka 2017 na Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Biashara na Uwekezaji katika utajiriasilia na maliasilia za nchi ya mwaka 2017, Wizara yangu tayari imeandaa rasimu ya Mkakati unganishi wa juhudni mbalimbali za wadau wa sheria hiyo. Hivi sasa Wizara inaendelea kufanya maandalizi ya kuiwasilisha Rasimu hiyo kwenye majukwaa mbalimbali ya wadau kwa ajili ya maboresho na umiliki wake. Maelezo ya kina kuhusu eneo hili yanapatikana katika Ibara ya 18 na 19 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria; Wizara imeendelea na maandalizi ya Awamu ya Pili ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria kwa kuendesha m Kutano wa awali wa wadau waliopata fursa ya kuchangia uzoefu wao katika historia ya maboresho hapa nchini na pia kupendekeza kuhusu mambo muhimu ya kuzingatiwa katika awamu ijayo ya sekta ya sheria. Kutokana na maoni hayo Wizara yangu imeandaa rasimu ya awali ya awamu ya pili ya maboresho ya sekta ya sheria ambayo itaendelea kuboreshwa kwa njia ya tafiti na ushirikishwaji wa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maboresho ya Mfumo wa Utoaji Haki; itakumbukwa kwamba, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, alifanya marekebisho ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuititia Matangazo ya Serikali Na.48, 49 na 50 ya tarehe 13 Februari, 2018. Kuititia marekebisho hayo Rais alianzisha taasisi mbili mpya ambazo ni Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Hivyo, napenda kulifahamisha Bunge lako kuwa mwezi Julai, 2018, Mheshimiwa Rais aliridhia rasmi kuanza kutumika kwa miundo mipy ya Ofisi hizi ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na tija zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usikilizwaji wa mashauri; kwa muda mrefu sasa suala la kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani limekuwa ni moja ya vipaumbele muhimu vyta Serikali katika kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata haki sawa na kwa wakati. Katika kufanikisha azma hiyo, Mahakama ya Tanzania iliendelea na jukumu lake la kusikiliza mashauri mbalimbali katika Mahakama ya Rufani, Mahakama Kuu, Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya na Mahakama ya Mwanzo. Maelezo ya kina kuhusu hatua mbalimbali zilizochukuliwa yanapatikana katika Ibara ya 24 hadi 28 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha utawala bora, maadili na uwajibikaji wa watumishi, Mahakama ya Tanzania ilifanya ukaguzi wa huduma za kimahakama katika kanda zote kumi na nne za Mahakama Kuu na kuhusisha vituo 839 vyta Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya na Mahakama Kuu, kati ya vituo 980 vilivypopo nchini, sawa na asilimia 86. Aidha, jumla ya malalamiko 1,046 ya wananchi yanayohusu kero za upatikanaji wa huduma mbalimbali za mahakama yalipokelewa ambapo malalamiko 951, sawa na asilimia 91 yalishughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Ujenzi wa Majengo ya Mahakama; Mahakama imeendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Kuboresha Huduma za Mahakama ikiwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa Mahakama katika ngazi mbalimbali nchini. Miradi iliyotekelizwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 ni ujenzi wa majengo ya Mahakama Kuu katika Mikoa ya Kigoma na Mara ambayo imefikia asilimia 85 na kwamba huduma za kimahakama zimeanza kutolewa katika Mahakama hizo kama ilivyoelezwa katika Ibara 30 na 31 na kiambatisho A cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuboresha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kimahakama; katika kuhakikisha ubora na ufanisi wa huduma za kimahakama nchini, Mahakama ya Tanzania inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika usikilizaji wa mashauri na

shughuli za utawala. Mfumo huu umemwezesha mwananchi kufungua shauri moja kwa moja bila ya kulazimika kufika mahakamani kwa ajili hiyo. Haya ni mafanikio makubwa katika kuharakisha upatikanaji wa huduma bora za kimahakama na kwa gharama nafuu kwa Serikali na mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uandishi, Urekebu na Ufasiri wa Sheria; kama nilivyoeleza hapo awali, moja ya majukumu ya msingi ya Wizara yangu ni kuhakikisha kuwa wakati wote sheria za nchi zinakwenda na wakati na zinaakisi sera na vipaumbele vya Serikali kuhusu maendeleo katika nyanja za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, mazingira na teknolojia. Hivyo, katika mwaka 2018/2019, Wizara kuititia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, iliandaa Miswada 11 na Sheria Ndogo 271 ziliandaliwa au kuhakikiwa na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilifanya ufasiri wa Sheria Kuu saba na Sheria Ndogo 22 kwa lugha ya Kiswahili ili kuongeza ulewa wa sheria kwa wananchi. Kadhalika, jumla ya sheria 55 zilifanyiwa urekebu ili kukidhi mahitaji ya sasa ya jamii. Maelezo ya kina kuhusu eneo hili yanapatikana katika viambatisho B, C na D ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi wa Masuala ya Mikataba, kuititia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara yangu inaendelea kushiriki na kutoa ushauri wa kisheria katika majadiliano mbalimbali ya mikataba ya kibishara, mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa, ambapo katika kipindi hicho jumla ya mikataba ya kitaifa na kimataifa 1,032 ilifanyiwa upekuzi. Kati ya mikataba hiyo, mikataba 357 ilikuwa ni ya ununuzi na 316 ni ya makubaliano ya kimataifa na makubaliano katika masuala ya fedha.

Aidha, mikataba 376 ilithamanishwa kwa fedha za Kitanzania Shilingi triliioni 2.7; mikataba 65 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 3.2 na mikataba 20 yenye thamani ya Euro milioni 1.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utoaji wa Ushauri wa Kisheria; katika kuimariswa ushauri wa kisheria unaotolewa kuititia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara imepanga kuwa na mfumo wa mawasiliano ya ndani na nje ya ofisi kwa njia za kielektroniki. Katika kufikia azma hii, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanya upembuzi yakinifu wa mradi wa kielektroniki ili kubaini mahitaji halisi kwa ajili ya hatua nyineza za kiutendaji. Mradi huu utasaidia taarifa zinazohusu mikataba, makubaliano ya kimataifa, utoaji wa ushauri, taarifa za Mawakili wa Serikali, mwenendo wa safari za watumishi, mawasiliano ya ndani ya ofisi, usimamizi wa maktaba ya taarifa za kisheria, kumbukumbu za matukio muhimu, uandishi wa sheria, tafsiri na urekebu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuendesha Mashtaka; utawala wa sheria ni nguzo muhimu katika kudumisha amani, utulivu na umoja wa Taifa. Kwa kutambua hilo, Wizara yangu, kuititia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, iliendelea na uratibu wa shughuli za upelelezi wa makosa ya jinai, yakiwemo makosa dhidi ya watu kama vile ujambazi na mauaji, kufungua na kuendesha mashtaka ya jinai mahakamani ambapo jumla ya mashauri ya jinai 5,709 katika Mahakama Kuu ya Tanzania yaliendeshwa. Kati ya mashauri hayo 1,322 ni ya vikao vya Mahakama Kuu na 4,387 yanahusu rufani za Mahakama Kuu. Kati ya hayo, mashauri 2,000 yalihitimishwa, sawa na asilimia 35 na mashauri mengine 3,709 yanaendelea katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, washtakiwa waliotiwa hatiani kutokana na makosa hayo walipewa adhabu zikiwemo vifungo na faini ambapo kiasi cha shilingi bilioni 4.8 zililipwa mahakamani kama faini na mali zinazokadiriwa kuwa na thamani ya shilingi bilioni 39.6 zilitaifishwa kwa amri ya Mahakama. Maeleo ya kina yanapatikana katika Ibara 36 hadi 38 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha mfumo wa utoaji haki nchini, Serikali iliamua kutenganisha shughuli za upelelezi na uendeshaji mashtaka. Ili kufanikisha azma hii Wizara kuititia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea

kuchukua hatua mbalimbali, zenyе lengo la kufikisha huduma ya mashtaka katika wilaya zote nchini ifikapo mwaka 2022. Hivisasa Ofisi inaendesha mashauri ya jnai katika mahakama zote ishirini na sita za hakimu mkazi nchini na katika mahakama tano za Wilaya za Nzega, Tarime, Chato, Temeke na Monduli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uendeshaji wa Mashauri ya Madai na Usuluhishi; jukumu la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni kusimamia, kuratibu na kuimarisha uendeshaji wa mashauri ya madai, haki za binadamu, usuluhishi na mashauri ya kikatiba yanayoihusu Serikali. Katika kipindi cha mwaka 2018/2019, jumla ya mashauri ya madai 2,611 yalishughulikiwa. Kati ya hayo mashauri 214 yalihitimishwa, sawa na asilimia 8.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza wajibu huo, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imefanikiwa kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 9.02 ambazo zingelipwa kwa Mawakili Binafsi kwa kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali. Maelezo ya kina kuhusu eneo hili yanapatikana katika Ibara ya 41 hadi 43 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Haki za binadamu, Utawala Bora na Msaada wa Kisheria; Serikali ya Awamu ya Tano inatambua na kuheshimu wajibu iliyonayo wa kulinda, kukuza na kuendeleza haki za binadamu nchini kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi pamoja na mikataba ya kikanda na kimataifa ambayo nchi yetu imeridhia. Katika kutekeleza wajibu huu, Wizara ilishiriki Mkutano wa Viongozi wa Juu wa Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa ambapo ilipata fursa ya kuelezea hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kulinda, kukuza na kuendeleza haki za binadamu hapa nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa Mpango Kazi wa Kitaifa na Mpango Mkakati wa Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendeleko ya Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Mapitio katika Kipindi Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kuhakikisha kuwa watu walio kwenye makundi yenye mahitaji maalum

wanawezeshwa kuifikia haki, wakiwemo wanawake, watoto, wazee na watu wenye ulemavu. Jaji Mkuu wa Tanzania ameandaa kanuni za uendeshaji wa mashauri ya watu wenye mahitaji maalum Namba. 110 za mwaka 2019 zinazotoa mwongozo unaozitaka mamlaka husika kukamilisha usikilizwaji wa mashauri yanayohusisha na makundi haya ndani ya muda usiozidi miezi sita. Mwongozo huu umeanza kutekelezwa na mahakama za ngazi zote nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kusimamia hifadhi ya haki za binadamu na utawala bora nchini, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliendelea kupokea na kushughulikia malalamiko ya wananchi kuhusu uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Vilevile Tume ya Haki ya Binadamu iliendelea kuelimisha umma kuhusu haki za binadamu kupitia vyombo vya habari, mikutano, machapisho na warsha katika Mikoa ya Mara, Mtwara, Mbeya, Manyara, Shinyanga, Dodoma, Tabora, Kagera, Kigoma, Tanga, Lindi, Kilimanjaro na Iringa. Maelezo ya kina kuhusu eneo hili yanapatika katika Ibara ya 44 - 48 ya hotuba yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, misaada ya kisheria, Wizara yangu iliendelea kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa huduma ya msaada wa kisheria nchini kwa kuandaa Kanuni za Sheria ya Msaada wa Kisheria pamoja na utungaji wa kanuni za maadili kwa watoa msaada wa kisheria. Vilevile, Wizara iliendelea na usajili, usimamizi na uratibu wa watoa huduma ya msaada wa kisheria kwa kuwapa mafunzo kuhusu utekelezaji wa majukumu yao wakiwemo maafisa themanini na tisa wa Jeshi la Polisi na sabini na sita wa Jeshi la Magereza. Maelezo ya kina kuhusu eneo hili yanapatikana katika Ibara ya 49 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya Mifumo ya Sheria Mbalimbali. Wizara iliendelea kuhakikisha kwamba sheria za nchi zinakwenda na wakati ikiwa ni pamoja na kuakisi mahitaji ya sasa ya jamii kuhusu maendeleo. Hivyo, kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Wizara yangu ilifanya mapitio ya sheria na tafiti katika mfumo wa sheria za utatuzi

wa migogoro ya ardhi Tanzania, mfumo wa sheria za ujenzi wa majengo, sheria za uchaguzi wa serikali za mitaa na mfumo wa sheria za masoko ya mazao ya kilimo na kukamilisha maandalizi ya andiko la majadiliano kwa tafiti zote. Maelezo ya kina kuhusu eneo hili yanapatikana katika Ibara ya 50 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, urejeshwaji wa wahalifu na ushirikiano wa kimataifa kuhusu makosa ya jinai. Katika kukabiliana na vitendo vya kihalifu, hususan uhalifu wa kuvuka mipaka ya nchi, Wizara yangu iliendelea kushughulikia masuala ya urejeshwaji wa wahalifu na kushirikiana na mataifa mengine. Katika kipindi cha mwaka 2018/2019, Wizara ilipokea na kushughulikia maombi saba ya kurejesha watuhumiwa wa makosa mbalimbali ya jinai waliokimbilia nchini na ilipeleka nje ya nchi maombi mawili ya kukusanya vielelezo ambayo yanaendelea kushughulikiwa katika nchi hizo. Maelezo zaidi yanapatikana katika Ibara ya 51 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkakati wa Kitaifa wa Usajili wa Matukio muhimu ya Binadamu na Takwimu. Wizara yangu iliendelea kuimarisha shughuli za usajili wa vizazi, vifo, ndoa, talaka na watoto wa kuasili, Mkakati wa Taifa wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu, ikiwa ni haki ya msingi ya utambuzi na upatikanaji wa takwimu kwa ajili ya maendeleo. Katika kipindi hicho Wakala wa Usajili Ufili na Udhamini ulisajili jumla ya vizazi milioni moja mia mbili sabini na moja elfu mia tatu sabini na mbili; vifo ishirini na nane elfu mia mbili themanini na tano; ndoa ishirini na sita elfu mia tisa hamsini na tatu; talaka mia moja ishirini na mbili na hati ishirini na nane za watoto wa kuasili, na kufanya kiwango cha kusajili watoto wa umri wa chini ya miaka mitano kufikia asilimia thelathini na nane ikilinganishwa na asilimia kumi na tatu mwaka 2012. Maelezo ya kina kuhusu eneo hili yanapatikana katika Ibara ya 52 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi za Mafunzo ya Masuala ya Sheria. Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto. Katika kuhakikisha watumishi wa sekta ya sheria

wanakuwa na ujuzi na weledi wa kutosha, Wizara yangu kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto imeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za Astashahada na Stashahada ya Sheria, mafunzo endelevu ya kimahakama kwa watumishi wa Mahakama na pia mafunzo ya muda mfupi kwa wadau wa sekta ya sheria nchini. Aidha, katika kipindi mwaka 2018/2019, Chuo kimeweza kuongeza kiwango cha udahili kutoka wanachuo mia saba ishirini hadi wanachuo mia nane arobaini na sita ikiwa ni ongezeko la asilimia kumi na nane ya lengo lilitlowekwa. Maelezo ya kina kuhusu eneo hili yanapatikana katika Ibara ya 53 na 54 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania. Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kutoa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo. Katika kipindi cha mwaka 2018/2019, Taasisi ilifanikiwa kutoa mafunzo kwa wanafunzi elfu moja mia saba tisini na moja. Idadi hii inajumuisha wanafunzi mia sita thelathini wa kundi la 28 ambao ni sawa na ongezeko la asilimia tano ya malengo ya udahili wa wanafunzi mia sita kwa kundi moja; wanafunzi mia tano ishirini na sita wa kundi la 27 sawa na asilimia themanini na nane ya malengo ya udahili na wanafuni mia sita thelathini na tano wa kundi la 26 sawa na ongezeko la asilimia sita ya malengo ya udahili. Maelezo ya kina kuhusu eneo hili yanapatikana katika Ibara ya 55 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maadili ya Watumishi na Maendeleo ya Rasilimali Watu. Sekta ya Sheria ni moja ya sekta ambazo hutegemea zaidi nguvu kazi inayotokana na rasilimali watu iliyopo katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake. Kwa kutambua hilo, Wizara yangu imeendelea kuwekeza katika rasilimali watu kwa kuajiri, kutoa mafunzo na kuimarisha shughuli za usimamizi ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma ambapo katika kipindi hicho, Wizara iliajiri jumla ya watumishi wapya mia moja sabini na tisa na kuwapatia mafunzo ya kuongeza ujuzi watumishi

mia tano tisini na tisa ikiwa ni pamoja na kuthibitisha kazini watumishi tisa na kupandisha vyeo watumishi ishirini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Tume ya Utumishi wa Mahakama ilijaza nafasi mpya za ajira ya watumishi wa Mahakama wapatao arobaini na nne, ilipandisha vyeo jumla ya watumishi mia tisa hamsini na nane, ilithibitisha kazini jumla ya watumishi mia mbili tisini na mbili pamoja na kuajiri katika masharti ya kudumu na malipo ya pensheni jumla ya watumishi mia mbili tisini na nane, na Majaji kumi na tano wa Mahakama Kuu waliteuliwa. Aidha, katika waliteuliwa Majaji sita wa Makahakama ya Rufani. Maelezo ya kina kuhusu eneo hili yanapatikana katika Ibara ya 56 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020. Wizara yangu imeendelea kuwajibika kikamillifu kwa wananchi kupitia utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi, ahadi na maelekezo mbalimbali yaliyotolewa na viongozi wa kitaifa. Miongoni mwa ahadi hizo ni pamoja na kuendeleza vita dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma; kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na kuendeleza utawala wa sheria; na kuimarisha mfumo wa utoaji haki. Katika kufikia azma hiyo, Wizara imeendelea kubuni mikakati na kutumia mbinu mbalimbali kulingana na mazingira ya eneo husika, ikiwa ni pamoja na kuendeleza vita dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma, kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na utawala bora na kuimarisha mfumo wa utoaji haki nchini kwa wakati. Maelezo ya kina kuhusu eneo hili yanapatikana katika Ibara ya 58 hadi 64 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtiririko wa mapato na maduhuli ya Serikali. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi bilioni mia moja tisini milioni mia nne tisini na tatu mia tisa themanini na mbili elfu kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya hizo, shilingi bilioni sabini na saba milioni mia moja sabini na tatu mia mbili tisini na tatu elfu ni Mishahara, shilingi bilioni sitini na nane milioni mia tano hamsini

na tatu mia nne sabini elfu ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni arobaini na nne milioni mia saba sitini na saba mia mbili kumi na tisa elfu kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Maendeleo jumla ya shilingi bilioni kumi na nane ni fedha za ndani na shilingi bilioni ishirini na sita milioni mia saba sitini na saba mia mbili kumi na tisa elfu ni fedha za nje. Maelezo ya kina kuhusu eneo hili yanapatikana katika Ibara ya 65 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi, 2019, Wizara ilipokea jumla ya shilingi bilioni mia moja kumi na moja milioni mia sita thelathini na tano mia mbili sabini na tatu elfu mia tatu hamsini na tisa sawa na asilimia hamsini na tisa ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni arobaini na nne milioni mia saba kumi na sita mia moja hamsini na moja elfu mia tatu thelathini na sita ni Mishahara na shilingi bilioni arobaini na tano milioni mia moja sitini na tano mia nne arobaini na tisa elfu mia moja sabini na tano ni Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Maendeleo ni shilingi bilioni ishirini na moja milioni mia saba hamsini na tatu mia sita sabini na mbili elfu mia nane arobaini na nane sawa na asilimia arobaini na tisa ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni saba ni fedha za Maendeleo za ndani na shilingi bilioni kumi na nne milioni mia saba hamsini na tatu mia sita sabini na mbili elfu mia nane arobaini na nane ni fedha za Maendeleo za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuli. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ilipanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni ishirini na saba milioni tisini na saba mia sita arobaini na sita elfu mia nane sitini na mbili kama maduhuli ya Serikali kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019, Wizara ilikusanya jumla ya shilingi bilioni nane milioni mia saba kumi na mbili mia saba elfu sawa asilimia thelathini na mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na wananchi wengi

kuwa na uhakika kuhusu upatikanaji wa huduma muhimu za kimahakama kutokana na miradi ya maboresho ya Mahakama inayotekelawa nchini; ongezeko la usajili wa vizazi; ujenzi, ukarabati wa majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali na kuanzishwa kwa huduma ya Mahakama zinazotembea (*mobile courts*); ujenzi wa Ofisi za kudumu kwa ajili ya Wizara na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Jiji la Dodoma; na kiasi kikubwa cha fedha na mali zilizopatikana kwa njia za kihalifu kurejeshwa. Maelezo ya kina kuhusu eneo hili yanapatikana katika Ibara ya 68 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto na mikakati ya kukabiliana nayo. Changamoto zilizokuwepo ni pamoja na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu masuala ya sheria na mwamko mdogo wa wananchi katika kuzitumia Kamati za Maadili kama ambavyo imefafanuliwa katika Ibara ya 69 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana ni kutokana na juhudzi za pamoja kati ya Wizara na wadau mbalimbali wa maendeleo. Nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa ushirikiano mzuri uliopo kati yetu na wadau hao ambao orodha yao inapatikana katika Ibara ya 71. Aidha, napenda niwahakikishie kuwa Wizara yangu inatambua na kuthamini uhusiano mzuri uliopo na tutafanya kila lililo ndani ya uwezo wetu kuhakikisha kuwa unaimarishwa kwa maendeleo ya sekta ya sheria na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimesimama mbele yako kusoma hotuba hii nyuma yangu kuna kikundi kikubwa cha watendaji na watumishi walioniwezesha kutekeleza majukumu yangu haya kwa ufanisi mkubwa. Vilevile naomba kutumia fursa hii kuwashukuru watumishi na watendaji wote kwa kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu. Kwa namna ya pekee, napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru viongozi wenzangu katika Wizara kwa kazi kubwa waliyofanya. Kipekee ninapenda kumshukuru Profesa Sifuni Ernest Mchome, Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria; Bwana Amon Anastas Mpanju, Naibu Katibu Mkuu; Mhe. Profesa

Ibrahimu Hamisi Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania; Profesa Adelardus Lubango Kilangi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na viongozi wote wakuu na watendaji wa Wizara na Taasisi kama inavyoonekana katika Ibara ya 72 ya hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango na bajeti kwa mwaka 2019/2020. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara yangu itaendelea kuboresha utoaji wa huduma za kisheria kwa umma ili kuendana na dhima ya kuwa na mfumo madhubuti wa kikatiba na kisheria wenye kufanikisha utekelezaji wa sera na mipango kwa maendeleo ya Taifa. Ili kufikia azma hiyo, Wizara yangu imeainisha maeneo muhimu ya kipaumble na kuyawekea mikakati ya utekelezaji wake kama ilivyoainishwa katika kifungu (f) cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele hivi, Wizara yangu inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 55,175,163,302/= kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na miradi ya maendeleo kwa mafungu yafuatayo:-

Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama, Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Fungu - 19 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashitaka, Fungu 48 - Wizara ya Katiba na Sheria, Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria. Maelezo ya kina kuhusu eneo hili yanapatikana katika Ibara ya 74 hadi 75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naliomba Bunge lako kuidhinisha jumla ya shilingi 126,162,468,756/= kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama. Kati ya fedha hizo, shilingi 108,004,000,564/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 22,157,900,576/= ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Maelezo ya ziada tapo kwenye Ibara ya 76.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara yangu inatarajia kusimamia na kukusanya jumla ya shilingi 12,606,487,000/= ikiwa ni maduhuli ya Serikali kutoka katika vyanzo mbalimbali kama ilivyoainishwa Ibara ya 77 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. AUGUSTINE PHILLIP
MAHIGA (MB), WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA AKIWASILISHA
BUNGENI MPANGO WA MAKADIRIO YA BAJETI YA WIZARA
KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 - KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kuitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Shukrani na Pole

2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim kwa wingi wa rehema zake na kwa kuniruzuku uhai na kunipa afya njema iliyoniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Aidha, kipekee kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kunitfea tena kuitumikia Serikali ya Awamu ya Tano katika nafasi nydingine ya Waziri wa Katiba na Sheria. Naahidi kuitumikia nafasi hii kwa uadilifu, uaminifu na unyenyekevu mkubwa kwa maslahi mapana ya Taifa na wananchi wote.

3. **Mheshimiwa Spika**, kwa majonzi makubwa nikupe pole wewe, Bunge lako, familia na wananchi wote wa Korogwe Vijijini kwa kuondokewa na mwenzetu Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijijini, kuititia Chama cha Mapinduzi na mjambe wa kamati ya kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, aliyefariki tarehe 2 Julai, 2018. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

Salamu za Pongezi

4. **Mheshimiwa Spika**, kwa moyo mkunjufu napenda kukupongeza wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri wa kuliongoza na kulisimamia Bunge letu katika kuisimamia na kuishauri Serikali. Nampongeza pia Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb) na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kutekeleza majukumu yao kwa umahiri na kwa kuzingatia Katiba, sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

5. **Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri ambayo imeweka msingi wa mwelekeo wa kisera na kiutendaji katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Aidha, nampongeza kwa uongozi wake mahiri katika kusimamia shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge lako tukufu.

6. **Mheshimiwa Spika**, kwa ridhaa yako naomba niwapongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mohamed Omari Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kwa uongozi wao mahiri ikiwa ni pamoja na kuziwesha kamati wanazoziongoza kutekeleza majukumu yake kikamilifu na ufanisi. Wizara yangu inayo imani kubwa kwao na itaendelea kuwapatia ushirikiano unaostahili katika kipindi chote cha uongozi wao. Vilevile, natoa shukrani za dhati kwa Kamati hizo kwa kazi kubwa ya kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Nilihakikishie Bunge lako tukufu kuwa Wizara yangu inatambua na kuthamini mchango wa Kamati hizi katika kuhakikisha Sekta ya Sheria inachangia kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu katika nyanja za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, mazingira na teknolojia.

7. **Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii pia kuwapongeza kwa dhati Wabunge wenzangu waliochaguliwa hivi karibuni

kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni Mheshimiwa Eng. Christopher Kajoro Chizza, Mbunge wa Jimbo la Buyungu; Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Jimbo la Monduli; Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Jimbo la Ukonga; Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijiji; Mheshimiwa Zuberi Mohammed Kuchauka, Mbunge wa Jimbo la Liwale; Mheshimiwa James Kinyasi Millya, Mbunge wa Jimbo la Simanjiro; Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Jimbo la Ukerewe; Mheshimiwa Ryoba Chacha Marwa, Mbunge wa Jimbo la Serengeti; Mheshimiwa Paulina Philipo Gekul, Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini; na Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea, Mbunge wa Jimbo la Temeke. Binafsi, nawatachia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yao ya Ubunge.

8. **Mheshimiwa Spika**, naomba kuwapongeza mawaziri wenzangu na naibu mawaziri tulioleuliwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/19 na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kuziongoza wizara mbalimbali za Serikali ya Muungano. Nimpongeze Mheshimiwa Joseph George Kakunda (Mb), Waziri wa Viwanda na Biashara; Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga (Mb), Waziri wa Kilimo; Mheshimiwa Anjellah Jasmine Mbelwa Kairuki (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji; Mheshimiwa Doto Biteko (Mb), Waziri wa Madini na Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Pia, niwapongeze Mheshimiwa Mary Machuche Mwanjelwa (Mb), Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Mheshimiwa Constantine John Kanyasu (Mb), Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii; Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara (Mb), Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa (Mb), Naibu Waziri wa Kilimo. Aidha, niwapongeza Mheshimiwa January Henry Msffe (JR Mst.) ambaye ameteuliwa kuwa mwenyekiti wa tume ya kurekebisha sheria na Bwana Iddi Mandi na Bwana Kalolo Bundala kwa kuteuliwa kuwa makamishna wa Tume ya Kurekebisha Sheria.

Niwatakie walioteuliwa na Mheshimiwa Rais, kushika nafasi mbalimbali katika Utumishi wa Umma, kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao mapya.

B. DIRA NA DHIMA

9. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inaongozwa na Dira ambayo ni Katiba na Sheria wezeshi kwa maendeleo ya Taifa. Dira hii inalenga kuweka mazingira rafiki ya kisera na ya kisheria kuwezesha utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Taifa, kudumisha hali ya amani, utulivu na utangamano wa kitaifa ambazo ni nguzo muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu. Aidha, Dhima ya Wizara ni kuwa na mfumo madhubuti wa kikatiba na kisheria wenye kufanikisha utekelezaji wa sera na mipango kwa maendeleo ya Taifa ambayo inahimiza ubunifu katika kujenga mazingira wezeshi ya upatikanaji haki na huduma bora za kisheria kwa wananchi.

C. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA

10. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inajumuisha Mhimili wa Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu/ Wakala wa Usajili Ufiliisi na Udhamini, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto. Aidha, Wizara yangu imeendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Hati ya Mgawanyo wa Majukumu kwa Mawaziri, kuititia matangazo Serikali Na. 144 la Aprili, 2016 na Na. 144A la Juni, 2016, ambayo ni kutunga Sera zinazohusu masuala ya kisheria na kusimamia utekelezaji wake; kushughulikia mambo ya kikatiba; kusimamia mfumo wa haki na utoaji haki; uandishi wa sheria; kuendesha mashtaka ya jinai; kushughulikia uendeshaji wa mashauri ya madai na mikataba mbalimbali inayohusu Serikali na uratibu wa sheria za kimataifa; kushughulikia masuala ya haki za binadamu na

msaada wa kisheria; kurekebisha sheria; kushughulikia urejeshwaji wa wahalifu na masuala ya ushirikiano wa kimataifa kwenye makosa ya jinai; kusajili matukio muhimu ya binadamu (vizazi, vifo, ndoa, talaka na uasili), kushughulikia masuala ya ufilisi na udhamini; kuboresha utendaji na maendeleo ya rasilimali watu iliyo chini ya Wizara.

D. MAPITIO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2018/2019

11. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara yangu ilipanga na kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maeneo mahsusи ya kipaumbele kama msingi wa kufanikisha utekelezaji wa Dira na Dhima ya Wizara. Maeneo hayo ya kipaumbele ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Sheria kwa ajili ya mambo ya kisheria na utekelezaji wake; kufanya mapitio na maboresho ya sheria mbalimbali; kuweka mfumo wa kimkakati wa kusimamia masuala ya utajiri na rasilimali asilia; kukamilisha maandalizi ya kutekeleza awamu ya pili ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria; haki na mfumo wa utoaji haki; usikilizaji wa mashauri; kuendelea na ujenzi wa majengo mahakama nchini kote; kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika huduma mbalimbali za kimahakama; uandishi, urekebu na ufasiri wa sheria; kuimarisha usimamizi wa masuala ya mikataba; uimarishaji wa miundombinu ya utoaji wa ushauri wa kisheria; kuendesha mashtaka; uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi; haki za binadamu, utawala bora na msaada wa kisheria; mapitio ya mifumo ya sheria mbalimbali; urejeshwaji wa wahalifu na ushirikiano wa kimataifa kuhusu makosa ya jinai; kuimarisha utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu; kuweka mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji kwa kuratibu upatikanaji wa sheria mahsusи ya ufilisi; kuboresha utoaji wa mafunzo sheria; kuboresha utendaji na maendeleo ya rasilimaliwatu; na kutekeleza mipango na miradi ya maendeleo.

12. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia vipaumbele hivyo, Wizara ilianda na kuwasilisha mbele ya Bunge lako Mpango

na Makadirio ya Bajeti yaliyopitishwa kwa ajili ya utekelezaji. Hivyo, kwa ridhaa yako naomba sasa niwasilishe taarifa kuhusu hatua mbalimbali zilizochukuliwa katika kutekeleza Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/19, mafanikio yaliyopatikana na changamoto mbalimbali zilizojiteza wakati wa utekelezaji na utatuzi wake, kama itakavyobainisha hapo chini:-

I. Maandalizi ya Sera ya Taifa ya Sheria

13. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu, kwa ushirikiano na wadau muhimu wa sekta ya sheria, imeendelea na utunzi wa Sera ya Taifa ya Sheria kama moja ya mikakati ya Wizara kuimarisha sekta ya sheria ili iweze kutoa mchango stahiki kwa maendeleo ya Taifa na wananchi kwa ujumla, hususan katika kufikia maendeleo ya uchumi wa kati wenye kutegemea viwanda na kupunguza umaskini. Katika kufikia azma hiyo, Wizara yangu iliandaa rasimu ya awali ya Sera ya Taifa ya Sheria kwa ushirikiano na wadau wa makundi mbalimbali ya kijamii. Hivi sasa Rasimu hiyo iko kwenye hatua ya kujadiliwa katika vikao vya ndani na hatimaye kupelekwa kwenye vyombo vya maamuzi serikalini. Tulitaraja Sera hii iwe imekamilika mwezi Septemba, 2018 lakini kutokana na ukweli kuwa sekta ya sheria ni mtambuka na ina wadau wa aina mbalimbali wenye maoni na mahitaji tofauti ya huduma ya sheria imekuwa vigumu kuikamilisha katika muda tuliotaraja. Ni matumaini yangu kuwa safari hii tulioianza itakamilika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 na kuweza kufanya mageuzi makubwa kabisa ya kisera katika historia ya sekta ya sheria hapa nchini.

II. Mapitio na maboresho ya sheria mbalimbali

14. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2018/19, Wizara yangu ilifanya uchambuzi wa kisera na kisheria wa mfumo wa sheria zinazosimamia utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala na kuandaa mapendelekezo ya kuwezesha kutungwa kwa sheria mahsus ya utatuzi wa migogoro kwa njia za majadiliano, upatanishi, maridhiano na usuluhishi kama njia mbadala ya utatuzi wa migogoro. Hatua hii ni utekelezaji wa masharti ya Kifungu cha 11 cha Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Umiliki na Usimamizi wa Utajiriasilia na Maliasilia

za Nchi ya mwaka 2017 ambacho kinaelekeza mashauri yote ya migogoro yanayohusisha utajiriasilia na maliasilia za nchi kuendeshwa hapa nchini kwa kutumia sheria na mifumo ya utatuzi wa migogoro ilivyopo hapa nchini. Aidha, hatua hii itasaidia kutoa ajira kwa wananchi wetu badala ya kuendelea kupeleka masuala ya aina hiyo na fedha nje ya nchi na hivyo kuviimarisha na kuvinufaisha vyombo vya nje na wataalamu waliopo huko.

15. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utendaji wa Sekta ya Sheria, Wizara iliwasilisha Bungeni mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Utekelezaji ya Majukumu ya Ofisi wa Kabidhi Wasii Mkuu, Sura ya 27, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20; Sheria ya Urejeshwaji wa Wahalifu, Sura ya 368; Sheria ya Tafsiri za Sheria, Sura ya 1; Sheria ya Ukomo, Sura ya 89; Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Sura ya 171; Sheria ya Kusaidiana katika Masuala ya Jinai, Sura ya 256; Sheria ya Huduma ya Mashtaka, Sura ya 430; Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268; Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura 329; Sheria ya Kuzuia Ugaidi, Sura ya 19; Sheria ya Kurejesha Mali Zitokanazo na Uhali, Sura ya 256; Sheria ya Chama cha Wanasheria Tanganyika, Sura ya 307, Sheria ya Mamlaka za Rufaa, Sura ya 141; Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, Sura ya 33; na Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11. Marekebisho ya sheria hizi yalilenga kuufanya mfumo wa sheria kuweza kuakisi mabadiliko mbalimbali ya kisera, kiutawala na uongozi yaliyofanyika nchini hivi karibuni ili kuleta tija katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali.

16. Mheshimiwa Spika, sambamba na maboresho yaliyofanyika Wizara inaendelea kuimarisha sekta ya sheria kwa kufanya marekebisho kwenye sheria ambazo zimeonekana kuwa na upungufu ili kuongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma. Hivyo, kuititia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara inatarajia kuwasilisha katika Mkutano huu wa Bunge marekebisho ya Sheria ya Mawakili, Sura 341; Sheria ya Usajili ya Vizazi na Vifo, Sura 108; Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20; Sheria ya

Urejeshwaji wa Wahalifu, Sura 368; Sheria ya Mashauri Dhidi ya Serikali, Sura ya 5; Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11; Sheria ya Mapato ya Uhalifu, Sura ya 256 na Sheria ya Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, Sura ya 66. Hali kadhalika Wizara imeandaa rasimu ya Kanuni za Wanasheria katika utumishi wa umma ambazo zitawawezesha kuwa na umoja wao na hivyo kusaidia kuimarisha utawala wa sheria nchini. Kwa sasa Kanuni hizo zinafanyiwa kazi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kukamilisha taratibu zilizosalia kabla ya kuanza kutumika.

17. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha Sekta ya Sheria kwa kurekebisha sheria na kuondoa vikwazo mbalimbali vinavyokwamisha usimamizi na utoaji haki nchini. Aidha, kwa kufahamu kwamba kazi ya kutunga na kurekebisha sheria ni ya Bunge, nichukue nafasi hili kukushukuru wewe na Bunge lako kwa kutunga mkono katika mabadiliko haya na hivyo kuipitisha miswada husika kuwa sheria.

III. Mkakati wa kusimamia masuala ya Utajiriasilia na Rasilimaliasilia

18. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa kunakuwa na ufanisi katika utekelezaji wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Umiliki na Usimamizi wa Utajiriasilia na Maliasilia za Nchi ya mwaka 2017 na Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Biashara na Uwekezaji katika utajiriasilia na maliasilia za nchi ya mwaka 2017, Wizara yangu tayari imeandaa rasimu ya Mkakati unganishi wa juhudhi mbalimbali za wadau wa sheria hiyo. Hivi sasa Wizara inaendelea kufanya maandalizi ya kuiwasilisha Rasimu hiyo kwenye majukwaa mbalimbali ya wadau kwa ajili ya maboresho na umiliki wake.

19. Mheshimiwa Spika, chimbuko la Sheria hizi ni Ibara ya 9(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inayoelekeza utajiri wa Taifa kuendelezwa, kuhifadhiwa na kutumiwa kwa manufaa ya wananchi wote na Ibara ya 27 inayoweka wajibu wa kulinda maliasilia za

nchi kwa ujumla. Kwa sababu hiyo, Sheria hizi, pamoja na Mkakati unaondaliwa, zinalenga kuhakikisha matumizi ya utajiri wa Taifa yanatilia mkazo maendeleo ya wananchi katika kupunguza umaskini, ujinga na maradhi; na kuhakikisha kuwa utajiriasilia na maliasilia za nchi, mali za mamlaka za nchi na mali yote inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi zinalindwa, mambo ambayo yametiliwa msisitizo katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo na Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2015.

IV. Utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria

20. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na maandalizi ya Awamu ya Pili ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria kwa kuendesha m kutano wa awali wa wadau wallopata fursa ya kuchangia usoefu wao katika historia ya maboresho hapa nchini na pia kupendekeza kuhusu mambo muhimu ya kuzingatiwa katika awamu ijayo ya sekta ya sheria. Ni kutohana na maoni hayo ambapo Wizara yangu imeweza kuandaa Rasimu ya awali ya Awamu ya Pili ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria ambayo itaendelea kuboreshwa kwa njia ya tafiti na ushirikishwaji wa wadau. Matumaini ya Wizara yangu ni kukamilisha zoezi hili kabla ya kuisha kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na kuingia katika hatua ya utekelezaji ikiwa ni pamoja na kufanya majadiliano na wadau wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi kuhusu upatikanaji wa rasilimali muhimu.

V. Maboresho ya Mfumo wa Utoaji Haki

21. Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya marekebisho ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Matangazo ya Serikali Na.48, 49 na 50 ya tarehe 13 Februari, 2018. Kupitia marekebisho hayo, Rais alianzisha Ofisi mbili mpya ambazo ni Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Marekebisho hayo yalikusudia kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa mashtaka ya jinai nchini ikiwa ni azma ya Serikali ya kutenganisha uendeshaji wa mashtaka

na shughuli za upelelezi na pia kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya madai pamoja na kuimarisha weledi na ubobezi wa kitaalamu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutoa ushauri kwa Serikali na uandishi wa miswada ya sheria ili kuendana na mabadiliko makubwa katika tasnia ya sheria kitaifa, kikanda na kimataifa.

22. Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako kuwa mwezi Julai, 2018 Mheshimiwa Rais aliridhia rasi kuanza kutumika kwa miundo mipy ya Ofisi hizi ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na tija zaidi. Kufuatia uamuzi huo, Wizara yangu imekamilisha zoezi la uchambuzi wa kazi na majukumu ya watumishi kitaasisi pamoja na kupangilia upya watumishi waliopo kulingana na mahitaji ya kila taasisi kwa njia ya uhamisho. Ni matumaini yangu kwamba kukamilika kwa zoezi hili kutaendelea kuimarisha uwezo wa Wizara katika kutekeleza majukumu yake ya kuwashudumia wananchi.

23. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 219(5) na (6) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20, Waziri mwenye dhamana ya masuala ya sheria anayo mamlaka ya kuwaachia huru watu waliotenda makosa mbalimbali ya jinai yakiwemo ya mauaji ambao kutoptana na kuwa na maradhi ya akili wakati wa kutenda makosa hayo Mahakama haikuwatia hatiani na badala yake iliamuru wahifadhiwe katika hospitali ya maradhi ya akili. Kutoptana na mamlaka hayo na kwa kuzingatia ushauri wa Bodi ya Ushauri iliyoundwa chini ya Sheria ya Afya ya Akili, Sura ya 98, Wizara iliendelea na jukumu lake katika utekelezaji wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kwa kuwaachia huru watuhumiwa 53 ambao Bodi ilithibitisha wamepona. Nilihakikishie Bunge lako kwamba Wizara yangu itaendelea kufanya kazi kwa karibu na mamlaka zote zinazohusika na jambo hili ili kuendelea kutekeleza matakwa haya ya kisheria kwa ufanisi na umakini wa hali ya juu.

VI. Usikilizwaji wa mashauri

24. Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa suala la kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani limekuwa

ni moja ya vipaumbele muhimu vya Serikali katika kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata haki sawa na kwa wakati. Katika kufanikisha azma hiyo, Mahakama ya Tanzania ilianza mwaka 2018 ikiwa na jumla ya mashauri 65,223, na kusajili mashauri mapya 259,476 katika ngazi zote za Mahakama. Mashauri 255,836 yalitolewa uamuvi ikiwa ni sawa na asilimia 99 ya mashauri yote yaliyofunguliwa katika kipindi hicho, sawa na ongezeko la asilimia 3 katika usikilizwaji na umalizikaji wa mashauri ikilinganishwa na mwaka 2017. Aidha, mashauri yaliyobaki mahakamani ni 68,863 kati ya hayo, mashauri yenye umri zaidi ya miaka miwili (mashauri ya mlundikano) ni 3,435 sawa na asilimia 5 tu ya mashauri yote yaliyobaki.

25. Mheshimiwa Spika, Kwa ngazi ya Mahakama ya Rufani, mwaka 2018 ulianza na mashauri 2,933 na kusajili mashauri mapya 1,499 ambapo mashauri 1,184 yalisikilizwa na kutolewa uamuvi, sawa na asilimia 79 ya mashauri yote yaliyosajiliwa katika kipindi hicho. Mashauri yaliyobaki mahakamani ni 3,248. Kati ya hayo, mashauri yenye umri zaidi ya miaka miwili 2 ni 729, ikilinganishwa na mashauri 335 mwaka 2017, sawa na asilimia 22 ya mashauri yote yaliyobaki. Bila shaka, ongezeko la idadi ya majaji wa Mahakama ya Rufani baada ya uteuzi wa hivi karibuni wa majaji 6 wa mahakama hiyo litasaidia kuharakisha usikilizaji wa mashauri ikilinganishwa na miaka iliyopita.

26. Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya Mahakama Kuu, Masjala Kuu, Kanda na Divisheni, mashauri yaliyokuwepo ni 19,207 na mashauri mapya yaliyosajiliwa ni 18,284. Mashauri yaliyoamuliwa katika kipindi hicho ni 17,046, sawa na asilimia 93 ya mashauri yaliyosajiliwa. Mashauri yenye umri wa miaka miwili na zaidi ni 1,860 sawa na asilimia 6 ya mashauri yaliyobaki, yakiwemo mashauri 100 yenye miaka 5 na zaidi. Ni matarajio ya Wizara yangu kwamba hali ya mlundikano wa mashauri itaanza kuimarika kwa kiasi kikubwa kutokana na uteuzi wa hivi karibuni wa majaji wapya 15 wa Mahakama Kuu.

27. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya, zilianza mwaka 2018 na mashauri

24,840 na kusajili mashauri mapya 51,161. Jumla ya masahuri 47,089 yalimalizika, sawa na asilimia 92 na kubakiwa na mashauri 28,912, yakiwemo mashauri 837 yene umri wa kati ya mwaka mmoja na miaka miwili. Idadi hiyo inajumuisha mashauri mengi ambayo Mahakama hizo hazina uwezo wa kuyasikiliza yakiwa yanabiri upetelezi ukamilike na kupelekwa Mahakama Kuu yene mamlaka ya kuyasikiliza.

28. Mheshimiwa Spika, mahakama za mwanzo nchini ndizo zinazoongoza kwa kufungua na kusikiliza idadi kubwa ya mashauri kuliko mahakama za ngazi nyngine ambapo katika mwaka 2018 mahakama hizi zilanza na mashauri 15,055 na kusajili mashauri mapya 177,566. Mashauri yaliyomalizika ni 176,542 sawa na asilimia 99, na kubakia mashauri 16,079 tu kwa nchi nzima. Kati ya mashauri 16,079 yaliyobaki, mashauri ya mlundikano yaliyokuwa na zaidi ya mlezi 6 Mahakamani kwa ukomo wa Mahakama hizi ni tisa ambayo yapo katika wilaya za Babati (1), Muleba (6) na Tarime (2).

29. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utawala bora, maadili na uwajibikaji wa watumishi, Mahakama ya Tanzania ilifanya ukaguzi wa huduma za kimahakama katika kanda zote 14 za Mahakama Kuu na kuhusisha vituo 839 vya mahakama za mwanzo, mahakama za wilaya na Mahakama Kuu kati ya 980 vilivypo nchini, sawa na asilimia 86. Vituo vya mahakama za mwanzo ni 717 kati ya 841 sawa na asilimia 85; mahakama za wilaya 97 kati ya mahakama 111, sawa na asilimia 89 na mahakama za hakimu mkazi vituo 25 kati ya 28 sawa na asilimia 89. Aidha, jumla ya malalamiko 1,046 ya wananchi yanayohusu kero za upatikanaji wa huduma mbalimbali za mahakama yalipokelewa ambapo malalamiko 951, sawa na asilimia 91 yalishughulikiwa.

VII. Miradi ya Ujenzi wa Majengo ya Mahakama

30. Mheshimiwa Spika, Mahakama imeendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Kuboresha Huduma za Mahakama ikiwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa Mahakama katika ngazi mbalimbali nchini. Miradi iliyoendelea kutekelezwa

katika mwaka wa fedha 2018/2019 ni ujenzi wa majengo ya Mahakama Kuu katika mikoa ya Kigoma na Mara ambayo imefikia asilimia 85 na kwamba huduma za kimahakama zimeanza kutolewa katika Mahakama hizo; ukarabati wa nyumba tatu za kufikia majaji mkoani Mtwara ambao umekamilika; ujenzi wa Mahakama za Wilaya za Kilwa, Ruangwa, Bukombe, Geita na Chato umekamilika; ujenzi wa jengo la Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Manyara uko kwenye hatua za mwisho kukamilika; Ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi, Simiyu, Njombe, Katavi na Lindi, na Mahakama za Wilaya za Longido, Kondoa, Sikonge, Kilindi, Kasulu, Ruangwa, Rungwe, Bunda, Makete, Wanging'ombe na Chunya upo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

31. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa majengo ya Mahakama za Mwanzo Ngerengere, Mang'ula na Mlimba (Morogoro) Mkunya (Newala), Laela, Msanzi na Mtowisa (Rukwa), Mtae (Lushoto) na Uyole (Mbeya) ujenzi upo kwenye hatua mbalimbali za kukamilika. Aidha, huduma ya Mahakama Zinazotembea ilizinduliwa mwezi Februari, 2019 ili kusogezza huduma za Mahakama karibu na wananchi hasa sehemu zisizo na Mahakama na zitaanza kutoa huduma katika mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza. Aidha, mahakimu na wadau wengine wa mahakama wamepatiwa mafunzo kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kuititia mahakama hizo. Kwa urahisi wa rejea, **Kiambatisho A** kinaonesha hali halisi ya ujenzi wa majengo ya Mahakama nchini.

VIII. Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kimahakama

32. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha ubora na ufanisi wa huduma za kimahakama nchini, Mahakama ya Tanzania inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika usikilizaji wa mashauri na shughuli za utawala. Kutokana na juhudhi hizo Mahakama imeanza rasmi kutumia mfumo wa kielektroniki wa uendeshaji wa mashauri ulioboreshwu katika Mahakama za ngazi ya Wilaya hadi Mahakama ya Rufani.

Pamoja na mambo mengine, mfumo huu unamwezesha mwananchi kufungua shauri moja kwa moja bila ya kulazimika kufika mahakamani kwa ajili hiyo. Haya ni mafanikio makubwa katika kuharakisha upatikanaji wa huduma bora za kimahakama na kwa gharama nafuu, kwa Serikali na kwa mwananchi binafsi.

IX. Uandishi, Urekebu na Ufasiri wa Sheria

33. **Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoeleza hapo awali, moja ya majukumu ya msingi ya Wizara yangu ni kuhakikisha kuwa wakati wote sheria za nchi zinakwenda na wakati na zinaakisi sera na vipaumbele vya Serikali kuhusu maendeleo katika nyanja za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, mazingira na teknolojia. Hivyo, katika mwaka 2018/2019 Wizara, kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, iliandaa miswada 11 iliyopitishwa na Bunge kuwa sheria kama ilivyooneeshwa kwenye **Kiambatisho B**. Aidha, sheria ndogo 271 ziliandaliwa au kuhakikiwa na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali. Sheria hizo zinajumuisha kanuni, taarifa, amri na matangazo au matamko ya Serikali. Kupitishwa kwa sheria hizi kunalenga kuimarisha taratibu za utekelezaji wa mipango na programu za maendeleo pamoja na masharti mbalimbali ya kisheria yaliyomo ikiwa ni pamoja na utoaji wa misamaha ya kodi, utangazaji wa maeneo ya kiuchumi, taratibu za utekelezaji wa masuala mbalimbali yaliyo chini ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Vilevile, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilifanya ufasiri wa sheria kuu saba na sheria ndogo 22 kwa lugha ya Kiswahili ili kuongeza uelewa wa sheria kwa wananchi. Hii ni pamoja na kufanya urekebu wa jumla ya sheria 55 ili kuweza kukidhi mahitaji ya sasa ya jamii, kama ilivyoofafanuliwa kwenye **Kiambatisho C** na **Kiambatisho D**.

X. Usimamizi wa Masuala ya Mikataba

34. **Mheshimiwa Spika**, kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara yangu imeendelea kushiriki na kutoa ushauri wa kisheria katika majadiliano mbalimbali ya mikataba ya kibishara, mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa ambapo katika kipindi hicho jumla ya mikataba

ya kitaifa na kimataifa 1,032 ilifanyiwa upekuzi. Hii ni mikataba iliyowasilishwa kutoka wizara, idara na taasisi mbalimbali za Serikali na mamlaka za serikali za mitaa ikihusisha masuala ya ununuzi, ujenzi na ukarabati wa majengo mbalimbali. Kati ya hiyo, mikataba 657 ilikuwa ni ya ununuzi na 316 ni ya makubaliano ya kimataifa na makubaliano katika masuala ya fedha. Kati ya hiyo, ilikuwepo mikataba 376 ya thamani ya fedha za kitanzania Shilingi 2,714,508,623,825.10, mikataba 65 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 3,189,538,959.42 na mikataba 20 iliyokuwa na thamani ya Euro 1,267,460,554.01.

XI. Utoaji wa Ushauri wa Kisheria

35. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ushauri wa kisheria unaotolewa kuititia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara imepanga kuwa na mfumo wa mawasiliano ya ndani na nje ya Ofisi, kwa njia za kieletroniki. Katika kuflikia azma hii, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanya upembuzi yakinifu wa mradi huu ili kubaini mahitaji halisi kwa ajili ya hatua nyingine za kiutendaji. Mfumo huu ni mahsusini kwa ajili ya taarifa zinazohusu mikataba, makubaliano ya kimataifa, utoaji wa ushauri, taarifa za mawakili wa serikali, mwenendo wa safari za watumishi, mawasiliano ya ndani ya ofisi, usimamizi wa maktaba ya taarifa za kisheria, kumbukumbu za matukio muhimu, uandishi wa sheria, tafsiri na urekebu.

XII. Kuendesha Mashtaka

36. Mheshimiwa Spika, utawala wa sheria ni nguzo muhimu katika kudumisha amani, utulivu na umaja wa kitaifa. Kwa kutambua hilo, Wizara yangu, kuititia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, iliendelea na uratibu wa shughuli za upelelezi wa makosa ya jinai, yakiwemo makosa dhidi ya watu kama vile ujambazi na mauaji, kufungua na kuendesha mashtaka ya jinai mahakamani ambapo Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha jumla ya mashauri ya jinai 5,709 katika Mahakama Kuu ya Tanzania. Kati ya mashauri hayo 1,322 ni ya vikao vya Mahakama Kuu na 4,387 yanahusu rufani za Mahakama Kuu. Kati ya hayo, mashauri 2,000 yalihitimishwa, sawa na asilimia

35 na mashauri mengine 3,709 yanaendelea katika hatua mbalimbali. Aidha, jumla ya rufaa 360 za jinai zilifunguliwa katika Mahakama ya Rufani ambapo kati ya rufaa hizo, 190 zilihitimishwa, sawa na asilimia 53 na nyingine 170 zinaendelea katika hatua mbalimbali. Vilevile, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendesha mashauri ya jinai katika mahakama za chini ikiwa ni pamoja na kuratibu shughuli za vyombo vyta upelelezi ambapo katika kipindi hicho, jumla ya mashauri ya jinai 24,807 yalishughulikiwa, na mashauri 8,913 kati ya hayo kuhitimishwa, sawa na asilimia 36.

37. Mheshimiwa Spika, mashauri ya jinai yaliyoshughulikiwa ni pamoja na ya wanyamapori, dawa za kulevyu, uhujumu uchumi, rushwa na mauaji. Mashauri ya wanyamapori yaliyoshughulikiwa ni 1,293 ambapo mashauri 204 kati ya hayo yalihitimishwa na mengine yanaendelea katika hatua mbalimbali. Kesi za dawa za kulevyu zilizoshughulikiwa ni 2,545 na kati ya hizo 756 zilihitimishwa; ambapo mashauri 591 ya uhujumu uchumi yalishughulikiwa na mashauri 113 kati ya hayo kuhitimishwa. Hali kadhalika, katika kipindi husika jumla ya majalada 234 ya makosa ya rushwa yalipokelewa kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ambapo kati ya hayo majalada 56 yaliandaliwa hati za mashtaka na kupatiwa vibali vyta kushtaki, majalada 94 yalirudishwa TAKUKURU kwa upelelezi zaidi, jalada moja (1) lilitfungwa na majalada 83 yanaendelea kufanyiwa kazi.

38. Mheshimiwa Spika, washtakiwa walioitiwa hatiani kutokana na makosa hayo walipewa adhabu mbalimbali zikiwemo vifungo na faini ambapo kiasi cha shilingi 4,782,877,720 zillipwa mahakmani kama faini na mali zinazokadiriwa kuwa na thamani ya shilingi 39,640,000,832 zilitaifishwa kwa amri ya Mahakama. Baadhi ya mali hizo ni pamoja na madini ya dhahabu na vito yenye thamani ya shilingi 32,752,210,132; Mashine ya kupima ubora wa dhahabu yenye thamani ya shilingi 305,000,000, ng'ombe 2,469, malori manne na magari madogo manne. Mali nyingine ni mbao vipande 1,506; magunia ya mkaa 100, injini ya boti moja, mitumbwi miwili, nyumba moja, meno ya tembo manne,

kemikali lita 260, pipipiki 11 na vilainishi vya injini lita 200. Mali hizi zitaondoshwa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.

39. Mheshimiwa Spika, kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Wizara iliendelea na utaratibu wake wa kawaida wa kufanya ukaguzi magerezani kama moja ya mkakati wa kupunguza mlundikano wa mahabusu na pia kusikiliza na kutatua kero za mahabusu ambapo masuala na malalamiko mbalimbali yaliyoibuliwa yalipatiwa ufumbuzi. Magereza yaliyotembelewa ni Bangwe, Kasulu, Bukoba, Biharamulo, Urambo, Uyui, Nzega, Singida Mjini, Manyoni, Butimba, Kasungamile, Chato, Isanga, Malya, Bariadi, Iringa, Njombe, Songea, Mbinga, Shinyanga, Lilungu, Masasi na Newala

40. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mfumo wa utoaji haki nchini Serikali iliamua kutenganisha shughuli za upetelezi na uendeshaji mashtaka. Ili kufanikisha azma hii ya Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendelea kuchukua hatua mbalimbali, kulingana na upatikanaji wa rasilimali muhimu, zenyelengo la kufikisha huduma ya mashtaka katika wilaya zote nchini ifikapo mwaka 2022. Hivi sasa Ofisi inaendesha mashauri ya jinai katika mahakama zote 26 za hakimu mkazi nchini na katika mahakama tano za wilaya za Nzega, Tarime, Chato, Temeke na Monduli. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inatoa huduma zake katika wilaya za Illemela, Kigamboni, Ilala na Kinondoni kupitia ofisi za mashtaka za mikoa husika. Wizara itaendelea kuweka mkazo katika utekelezaji wa Mpango huu, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa rasilimali muhimu za kutosha kufanikisha azma hiyo ya Serikali ili kuweza kuzifikia wilaya zote nchini katika kipindi hicho.

XIII. Uendeshaji wa Mashauri ya Madai na Usuluhishi

41. Mheshimiwa Spika, jukumu la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni kusimamia, kuratibu na kuimarisha uendeshaji wa mashauri ya madai, haki za binadamu, usuluhishi na mashauri ya kikatiba yanayoishusu Serikali. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya mashauri ya madai 2,611 yалишугхулика, kati ya hayo mashauri 218 yалихитишва, sawa na asilimia 8.3. Aidha, Ofisi hii ilishughulikia mashauri

matano ya uchaguzi ambayo kwa sasa yapo katika hatua mbalimbali za kusikilizwa mahakamani yakiwemo mashauri matatu ya nafasi ya ubunge kutoka majimbo ya Kinondoni, Tanga na Korogwe Vijijini; na mashauri mawili ya nafasi ya udiwani kutoka Jimbo la Ubungo.

42. Mheshimiwa Spika, mashauri ya kikatiba yalikuwa 52 yaliyofunguliwa Mahakama Kuu na mashauri mengine tisa yalikatiwa rufaa katika Mahakama ya Rufani yote yakiwa katika hatua mbalimbali za usikilizwaji. Aidha, mashauri 14 ya haki za binadamu yalisikilizwa kwenye Mahakama ya Haki za binadamu ya Afrika Mashariki na mashauri mengine 19 ya Haki za Binadamu yalisikilizwa katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Mashauri yote haya yapo katika hatua mbalimbali za usikilizwaji. Vilevile, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilishughulikia jumla ya mashauri 44 ya usuluhishi katika mabaraza ya usuluhishi ya kitaifa na kimataifa. Kati ya hayo mashauri 29 ni ya kitaifa na 15 ni ya kimataifa. Mashauri manne ya kitaifa na mawili ya kimataifa yalihitimishwa na mengine yanaendelea katika hatua mbalimbali.

43. Mheshimiwa Spika, kutohana na kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na kuchukua na kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi dhidi ya Serikali na Taasisi zake, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 mashauri ya madai na usuluhishi yaliendeshwa ambapo Ofisi iliokoa kiasi cha shilingi 9,018,957,011 ambazo zingelipwa kwa Mawakili Binafsi. Aidha, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeanza kuchukua hatua za kuimarisha utoaji wa huduma zake kwa kuanzisha mfumo wa ki-elektroniki wa utunzaji wa taarifa za mashauri na kutuma nyaraka.

XIV. Haki za Binadamu, Utawala Bora na Msaada wa Kisheria

Haki za Binadamu na Utawala Bora

44. Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano inatambua na kuheshimu wajibu iliyonayo wa kulinda, kukuza na kuendeleza haki za binadamu nchini kwa mujibu wa

Katiba na Sheria za nchi pamoja na mikataba ya kikanda na kimataifa ambayo nchi yetu imeridhia. Katika kutekeleza wajibu huu Wizara iliwakilisha nchi yetu kwenye mukutano wa viongozi wa juu wa Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa uliofanyika Geneva, Uswisi, kuanzia tarehe 25 Februari hadi 01 Machi, 2019 ambapo kiongozi wa ujumbe wa Tanzania, Waziri wa Katiba na Sheria, aliweza kutumia fursa hiyo kuelezea hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kulinda, kukuza na kuendeleza haki za binadamu hapa nchini. Ni dhahiri kuwa ushiriki wa Tanzania kwa ngazi ya Waziri katika mukutano huo ilikuwa ni ishara tosha kwamba Serikali inathamini na kutambua umuhimu wa haki za binadamu pamoja na nafasi ya Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa katika kushauri na kusimamia utekelezaji wa haki za binadamu kwenye nchi wanachama wa Umoja huo.

45. Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wizara yangu inaandaa Mpango Kazi wa Pili wa Kitifa wa Haki za Binadamu wa kipindi cha 2019 - 2023 kwa kushirikina na wadau mbalimbali baada ya kumalizika kwa Mpango Kazi wa awali. Umuhimu wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu ni kuiwezesha Serikali kuwa na mwongozo wa kisera unaoonyesha vipaumbele kwenye masuala ya haki za binadamu na kuharakisha utekelezaji wa mapendekezo ambayo Serikali ilikubali kuyatekeleza chini ya Mfumo wa Umoja wa Mataifa katika Kipindi Maalumu (Universal Periodic Review).

46. Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizotekelawa ni pamoja na maandalizi ya taarifa ya nchi ya utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemevu wa mwaka 2006. Aidha, katika kuhakikisha kuwa watu walio kwenye makundi yenye mahitaji maalum wanawezeshwa kuifikia haki (wakiwemo wanawake, watoto, wazee na watu wenye ulemavu), Jaji Mkuu ameandaa kanuni za uendeshaji wa mashauri ya watu wenye mahitaji maalum (The Judicature and Application of Laws (Practice and Procedure of Cases Involving Vulnerable Groups) Rule No. 110 of 1st February, 2019) zinazotoa muongozo unaozitaka mamlaka husika kukamilisha usikilizwaji wa mashauri yanayohusisha makundi haya ndani

ya muda usiozidi miezi sita. Mwongozo huu umeanza kutekelezwa na mahakama za ngazi zote nchini.

47. Mheshimiwa Spika, katika kusimamia hifadhi ya haki za binadamu na utawala bora nchini, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliendelea kupokea na kushughulikia malalamiko ya wananchi kuhusu uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Jumla ya malalamiko yaliyokuwepo ni 6,928 ambapo kati ya hayo, malalamiko 564 yalichunguzwa na yapo katika hatua ya kuhitimishwa ambapo malalamiko 211 yaliyokuwa nje ya mamlaka ya Tume yalielekezwa katika taasisi zenye mamlaka ya kuyashughulikia. Vilevile, Tume ilifanya ukaguzi wa magereza tisa na vituo vya polisi sita katika Mikoa ya Tabora, Singida, Kilimanjaro, Arusha Shinyanga, Simiyu, Kagera, Geita, Njombe, Ruvuma, Morogoro na Dodoma na pia katika vyuo vya mafunzo tisa, shule moja ya maadilisho ya watoto na vituo vya polisi 32 huko Zanzibar. Taarifa ya ukaguzi na mapendekezo ya Tume yamewasilishwa kwenye mamlaka husika kwa mujibu wa sheria, kwa hatua za utekelezaji.

48. Mheshimiwa Spika, Tume iliendelea kuelimisha umma kuhusu haki za binadamu kuititia vyombo vya habari, mikutano, machapisho na warsha. Pia, jumla ya wananchi 468 kutoka mikoa ya mikoa ya Mara, Mtwara, Mbeya, Manyara, Shinyanga, Dodoma, Tabora, Kagera, Kigoma, Tanga, Lindi, Kilimanjaro na Iringa walijengewa uwezo wa kuwa wakufunzi wa masuala ya utawala bora, haki za binadamu na upatikanaji wa haki za kisheria katika. Aidha, mafunzo kama hayo yalitolewa kwa maafisa watendaji kata 843 kutoka mikoa ya Mara, Shinyanga Mtwara, Mbeya na Manyara kwa lengo la kusaidia kuimarisha masuala ya utawala bora kwenye maeneo yao ya utawala.

Msaada wa kisheria

49. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa huduma ya msaada wa kisheria nchini kwa kuandaa Kanuni za Sheria ya Msaada wa Kisheria. Pia Wizara inakamilisha utungaji wa kanuni za maadili

kwa watoa msaada wa kisheria ambazo zitaanza kutumika hivi karibuni. Vilevile, Wizara iliendelea na usajili, usimamizi na uratibu wa watoa huduma ya msaada wa kisheria kwa kuwapa mafunzo kuhusu utekelezaji wa majukumu yao wakiwemo maafisa 89 wa Jeshi la Polisi na 76 wa Jeshi la Magereza waliopatiwa mafunzo ya kuwawezesha kuendesha utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria katika maeneo yao. Hali kadhalika, Wizara imeandaa mfumo wa kielektroniki ili kurahisisha shughuli za uratibu wa utoaji wa msaada wa kisheria nchini. Aidha, Wizara iliendelea kuratibu maadhimisho ya Wiki ya Msaada wa Kisheria nchini, kwa mara ya pili mfululizo, ambayo yalifanyika nchini kote kuanzia tarehe 26 Novemba hadi 01 Desemba, 2018. Huduma zilizotolewa kuititia maadhimisho hayo ni pamoja na ushauri wa kisheria, elimu kwa umma kwa njia ya vijarida, vipeperush, na machapisho. Wananchi walionufaika na maadhimisho hayo ni pamoja na wafungwa na mahabusi ambao walipatiwa huduma ya msaada wa kisheria.

XV. Mapitio ya Mifumo ya Sheria Mbalimbali

50. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kuhakikisha kwamba Sheria za nchi zinakwenda na wakati ikiwa ni pamoja na kuakisi mahitaji ya sasa ya jamii kuhusu maendeleo. Hivyo, kuititia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Wizara yangu ilifanya mapitio ya sheria na tafiti katika mfumo wa Sheria za utatuzi wa migogoro ya ardhi Tanzania, Mfumo wa Sheria za ujenzi wa majengo, Sheria za uchaguzi wa serikali za mitaa na Mfumo wa sheria za masoko ya mazao ya kilimo na kukamilisha maandalizi ya andiko la majadiliano kwa tafiti zote. Aidha, Tume, ilifanya mapitio ya Mfumo wa Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa kuendesha mikutano ya wadau katika mikoa ya Arusha, Simiyu, Mara na Dodoma ambapo kazi ya uchambuzi na uhakiki wa maoni na mapendekezo ya wadau imekamilika. Vilevile, Tume kwa kushirikiana na Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini imefanya mapitio ya Mfumo wa sheria za ufilisi ili kuweka misingi ya kutungwa kwa sheria mahsus ya kusimamia masuala ya ufilisi nchini. Hii ni pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu mfumo wa marekebiso ya sheria,

Sheria ya Dhamana na Mwenendo wa Madai Mahakamani, kupitia vipindi 52 vya redio.

XVI. Urejeshwaji wa Wahalifu na Ushirikiano wa Kimataifa katika Makosa ya Jinai

51. **Mheshimiwa Spika**, katika kukabili ana na vitendo vya kihalifu, hususan uhalifu wa kuvuka mipaka ya nchi, Wizara yangu iliendelea kushughulikia masuala ya urejeshwaji wa wahalifu na kushirikiana na mataifa mengine. Katika kipindi hicho, Wizara ilipokea na kushughulikia maombi saba ya kurejesha watuhumiwa wa makosa mbalimbali ya jinai waliokimbia nchini baada ya kutenda makosa kwenye nchi husika. Kati ya Maombi hayo maombi matatu yalikamilishwa na watuhumiwa kurejeshwa na maombi mengine manne yanaendelea kufanyiwa kazi katika ngazi mbalimbali. Aidha, Wizara imeendelea kushirikiana na mataifa mengine katika kubadilishana mashahidi na vielelezo ambapo ilipokea jumla ya maombi tisa ya kukusanya ushahidi na vielelezo kutoka mataifa mbalimbali. Maombi manne yalikamilika na mengine matano yanaendelea kushughulikiwa. Aidha, Tanzania ilipeleka nje ya nchi maombi mawili ya kukusanya ushahidi na vielelezo ambayo yanaendelea kushughulikiwa katika nchi hizo.

XVII. Mkakati wa Kitaifa wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu

52. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu iliendelea kuimarisha shughuli za usajili wa vizazi, vifo, ndoa, talaka na watoto wa kuasili ikiwa ni haki ya msingi ya utambuzi na upatikanaji wa takwimu kwa ajili ya maendeleo. Katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini uliweza kusajili vizazi 1,271,372; vifo 28,285; ndoa 26,953; talaka 122 na hati 28 za watoto wa kuasili. Aidha, kupitia utekelezaji wa Mkakati huo, Serikali imefanikiwa kuongeza kiwango cha usajili kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kutoka asilimia 13, kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 38 kwa mwaka 2019. Vilevile, Wizara iliendelea na usimamizi wa mirathi, usajili wa bodi za wadhamini, uandishi

na uhifadhi wa wosia ambapo wosia 38 zimeandikwa na kuhifidhiwa katika kipindi cha 2018/2019.

XVIII. Taasisi za Mafunzo

Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto

53. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha watumishi wa sekta ya sheria wanakuwa na ujuzi na weledi wa kutosha, Wizara yangu kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto imeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za Astashahada na Stashahada ya Sheria, mafunzo endelevu ya kimahakama kwa watumishi wa Mahakama na pia mafunzo ya muda mfupi kwa wadau wa sekta ya sheria nchini. Hii ni pamoja na kuongeza uwezo wa Chuo katika kubuni na kuendesha programu mbalimbali za mafunzo ili kukidhi mahitaji ya sekta ya sheria na Taifa kwa ujumla. Aidha, kipindi mwaka wa fedha 2018/2019 Chuo kimeweza kuongeza udahili wa wanachuo 720 hadi kufikia wanachuo 846 ambalo ni ongezeko la asilimia 18 ya lengo liliowerkwa.

54. **Mheshimiwa Spika**, Chuo hiki kimeendelea kuwa nguzo muhimu kwa Mhimili wa Mahakama kwa kutoa mafunzo elekezi na endelevu ya kimahakama kwa watumishi wa Mahakama wa kada mbalimbali. Mafunzo hayo yamewanufaisha jumla ya watumishi 368 hadi sasa. Miongoni mwa watumishi hao ni majaji wa Mahakama ya Rufani, majaji wa Mahakama Kuu, mahakimu wa ngazi mbalimbali na watumishi wa kada nyingine za Mahakama. Aidha, Wizara kupitia chuo hiki imeendelea kutoa mafunzo kwa wadau wanaohusika moja kwa moja na mashauri ya mototo akiwa mahakamani ambao ni Mahakimu, Mawakili wa Serikali, Waendesha Mashtaka na Maafisa Ustawi wa jamii. Mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo washiriki juu ya namna bora ya kulinda, kutetea na kutoa haki ya kundi la wenye mahitaji maalum hususan watoto.

Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania

55. **Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania imeendelea kutekeleza jukumu lake

la msingi la kutoa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 Taasisi ilifanikiwa kutoa mafunzo kwa wanafunzi 1,791. Idadi hii inajumuhiha wanafunzi 630 wa kundi la 28 ambao ni sawa na ongezeko la asilimia tano ya malengo ya udahili wa wanafunzi 600 kwa kundi moja; wanafunzi 526 wa kundi la 27 sawa na asilimia 88 ya malengo ya udahili na wanafuni 635 wa kundi la 26 sawa na ongezeko la asilimia sita ya malengo ya udahili. Aidha, katika kipindi hicho Taasisi iliendesha mitihani ya mwisho kwa jumla ya wanafunzi 1,135 wa kundi la 25 na 26 ambapo kati yao wanafunzi 260 walifaulu, sawa na asilimia 23 na wanafunzi 299 walifeli, sawa na asilimia 26. Pia, kulikuwa na mitihani ya marudio iliyo husisha wanafunzi 3,279 ambapo jumla ya wanafunzi 980 walifaulu, sawa na asilimia 30, na kwamba wanafunzi wengine walibaki wataendelea kufanya mitihani hiyo ya marudio mpaka hapo watakapofaulu.

XIX. Maadili ya Watumishi na maendeleo ya rasilimaliwateru

56. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Sheria ni moja ya sekta ambazo hutegemea zaidi nguvu kazi inayotokana na rasilimali watu wake katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake. Kwa kutambua hilo Wizara yangu imeendelea kuwekeza katika rasilimaliwateru kwa kuajiri, kutoa mafunzo na kuimarisha shughuli za usimamizi ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma. Kwa kuzingatia hilo, Wizara iliajiri jumla ya watumishi wapya 179 na kuwapatia mafunzo ya kuongeza ujuzi watumishi 599 ikiwa ni pamoja na kuthhibitisha kazini watumishi tisa na kupandisha vyeo watumishi 20. Aidha, katika kudhibiti nidhamu kazini, mtumishi mmoja alisimamishwa kazi, 33 waliachishwa kazi na wawili walistaafishwa kwa maslahi ya umma kama ilivyofanuliwa kwenye **Kiambatisho E. Vilevile**, Tume ya Utumishi wa Mahakama ilijaza nafasi mpya za ajira ya watumishi 44 wa mahakama, ilipandisha vyeo jumla ya watumishi 958, ilithhibitisha kazini jumla ya watumishi 292 pamoja na kuajiri katika masharti ya kudumu na malipo ya pensheni jumla ya watumishi 298. Aidha, majaji 15 wa Mahakama Kuu na majaji sita wa Makahakama ya Rufani waliteuliwa. Hali kadhalika,

Tume ya Utumishi wa Mahakama ilifanya vikao vitano vyakira na kufanya maamuzi juu ya masuala 34 ya nidhamu kwa watumishi wa kada mbalimbali ambapo watumishi 20 walifukuzwa kazi, watumishi wawili walirejeshwa kazini, wawili walipewa onyo na 10 wanaendelea kuchunguzwa.

XX. Mipango na Miradi ya Maendeleo

57. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ubora na upatikanaji wa huduma za kisheria nchini, Wizara yangu imeendelea kubuni na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo Mradi wa *Strengthening Access to Justice, Building Sustainable Anti-Corruption Action in Tanzania, e-Justice na Ujenzi wa Majengo ya Ofisi*. Kupitia miradi hiyo Wizara imefanikiwa kutengeneza mfumo jumuishi wa kukusanya, kuchambua na kuhifadhi takwimu na taarifa muhimu zinazohusu haki na upatikanaji wake; kukamilisha kazi ya upembizi yakinifu wa mradi wa e-justice, kufunga mifumo ya ki-elektroniki ya ulinzi na usalama na mahudhurio ya watumishi na kununua vifaa mbalimbali vya TEHAMA. Pia, Wizara imekamilisha ujenzi wa majengo mpya ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Makao Makuu ya Wizara katika eneo la Mji wa Serikali, jijini Dodoma.

E. MIKAKATI YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI YA MWAKA 2015

58. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kuwajibika kikamilifu kwa wananchi kupitia utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ahadi na maelekezo mbalimbali yaliyotolewa na viongozi wa kitaifa. Miongoni mwa ahadi hizo ni pamoja na kuendeleza vita dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma; kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na kuendeleza utawala wa sheria; na kuimarisha mfumo wa utoaji haki. Katika kufikia azma hiyo, Wizara imeendelea kubuni mikakati na kutumia mbinu mbalimbali kulingana na mazingira ya eneo husika, ikiwa ni pamoja na kuendeleza vita dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma, kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na utawala bora na kuimarisha mfumo wa utoaji haki.

I. Kuendeleza vita dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma

59. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia kuanzishwa kwa Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ya Mahakama Kuu, Wizara imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali yenye lengo la kuimarisha vita dhidi ya rushwa nchini na pia kuiwezesha Divisheni hiyo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Katika mikakati hiyo Serikali imefanya marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 ambayo imefanyiwa marekebisho kumwezesha shahidi kutoa ushahidi wake kwa njia za kielektroniki bila kulazimika kuwepo mahakamani. Marekebisho haya yanalenga kuimarisha mfumo wa ulinzi na usalama wa mashahidi pamoja na kuleta ufanisi wa usikilizaji wa mashauri makubwa, kama vile mashauri ya ugaidi. Pia, Wizara imefanya marekebisho Sheria ya Kusaldiana katika Masuala ya Jinai yenye lengo la kuimarisha upelelezi wa makosa kwa kubadilishana nyaraka kati ya vyombo vya ndani na vile vya nje ya nchi. Vilevile, Serikali inakusudia kuwasilisha bungeni mswada wa sheria ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala. Kutungwa kwa Sheria hii ni sehemu ya utekelezaji wa Sheria ya usimamizi wa utajiriasilia na rasilimaliasilia za nchi, hususan kifungu cha 11, na pia kuwezesha utatuzi wa migogoro ya biashara na uwekezaji kufanyika kwa sheria na vyombo vya hapa nchini ili kuhakikisha uwazi na kuepukana na gharama kubwa zisizo za lazima.

II. Kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na utawala bora

60. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Katiba na mikataba ya kikanda na kimataifa, iliyordihiwa na nchi yetu, Serikali inalo jukumu la kukuza, kulinda na kuendeleza haki za binadamu na pia kuimarisha misingi ya utawala bora. Katika kufanikisha majukumu haya Serikali imeendelea kubuni na kutekeleza mikakati kadhaa kwa kutunga na kurekebisha sheria pamoja na kanuni zake; kuendesha tafiti za kisheria; kutoa elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na za kiraia; kupokea na kufanya uchunguzi malalamiko ya wananchi

yanayohusu ukiukwaji wa Haki za Binadamu na misingi ya Utawala Bora. Sanjari na mikakati hiyo, Wizara ya Katiba na Sheria iliandaan na kuratibu maadhimisho ya Wiki ya Msaada wa Kisheria yaliyofanyika nchini kote kuanzia tarehe 26 hadi 30 Novemba, 2018. Maadhimisho hayo yaliwezesha kufikisha huduma ya msaada wa kisheria kwa wananchi wengi, kwa mara moja, ikiwemo huduma ya ushauri na elimu kwa umma. Aidha, Serikali iliendelea kuimarisha usajili wa vizazi, vifo, ndoa, talaka na watoto wa kuasili kwa lengo la kuwapatia wananchi haki za msingi za kiraia. Mikakati imekuwa ikitumika katika masuala ya usajili ikiwa ni pamoja na njia za kielektroniki, kampeni za usajili, usajili kwa misingi ya rika unaohusisha watoto wa umri wa chini ya miaka mitano na watoto waliopo shulenii pamoja na usajili wa kawaida.

61. Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha rasimu ya Mpango Kazi wa Pili wa Kitaifa wa Haki za Binadamu kwa kipindi cha mwaka 2019 hadi 2022 na kushirikisha wadau mbalimbali kutoka eneo lote la Jamhuri ya Muungano. Aidha, Wizara illiwakilisha nchi yetu katika Mkutano wa viongozi wa juu wa Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa uliofanyika Geneva, Uswis kuanzia tarehe 25 Februari hadi 1 Machi, 2019. Katika mkutano huu, Tanzania ilitoa taarifa kuhusu hatua zinazoendelea kuchukuliwa Serikali katika kuimarisha upatikanaji wa haki za binadamu ikiwemo kutungwa kwa Sheria ya Msaada wa Kisheria ya mwaka 2017 na kuitishwa kwa Mkakati wa Kitaifa kuhusu ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa kipindi cha mwaka 2017 hadi 2021 ukiwa na lengo la kuhakikisha kuwa haki za wanawake, watoto na watu wenye ulemavu zinalindwa na kuendelezwa. Aidha, Wizara imeandaa taarifa ya nchi juu ya utekelezwaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemevu wa mwaka 2006. Rasimu ya mwisho ya taarifa hii imekamilika na sasa inapitiwa na wadau kwa ajili ya uhakiki kabla ya kuwasilishwa kwenye vyombo vya juu vya Serikali na Kamati ya Umoja wa Mataifa yenyeye dhamana ya kusimamia utekelezwaji wa Mkataba wa Haki za Watu wenye Ulemevu. Vilevile, Mahakama ya Tanzania imetoea mwongozo unaoelekeza mashauri yote yanayohusu watu walio katika

makundi maalum kumalizika katika muda wa kipindi cha miezi sita.

III. Kuimarisha mfumo wa utoaji haki

62. Mheshimiwa Spika, Wizara imechukua hatua madhubuti za kuimarisha mifumo ya utoaji haki nchini kwa kufunga mifumo ya kielektroniki ya utoaji wa huduma za kimahakama, ikiwa ni pamoja na Mfumo wa kusajili na kuratibu mashauri ambao tayari umeanza kufanya kazi. Pamoja na mambo mengine, Mfumo huu umerahisha masuala ya usimamizi wa mashauri mahakamani ikiwa ni pamoja na ufunguaji wa mashauri, kuendesha benki ya kuhifadhi hukumu, kusajili na kuratibu shughuli za mawakili na kufanya utambuzi wa mahitaji ya mahakama. Kwa kutumia Mfumo wa Kusajili na Kuratibu Mashauri, hivi sasa haitakuwa lazima kwa mwananchi kufanya safari kwenda kufunga shauri kwenye mahakama kuu za Dar es Salaam, Mbeya, Dodoma na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisitu. Kazi iliyopo mbeleni hivi sasa kueneza mfumo huu katika mahakama zote nchini. Aidha, mfumo wa kutambua mahitaji ya mahakama unawezesha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za kimahakama kutoka sehemu yoyote nchini kama vile watumishi, hali ya majengo na umbali kutoka makao makuu ya mkoa kupatikana moja kwa moja kuitia mfumo wa kompyuta.

63. Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zilizochukuliwa na Wizara ni kuanzishwa kwa huduma ya mahakama maalum zinazotembea iliyowezesha kusogea huduma za mahakama karibu na wananchi hususan walio katika sehemu zisizo na huduma ya mahakama. Katika awamu ya kwanza ya majaribio yamenunuliwa magari mawili yatakayotumika kutoa huduma katika mikoa ya Dar es Salaam, Wilaya ya Kindondoni (Bunju), Wilaya ya Ilala (Chanika), Wilaya ya Temeke (Buza) na Wilaya ya Ubungo (Kibamba); na Mkoa wa Mwanza, Wilaya ya Illemela (Nyegezi).

64. Mheshimiwa Spika, kwa asili yake majukumu yaliyo chini ya Sekta ya sheria ni mtambuka na yenye kuhusisha

wadau mbalimbali wa mamlaka zote za Dola, yaani Bunge, Mahakama na Utawala. Kutokana na ukubwa wa sekta hii na umuhimu wake kwa maendeleo ya nchi hivi sasa Wizara inaendelea na maandalizi ya mfumo wa kielektroniki wa e-Justice ambao, utakapokamiliika utaongeza ufanisi katika masuala ya usimamizi na uratibu wa Mfumo wa sheria nchini. Pamoja na mambo mengine, Mradi huu unalenga kuunganisha mifumo ya kielektroniki inayotumiwa na taasisi mbalimbali za sekta ya sheria. Pia, Serikali inaendelea na mchakato wa kutunga Sera ya Taifa ya Sheria ya kusimamia masuala ya sheria nchini ili kuimarisha hali ya tija na ufanisi wa sekta hiyo.

F. MTIRIRIKO WA MAPATO NA MADUHULI YA SERIKALI

i. *Mapato ya Bajeti*

65. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara ya Katiba na Sheria ilidhinishiwa na Bunge jumla ya Shilingi. 190,493,982,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya hizo Shilingi 77,173,293,000 ni za mishahara, Shilingi 68,553,470,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi 44,767,219,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za Maendeleo jumla ya Shilingi 18,000,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 26,767,219,000 fedha za nje.

66. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2019 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi 111,635,273,359 sawa na asilimia 59 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya hizo Shilingi 44,716,151,336 ni mishahara na Shilingi 45,165,449,175 ni matumizi mengineyo. Fedha za maendeleo ni Shilingi 21,753,672,848 sawa na asilimia 49 ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa. Kati ya hizo Shilingi 7,000,000,000 ni fedha za maendeleo za ndani na Shilingi 14,753,672,848 ni fedha za maendeleo za nje

ii. *Makusanyo ya Maduhuli*

67. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi **27,097,646,862** kama maduhuli ya Serikali kutoka vyanzo mbalimbali vya

mapato. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 Wizara ilikusanya jumla ya Shilingi 8,712,700,000, sawa asilimia 32 ya lengo la makukusanyo

G. MAFANIKIO YALIYOPATIKANA

68. Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/19 ni pamoa na:-

- (i) Wananchi wengi kuwa na uhakika kuhusu upatikanaji wa huduma muhimu za kimahakama kutokana na miradi ya maboresho ya Mahakama inayotekelze wa nchini;
- (ii) Upatikanaji wa ofisi za kudumu za Wizara na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hii ni kutokana na kukamilika kwa majengo ya Ofisi za Wizara na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali jijini Dodoma;
- (iii) Kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa huduma za kisheria kwa njia ya TEHAMA;
- (iv) Wananchi wengi, kutoka makundi mbalimbali ya kijamii, kufikiwa na mtandao wa huduma ya msaada wa kisheria;
- (v) Kuimarika kwa viwango vya usajili wa vizazi kitaifa hususan kwa watoto wa umri chini ya miaka mitano;
- (vi) Kuimarika kwa uwezo wa kudahili wanafunzi katika taasisi za mafunzo ya sheria na ubunifu katika kuandaa wa program mpya za mafunzo;
- (vii) Kiasi kikubwa cha fedha na mali nyingi kilichookolewa na kurejeshwa Serikalini kutokana na uendeshaji wa mashauri ya jinai na daawa;
- (viii) Kuimarika kwa shughuli za utafiti na mapitio ya sheria;
- (ix) Kuimarika kwa usimamizi wa watumishi kimaadili na katika kuwaendeleza kitaaluma.

H. **CHANGAMOTO NA MIKAKATI ILIYOPO**
Changamoto Zilizopo

69. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/19, kumekuwepo na changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na;

(i.) Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu masuala ya sheria na kupelekea wananchi wengi kusisitiza zaidi juu ya kupatiwa haki bila kutimiza wajibu;

(ii.) Mwamko mdogo wa wananchi katika kuzitumia Kamati za maadili ya Mahakimu na hivyo kutopeleka taarifa au malalamiko yao dhidi ya ukiukaji wa maadili wa mahakimu kwenye kamati hizo;

(iii.) Uchache wa rasilimali watu wakiwemo maafisa sheria na mawakili wa serikali, wakufunzi katika taasisi za mafunzo, maafisa usajili na wasimamizi wa watoa huduma ya msaada wa kisheria katika ngazi za wilaya na kwenye jamii

(iv.) Mfumo wa sheria za usajili zilizopo kutokukidhi mahitaji ya sasa ya kuendesha shughuli za usajili hadi ngazi ya chini kwenye jamii

Mikakati ya kutatua Changamoto

70. **Mheshimiwa Spika**, hatua kadhaa zimeendelea kuchukuliwa na mamlaka za Wizara katika kukabiliana na changamoto hizo. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha ushirikiano wa kitaasisi katika matumizi ya rasilimali watu, fedha na vifaa;

(ii) Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Sheria imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu sheria mbalimbali, haki na wajibu wa wananchi;

(iii) Kuendelea kuwashirikisha wadau katika kufanikisha utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Usajili wa Matukio Muhimu

ya Binadamu na Takwimu ili kukabiliana na changamoto zilizopo hususan za kimfumo na rasilimali fedha;

(iv) Kuendelea kuboresha mazingira ya kazi na kutoa motisha kwa watumishi wachache waliopo ili kuongeza tija na ufanisi wa kazi.

71. Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana ni juhudzi za pamoja kati ya Wizara wadau wetu wa maendeleo katika sekta ya sheria. Hivyo, nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa ushirikiano mzuri uliopo kati yetu na Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa ya Kuhudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake (UN Women), Jumuia ya Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza (DfID), Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA), Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP) na Shirika la Misaada ya Kimataifa la Watu wa Marekani (USAID). Wengine ni Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kushughulikia Dawa za Kulevyia na Uhalifu (UNODC), PAMS Foundation, Mfuko wa Kimataifa wa kuhudumia Wanyapori (WWF), Shirika la Maendeleo la Ujeruman (GIZ), Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), Shirika la Udhibiti wa Usafirishaji Haramu wa Wanyamapori na Misitu (TRAFFIC), Bloomberg DHI na Shirika la Maendeleo la Italia (AICS). Napenda niwahakikishie kuwa Wizara yangu inatambua na kuthamini uhusiano mzuri uliopo kati yetu na wadau hawa na tutahakikisha kuwa unaimarishwa kwa maendeleo ya sekta ya sheria na taifa kwa ujumla.

72. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwashukuru viongozi na watendaji wa Wizara na taasisi zake kwa ushirikino mkubwa wanaonipatia katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya uwaziri. Hakika, ni kutohana na ushirikiano huo nimeweza kusimama leo hii mbele ya Bunge lako tukufu kuelezea mafanikio, mipango na mikakati tuliyonayo katika kuwahudumia wananchi wetu. Hivyo, kipekee nimshukuru

Prof. Sifuni Ernest Mchome, Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria; Bw. Amon Anastos Mpanju, Naibu Katibu Mkuu, Mhe. Prof. Ibrahimu Hamisi Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Adelardus Lubango Kilangi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Jaji Kiongozi, Bw. Hussein Kattanga, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Mhe. Katarina Revokati, Msajili Mkuu wa Mahakama Tanzania, Bw. Biswalo Eutropius Kachele Mganga, Mkurugenzi wa Mashtaka, Dkt Julius Clement Mashamba, Wakili Mkuu wa Serikali, Bibi Emmy Kalomba Hudson, Kaimu Kabidhi Wasii Mkuu na Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili Ufili na Udhamini, Bw. Casmir Sumba Kyuki, Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Bibi Fatuma Muya, Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Dkt. Zakayo Ndobir Lukumay, Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, Mhe. Jaji Dkt. Paul Faustine Kihwelo Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama-Lushoto, wakurugenzi na watumishi wote wa Wizara.

I. MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2019/ 2020

73. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara yangu itaendelea kuboresha utoaji wa huduma za kisheria kwa umma ili kuendana na Dhima ya kuwa na mfumo madhubuti wa kikatiba na kisheria wenye kufanikisha utekelezaji wa sera na mipango kwa maendeleo ya Taifa. Ili kufikia azma hiyo Wizara yangu imeainisha maeneo mahususi ya vipaumbele na kuyawekea mikakati ya utekelezaji wake kama ilivyofafanuliwa katika **Kiambatisho F** cha Hotuba hii.

74. Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele hivi, Wizara yangu inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 55,175,163,302** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo, kama ilivyooneshwa kwenye jedwali lifuatalo:-

Mchanganuo wa Makadirio ya Bajeti kwa Wizara ya Katiba na Sheria

Na.	Fungu la Matumizi	Bajeti 2019/20
1.	Mishahara ya watumishi	25,231,984,000
2.	Matumizi mengineyo	22,051,581,000
3.	Miradi ya Maendeleo	7,891,598,302
	JUMLA	55,175,163,302

75. **Mheshimiwa Spika**, kiasi hicho cha fedha kinaombwa kupitia mafungu saba ya bajeti yaliyo chini ya Wizara kama kama ifuatavyo: -

(i) Fungu 12: Tume ya Utumishi wa Mahakama

Matumizi ya Mishahara	-	Sh.	304,962,000
Matumizi Mengineyo	-	Sh.	1,000,000,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	-	Sh.	0
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	-	Sh.	0
Jumla	-	Sh.	1,304,962,000

(ii) Fungu 16: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Matumizi ya Mishahara	-	Sh.	3,013,570,000
Matumizi Mengineyo	-	Sh.	3,618,731,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	-	Sh.	0
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	-	Sh.	0
Jumla	-	Sh.	6,632,301,000

(iii) Fungu 19: Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

Matumizi ya Mishahara	-	Sh.	1,641,327,000
Matumizi Mengineyo	-	Sh.	5,398,637,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	-	Sh.	0
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	-	Sh.	248,363,000
Jumla	-	Sh.	7,288,327,000

(iv) Fungu 35: Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

Matumizi ya Mishahara	-	Sh.	10,980,893,000
Matumizi Mengineyo	-	Sh.	6,723,265,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	-	Sh.	0
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	-	Sh.	0
Jumla	-	Sh.	17,704,158,000

(v) Fungu 41: Wizara ya Katiba na Sheria

Matumizi ya Mishahara	-	Sh.	5,567,737,000
Matumizi Mengineyo	-	Sh.	2,765,859,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	-	Sh.	1,000,000,000
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	-	Sh.	4,075,853,500

(vi) Fungu 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Matumizi ya Mishahara	-	Sh.	2,716,729,000
Matumizi Mengineyo	-	Sh.	1,566,080,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	-	Sh.	0
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	-	Sh.	2,567,381,802
Jumla	-	Sh.	6,850,190,802

(vii) Fungu 59: Tume ya Kurekebisha Sheria

Matumizi ya Mishahara	-	Sh.	1,006,766,000
Matumizi Mengineyo	-	Sh.	979,009,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	-	Sh.	0
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	-	Sh.	0
Jumla	-	Sh.	1,985,775,000

76. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, naliomba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 126,162,464,756 kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama. Kati ya fedha hizo, Shilingi 104,004,564,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 22,157,900,576 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Mchanganuo wa matumizi ya bajeti kwa Mfuko wa Mahakama ni kama ifuatavyo: -

Fungu 40: Mfuko wa Mahakama

Matumizi ya Mishahara	-	Sh.	52,523,182,000
Matumizi Mengineyo	-	Sh.	51,481,382,000
Matumizi ya Maendeleo (Ndani)	-	Sh.	15,000,000,000
Matumizi ya Maendeleo (Nje)	-	Sh.	7,157,900,576
Jumla	-	Sh.	126,162,464,576

Makusanyo ya Maduhuli ya Serikali

77. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara yangu inatarajia kusimamia na kukusanya jumla ya **Shilingi 12,606,487,000** ikiwa ni maduhuli ya Serikali, kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:-

Fungu 12	-	Sh.	0
Fungu 16	-	Sh.	3,332,000
Fungu 19	-	Sh.	1,002,000
Fungu 35	-	Sh.	14,432,000
Fungu 40	-	Sh.	12,571,199,000
Fungu 41	-	Sh.	16,520,000
Fungu 55	-	Sh.	2,000
Fungu 59	-	Sh.	0
JUMLA		Sh.	12,606,487,000

78. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imatolewa imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho lako zuri na ndani ya muda. Tunaendelea, tupate taarifa kutoka kwenye Kamati ya Katiba na Sheria ambayo ndio ilichambua mafungu mengi yaliyopo katika Wizara hii na baadaye tutasikia Mfuko wa Mahakama.

Mheshimiwa Mchengerwa, una muda usiozidi dakika 30.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Rufiji amba leo hii wamewakilishwa na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Rufiji, yuko kwenye Bunge lako hili tukufu, Ndugu Kaswakala Mbonde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nakushukuru kuniruhusu nisimame mbele ya Bunge lako hili tukufu kuwasilisha taarifa hii. Aidha, napenda nimpongeze Mheshimiwa Spika kwa umahiri wake katika kasi ya kuliendesha Bunge hili kwa hekima na weledi mkubwa katika kuishauri vyema Serikali kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa weledi na umahiri wake katika kumsaidia Mheshimiwa Spika kuongoza Bunge hili. Nawapongeza pia Wenyevit wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuishauri na kumsaidia Mheshimiwa Spika kuendesha vikao vyta Bunge. Wote kwa pamoja

tunawaombea afya njema na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na tunamshukuru sana kwa ushirikiano wake kwa Kamati ya Katiba na Sheria wakati wote alipokuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Hivyo tunamtakia utumishi uliotukuka kwa majukumu yake mapya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustino Mahiga kwa kupewa majukumu mapya ya kuwa Waziri wa Katiba na Sheria na pia tunamshukuru kwa ushirikiano anaoendelea kuutoa kwa Kamati yangu pamoja na timu yake ya watendaji ikiongozwa na Katibu Mkuu, Profesa Sifuni Mchome, Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Amon Mpanju, Watendaji Wakuu na wataalam wote wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, nikitambua uwepo wa Mheshimiwa Jaji Kiongozi wa Tanzania hapa katika Bunge lako Tukufu. Kamati inawashukuru kwa ushirikiano wao wakati wa uchambuzi wa bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii itakuwa tayari muda wote kulisaidia Bunge lako Tukufu katika kusimamia Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa ili kuhakikisha Wizara na Taasisi zake zinatkeleza mipango yake ya maendeleo kwa ufanisi mkubwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake. Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 6 (2) (b) na Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane

ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2018/2019, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Maelezo ya miradi ya maendeleo iliyokaguliwa; Kamati imeridhidhishwa kwa kiasi kikubwa na ujenzi wa majengo ya Mahakama Kuu katika Mikoa ya Kigoma na Mara ambao umezingatia matumizi ya TEHAMA. Aidha, Kamati imeridhidhishwa na ukarabati wa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya ambao pia umezingatia matumizi ya TEHAMA katika usikilizwaji wa mashauri pamoja na utunzaji wa Kumbukumbu za Mahakama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kamati inaipongeza Mahakama ya Tanzania kwa kuanza kuzingatia matumizi ya TEHAMA katika mfumo wa uendeshaji wa shughuli za Mahakama nchini kwa kuwa mfumo huo utarahisisha utoaji haki kwa wakati na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukaguzi wa miradi husika, pia Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo juu ya ujenzi wa Mahakama 35 nchini inayoendelea kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mgawanyo ulioainishwa katika Taarifa hii; maoni ya Kamati ni kuwa endapo Serikali itatoa kiasi kilichobaki cha fedha za maendeleo zilizotengwa na kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2018/2019, ujenzi wa Mahakama hizi unaweza kukamilika ifikapo mwezi Julai, 2019.

Aidha, kukamilika kwa miradi hiyo, kutaboresha mazingira ya utoaji haki nchini ikiwemo kupungua usumbufu

wa baadhi ya wananchi kutembea kilomita nyingi kutoka Wilaya moja kwenda Wilaya nyingine ili kufuata haki ya Mahakama katika mashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia, ilipokea, kujadili na kuridhia Taarifa ya Mahakama ya Tanzania kuhusu utekelezaji wa mpango wa miaka mitano yaani 2016/2017 - 2020/2021 wa maendeleo ya miundombinu kuhusu ukarabati na ujenzi wa Mahakama mbalimbali katika ngazi ya Kata, Wilaya, Mikoa na Kitaifa pamoja na nyumba za makazi ya Majaji, Mahakimu na watumishi wengine wa Mahakama nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu pamoja na mambo mengine, unalenga kuiwezesha Mahakama nchini kupunguza kwa kiasi kikubwa au kuondokana kabisa na changamoto ya uhaba na uchakavu wa majengo ya muhimili huo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kamati ni kuwa endapo Mpango huu wa Miaka Mitano utatekelezwa kwa wakati, utaiwezesha Mahakama kujenga jumla ya majengo ya Mahakama 233; Jengo la Mahakama Kuu na Makama ya Rufani Jijini Dodoma pamoja na jumla ya nyumba 21 za Waheshimiwa Majaji, Mahakimu na Watumishi wengine wa Mahakama. Mchanganuo wa idadi ya majengo yatakayojengwa chini ya mpango huu ni kama ilivyoidhinishwa katika taarifa yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhishwa na Mpango huu kwa kuwa unalenga kuongeza upatikanaji wa haki kwa wananchi na pia umeandaliwa kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali na Mahakama kwa kuendelea kufanya maboresho makubwa katika majengo ya Mahakama mbalimbali nchini kwa lengo la kuongeza ufanisi na mazingira rafiki katika suala zima la utoaji haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake pamoja na uzingatiaji wa Maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2018/2019; na uchambuzi wa Taarifa kuhusu ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2018/2019:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Bunge liliidhinisha Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli yenye jumla ya shilingi 27,097,646,862/= . Hadi kufikia Februari, 2019 kiasi cha maduhuli kilichokusanywa na Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake ni shilingi 6,709,016,307/= sawa na asilimia 25 ya lengo liliokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kushuka kwa makusanyo ya maduhuli kunatokana na kubadilika kwa sera ya gharama za utoaji haki nchini ambayo imefuta gharama za ada mbalimbali ambazo zilibainika kuwa kikwazo kwa mwananchi wa kawaida katika kupata haki mbele ya Mahakama. Hatua hiyo imeirejesha Mahakama katika nafasi yake ya kuwa chombo cha utoaji haki badala ya kuwa chombo cha kukusanya mapato yanayotokana na utoaji haki ili haki iweze kutolewa kwa kila mwananchi bila kujali uwezo wake kiuchumi na haki hiyo ipatikane kwa gharama nafuu na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhishwa na mabadiliko hayo na inaipongeza Mahakama kwa kurahisisha na kuweka mazingira rafiki ya utekelezaji wa Ibara ya 13(1) ikisomwa pamoja na Ibara ya 107A(2)(a) za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuhusu utoaji haki nchini kwa wananchi wote bila ya kujali hali yao kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 mafungu yanayosimamiwa na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake yalitengewa shilingi 145,726,763,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 77,173,293,000/= zilikuwa ni za mishahara; na shilingi 68,553,470,000/= zilikuwa ni kwa ajili ya

matumizi mengineyo. Hadi kufikia Februari 2019 Wizara na Taasisi zake zilipokea jumla ya shilingi 87,563,214,445/= sawa sawa na asilimia 46 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi unaonyesha kuwa, kumekuwa na mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha za matumizi mengineyo kwa kuwa hadi kufika Mwezi Februari, 2019 jumla ya shilingi 36,169,958,982/= sawa na asilimia 51 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa matumizi mengineyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kamati ni kwamba Serikali ihakikishe upatikanaji wa fedha zilizobaki zinapatikana kabla ya kwisha kwa mwaka huu wa fedha 2018/2019 na ihakikishe fedha zitakazoidhishwa na Bunge zinapatikana kwa wakati kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali kwa wakati na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019; katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake iliyodhinishwa fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha shilingi 44,767,219,000/= kwa ajili ya mpango wa maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 18,000,000,000/= ni fedha za ndani na shilingi 26,767,219,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Februari, 2019 fedha za miradi ya maendeleo zilizopokelewa ni shilingi 12,889,124,095/= sawa na asilimia 29 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa; fedha za ndani ni shilingi 7,000,000,000/= sawa na asilimia 38.9 na fedha iliyokuwa imetengwa kama bajeti ya ndani. Aldha, fedha za nje zilizopokelewa hadi mwezi Februari, 2019 ni shilingi 5,889,120,095/= sawa na asilimia 22 ya fedha za nje zilizotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu yatokanayo na uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kamati imebaini kuwa miradi ya maendeleo inayotekelawa chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu ujenzi wa Mahakama nchini kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ilitegemea kwa kiasi kikubwa fedha za nje na fedha hizo hazijatolewa kwa wakati na fedha zinazoonekana kuwa ni za uhakika ni fedha za ndani.

Hivyo, maoni ya Kamati ni kuwa, Serikali iendelee kutumia vyanzo vya ndani katika kutekeleza miradi mbalimbali chini ya Wizara ya Katiba na Sheria hususan miradi ya ujenzi wa Mahakama badala ya kutegemea misaada kutoka nje ya nchi ambayo haina uhakika.

Aidha, kwa kuwa Mahakama imedhihirisha utendaji bora na wa kuridhisha katika kusimamia utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa Mahakama mbalimbali nchini kwa kutumia kiasi kidogo cha fedha kilichopokelewa kwa ufanisi mkubwa, maoni ya Kamati ni kuwa miradi inayotekelawa inaweza kukamilika kati ya mwezi Mei hadi Julai, 2019 endapo kiasi kilichobaki cha fedha za ndani kitatolewa kabla ya kwisha kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Kamati imeridhishwa na vipaumbele viliyowekwa na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kama vilivyoainishwa katika Taarifa hii, kwa sababu vinaendana na Mpango wa Taifa wa mwaka 2019/2020 pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025. Aidha, Kamati imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya Msingi ambayo yanaleta mantiki ya uwepo wa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na vipaumbele hivyo, Kamati inatoa rai kwa Wizara ya Katiba na Sheria kuhakikisha kwamba vipaumbale vyake vinakidhi udhibiti wa rasilimali za nchi, uharakishwaji wa utoaji haki, uboreshaji wa

taaluma ya Sheria, uboreshaji wa mazingira ya utoaji haki na upatikanaji wa haki kwa wakati na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 35,288,000/=. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 0.13 ya maduhuli yaliyopangwa kukusanya kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa kupungua kwa makadirio ya maduhuli chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake, kunatokana na mabadiliko ya Sera ya Utoaji Haki Nchini ambapo kwa sasa gharama za ada mbalimbali zilizokuwa zikitozwa na Mahakama zimefutwa ili kupanua uwigo wa upatikanaji wa haki nchini kwa kila mwanachi, kwa bei nafuu na kwa wakati. Mchanganuo wa kiasi cha maduhuli kinachotegemewa kukusanya kwa kila fungu husika ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ya Katiba na Sheria inaomba jumla ya shilingi 47,283,565,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi mengineyo. Kati ya fedha hizo, shilingi 25,231,984,000/= ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 22,051,581,000/= ni fedha za Matumizi Mengineyo. Kwa mchanganuo wa mapato na matumizi kwa kila fungu chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2019/2020, ni kama ilivyoorodheshwa katika Jedwali Na. 2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake zinaombewa shilingi 7,891,598,302/= kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake imeongezeka kwa kiasi cha shilingi bilioni 6.27,

ongezeko ambalo ni sawa na asilimia 4.64 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Ongezeko hilo limezingatia mahitaji ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopangiwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Hii ni pamoja na kuongeza bajeti ya Fungu 19 - Ofisi mpya ya Wakili Mkuu wa Serikali ikiwemo bajeti ya maendeleo kwa lengo ya kuiwezesha ofisi hiyo kutekeleza majukumu yake ndani na nje ya nchi kwa ufanisi zaidi ikiwemo kuimarisha nguvu kazi ya ofisi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhishwa na ofisi hiyo sambamba na utendaji wake wa kazi kwa sasa, kwani ndani ya miaka miwili ya uwepo wa ofisi hiyo Serikali imeweza kushinda kesi muhimu za madai ndani na nje ya nchi na hivyo kurejesha heshima ya nchi yetu kwa viwango vinavyoiridhisha na kwa uzalendo mkubwa. Aldha, ongezeko hill la bajeti ya Wizara hii pia limetokana na kuboresha bajeti ya Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ambapo Kamati imebaini ongezeko la Sh.2,484,266,802 ongezeko ambalo ni sawa na asilimia 56.9 ya bajeti ya Tume hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini pia ongezeko la shilingi bilioni 1.2 katika bajeti ya Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, ongezeko ambalo litaiwezesha ofisi hiyo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi hususani katika ngazi za mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhishwa na maboresho katika Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa kuwa yamezingatia maoni na ushauri wa Kamati yangu yaliyotolewa wakati wa kupokea na kujadili bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati; kutokana na ufinyu wa muda nitasoma kwa uchache baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati, hivyo naomba kila hoja ya Kamati katika sehemu hii iingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*) kwa ajili ya utekelezaji wa Serikali. Kwa

muktadha huo naomba sasa kuwasilisha baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama; kwa kuwa Kamati imebaini kuwa kwa sasa Mahakama nydingi za Mwanzo zina Mahakimu wenyewe elimu ya shahada ya kwanza ya sheria na hivyo kuwa na uwezo wa kutosha kitaaluma kuendesha mashauri ya jinai na madai katika Mahakama za Mwanzo nchini, hivyo Kamati inaishauri Serikali kufanya maboresho katika Sheria ya Mahakama za Mahakimu ili kuondoa ulazima wa maamuzi ya mahakama za mwanzo kufanyika kwa kura ya wazee wa mahakama na badala yake wazee wa mahakama wawepo kushauri tu, lakini ushauri wao usiwe wa lazima kiasi cha kuingilia maamuzi ya Hakimu yenyeye kuzingatia sheria za nchi au Serikali, ione umuhimu wa kuondoa wazee hao au kwa namna itakavyoona inafaa bila kuathiri maamuzi ya Mahakimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa ushauri wa Kamati ni kwamba pamoja na uwepo wa mila na desturi katika jamii zetu zenye kuhitaji wazee washauri katika baadhi ya mashauri kwenye ngazi za Mahakama za Mwanzo sio mara zote ushauri wa walio wengi katika ngazi ya Mahakama za Mwanzo unaendana na matakwa ya sharia. Pia hatua hiyo itarahisisha utoaji haki kwa wakati katika Mahakama za Mwanzo ikiwemo kupunguza gharama za uendeshaji wa mahakama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo ya mahakama katika Mkoa wa Arusha, Wilayani Longido, Kamati ilibaini uwepo wa vitendo vingi vya uhalifu katika mpaka wa Tanzania na Kenya Namanga na kwa kuwa eneo hilo halina Mahakama ya Mwanzo ambayo ingesaidia utoaji haki kwa haraka kutokana na makosa ya jinai yanayotokana na usafirishaji dawa za kulevyta hususan mirungi na bangi baina ya nchi hizo, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango iridhie maombi ya Wilaya ya Longido kuhusu jengo la Namanga liliokuwa ofisi ya TRA litolewe kwa mahakama ili ofisi hizo zitumike kuwa ni Mahakama ya Mwanzo ya Namanga kwa lengo la kuharakisha utoaji haki mpakani hapo ili kuimarissha udhibiti

wa vitendo vya uharifu na kulinda usalama katika mpaka huo. Hatua hiyo inawezekana kwa kuwa tayari *TRA* wamehamia katika ofisi mpya katika kituo cha *One Stop Center* cha hapo hapo Namanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mahakama imeiridhisha Kamati na umma wa Watanzania kwa ujumla kuhusu namna inavyoendelea kutekeleza miradi 35 ya ujenzi wa mahakama katika mikoa mbalimbali nchini yakiwemo matumizi mazuri ya kuridhisha ya fedha inayotolewa na Hazina na imebainika kuwa endapo Serikali itatoa shilingi bilioni 10 kiasi kilichobaki cha bajeti, ujenzi wa mahakama kwa mwaka wa fedha 2018/2019 miradi hiyo inaweza kukamilika na kukabidhiwa kwa mahakama ifikapo Julai 2019. Kamati inashauri Serikali kuona umuhimu na ulazima kwa kutoa kiasi hicho cha fedha kilichobaki ili kuiwezesha mahakama kukamilisha miradi husika kwa wakati kwa lengo la kuboresha mazingira stahiki ya utoaji haki nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, kwa kuwa ofisi hii kwa sasa inakabiliana na kesi nyingi nyeti za kijinai ambazo zinaweza kuwepo kwa mazingira hatarishi kwa Waendesha Mashtaka nchini na kwa kuwa nguvu kazi ya ofisi hii inahitaji kuboresha stahiki zao mbalimbali ili kuwezesha kutekeleza majukumu kwa weledi na ufanisi zaidi, Kamati inashauri yafuatayo:-

(1) Ofisi hii ianze kutekeleza matakwa ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria Na.2 ya mwaka 2018 ambapo Sheria ya Taifa ya Mashataka, Sura 430 pamoja na mambo mengine muhimu inampa Mamlaka Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka kuanzisha kitengo maalumu cha kukabiliana na maeneo maalum yenye matukio sugu ya kihalifu ili kuhakikisha kuwa maeneo hayo yanapewa kipaumbele katika usimamizi wa haki jinai kwa maslahi mapana ya nchi.

(2) Serikali ione umuhimu wa kuanzisha Mfuko wa Huduma Maalum, Mfuko wa Dharura chini ya ofisi hii kwa mujibu wa sheria ambapo utapokea fedha moja kwa moja kutoka Serikalini na vyanzo vingine kama vilivyoainishwa na

sheria ili kuimarisha utendaji kazi wa ofisi hii muhimu katika kuendesha mashauri ya haki jinai nchini hususan kusimamia na kuharakisha haki jinai katika maeneo yaliyobainika kuwa na matukio ya hatarishi nchini.

(3) Serikali ione umuhimu wa kubakiza chini ya ofisi hii asilimia 10 ya fedha zinazookolewa na ofisi hii kutohana na kesi za ubadhilifu zinazosimamiwa na waendesha mashtaka ili fedha hizo ziingizwe moja kwa moja kwenye Mfuko wa Dharura wa ofisi hiyo kama ilivyo kwenye vyombo vingine nchini vyenye majukumu maalum kama ya ofisi hii muhimu. Ofisi hii ihakikishe kuwa majukwaa ya haki jinai ya Wilaya na Mikoa yaliyoanzishwa kwa mujibu wa sheria yanatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria ikiwemo kutembelea na kukagua mrundikano wa watuhumiwa katika mahabusu zote nchini ili kubuni na kutekeleza mpango mkakati wa kuondokana na changamoto inayoathiri utoaji haki nchini na kuibua malalamiko kwa wananchi. Hii ni pamoja na kuhakikisha dhamana zinazotolewa na polisi zinatolewa kwa wakati kwa mujibu wa sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ofisi hii imetekekeleza ushauri wa Kamati ya Bunge lako Tukufu kuhusu kufungua ofisi zake katika mikoa na wilaya mbalimbali kwa lengo la kuongeza wigo wa utoaji haki jinai katika maeneo husika kwa kusogea huduma stahiki karibu na kwa wananchi, Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha zote zilizoombwa na ofisi hii kwa wakati kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hii ni pamoja na kuboresha mishahara na stahiki nyingine za Waendesha Mashtaka kote nchini ili kutoa motisha kwa watumishi hao ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, hii ni pamoja na mahakimu wote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria; kwa kuwa tayari Serikali na vyombo vyake imeshahamia Dodoma na kwa kuwa tayari Bunge lako Tukufu limeshatoa baraka zote kwa kutunga Sheria ya Kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi na Kamati inaishauri Wizara ya Katiba na Sheria kusimamia mpango wa kujenga jengo la

Mahakama Kuu ya Mahakama ya Tanzania hapa Dodoma kama ilivyoidhinishwa katika mpango kazi wa miaka mitano wa Mahakama ya Tanzania. Hii ni pamoja na kuendelea kuboresha miundombinu ya utoaji haki kwa mahakama zote kulingana na bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge na watendaji wake wote...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo , naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zote zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara

ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6 (2) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Wizara tatu ikiwemo Wizara ya Katiba na Sheria.

Aidha, Kifungu cha 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inatoa Mamlaka kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara inazosizimamia. Jukumu hili la Uchambuzi wa Bajeti linaendana sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Ujenzi wa Mahakama nchini, kuanzia tarehe 12 hadi 18 na tarehe 29 hadi 31 Machi 2019. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake tarehe 26 na 27 Machi, 2019.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria ina Mafungu 8 ya bajeti kama ifuatavyo:-

- i) **Fungu 12** – Tume ya Utumishi wa Mahakama,
- ii) **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,
- iii) **Fungu 19** – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali,
- iv) **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka
- v) **Fungu 40** – Mfuko wa Mahakama,
- vi) **Fungu 41** – Wizara ya Katiba na Sheria,
- vii) **Fungu 55**- Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, na

viii) **Fungu 59** –Tume ya Kurekebisha Sheria

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo Manne yafuatayo:-

- i) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;
- ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;
- iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, na;
- iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

**2.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO
ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA
2018/2019**

2.1 Maelezo ya Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara ya Ugaguzi wa Miradi ya Ujenzi wa Mahakama nchini katika Mikoa ya Mbeya, Njombe, Manyara na Arusha. Aidha, kwa kibali chako, Kamati ilifanya ziara maalum kwa ajili ya kutembelea na kukagua Ujenzi wa Mahakama Kuu katika Mikoa ya Kigoma na Mara, kwa tarehe zilizoainishwa hapo awali.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhidhishwa kwa kiasi kikubwa na ujenzi wa Majengo ya Mahakama Kuu katika Mikoa ya Kigoma na Mara ambao umezingatia matumizi ya TEHAMA. Aidha, Kamati imeridhidhishwa na ukarabati wa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya ambao pia umezingatia matumizi ya TEHAMA katika usikilizaji wa mashauri pamoja na utunzaji wa Kumbukumbu za Mahakama hiyo. Hivyo, Kamati inaipongeza Mahakama ya Tanzania kwa kuanza kuzingatia matumizi ya TEHAMA katika mfumo wa uendeshaji

wa shughuli za Mahakama nchini, kwa kuwa mfumo huo, utarahisisha utoaji haki kwa wakati na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukaguzi wa Miradi husika, pia Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo juu ya ujenzi wa Mahakama 35 nchini, inayoendelea kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa mgawanyo ufuatao:-

- a) Mahakama Kuu Tatu (3),
- b) Mahakama za Hakimu Mkazi Sita (6),
- c) Mahakama za Wilaya Kumi na Nne (14), na
- d) Mahakama za Mwanzo Kumi na Mbili (12)

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati ni kuwa, endapo Serikali itatoa kiasi kilichobaki cha fedha za maendeleo zilizotengwa na kuidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Ujenzi wa Mahakama hizi unaweza kukamilika ifikapo Mwezi Julai, 2019. Aidha, kukamilika kwa miradi hiyo kutaboresha mazingira ya utoaji haki nchini ikiwemo kupunguza usumbufu kwa baadhi ya Wananchi kutembea Kilomita nyingi kutoka Wilaya moja kwenda Wilaya nyingine ili kufuata haki ya Mahakama katika mashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia, ilipokea, kujadili na kuridhia Taarifa ya Mahakama ya Tanzania kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano (2016/2017-2020/2021 wa Maendeleo ya Miundombinu kuhusu Ukarabati na Ujenzi wa Mahakama mbalimbali katika ngazi ya Kata, Wilaya, Mikoa na Kitifa pamoja na Nyumba za Makazi ya Majaji, Mahakimu na Watumishi wengine wa Mahakama nchini. Mpango huu pamoja na mambo mengine unalenga kuiwezesha Mahakama nchini kupunguza kwa kiasi kikubwa au kuondokana kabisa na changamoto ya uhaba na uchakavu wa majengo ya muhimili huo muhimu.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati ni kuwa, endapo Mpango huu wa miaka Mitano (5) utatekelezwa kwa wakati, utaiwezesha Mahakama kujenga Jengo la Makao Makuu na Mahakama ya Rufani Jijini Dodoma, Majengo ya Mahakama Kuu katika Mikoa Kumi na Mbili (12), Majengo ya Mahakama za Hakimu Mkazi Kumi na Saba (17), Mahakama za Wilaya Mia Moja na Nne (104) na Mahakama za Mwanzo Mia Moja (100), Nyumba za Majaji Kumi na Moja (11) na Nyumba za Mahakimu na Watumishi wengine Kumi (10).

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na Mpango huu kwa kuwa unalenga kuongeza upatikanaji wa haki kwa Wananchi, na pia umeandaliwa kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025.

Mheshimiwa Spika, Kamati inalpongeza Serikali na Mahakama kwa kuendelea kufanya maboresho makubwa katika Majengo ya Mahakama mbalimbali nchini kwa lengo la kuongeza ufanisi na mazingira rafiki katika suala zima la utoaji haki.

3.0 UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA NA TAASISI ZAKE PAMOJA NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, tarehe 26 na 27 Machi, 2019. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ultazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinisha na Bunge katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi kufikia Mwezi Machi 2019. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 ili kujuu vipaumbele vya kibajeti.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati ultazama pia eneo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa kulinganisha kiasi kilichokusanywa katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi 2019 na ukamilishaji wa lengo la ukusanyaji lililowekwa wakati wa kupitisha bajeti Mwezi Aprili 2018. Lengo la uchambuzi wa namna hii ni kufahamu uwezo wa Serikali katika kukusanya Maduhuli. Kamati ilitumia njia mbalimbali katika uchambuzi wake kama kutazama hali halisi ya kila Taasisi, kujiridhisha na taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu kwenye Kamati.

3.2 *Uchambuzi wa Taarifa Kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019*

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Bunge liliidhinisha Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli yenye jumla ya **Shilingi Bilioni Ishirini na Saba, Milioni Tisini na Saba, Laki Sita Arobaini na Sita Elfu na Mia Nane Sitini na Mbili (27,097,646,862/=)**. Hadi kufikia Februari, 2019 kiasi cha Maduhuli kilichokusanywa na Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake ni **Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Saba na Tisa,Laki Sita na Kumi na Sita Elfu, Mia Tatu na Saba(6,709,616,307)** sawa na **asilimia 25** ya lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kushuka kwa makusanyo ya maduhuli kunatokana na

kubadilika kwa Sera ya gharama za utoaji haki nchini ambayo imefuta gharama za ada mbalimbali ambazo zilibainika kuwa kikwazo kwa Mwananchi wa kawaida katika kupata haki mbele ya Mahakama. Hatua hiyo imeirejesha Mahakama katika nafasi yake ya kuwa chombo cha utoaji haki badala ya kuwa chombo cha kukusanya mapato yatokanayo na utoaji haki ili haki iweze kutolewa kwa kila Mwananchi bila kujali uwezo wake kiuchumi na haki hiyo ipatikane kwa gharama nafuu na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na mabadiliko hayo na inaipongeza Mahakama kwa kurahisisha na kuweka mazingira rafiki ya utekelezaji wa Ibara ya 13(1) ikisomwa pamoja na Ibara ya 107A(2)(a) za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuhusu utoaji haki nchini kwa Wananchi wote bila ya kujali hali yao kiuchumi.

3.3 *Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina*

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Mafungu yanayosimamiwa na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake yalitengewa *Shilingi Bilioni Mia Moja Arobaini na Tano, Milioni Mia Saba Ishirini na Sita, Laki Saba Sitini na Tatu Elfu (145, 726,763,000/=)* kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, *Shilingi Bilioni Sabini na Saba, Milioni Mia Moja Sabini na Tatu, Laki Mbili Tisini na Tatu (77,173,293,000)* zilikuwa ni za Mishahara na *Shilingi Bilioni Sitini na Nane, Milioni Mia Tano Hamsini na Tatu, Laki Nne Sabini Elfu(68,553,470,000)* zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia Februari 2019 Wizara na Taasisi zake zilipokea *Jumla ya Shilingi Bilioni Themanini na Saba, Milioni Mia Tano Sitini na Tatu, Laki Mbili Kumi na Nne Elfu, Mia Nne Arobaini na Tano (87,563,214,445)* sawa na asilimia 46% ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi unaonyesha kuwa kumekuwa na mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu

upatikanaji wa fedha za Matumizi Mengineyo kwa kuwa hadi kufika Mwezi Februari, 2019 jumla ya **Shilingi Bilioni Thelathini na Sita, Milioni Mia Moja Sitini na Tisa, Laki Tisa Hamsini na Nane Elfu, Mia Tisa Themanini na Mbili** (36,169,958,982) sawa na **asilimia 51%** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa matumizi mengineyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati ni kwamba Serikali ihakikishe upatikanaji wa fedha zilizobaki zinapatikana kabla ya kuisha kwa Mwaka huu wa Fedha 2018/2019 na ihakikishe fedha zitakazoidhishwa na Bunge zinapatikana kwa wakati kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali kwa wakati na kwa ufanisi.

3.4 *Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019,*

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake iliyodhinishwa Fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha **Shilingi Bilioni Arobaini na Nne, Milioni Mia Saba Sitini na Saba, Laki Mbili Kumi na Tisa Elfu** (44,767,219,000/=) kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizi **Shilingi Bilioni Kumi na Nane** (18,000,000,000/=) ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni Ishirini na Sita Milioni Mia Saba Sitini na Saba, Laki Mbili Kumi na Tisa Elfu** (26, 767,219,000/=) ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hadi Februari, 2019 Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa ni **Shilingi Bilioni Kumi na Mbili, Milioni Mia Nane Themanini na Tisa, Laki Moja Ishirini Elfu na Tisini na Tano** (12,889,120,095/=) sawa na **asilimia 29 %** ya Fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, fedha za ndani ni **Shilingi Bilioni Saba** (7,000,000,000/=) sawa na **asilimia 38.9%** ya Fedha iliyokuwa imetengwa kama bajeti ya Ndani. Aidha, fedha za Nje zilizopokelewa hadi Mwezi Februari, 2019 ni **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Nane Themanini na Tisa, Laki Moja Ishirini Elfu na Tisini na Tano** (5,889,120,095/=) sawa na **asilimia 22** ya fedha za nje zilizotengwa.

3.5 Yatokanayo na Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Miradi ya Maendeleo inayotekelizwa chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Ujenzi wa Mahakama nchini kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ilitegemea kwa kiasi kikubwa fedha za Nje na Fedha hizo hazijatolewa kwa wakati na fedha zinazoonekana kuwa ni za uhakika zaidi ni fedha za ndani.

Hivyo, maoni ya Kamati ni kuwa, Serikali iendelee kutumia vyanzo vya ndani katika kutekeleza Miradi mbalimbali nchini ya Wizara ya Katiba na Sheria hususan Miradi ya ujenzi wa Mahakama badala ya kutegemea misaada kutoka nje ya nchi ambayo haina uhakika.

Aidha, kwa kuwa Mahakama imedhihirisha utendaji bora na wakuridhisha katika kusimamia utekelezaji wa Miradi ya ujenzi wa Mahakama mbalimbali nchini kwa kutumia kiasi kidogo cha fedha kilichopokelewa kwa ufanisi mkubwa, Maoni ya Kamati ni kuwa, Miradi inayotekelizwa inaweza kukamilika kati ya Mwezi Mei hadi Julai, 2019 endapo kiasi kilichobaki cha Fedha za ndani kitatolewa kabla ya kuisha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Mpango huu wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 umeandalila kwa kuzingatia llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mpango ambao umelenga utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/2021).

4.1 Uchambuzi wa Vipaumbele vya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2019/

2020 umeainisha maeneo zaidi ya Hamsini (50) ya viapumbele kwa Taasisi zote zilizo Chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, ya kiwemo;

- i) Kuendelea na Ujenzi wa majengo ya Makao Makuu ya Wizara katika eneo la Mji wa Serikali, IHUMWA Jijini Dodoma,
- ii) Kukamilisha na kutekeleza Awamu ya Pili ya Programu ya Maboresho ya Sheria,
- iii) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mpango wa kutenganisha Mashtaka na Upelelezi,
- iv) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Miradi mbalimbali chini ya Wizara na Taasisi zake,
- v) Kujenga na kuboresha Majengo ya Mahakama nchini,
- vi) Kuimarisha Matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kisheria nchini,
- vii) Kuwajengea uwezo Watumishi kwa lengo la kuendeleza vipaji vyao, kuimarisha weledi na kuongeza tija kuititia mafunzo ya muda mfupi,
- viii) Kuimarisha Mfumo wa uandishi na urekebishaji wa Sheria,
- ix) Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa mashauri ya madai ambayo Serikali ina maslahi ndani na nje ya nchi,
- x) Kuimarisha utoaji wa Elimu kwa Umma juu ya masuala ya Haki za Binadamu na Misingi ya Utawala Bora nchini,
- xi) Kuimarisha Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama za Wilaya na Mikoa nchini,

- xii) Kuongeza udahili wa Wanafunzi katika Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo ili kuongeza idadi ya Wataalam wa Sheria nchini,

- xiii) Kuendelea na Mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI na Magonjwa sugu yasiyoambukizwa mahali pa kazi,
- xiv) Kuimarisha uwezo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili itoe huduma kwa ufanisi,
- xv) Kuimarisha Mifumo ya usimamizi wa mashauri na udhibiti wa ubora,
- xvi) Kuimarisha uhusiano wa Masuala ya kisheria baina ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Kitaifa na Kimataifa,
- xvii) Kuimarisha Mfumo wa Utatuzi wa mashauri ya kawaida na ya siku nyingi kwa lengo la kupunguza mlundikano,
- xviii) Kuanza Utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria,
- xix) Kuimarisha upatikanaji haki kwa Watu wasio na uwezo na kuratibu utekelezaji wa wajibu wa nchi katika Mikataba ya Kikanda na Kimataifa kuhusu Haki za Binadamu, na
- xx) Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa kujenga na kukarabati Miundombinu ya Mahakama katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na Vipaumbele viliyowekwa na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kwa sababu vinaendana na Mpango wa Taifa wa Mwaka 2019/2020 pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025. Aidha, Kamati imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya Msingi ambayo yanaleta mantiki ya uwepo wa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na vipaumbele hivyo Kamati inatoa rai kwa Wizara ya Katiba na Sheria kuhakikisha kwamba vipaumbele vyake vinaakisi udhibiti wa rasilimali za nchi, uharakishwaji wa utoaji haki, uboreshaji wa Taaluma ya Sheria, uboreshaji wa mazingira ya utoaji haki na upatikanaji wa haki kwa wakati na kwa gharama nafuu.

4.2 *Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi Milioni Thelathini na Tano, Laki Mbili Themanini na Nane Elfu (35,288,000/=)**. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 0.13% ya Maduhuli yaliyopangwa kukusanya kwa mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, kupungua kwa makadirio ya Maduhuli chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake, kunatokana na mabadiliko ya Sera ya utoaji haki nchini ambapo kwa sasa, gharama za ada mbalimbali zilizokuwa zikitozwa na Mahakama zimefutwa ili kupanua uwigo wa upatikanaji wa haki nchini kwa kila Mwanachi, kwa bei nafuu na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa kiasi cha Maduhuli kinachotegemewa kukusanya kwa kila Fungu husika ni kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na.1**

JEDWALI NA.1: Mpango wa Ukusanyaji Maduhuli ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

FUNGU	JINA LA FUNGU	KIASI CHA FEDHA KILICHOPANGWA KUKUSANYWA 2019/2020
12	Tume ya Utumishi wa Mahakama	0
16	Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali	3,332,000
19	Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali	1,002,000
35	Ofisi ya Taifa ya Mashtaka	14,432,000
41	Wizara ya Katiba na Sheria	16,520,000
55	Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora	2,000
59	Tume ya Kurebisha Sheria	0
JUMLA KUU		35,288,000

Chanzo: Taarifa ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria ya tarehe 26 Machi, 2019

4.3 *Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020*

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ya Katiba na Sheria inaomba jumla ya **Shilingi Bilioni Arobaini na Saba, Milioni Mia Mbili Themanini na Tatu, Laki Tano Sitini na Tano Elfu, (47, 283, 565,000/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Ishirini na Tano, Milioni Mia Mbili Thelathini na Moja, Laki Tisa Themanini na Nne Elfu (25, 231, 984,000/=)** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi Bilioni Ishirini na Mbili, Milioni Hamsini na Moja, Laki Tano Themanini Moja Elfu (22,051,581,000/=)** ni fedha za Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Spika, katika mchanganuo wa Mapato na Matumizi kwa kila Fungu chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, ni kama ilivyoinishwa katika **Jedwali Na.2**.

Jedwali Na.2: Kiasi cha Fedha kinachoombwa kwa Mafungu ya Bajeti yaliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

FUNGU	JINA LA FUNGU	KIASI CHA FEDHA KINACHOOOMBWA
12	Tume ya Utumishi wa Mahakama	1,304,962,000
16	Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali	6,632,301,000
19	Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali	7,288,327,000
35	Ofisi ya Taifa ya Mashtaka	17,704,158,000
41	Wizara ya Katiba na Sheria	13,409,449,500
55	Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora	6,850,192,802
59	Tume ya Kurekebisha Sheria	1,985,775,000
JUMLA KUU		55,175,163,302

Chanzo: Taarifa ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Serikali ya Tarehe 26 Machi, 2019

4.4 Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake zinaombewa **Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Nane Tisini na Moja, Laki Tano Tisini na Nane Elfu, Mia Tatu na Mbili (7,891,598,302/=)** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake imeongezeka kwa kiasi cha **Shilingi Blioni 6.27** ongezeko ambalo ni sawa na asilimia **4.64%** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, ongezeko hilo limezingatia mahitaji ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kutokana na vipaumbele vilivyopangwa kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Hii ni pamoja na kuongeza bajeti ya Fungu 19; Ofisi mpya ya Wakili Mkuu wa Serikali ikiwemo bajeti ya Maendeleo kwa lengo la kuiwezesha Ofisi hiyo kutekeleza majukumu yake ndani na nje ya nchi kwa ufanisi zaidi ikiwemo kuimarisha Nguvu kazi ya Ofisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na uwepo wa Ofisi hiyo sambamba na utendaji wake wa kazi kwa sasa, kwani ndani ya miaka miili ya uwepo wa Ofisi hiyo, Serikali imeshinda kesi muhimu za madai ndani na nje ya nchi, na hivyo kurejesha heshima ya nchi kwa viwango vinavyoridhisha na kwa uzalendo mkubwa.

Aidha, Ongezeko hili la Bajeti ya Wizara hii pia imetokana na kuboresha Bajeti ya **Fungu 55**; Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ambapo Kamati imebaini ongezeko la **Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nne Themanini na Nne, Laki Mbili Sitini na Sita Elfu, Mia Nane na Mbili (2,484, 266, 802/=)**, ongezeko ambalo ni sawa na **asilimia 56.9%** ya Bajeti ya Tume hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa, Spika, Kamati imebaini pia ongezeko la **Shilingi Bilioni 1.2** katika Bajeti ya Fungu 35; Ofisi ya Taifa ya

Mashtaka, ongezeko ambalo litaiwezesha Ofisi hiyo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi hususan katika ngazi ya Mikoa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na maboresho katika Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa kuwa yamezingatia maoni na Ushauri wa Kamati yaliyotolewa wakati wa kupokea na kujadili Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake.

5.1 FUNGU 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama

i) **Mheshimiwa Spika**, wakati wa ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ilibainika kuwepo kwa changamoto ya Watumishi wa Mahakama wakiwemo Mahakimu kukaa kwenye cheo kimoja kwa muda mrefu bila kupandishwa daraja, na uwepo wa mazingira ya kazi yasiyoridhisha kwa upande wa Mahakimu ikiwemo ukosefu wa stahiki zenyetukidhi hali halisi ya maisha kwa Watumishi hao, Kamati inaishauri Tume ya Utumishi wa Mahakama kuhakikisha inatatau changamoto hizo kwa kuendelea kuboresha mazingira ya kazi na stahiki nyingine kwa Watumishi wake wote ili kuchochaea motisha ya utendaji kazi kwa Watumishi hao ikiwa ni pamoja na kuimarisha usalama wao wawapo kazini.

ii) **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Kamati imebaini kuwa, kwa sasa, Mahakama nyingi za Mwanzo zina Mahakimu wenye Elimu ya Shahada ya Kwanza ya Sheria na hivyo kuwa na uwezo wa kutosha kitaaluma kuendesha mashauri ya jinai na madai katika Mahakama za mwanzo

nchini. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kufanya maboresho katika Sheria ya Mahakama za Mahakimu ili kuondoa ulazima wa Maamuzi ya Mahakama za Mwanzo kufanyika kwa kura za Wazee wa Mahakama na badala yake, Wazee wa Mahakama wawepo kushauri tu lakini ushauri wao usiwe wa lazima kiasi cha kuingilia maamuzi ya Hakimu yenyе kuzingatia Sheria za nchi, au Serikali ione umuhimu wa kuondoa Wazee hao au kwa namna itavyoona inafaa bila kuathiri maamuzi ya Mahakimu.

Mheshimiwa Spika, Msingi wa ushauri wa Kamati ni kwamba, pamoja na uwepo wa mila na desturi katika jamii zetu zenye kuhitaji Wazee washauri katika baadhi ya mashauri kwenye ngazi ya Mahakama za Mwanzo, siyo mara zote ushauri wa Walio wengi katika ngazi ya Mahakama za Mwanzo unaendana na matakwa ya Sheria, lakini pia, hatua hiyo itarahisisha utoaji haki kwa wakati katika Mahakama za Mwanzo ikiwemo kupunguza gharama za uendeshaji wa Mahakama hizo.

iii) **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa wakati wa Ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ya Mahakama katika Mkoa wa Arusha, Wilayani Longido, Kamati ilibaini uwepo wa vitendo vingi vya uharifu katika Mpaka wa Tanzania na Kenya (Namanga), na kwa kuwa, eneo hilo halina Mahakama ya Mwanzo ambayo ingesaidia utoaji haki kwa haraka kutokana na makosa ya jinai yanayotokana na usafirishaji dawa za kulevyaa hususan mirungi na bangi baina ya nchi hizo mbili, Kamati inashauri, Wizara ya Fedha na Mipango iliridhie maombi ya Wilaya ya Longido kuhusu Jengo lilitokuwa Ofisi za TRA litolewe kwa Mahakama ili Ofisi hizo zitumike kuwa Mahakama ya Mwanzo ya Namanga kwa lengo la kuharakisha utoaji haki mpakani hapo ili kuimarissha udhibiti wa vitendo vya uharifu na kulinda usalama katika Mpaka huo. Hatua hiyo inawezekana kwa kuwa, tayari TRA wamehamia katika Ofisi mpya katika *Kituo cha One Stop Centre* cha hapo hapo Namanga.

iv) **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kuridhishwa na utendaji kazi wa Mahakama katika jitihada

zake za kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani, Kamati inashauri kuwa, Waheshimiwa Majaji kwa kushirikiana na vyombo husika, waendelee kutekeleza utaratibu wao waliojiwekea wa kutembelea Magereza pamoja na Mahabusu nchini ili kujionea hali halisi ya Mlundikano wa Watuhumiwa na Wafungwa, kwa lengo la kuchochea utekelezaji wa miongozo ya Mahakama kuhusu kusikiliza na kumaliza mashauri mbalimbali kwa wakati, kama sehemu ya utekelezaji wa moja ya vipaumbele vya Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

v) **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Mahakama imeiridhisha Kamati na Umma wa Tanzania kwa ujumla kuhusu namna inavyoendelea kutekeleza Miradi 35 ya Ujenzi wa Mahakama katika Mikoa na Wilaya mbalimbali nchini, ikiwemo matumizi mazuri na ya kuridhisha ya fedha inayotolewa na Hazina, na kwa kuwa, imebainika wazi kuwa endapo Serikali itatoa kiasi cha **Shilingi Bilioni Kumi** kilichobaki katika bajeti ya Ujenzi wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Miradi hiyo inaweza kukamilika na kukabidhiwa kwa Mahakama ifikapo Julai, 2019. Kamati inashauri Serikali kuona umuhimu na ulazima wa kutoa kiasi hicho cha fedha kilichobaki ili kuiwezesha Mahakama kukamilisha miradi husika kwa wakati kwa lengo la kuboresha mazingira stahiki ya utoaji haki nchini.

vi) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuwa, fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo pamoja na fedha za Matumizi ya Kawaida zitolewe kwa wakati ili kuiwezesha Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi hususan utoaji haki kwa wakati na kwa gharama nafuu, kwa mwaka wa Fedha 2019/2020.

5.2 Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali kuhakikisha inaimarisha Mfumo wa uandishi wa Sheria na Usimamizi wa Masuala ya

Mikataba inayohusu rasilimali za nchi katika Sekta zote nchini. Hii ni pamoja na kuongeza idadi ya Rasilimali Watu wa Taaluma mbalimbali, kuwajengea uwezo kwa njia ya Uanagenzi kuititia Wadau mbalimbali wa Maendeleo ndani na nje ya nchi, pamoja na kuboresha stahiki za Wansheria wa Serikali na mazingira yao ya kazi kwa lengo la kuongeza Weledi na ufanisi wa Watumishi hao katika kusimamia maslahi ya nchi na rasilimali zake.

5.3 *Fungu 19: Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali,*

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kuridhishwa na utendaji wenye tija kwa Ofisi hii ndani ya Miaka miwili ya kuanzishwa kwake, na kwa kuwa Serikali imeanzisha Ofisi hii mahsusini kwa ajili ya ufuatiliaji wa mashauri ya madai ambayo Serikali ina maslahi ndani na nje ya nchi, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuwa na rasilimali ya kutosha, iendelezwie na kupewa stahiki zenye kuridhishwa ili kuimarisha uwezo wa Mawakili wa Serikali katika kushughulikia mashauri ya usuluhishi na mashauri ya madai kwa maslai ya nchi na kwa ufanisi zaidi.

5.4 *Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka*

i) **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa, Ofisi hii kwa sasa inakabiliana na kesi nyeti za kijinai ambazo zinaweza kuwepo kwa mazingira hatarishi kwa Waendesha Mashtaka nchini, na kwa kuwa, nguvu kazi ya Ofisi hii inahitaji kuboreshewa stahiki zao mbalimbali ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi zaidi, Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Ofisi hii ianze kutekeleza matakwa ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.2 ya Mwaka 2018 ambapo, Sheria ya Taifa ya Mashtaka, Sura 430 pamoja na mambo mengine muhimu, inampa Mamlaka Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka kuanzisha kitengo Maalum cha kukabiliana na maeneo Maalum yenye matukio sugu ya kiuahrifu ili kuhakikisha kuwa, maeneo hayo yanapewa

kipaumbele katika usimamizi wa haki jinai kwa maslahi mapana ya nchi.

b) Serikali ione umuhimu wa kuanzisha Mfuko wa Huduma Maalum (Mfuko wa Dharura) chini ya Ofisi hii kwa mujibu wa Sheria, ambao utapokea fedha moja kwa moja kutoka Serikalini na vyanzo vingine kama vilivyoainishwa na Sheria, ili kuimarisha utendaji kazi wa Ofisi hii muhimu katika kuendesha mashauri ya haki jinai nchini hususan kusimamia na kuharakisha haki jinai katika maeneo yaliyobainika kuwa na matukio hatarishi nchini.

c) Serikali ione umuhimu wa kubakiza chini ya Ofisi hii **asilimia 10% ya fedha** zitakazokuwa zinaokolewa na Ofisi hii kutokana na kesi za ubadhilifu zitakazosimamiwa na Waendesha Mashtaka, ili fedha hizo zilingizwe moja kwa moja kwenye Mfuko wa dharura wa Ofisi hiyo, kama ilivyo kwenye vyombo vingine nchini vyenye majukumu maalum kama ya Ofisi hii muhimu.

d) Ofisi hii ihakikishe kuwa, Majukwaa ya Haki Jinai ya Wilaya na Mikoa yaliyoanzishwa kwa Mujibu wa Sheria, yanatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ikiwemo kutembelea na kukagua mlundikano wa Watuhumiwa katika Mahabusu zote nchini ili kubuni na kutekeleza Mpango Mkakati wa kuondokana na changamoto hiyo inayoathiri utoaji haki nchini na kuibua malalamiko kutoka kwa Wananchi. Hii ni pamoja na kuhakikisha dhamana zinazotolewa na Polisi zinatolewa kwa wakati kwa mujibu wa Sheria za nchi.

e) Kuwepo kwa ushirikiano wa karibu katika kuratibu Mfumo mzima wa utoaji haki nchini baina ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Mahakama, Polisi na vyombo vingine vya upelelezi. Hatua hii itarahisisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka pamoja na kuongeza uwigo wa utoaji haki bila kuingilia uhuru wa vyombo vingine vya kiupelelezi.

ii) **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Ofisi hii imetekeleza ushauri wa Kamati na Bunge lako Tukufu, kuhusu kufungua Ofisi zake katika Mikoa na Wilaya mbalimbali kwa lengo la kuongeza uwigo wa utoaji haki katika maeneo husika kwa kusogeza huduma stahiki karibu na Wananchi, Kamati inashauri Serikali, kutoa fedha zote zilizoombwa na Ofisi hii kwa wakati, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hii ni pamoja na kuboresha Mishahara na stahiki nyingine za Waendesha Mashtaka wa Serikali nchini ili kutoa motisha kwa Watumishi hao waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

5.5 FUNGU 55 -Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kutekeleza kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati kuhusu kuboresha Bajeti ya Tume hii muhimu ambapo, kwa mwaka huu bajeti imeongezeka kwa zaidi asilimia 56% ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019, na kwa kuwa bado yapo malalamiko mengi kuhusu uvunjwaji wa Haki za Binadamu, ukiukwaji wa Misingi ya Utawala Bora nchini pamoja na tuhuma za kushikiliwa Watu Magerezani, Polisi na sehemu nyinginezo nchini pasipo kuwepo utoaji haki au majibu yanayoridhisha kwa wakati, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha fedha zilizotengewa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 zinatolewa kwa wakati ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Aidha, Tume ifanye ukaguzi katika sehemu zote nchini zenye malalamiko ya ucheleweshaji wa haki na kutoa taarifa kwa mujibu wa Sheria ili kutatua changamoto hizo endapo zitabainika kuwepo.

5.6 FUNGU 59 -Tume ya Kurekebisha Sheria

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Tume ya kurekebisha Sheria kuendelea kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kunakuwepo na Mfumo wa Sheria nchini unaozungumza lugha moja (*Uniformity of Law*) na hivyo kuondokana na mgogoro wa kisheria usio wa lazima (*unnecessary Conflict of Law*) unaoweza kujitokeza

wakati wa utekelezaji, kutokana na kazi kubwa ya kurekebisha Sheria mbalimbali iliyotekelizwa na Bunge kwa kipindi cha kuanzia Mwaka 2017 hadi Mwaka 2019.

5.7 FUNGU 41-Wizara ya Katiba na Sheria

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Taasisi zote zilizo chini yake, kuhakikisha inaendelea kutekeleza Mpango wake wa matumizi ya TEHAMA katika utoaji haki nchini pamoja na kusimamia mazingira wezeshi ya utoaji haki. Hatua hiyo, itarahisisha utoaji haki kwa wakati na kwa gharama nafuu na hivyo kuchochea Maendeleo ya nchi. Hii ni pamoja na kuendelea kuimarisha na kusimamia Misingi ya Haki za Binadamu na Utawala Bora mionganoni mwa Taasisi zote za kisheria zinazohusika na utoaji haki nchini kwa manufaa ya Wananchi wote bila kujali hali yao ya kijamili na kiuchumi.

ii) **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa tayari Serikali na Vyombo vyake imeshahamia Dodoma, na kwa kuwa tayari Bunge lako Tukufu limeshatoa Baraka zake kwa kutunga Sheria ya kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi na Serikali yake, Kamati inashauri Wizara ya Katiba na Sheria kusimamia Mpango wa kujenga Jengo la Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania hapa Dodoma kama ilivyoinishwa katika Mpango kazi wa Miaka Mitano wa Mahakama ya Tanzania. Hii ni pamoja na kuendelea kuboresha miundombinu ya utoaji haki kwa Mahakama zote nchini kulingana na Bajeti ya Serikali.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda nikupongeze kwa umahiri wako katika kasi ya kuliendesha Bunge hili kwa Hekima na Weledi Mkubwa katika kuishauri vema Serikali kwa manufaa ya Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mb, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge.

Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge. Wote kwa pamoja tunawaombea afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mhe. Prof. Palamagamba J.A.M Kabudi, (Mb), kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, na tunamshukuru kwa ushirikiano wake kwa Kamati wakati wote alipokuwa Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria, hivyo, tunamtakia utumishi uliotukuka kwa majukumu yake mapya.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mhe. Balozi Dkt. Augustine P. Mahiga, (Mb), kwa kupewa majukumu mapya ya kuwa Waziri wa Katiba na Sheria na pia tuna mshukuru kwa ushirikiano anaoendelea kuutoa kwa Kamati, pamoja na timu yake ya Watendaji Iklongozwa na Katibu Mkuu Prof. Sifuni Mchome, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Amon Mpanju, Watendaji Wakuu na Wataalam wote wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, Kamati inawashukuru kwa ushirikiano wao wakati wa uchambuzi wa Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii itakuwa tayari muda wote kulisaidia Bunge lako Tukufu katika kusimamia Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa ili kuhakikisha Taasisi hizo zinatekeleza Mipango yake ya Maendeleo kwa ufanisi mkubwa kwa mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake. **NAOMBA MAJINA YAO KAMA YALIVYO KATIKA TAARIFA HII YAINGIE KATIKA TAARIFA RASMI ZA BUNGE (HANSARD):-**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb – **Makamu /Mwenyekiti**
3. Mhe.Joseph Kizito Mhagama, Mb-Mjumbe;
4. Mhe. Ally Saleh Ally, Mb - Mjumbe;

5. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe;
6. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe;
8. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb - Mjumbe;
9. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb - Mjumbe;
10. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb - Mjumbe;
11. Mhe. Nimrod Elirehemah Mkono, Mb - Mjumbe;
12. Mhe. Susan Peter Maselle, MB - Mjumbe:-
13. Mhe. Alfredina Apilinary Kahigi, Mb - Mjumbe;
14. Mhe. Latifah Hassan Chande,Mb - Mjumbe;
15. Mhe. Jacqueline Kandidus Ngonyani Msongozi,Mb- Mjumbe;
16. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe;
17. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe;
18. Mhe. Hassan Seleman Kaunje, Mb - Mjumbe;
19. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe;
20. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb - Mjumbe;
21. Mhe. Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Emmanuel A.Mwakasaka, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Dkt.Suzan Alphonce Kolimba, Mb – Mjumbe

Mheshimiwa Spika, mwisho, kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, **Ndg.** **Stephen Kagaigai** kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina L. Sanga, Katibu wa Kamati hii, Ndg. Stanslaus Kagisa, na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Napenda pia kushukuru Watendaji wote wa Kitengo cha Taarifa rasmi za Bunge (*Hansard*) kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake, kwa Mwaka wa

Fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.

MWENYEKITI,

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA

17 APRILI, 2019

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa wasilisho lako kwa iaba ya Kamati ya Katiba na Sheria. Tunaendelea, tunaenda kwenye Mfuko wa Mahakama, taarifa inawasilishwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Mashimba Ndaki, una muda usiozidi dakika 30.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, niwasilishe maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mfuko wa Mahakama – Fungu 40 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti ilikutana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Kaimu Mtendaji Mkuu wa Mahakama ili kujadiliana na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka

wa fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020. Mashauriano haya yaliifanyika kwa mujibu wa kifungu cha 9(c) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze sasa utekelezaji wa majukumu ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Ibara 107A(1) Mahakama imepewa Mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki. Katika kutekeleza jukumu hili Mahakama imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kumaliza mashauri 240,891 kati ya mashauri 309,151 yaliyokuwepo mwaka 2018; na hivyo kubakia na mashauri 68,260 mwaka 2018/2019;

(b) Kuanzishwa na kukamilika kwa mfumo mpya wa usajili wa mashauri (*Judiciary Statistics Dashboard System*) na mfumo huu unawezesha mawasiliano na wadaiwa ambapo wanaweza kupata taarifa za mwenendo wa shauri kwa njia ya ujumbe mfupi (*sms*), hivyo kutohitajika kufika Mahakamani, shauri linapoahirishwa;

(c) Kuanzisha Mahakama inayotembea (*Mobile Court*), ambapo Magari mawili yalinunuliwa na yataanza huduma katika Mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza;

(d) Imekamilisha ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Ilala (Kinyerezi, Bukombe, Chato, Kilwa, Ruangwa na Geita; na Mahakama za mwanzo za Itinje kule Meatu na Mlowa kule Mbozi;

(e) Inategemea kuanza ujenzi wa Mahakama za Mwanzo za Mtae Lushoto, Mkunya Newala Ngerengere, Mlimba na Mang'ula Morogoro; Laela, Mtowisa na Msanzi Sumbawanga, Lugala wa Ludewa na Uyole Mbeya;

(f) Inaendelea na ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi za Manyara, Katavi, Simiyu, Njombe na za

Wilaya za Longido, Kondoa, Kasulu, Kilindi, Sikonge, Rungwe, Bunda, Chunya, Makete na Wanging'ombe.

(g) Inaendelea na ujenzi wa Mahakama Kuu Mkoani Mara na Kigoma ambazo zimefikia asilimia 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, Mahakama inakabiliwa na changamoto zifuatazo katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka 2018/2019:-

(i) Hali mbaya ya miundombinu ya Mahakama kutokana na uchakavu na uhaba wa majengo ya ofisi na makazi;

(ii) Uhaba wa vitendea kazi, hususani kompyuta na magari kwa ajili ya ukaguzi na vifaa vya TEHAMA. Kwa sasa Mahakama za Wilaya zinahitaji magari 36

(iii) Uhaba wa watumishi wenyewe sifa na maadili kwa kada mbalimbali;

(iv) Maslahi yasiyokidhi hali ya utendaji na mazingira ya kazi ukilinganisha na unyeti wa kazi ya utoaji haki; na

(v) Upimaji wa ardhi na upatikanaji wa viwanja kwa ajili ya ujenzi kutokana na mwitikio mdogo wa Halmashauri kutoa viwanja kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nипитie Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Mfuko wa Mahakama – Fungu 40 uliidihi nishowi na Bunge jumla ya kiasi cha Sh.141,584,737,540. Kati ya fedha hizo shilingi 52,754,477,540 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Mahakama; shilingi 1,875,156,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto; shilingi 50,981,382,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 35,973,722,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Katika

fedha za maendeleo, shilingi 15,000,0000,000 ni fedha za ndani na shilingi 20,973,722,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Februari, 2019 Mahakama ilipokea jumla ya shilingi 61,116,574,097 ambazo ni sawa na asilimia 43.17 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2018/2019. Kati ya fedha hizo shilingi 25,490,688,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asimilia 50; shilingi 24,250,999,782 ni kwa ajili ya mishahara ya Mahakama; shilingi 937,876,300 kwa ajili ya Mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto na shilingi 10,437,010,014 ni fedha za maendeleo kati ya hizo shilingi 5,000,000,000 ni fedha za ndani sawa na asilimia 33.33 na shilingi 5,437,010,014 ni fedha za nje sawa na asilimia 25.92 ya bajeti ya maendeleo iliyotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Mahakama katika mwaka wa fedha 2018/2019, ulipanga kukusanya maduhuli ya shilingi 12,328,200,862 ambapo hadi kufikia mwezi Januari, 2019 kiasi kilichokwuwa kimekusanywa ni shilingi 6,696,199,307 ikiwa sawa na asilimia 54 ya lengo la mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti ilifanya mashauriano na Serikali na kukubaliana kiasi cha fedha za maendeleo kwenye Fungu 40 zilizobakia ambazo ni jumla ya shilingi 25,536,711,986 ambapo kati ya fedha hizo shilingi 10,000,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 15,536,711,986 ni fedha za nje zitolewe kabla ya tarehe 30 Juni 2019 ili kukamilisha miradi ya maendeleo hasa ya ujenzi na ukarabati wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie sasa makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Mfuko wa Mahakama umepanga kutekeleza majukumu yake ya kikatiba, kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea na utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu;

(ii) Kuendelea kuboresha mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano (*TEHAMA*) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji wa huduma;

(iii) Kuendelea kuimarisha tija na utendaji kazi unaozingatia matokeo;

(iv) Kuongeza ushirikiano wa wadau wa haki jinai, ili kuhakikisha huduma ya utoaji haki inakuwepo;

(v) Kuimarisha uwezo katika ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama Kuu, Mahakama za Hakimu Mkazi, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo; na

(vi) Kuendelea na kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa Mahakama katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maduhuli, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Mfuko wa Mahakama umepanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha shilingi 12,571,199,235 ikiwa ni ongezeko la shilingi 242,998,373 ikilinganishwa na makadirio ya shilingi 12,328,200,862 kwa mwaka wa 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Mfuko wa Mahakama umepewa ukomo wa jumla ya Sh. 126,162,464,823. Kati ya fedha hizo, shilingi 50,145,969,914 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Mahakama, shilingi 2,377,212,333 ni kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, shilingi 51,481,382,000 ni kwa ajili ya matumizi ya mengineyo (*OC*) na shilingi 22,157,900,576 ni kwa ajili ya maendeleo ambapo kati ya kiasi hicho shilingi 15,000,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 7,157,900,576 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Mfuko huu umepewa kiasi hiki cha fedha, Kamati inaona kuwa ukomo wa bajeti unaowekwa na Serikali kwa Mfuko wa

Mahakama umeendelea kushuka mwaka hadi mwaka na hivyo kusababisha baadhi ya majukumu ya msingi ya Mahakama kushindwa kutekelezwa. Mathalani katika mwaka wa fedha 2019/2020 kushindwa kujenga nyumba ya Jaji Mkuu Dodoma, kuchelewa kuanzisha Mahakama za Wilaya katika wilaya 28 ambazo sasa hazina Mahakama za Wilaya pamoja na kushindwa kulipa gharama za uhamisho wa watumishi, hususan waliokaa katika kituo kimoja cha kazi kwa muda mrefu, pamoja na Mahakimu wanaotakiwa kuhamza kutoka ngazi ya Mahakama za Mwanzo kwenda Mahakama za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona kwamba ukomo wa bajeti unaowekwa na Serikali kwa Mfuko wa Mahakama umekuwa na athari kubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Mfuko. Aidha, mashauriano yamekuwa yakichukua muda mrefu na mwishoni yanakuwa hayana matokeo chanya kutokana na Serikali kutokuwa tayari kuondoa ukomo huo kwenye Fungu husika ili kuongeza fedha pale inapohitajika kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hii, wakati wa mashauriano, Kamati ya Bajeti ililazimika kukubaliana na maombi ya Waziri wa Fedha na Mipango kuwa Mahakama ifanye mabadiliko katika vifungu vyake kwa lengo la kupatikana fedha za kuhudumia Mahakama Kuu za Kanda kutoka kanda 14 hadi 16 baada ya Kanda ya Kigoma na Mara kuongezeka. Hatua hii ilimlazimu Kaimu Mtendaji Mkuu wa Mahakama kubadili kifungu cha Randama, kifungu 2003 Mahakama Kuu Kanda ili kiasi kilichotengwa cha Sh.7,846,271,600 kiweze kuhudumia kanda 16 badala ya 14 kama ilivyokusudiwa hapo awali.

Hivyo, Kamati inaona kuwa suala hili la ukomo wa bajeti lisipopatiwa ufumbuzi wa haraka litaendelea kuminya mawanda ya utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama hasa Fungu hili Namba 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na makubaliano hayo, Kamati iliazimia mambo yafuatayo:-

(i) Serikali ihakikishe inatoa fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya Mahakama Kuu Kanda zinatolewa kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli katika Kanda mpya mbili zilizoongezeka yaani Kanda ya Mahakama Kuu Kigoma na Mara.

(ii) Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe kuwa fedha za Mfuko wa Mahakama kwa ujumla zinatolewa kwa wakati kulingana na mahitaji ya Mfuko, huku ikizingatia maeneo yote ya vipaumbele vya Mfuko kama Mahakama ilivyoomba.

(iii) Taratibu za ndani zifanyike ili kusaidia utendaji wa Mahakama kuendelea kuleta tija na hasa katika kuwahamisha Mahakimu waliokaa muda mrefu katika Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Mwanzo na kuwahamisha katika Mahakama zenye uhitaji za idhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Jedwali hapo Namba 1 Waheshimiwa Wabunge wanaweza kuangalia, lakini niende kwenye Maoni na Ushauri wa Kamati. Maoni na Ushauri wa Kamati yetu, ni kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa, Mahakama ni chombo kinachotenda haki kwa watu wote bila kujali hali ya mtu kijamii au kiuchumi na kwa kuwa, Mahakama inatakiwa kuendesha na kutekeleza shughuli zake kwa uhuru na bila vikwazo kwani ndiyo taswira inayochochea upatikanaji wa haki kwa wananchi.

Aidha, kiasi cha bajeti kinachotengwa kwenye Fungu hili kulingana na ukomo wa bajeti hakitoshelezi mahitaji ya msingi ya Mfuko wa Mahakama na hivyo kupelekea kutotimiza majukumu yake ya utoaji wa haki kikatiba. Mfano, ukiangalia Jedwali Na.1 ambalo sijalisoma, lakini liko kwenye vitabu vyetu, utaona kwamba bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2019/2020 imeshuka kutoka kiasi cha Sh.141,584,737,540 hadi Sh.126,162,464,823 sawa na asilimia 10.9 wakati kwa ujumla Bajeti ya Serikali imeongezeka kwa asilimia 1.9. Hivyo basi, Kamati inaishauri

Serikali kuongeza fedha kwenye Fungu hili pamoja na kuendelea kulitazama Fungu hili kwa jicho la kipekee ili liweze kutekeleza majukumu yake ya msingi na kwa ufanisi.

(ii) Kwa kuwa, tathmini inaonesha kuwa mwenendo wa utolewaji wa fedha za maendeleo siyo wa kuridhisha ambapo kiasi kilichotolewa ni Sh.10,437,010,014 kati ya Sh.35,973,722,000 sawa na asilimia 29 na hivyo kusababisha Mfuko huu kukabiliwa na hali mbaya ya miundombinu ya Mahakama kutokana na uchakavu na uhaba wa majengo ya ofisi na makazi. Na kwa kuwa, bado kuna uhaba wa vitendea kazi, hususan magari kwa ajili ya ukaguzi na vifaa vya TEHAMA na kufanya mahakama kuwa na uhitaji wa magari 36 ya ukaguzi katika Wilaya mbalimbali nchini. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kiasi cha fedha kilichobakia cha Sh.25,536,711,986 kwa ajili matumizi ya miradi ya maendeleo kinatolewa kama zilliyoidhinishwa na Bunge lako ili kusaidia kukamilisha utekelezaji wa majukumu ya Fungu Na.40 pamoja na ukarabati wa baadhi ya Mahakama na nyumba za watumishi.

(iii) Kwa kuwa, Mfuko wa Mahakama unakabiliwa na uhaba wa watumishi wenyе sifa zinazotakiwa katika kada mbalimbali hususan Majaji, Mahakimu na Makarani. Na kwa kuwa, changamoto hii imekuwa ya muda mrefu na kusababisha Mahakama kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaongeza idadi ya watumishi wanaohitajika kwa awamu kwenye kada mbalimbali kulingana na maombi yaliyowasilishwa ili kusaidia kutekeleza majukumu ya Kimahakama. Hatua hii iende sambamba na upatikanaji wa fedha za uhamisho kwa watumishi waliokaa muda mrefu katika kituo kimoja cha kazi pamoja na ulipaji wa madeni ya watumishi na uongezwaji wa mishahara na maslahi ya watumishi ili kuongeza tija katika utendaji kazi.

(iv) Kwa kuwa, Mfuko wa Mahakama kupitia bajeti ya mwaka 2019/2020 unategemea kuanzisha Mahakama Kuu katika kanda ya Kigoma na Mara ili kuondokana na adha kwa wananchi wa mikoa hiyo kufuata

huduma za Mahakama kwa kutembea umbali mrefu. Na kwa kuwa, kutohana na ukomo wa bajeti uliopo Serikali imeshindwa kutenga kiasi cha shilingi bilioni 3.66 kilichoombwa na Mfuko wa Mahakama ili kutekeleza baadhi ya majukumu ya msingi katika mwaka wa fedha 2019/2020. Mathalani, ununuzi wa samani, vitendea kazi kama kompyuta, skana, mashine za kudurufu na gharama za uendeshaji wa Kanda Mpya za Mahakama Kuu Mara na Kigoma. Hivyo basi, Kamati inasisitiza Serikali itenge shilingi bilioni 3.66 katika mwaka wa fedha 2019/2020 ili kutekeleza shughuli zilizokusudiwa. Aidha, Serikali ihakikishe fedha zote za Mfuko wa Mahakama pamoja na kiasi cha Sh.7,846,271,600 kwa ajili ya matumizi ya Kanda 16, zinatolewa zote kwa wakati kama zinavyoombwa ili kusaidia uendeshaji wa Mahakama Kuu katika Kanda zote 16 ikiwa ni pamoja na Kanda mbili zilizoongezeka za Kigoma na Mara.

(v) Kwa kuwa, kati ya Wilaya 139 ni wilaya 27 tu zenye majengo yanayomilikiwa na Mahakama huku Wilaya nyingine 83 zinatumia majengo ya taasisi nyingine na nyumba za watu binafsi na Wilaya 23 zimeendelea kuhudumiwa na Wilaya jirani. Na kwa kuwa, kati ya Kata 3,963 zilizopo nchini ni Kata 960 tu zilizo na Mahakama za Mwanzo na wakati huo zinazotumika ni Kata 834 tu na Mpango Mkakati wa Mahakama ni kujenga Mahakama 100 za Mwanzo. Hivyo basi, Kamati inasisitiza kuwa Serikali ipeleke fedha za maendeleo kulingana na mahitaji kama yalivyokasimiwa kwenye vifungu husika. Hatua hii itawezesha kukamilisha utekelezaji wa Mpango Kazi wa Fungu Na.40 hivyo, kutatta changamoto ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama za Wilaya, Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Mwanzo kwani zote zina umuhimu katika suala la utoaji haki nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuhitimisha kwa kukushukuru wewe, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutuongoza vyama katika mashauriano kati ya Kamati na Serikali. Namshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa

ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, Kamati inamshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Augustine Mahiga, Waziri wa Katiba na Sheria na Ndugu Solanus M. Nyimbi, Kaimu Mtendaji Mkuu wa Mahakama kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya Bajeti ya Mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Mahakama. Naomba wote 26 watambuliwe kama ambavyo wametajwa kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii, pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo, pamoja na Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Ndg. Michael Kadebe, akisaidiana na Ndg. Godfrey Godwin, Ndg. Emmanuel Rhobi, Ndg. Maombi Kakozi na Ndg. Lilian Masabala kwa kuipa ushauri wa kitaalamu Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maeleo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama, Fungu Na.40, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA
MFUKO WA MAHAKAMA (FUNGU 40) KWA MWAKA WA
FEDHA 2018/2019 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 - KAMA
YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba

kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Kaimu Mtendaji Mkuu wa Mahakama ili kujadiliana na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/2020. Mashauriano haya yalifanyika kwa mujibu wa kifungu cha 9(c) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015.

2.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA 2018/19

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara 107(A)(1) Mahakama imepewa mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki. Katika kutekeleza jukumu hili Mahakama imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kumaliza mashauri 240,891 kati ya mashauri 309,151 yaliyokuwepo mwaka 2018; na hivyo kubakia na mashauri 68,260 mwaka 2018/2019;

(b) Kuanzishwa na kukamilika kwa mfumo mpya wa usajili wa mashauri (Judiciary statistics dashboard system) na mfumo huu unawezesha mawasiliano na wadaawa ambapo wanaweza kupata taarifa za mwenendo wa shauri kwa njia ya ujumbe mfupi (sms), hivyo kutohitajika kufika Mahakamani, shauri linapoahirishwa;

(c) Kuanzisha Mahakama inayotembea (mobile court), ambapo Magari mawili yalinunuliwa na yataanza huduma katika Mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza;

(d) Imekamilisha ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Ilala (Kinyerezi, Bukombe, Chato, Kilwa, Ruangwa na Geita;

na Mahakama za mwanzo za Itinje (Meatu) na Mlowo (Mbozi);

(e) Inategemea kuanza ujenzi wa Mahakama za Mwanzo za Mtae (Lushoto), Mkunya (Newala) Ngerengere, Mlimba na Mang'ula (Morogoro; Laela, Mtowisa na Msanzi (Sumbawanga), Lugalawa (Ludewa) na Uyole (Mbeya);

(f) inaendelea na ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi za Manyara, Katavi, Simiyu, Njombe, na za Wilaya za Longido, Kondoa, Kasulu, Kilindi, Sikonge, Rungwe, Bunda, Chunya, Makete na Wanging'ombe.

(g) Inaendelea na ujenzi wa Mahakama Kuu Mkoani Mara na Kigoma ambazo zimefikia asilimia 80.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Mahakama inakabiliwa na changamoto zifuatazo katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka 2018/2019:-:-

(i) Hali mbaya ya miundombinu ya Mahakama kutokana na uchakavu na uhaba wa majengo ya ofisi na makazi;

(ii) Uhaba wa vitendea kazi, hususan kompyuta na magari kwa ajili ya ukaguzi na vifaa vya TEHAMA. Kwa sasa Mahakama za Wilaya zinahitaji magari 36;

(iii) Uhaba wa watumishi wenyе sifa na maadili kwa kada mbalimbali;

(iv) Maslahi yasiyokidhi hali ya utendaji na mazingira ya kazi ukilinganisha na unyeti wa kazi ya utoaji haki; na

(v) Upimaji wa ardhi na upatikanaji wa viwanja kwa ajili ya ujenzi kutokana na mwitikio mdogo wa Halmashauri kutoa viwanja kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama;

3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Mfuko wa Mahakama – **Fungu 40** uliidhinishwa na Bunge jumla ya kiasi cha **Sh. 141,584,737,540**. Kati ya fedha hizo **Sh. 52,754,477,540** ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi wa Mahakama (PE), **Sh. 1,875,156,000** ni kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, **Sh. 50,981,382,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), na **Sh. 35,973,722,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika fedha za Maendeleo, **Sh. 15,000,0000,000** ni fedha za ndani na **Sh. 20,973,722,000** ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Februari, 2019 Mahakama ilipokea jumla ya **Sh. 61,116,574,097** ambazo ni sawa na **asilimia 43.17** ya fedha zilizoldhinishwa na Bunge kwa mwaka 2018/2019. Kati ya fedha hizo **Sh. 25,490,688,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo sawa na **asimilia 50**, **Sh. 24,250,999,782** kwa ajili ya mishahara ya Mahakama, **Sh. 937,876,300** kwa ajili ya Mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto na **Sh. 10,437,010,014** ni fedha za maendeleo kati ya hizo **Sh. 5,000,000,000** ni fedha za ndani sawa na **asilimia 33.33** na **Sh. 5,437,010,014** ni fedha za nje sawa na **asilimia 25.92** ya bajeti ya maendeleo iliyotengwa.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mahakama katika mwaka wa fedha 2018/2019 ulipanga kukusanya maduhuli ya **Sh. 12,328,200,862** ambapo hadi kufikia mwezi Januari, 2019 kiasi kilichokuwa kimekusanya ni **Sh. 6,696,199,307** ikiwa sawa na **asilimia 54** ya lengo la mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti ilifanya mashauriano na Serikali na kukubaliana kiasi cha fedha za maendeleo kwenye fungu 40 zilizobakia ambazo ni jumla ya **Sh. 25,536,711,986** ambapo kati ya fedha hizo **Sh. 10,000,000,000** ni fedha za ndani na **Sh. 15,536,711,986** ni fedha za nje zitolewe kabla ya tarehe 30 Juni 2019 ili kukamilisha miradi ya maendeleo hasa ya ujenzi na ukarabati wa Mahakama.

4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa Fedha 2019/2020, Mfuko wa Mahakama umepanga kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba kama yafuatayo:-

- a) Kuendelea na utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu;
- b) Kuendelea kuboresha mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji wa huduma;
- c) Kuendelea kuimarisha tija na utendaji kazi unaozingatia matokeo;
- d) Kuongeza ushirikiano wa wadau wa haki jinai ili kuharakisha huduma ya utoaji haki;
- e) Kuimarisha uwezo katika ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama Kuu, Mahakama za Hakimu Mkazi, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo; na
- f) Kuendelea na kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa Mahakama katika ngazi mbalimbali.

4.1 Maduhuli

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Mfuko wa Mahakama umepanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha **Sh. 12,571,199,235** ikiwa ni ongezeko la **Sh. 242,998,373** ikilinganishwa na makadirio ya **Sh.12,328,200,862** mwaka 2018/2019.

4.2 Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Mfuko wa Mahakama umepewa ukomo wa jumla ya **Sh. 126,162,464,823**. Kati ya fedha hizo; **Sh. 50,145,969,914** ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi wa Mahakama, **Sh. 2,377,212,333** ni kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Uongozi

wa Mahakama Lushoto, **Sh. 51,481,382,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Mengineyo (OC) na **Sh. 22,157,900,576** ni kwa ajili ya maendeleo ambapo kati ya kiasi hicho **Sh. 15,000,000,000** ni fedha za ndani na **Sh. 7,157,900,576** ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Mfuko huu umepewaa kiasi hiki cha fedha, Kamati inaona kuwa Ukomu wa Bajeti unaowekwa na Serikali kwa Mfuko wa Mahakama umeendelea kushuka mwaka hadi mwaka na hivyo kusababisha baadhi ya majukumu ya msingi ya Mahakama kushindwa kutekelezwa, mathalani katika mwaka wa fedha 2019/2020 kushindwa kujenga nyumba ya Jaji Mkuu Dodoma, kuchelewa kuanzisha Mahakama za Wilaya katika Wilaya 28 ambazo sasa hazina Mahakama za Wilaya pamoja na kushindwa kulipa gharama za uhamisho wa watumishi, hususan waliocaa katika kituo kimoja cha kazi kwa muda mrefu, pamoja na Mahakimu wanaotakiwa kuhama kutoka ngazi ya Mahakama za Mwanzo kwenda Mahakama za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kwamba, ukomo wa bajeti unaowekwa na Serikali kwa Mfuko wa Mahakama umekuwa na athari kubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Mfuko. Aidha, mashauriano yamekuwa yakichukua muda mrefu na mwishoni yanakuwa hayana matokeo chanya kutokana na Serikali kutokuwa tayari kuondoa ukomo huo kwenye fungu husika ili kuongeza fedha pale inapohitajika kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hii, wakati wa mashauriano, Kamati ya Bajeti ililazimika kukubaliana na maombi ya Waziri wa Fedha na Mipango kuwa Mahakama ifanye mabadiliko katika vifungu vyake kwa lengo la kupatikana fedha za kuhudumia Mahakama Kuu za Kanda kutoka kanda 14 hadi 16 baada ya Kanda ya Kigoma na Mara kuongezeka. Hatua hii ilimlazimu Kaimu Mtendaji Mkuu wa Mahakama kubadili kifungu cha Randama (kifungu 2003 Mahakama Kuu Kanda) ili kiasi kilichotengwa cha **Sh. 7,846,271,600** kiweze kuhudumia kanda 16 badala ya 14 kama

ilivyokusudiwa hapo awali. Hivyo, Kamati inaona kuwa suala hili la ukomo wa bajeti lisipopatiwa ufumbuzi wa haraka litaendelea kuminya mawanda ya utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama (Fungi – 40).

Mheshimiwa Spika, pamoja na makubaliano hayo Kamati iliazimia yafuatayo:-

i. Serikali ihakikishe inatoa fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya Mahakama Kuu Kanda zinatolewa kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli katika Kanda mpya mbili zilizoongezeka yaan Kanda ya Mahakama Kuu Kigoma na Mara;

ii. Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe kuwa fedha za Mfuko wa Mahakama kwa ujumla zinatolewa kwa wakati kulingana na mahitaji ya Mfuko, huku ikizingatia maeneo yote ya vipaumbele vya Mfuko kama Mahakama ilivyoomba;

iii. Taratibu za ndani zifanyike ili kusaidia utendaji wa Mahakama kuendelea kuleta tija na hasa katika kuwahamisha Mahakimu waliokaa muda mrefu katika Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Mwanzo na kuwahamishia katika Mahakama zenye uhitaji.

Jedwali 1: Mchanganuo wa Makisio ya Bajeti kwa mwaka 2019/2020

NA.	MAELEZO	BAJETI YA MWAKA 2018/2019	MAKISIO YA BAJETI 2019/2020	ASILIMIA
1.	Mishahara	52,754,477,540	50,145,969,914	(4.94)
2.	Mishahara – IJA	1,875,156,000	2,377,212,333	26.77
3.	Matumizi Mengineyo (OC)	50,981,382,000	51,481,382,000	0.98
	Matumizi Ya Maendeleo	35,973,721,700	22,157,900,576	(38.41)
4.	Fedha za Ndani	15,000,000,000	15,000,000,000	0
5.	Fedha za Nje	20,973,721,700	7,157,900,576	(65.87)
	Jumla ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo	141,584,737,540	126,162,464,823	(10.89)

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

5.1 Kwa kuwa, Mahakama ni chombo kinachotenda haki kwa watu wote bila kujali hali ya mtu kijamii au kiuchumi;

Na kwa kuwa, Mahakama inatakiwa kuendesha na kutekeleza shughuli zake kwa uhuru na bila vikwazo kwani ndiyo taswira inayochochea upatikanaji wa haki kwa wananchi. Aidha, kiasi cha bajeti kinachotengwa kwenye fungu hili kulingana na ukomo wa bajeti hakitoshelezi mahitaji ya msingi ya Mfuko wa Mahakama na hivyo kupelekea kutotimiza majukumu yake ya utoaji wa haki kikatiba. **Mfano, ukiangalia** jedwali Na. 1 utaona kwamba bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2019/2020 imeshuka kutoka kiasi cha **Shilingi 141,584,737,540 hadi Shilingi 126,162,464,823** sawa na **(asilimia 10.9)** wakati kwa ujumla Bajeti ya Serikali imeongezeka kwa asilimia 1.9.

Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuongeza fedha kwenye fungu hili pamoja na kuendelea kulitazama Fungu hili kwa jicho la kipekee ili liweze kutekeleza majukumu yake ya msingi na kwa ufanisi.

5.2 Kwa kuwa, tathmini inaonesha kuwa mwenendo wa utolewaji wa fedha za maendeleo sio wa kuridhisha ambapo kiasi kilichotolewa ni **Shilingi 10,437,010,014** katika **Shilingi 35,973,722,000** sawa na **(asilimia 29)** na hivyo kusababisha Mfuko huu kukabiliwa na hali mbaya ya miundombinu ya Mahakama kutokana na uchakavu na uhaba wa majengo ya ofisi na makazi;

Na kwa kuwa, bado kuna uhaba wa vitendea kazi, hususan magari kwa ajili ya ukaguzi na vifaa vya TEHAMA na kuifanya mahakama kuwa na uhitaji wa magari 36 ya ukaguzi katika Wilaya mbalimbali nchini;

Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kiasi cha fedha kilichobakia cha **Sh. 25,536,711,986** kwa ajili matumizi ya miradi ya maendeleo kinatolewa kama

zilivyoidhinishwa na Bunge ili kusaidia kukamilisha utekelezaji wa majukumu ya Fungu 40 pamoja na ukarabati wa baadhi ya Mahakama na nyumba za watumishi.

5.3 Kwa kuwa, Mfuko wa Mahakama unakabiliwa na uhaba wa watumishi wenye sifa zinazotakiwa katika kada mbalimbali hususan Majaji, Mahakimu na Makarani;

Na kwa kuwa, changamoto hii imekuwa ya muda mrefu na kusababisha Mahakama kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaongeza idadi ya watumishi wanaohitajika kwa awamu kwenye kada mbalimbali kulingana na maombi yaliyowasilihwa ili kusaidia kutekeleza majukumu ya Mahakama. Hatua hii iende sambamba na upatikanaji wa fedha za uhamisho kwa watumishi waliokaa muda mrefu katika kituo kimoja cha kazi pamoja na ulipaji wa madeni ya watumishi na uongezwaji wa mishahara na maslahi ya watumishi ili kuongeza tija katika utendaji kazi.

5.4 Kwa kuwa, Mfuko wa Mahakama kuitia bajeti ya mwaka 2019/20 unategemea kuanzisha Mahakama Kuu katika kanda ya Kigoma na Mara ili kuondokana na adha kwa wananchi wa mikoa hiyo kufuata huduma za Mahakama kwa kutembea umbali mrefu;

Na kwa kuwa, kutohana na ukomo wa bajeti uliopo Serikali imeshindwa kutenga kiasi cha shilingi **bilioni 3.66** kilichoombwa na Mfuko wa Mahakama ili kutekeleza baadhi ya majukumu ya msingi katika mwaka wa fedha 2019/2020. Mathalani, ununuzi wa samani, vitendea kazi kama kompyuta, skana, mashine za kurudifu, na gharama za uendeshaji wa Kanda Mpya za Mahakama Kuu Mara na Kigoma.

Hivyo basi, Kamati inasisitiza Serikali itenye **Sh. bilioni 3.66** katika mwaka wa fedha 2019/2020 ili kutekeleza shughuli zilizokusudiwa. Aidha, Serikali ihakikishe fedha zote za mfuko

wa Mahakama pamoja na kiasi cha **Sh. 7,846,271,600** kwa ajili ya matumizi ya Kanda 16, zinatolewa zote kwa wakati kama zinavyoombwa ili kusaidia uendeshaji wa Mahakama Kuu katika Kanda zote 16 ikiwa ni pamoja na Kanda mpya za Kigoma na Mara.

5.5 Kwa kuwa, kati ya Wilaya 139 ni wilaya 27 tu zenyе majengo yanayomilikiwa na Mahakama huku Wilaya nyingine 83 zinatumia Majengo ya Taasisi nyingine na Nyumba za watu binafsi na Wilaya 23 zimeendelea kuhudumiwa na Wilaya jirani;

Na kwa kuwa, kati ya Kata 3,963 zilizopo nchini ni Kata 960 tu zilizo na Mahakama za Mwanzo na wakati huo zinazotumika ni Kata 834 tu na Mpango mkakati wa Mahakama ni kujenga Mahakama 100 za Mwanzo;

Hivyo basi, Kamati inasisitiza kuwa Serikali ipeleke fedha za maendeleo kulingana na mahitaji kama yalivyokasmiwa kwenye vifungu husika. Hatua hii itawezesha kukamilisha utekelezaji wa Mpango kazi wa Fungu 40 na hivyo kutatua changamoto ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama za Wilaya, Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Mwanzo kwani zote zina umuhimu katika suala la utoaji haki nchini.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Namshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt Ashatu Kijaji (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, Kamati inamshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Augustine Mahiga, (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria na Ndg. Solanus M. Nyimbi Kaimu Mtendaji Mkuu wa Mahakama kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya Bajeti ya Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Mahakama. Naomba kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo;

- 1) Mhe. George Boniface Simbachawene, Mb – Mwenyekiti
- 2) Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb - M/ Mwenyekiti
- 3) Mhe. David Ernest Silinde, Mb
- 4) Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
- 5) Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
- 6) Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibajuka, Mb
- 7) Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb
- 8) Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb
- 9) Mhe. Abdallah Majura Bulembo, Mb
- 10) Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
- 11) Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb
- 12) Mhe. Dkt. Balozi Diodorus Buberwa Kamala , Mb
- 13) Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb
- 14) Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
- 15) Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
- 16) Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
- 17) Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb
- 18) Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
- 19) Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
- 20) Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
- 21) Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
- 22) Mhe. Stephen Julius Masele, Mb
- 23) Mhe. Andrew John Chenge, Mb
- 24) Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq, Mb
- 25) Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
- 26) Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo, pamoja na Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Ndg. Michael Kadebe, akisaidiana na Ndg. Godfrey Godwin, Ndg. Emmanuel Rhobi, Ndg. Maombi Kakozi na Ndg. Lilian

Masabala kwa kuipa ushauri wa kitaalamu Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama – Fungu 40, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama yalivowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

George B. Simbachawene, Mb

MWENYEKITI

KAMATI YA BUNGE YA BAJETI

17 Aprili, 2019

MWENYEKITI: Ahsante Makamu wa Mwenyekiti kwa wasilisho kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Tunaendelea na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Mheshimiwa Salome Makamba. Naomba uzingatие yale maelekezo niliyokupatia. (*Makofi/Kicheko*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MWENYEKITI: Mnacheka nini sasa?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MHE. SALOME W. MAKAMBA K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimia Mwenyekiti, ifuatayo ni hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Tundu Antipas Lissu, katika Wizara ya Katiba na Sheria, kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu taarifa hii ni ndefu, ningeomba yote iingie kwenye *Hansard* kama ilivyoandikwa.

MWENYEKITI: Isipokuwa yale maeneo ambayo nimeelekeza yasiingizwe. (*Makofii*)

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, nitafuta kadiri unavyoona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Msemadi Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Lissu, napenda kuwasilisha maoni ya kambi rasmi kuhusu utekelezaji wa Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijawasilisha maoni haya, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa rehema, kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili kuwasilisha maoni haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya CHADEMA kutoa pole kwa Watanzania wote wanaokumbana na madhila ya uvunjifu wa haki za binadamu, huku nikiwashukuru na kuwapongeza Watanzania wote ambaao ni waumini wa utawala wa sheria hapa nchini. Aidha, kipekee kabisa niwape pole viongozi wakuu wa CHADEMA kwa kesi lukuki za kila aina na dalili za uonevu zinazowaandama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upekee napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa viongozi wote wa Kanda hadi Msingi hasa katika Mikoa ya Kanda za Serengeti na wanawake wote wa Mkoa wa Shinyanga kwa kuniamini na ukomavu wao katika kutambua haki zao za msingi katika kutekeleza majukumu yao ya kisiasa licha ya vitisho vingi wanavyokumbana navyo kutoka kwa watendaji wanaolipwa na kodi za wananchi. Naomba niendelee kuwatia moyo

kwamba Tanzania inapitia katika kipindi cha mpito kuelekea katika demokrasia ya kweli, japo tunarudi nyuma, uvumilivu ni muhimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, naishukuru familia yangu kwa kunivumilia na kunipa moyo katika majukumu yangu haya ya kibunge na kisasa. Nasema ahsante sana, mmekuwa nguvu yangu, Mwenyezi Mungu awabariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kuwa nasoma hotuba ya Kambi...

MWENYEKITI: Hapana, tuachane na hiyo, twende *paragraph* ya 6.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ndiyo tunashauri Serikali, sisi ndiyo Serikali mbadala, nani amefuta?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salome, tusibishane. Nasema hivi, futa hiyo *paragraph* ya tano usiisome nenda ya sita haraka.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunachokifanya hakisaiddii Taifa letu. Niende *paragraph* ya ngapi?

MWENYEKITI: Ya sita.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria ndiyo yenyeye jukumu la kuhakikisha kuwa nchi hii inaongozwa kwa kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa na vyombo halali vya maamuzi. Aidha, majukumu mengine ya Wizara hii yameainishwa katika Hati ya Mgawanyo wa Majukumu ya Mawaziri. Miiongoni mwa

majukumu hayo ni pamoja na kushughulikia masuala ya kikatiba, kusimamia mfumo wa haki na utoaji haki nchini, uandishi wa sheria, kuendesha mashtaka ya jinai, kushughulikia uendeshaji wa mashauri ya madai na mikataba mbalimbali inayohusu Serikali na utaratibu wa sheria za kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii itajikita katika kuangazia, je, ni kweli Wizara ya Katiba na Sheria inatekeleza majukumu hayo na kuhakikisha nchi inaongozwa kwa kuzingatia Katiba, sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na vyombo mbalimbali nya maamuzi? Katika kufanya hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeonesha kwa kiwango gani majukumu haya yametekelawa au kutotekelawa, madhara na faida kama zipo na kuishauri Serikali hatua muhimu za kuchukua kulingana na eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, pamoja na mapungufu yake, ndiyo sheria mama ambayo Watanzania wamekubaliana kwa pamoja na misingi ya kuongoza nchi yao ambayo itazingatia uhuru, haki, udugu na amani. Wamesisitiza katika Katiba hiyo kuwa nchi yao itakuwa ya kidemokrasia kwa kusimamiwa na Bunge lenye wajumbe waliochaguliwa na linalowawakilisha wananchi. Pia nchi yao itakuwa yenye Mahakama huru zinazotekeliza wajibu wa kutoa haki bila uoga wala upendeleo wowote na hivyo kuhakikisha kwamba haki za binadamu zinadumishwa na kulindwa na wajibu wa kila mtu unatekelezwa kwa uaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja...

MWENYEKITI: Hapana. Twende...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niende wapi? Naomba uniongoze tafadhali.

MWENYEKITI: *Paragraph ya kumi. (Kicheko/Makofii)*

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inathibitishwa na kauli ya Mheshimiwa Rais kuwa hajawahi kuahidi kuhusu Katiba Mpya wala haikuwa sehemu ya ahadi zake za kampeni; kauli inayokinzana na llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ambapo katika ukurasa wake wa 206 - 207, kipengele cha 145(g) inasema; "Ili kuendeleza utawala bora, demokrasia na uwajibikaji katika kipindi cha miaka mitano ijayo yaani 2015 – 2020, CCM itahakikisha kuwa Serikali itatekeleza yafuatayo:-

Kukamilisha mchakato wa kutunga Katiba mpya na kuanza kuitekeleza kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya kiongozi wa nchi ndio dira na mtizamo wa Serikali anayoiongoza. Hivyo basi, kuweka pembeni mchakato wa Katiba mpya ni kufifisha ndoto za Watanzania walizokuvanazo baada ya kutoa maoni katika Tume ya Warioba, jambo linaloua ustawi na dira ya nchi kiuchumi, siasa na kijamii. (*Makofii*)

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kurejesha haraka mchakato wa Katiba mpya ambayo ndio matumaini ya Watanzania kama ilivyoahidi katika ilani yake ya uchaguzi ya 2015 - 2020. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitendo vinavyoashiria ukiukwaji na mgogoro wa Katiba; yafuatayo ni baadhi tu ya maeneo ambayo kutokana na matendo, kauli, matamko na sheria mbalimbali, nchi yetu imejiingiza katika mgogoro mkubwa wa Kikatiba na hatimaye kuwa

moja ya jambo linalozorotesha utawala bora, uchumi wa nchi na kushusha morali ya utendaji kazi kwa taasisi mbalimbali za Umma na sekta binafsi kwa ujumla wake...

MWENYEKITI: Haya twende.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi majuzi...

MWENYEKITI: Ibara ya 15.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, umefuta vipengele vinavyoshauri kuhusu mgogoro wa Spika na CAG. Jambo hili ni la muhimu sana kwa mustakabali wa Taifa letu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salome, Ibara ya 15.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nyakati mbalimbali Bunge lako Tukufu limetunga sheria ambazo katika utekelezwaji wake zinakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baadhi ya sheria na kanuni ambazo zinakiuka matakwa ya katiba ni pamoja na hizi zifuatazo:-

Sheria ya Makosa ya Mtandao. Mapema mwezi Aprili, 2015 Bunge lako lilipitisha sheria hii ambayo badala ya kuwa msaada kwa Watanzania imegeuka na kuwa fimbo ya watawala dhidi ya wananchi. Sheria hii imewapa mamlaka Jeshi la Polisi kuingia eneo lolote na kuchukua vifaa vyovyote vya kimawasiliano, eti wanapoamini kwamba vifaa hivyo vitatumika kama ushahidi dhidi ya kosa linalohisiwa kutendeka.

Hata hivyo, kifungu cha 16 cha sheria hii kinakiuka misingi ya Kimataifa ya uhuru wa kujieleza (*international standard of freedom of expression*). Kifungu hiki siyo tu kinaleta

usumbufu kwa wananchi, lakini pia ni vigumu kuthibitisha kosa Mahakamani kwa kutumia kifungu hiki. Pia ipo kesi ya kikatiba Mahakama Kuu ambayo inapinga sheria hii ambayo inakwenda kinyume na Katiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mitandao inakiuka tangazo la Umoja wa Mataifa kuhusu haki za binadamu, Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za Kijamii na Kisiasa. Pia Sheria hii haitambui haki ya faragha na ya usalama wa mtu kama inavyotajwa na Ibara ya 16 ya Katiba. Sheria hii inaminya uhuru wa kutoa maoni ambao uko katika Ibara ya 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba sheria zetu lazima zilenge kuisaidia jamii ya Watanzania kuliko dhamira ya kuwakomoa na kuwanyanyasa wananchi. Katika muktadha huo, sheria hili ni mionganoni mwa sheria ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuleta mabadiliko ya sheria ili kuweza kupata ufumbuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Takwimu (*Statistics Act, 2015*). Hii ni mionganoni mwa sheria ambazo zinaweka adhabu kubwa kwa wakosaji na ni mionganoni mwa sheria kandamizi ambazo zinatakiwa kufanyiwa marekebisho makubwa.

Aidha, katika dunia ya sasa hivi ambayo inategemea matokeo ya tafiti mbalimbali haiwezekani Taifa likawa na chanzo kimoja cha takwimu. Serikali kuititia sheria hii inajiwakea mazingira ya kutopingwa kwa takwimu zake hata kama takwimu hizo zinapotosha Umma. Ni maoni yetu kwamba sheria hii kandamizi ifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria nyingine ni *Media Service Act, 2016*. Sheria hii pia ni moja kati ya sheria ambazo iliridhiwa siku 11 tu baada ya kupitishwa na Bunge hili ikasainiwa na Mheshimiwa Rais. Waziri mwenye dhamana amepewa mamlaka makubwa sana na yanatumika kukandamiza vyombo vyahabari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 59 kimekuwa kikitumiwa vibaya na Waziri mwenye dhamana kufungia vyombo vya habari hasa magazeti. Baadhi ya magazeti kama Gazeti la Mawio, Tanzania Daima na Raia Mwema na Mwanahalisi yalifungiwa chini ya kifungu cha 59 cha sheria hii. Ubatili wa sheria hii unatokana na hukumu ya Mahakama ya Afrika Mashariki ambayo ilikubaliana na walalamikaji katika shitaka Na. 2/2017 kati ya Baraza la Habari Tanzania (*MCT*), Kituo cha Msaada wa Sheria na Haki za Binadamu na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali sasa kuleta marekebisho ya sheria hii kwa sababu sheria imetangaza kukiuka misingi ya Katiba ya nchi na utawala bora ambayo Tanzania imeridhia katika Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyingine ni Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa (*Access to Information Act*). Sheria hii ambayo inatumika Tanzania Bara peke yake ina baadhi ya vifungu ambavyo vinakiuka haki ya kupata taarifa kama ilivyoainishwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na mikataba mbalimbali ya Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii pia imeshindwa kuzingatia kwa kiwango kikubwa cha matakwa ya Sera ya Taarifa na Utangazaji ya mwaka 2003 ambayo inataka kusiwepo na vizuizi vya kupata habari. Sheria hii kama zilivyo kwa sheria mbili tajwa hapo juu, inabakia kuwa tishio kwa watumiaji wa mitandao hapa nchini, zikiwemo television za mitandaoni, (*online tv*) na *Blogers*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa ripoti ya CIPESA (2015) kuhusu uhuru wa matumizi ya mtandao Tanzania, Tanzania inatajwa kama Taifa ambalo Serikali yake imetunga sheria za kuminya matumizi ya mitandao na kudidimiza uhuru wa kujieleza mitandaoni. Ni kwa mantiki hii Kambi Rasmi Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuleta

marekebisho ya sheria hii ili kuondoa changamoto ambazo zimekuwa zikiwakumba watumiaji wa mitandao ya kijamii hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Kielektroniki na Mawasiliano ya Posta imeanzishwa kwa kanuni za maudhui ya Kimtandao zinazojulikana kama *Online Content Regulations* za mwaka 2018. Taarifa ya Wachambuzi wa Masuala ya Kimtandao (*Analysis of the Tanzania Content Regulations*)” inaonesha kwamba kanuni hizo ni mbaya na ni rungu dhidi ya uhuru wa kujieleza ambao unalindwa chini ya Katiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria nyingine ni Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971. Sheria hii imekuwa kandamizi na kichocheo cha janga kubwa la ndoa za utotoni. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, tunapongeza uamuzi wa Mahakama Kuu kubatilisha kifungu kilichokuwa kinaruhusu wasichana kuolewa kuanzia miaka 15. Hata hivyo, Serikali haikuridhishwa na maamuzi hayo ya busara na kuamua kukata rufaa ambapo tunaona hila ya wazi ya Serikali na Mahakama kuchelewesha rufaa hiyo, kwani tangu 2017 kesi hii hajatajwa kwa ajili ya kusikilizwa wala kufanyiwa maamuzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaanmini kwamba sheria hizi ni kandamizi na inaitaka Serikali kuleta ndani ya Bunge lako Tukufu Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, kufanya marekebisho Sheria za Makosa ya Kimtandao, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, Sheria ya Takwimu ya mwaka 2015, Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari na sheria zote kandamizi ambapo wadau mbalimbali wa sheria wamekuwa wakizipigia chapuo kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka pia Serikali kuleta marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (*The Criminal Procedure Act*) na sheria zote zinazohusu taratibu za kesi mbalimbali ili kuondoa tatizo la watuhumiwa kukaa rumande kwa miaka mingi kwa kisingizio cha kutokamilika kwa upelelezi. (*Makofii*)

Aidha, wapo baadhi ya watuhumiwa ambao wako mahabusu kwa miaka mingi kwa sababu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kila mara wanadai Mahakamani kwamba upelelezi haujakamilika. Kitendo hiki ni kutowatendea haki watuhumiwa na dhana nzima ya utuhumiwa kwa kuwa bado hawajahukumiwa. Sheria kama za utakatishaji wa fedha na Sheria ya Uhujumu Uchumi zimekuwa kichaka kwa ajili ya kukandamiza watuhumiwa na chanzo cha mapato ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Utumishi wa Mahakama imeundwa kwa mujibu wa Ibara ya 112 (1) ya Katiba yetu pamoja na Sheria ya Uendeshwaji wa Mahakama, Sheria Na. 4 ya mwaka 2011. Miiongoni mwa majukumu ya Tume ni pamoja na kumshauri Mheshimiwa Rais kuhusu uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu, kupandisha cheo na kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya watumishi ambao ni mamlaka ya Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupandishwa vyeo kwa watumishi. Taarifa ya utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria wakati wa kujadili Mpango na Mkadirio ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019, inaonesha Tume ya Utumishi wa Mahakama imepandisha vyeo watumishi katika namna ambayo inaacha maswali mengi yanayohitaji ufanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, watumishi 255 katika mwaka wa fedha 2014/2015 walipandishwa vyeo na inaonekana majina yao yaliingizwa katika mfumo wa *HCMIS* lakini watumishi hao hawakurekebishiwa mishahara yao na katika hali ya kustaajabisha Serikali imeelekeza barua zao zifutwe na badala yake zianzie tarehe 1/11/2017. Kitendo hiki ni batili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuwalipa watumishi wote madai yao ya miaka miwili, watumishi 255.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uteuzi wa Waheshimiwa Majaji; kwa mujibu lbara ya 113(1) ya Katiba, majukumu ya Tume yatakuwa ni kumshauri Rais kuhusu uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu. Pamoja na mambo mengine, uteuzi wa Waheshimiwa Majaji unatarajiwaka kuzingatia uwezo wa mteuliwa na historia ya utumishi uliotukuka. Kwa bahati mbaya zaidi, zipo teuzi ambazo zimekuwa zikifanyika na kuacha maswali mengi juu wa weledi wa kitaalam wa mteuliwa kama ulizingatiwa na au uteuzi ulichochewa na sababu nyiningine.

MWENYEKITI: Twende *paragraph* ya 32. (*Kicheko/Makofij*)

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ofisi ya Taifa ya Mashitaka; Mheshimiwa Rais wa Jamhuri mapema mwezi Februari, 2018, alifanya mabadiliko ya kimundo katika ya mashitaka ili kuboresha ufanisi. Aidha, Sheria ya Huduma ya Mashitaka ya 2018 kifungu cha 16(1) - (3) kinaleza majukumu ya Mkurugenzi wa Mashitaka kuwa ni pamoja na kuratibu shughuli za upelelezi wa vyombo vya uchunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi wa mashitaka anaweza kutoa maelekezo kwa chombo chunguzi chochote kufanya kufanya upelelezi kuhusu jambo lolote analolisikia au pale kunapokuwepo na malalamiko kwa lengo la kuhakikisha upelelezi unafanyika kwa kina ili kurahisisha utoaji wa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupewa mamlaka hayo yote, Ofisi ya Taifa ya Mashitaka imeshindwa kutekeleza majukumu yake ama kwa makusudi au kutokana na sababu ambazo huenda zinajulikana kwa Mkurugenzi wa Mashitaka mwenyewe, katika kufuatilia matukio makubwa na ya kutisha yanayolitia doa Taifa letu ndani na nje ya nchi.

MWENYEKITI: Haya, twende lbara ya 35, soma iliyopo kwenye taarifa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, unataka nisome ukurasa wa ngapi?

MWENYEKITI: *Paragraph 35.*

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hutaki nizungumzie upotevu wa watu na watu kupigwa risasi.

MWENYEKITI: Nasema hivi, tusibishane sasa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *licha ya kwamba kifungu cha 16 cha Sheria ya Huduma ya Mashitaka kinaeleza wazi kuwa Mkurugenzi wa Mashikata anaweza kutoa maelekezo kwa chombo chocohote kufanya upeletezi kuhusu jambo lolote analosikia au pale kunapokuwepo na malalamiko, lakini Mkurugenzi huyu amekuwa akikaa kimya na kutochukua hatua yoyote licha ya malalamiko mengi yanayotolewa na wananchi juu uhalifu ambao unataka kufanywa dhidi yao.*

MWENYEKITI: *Haya twende 17.*

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *this is unfair.*

MWENYEKITI: 17.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: *It is very unfair.*

MWENYEKITI: *Please.*

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:
Mheshimiwa Mwenyekiti...

MBUNGE FULANI: Hitimisha sasa.

MWENYEKITI: Hitimisha hoja yako basi. (*Kicheko*)

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama ingekuwa ni kuku kapigwa risasi, mwenye kuku lazima angechachamaa na kutafuta haki yake, lakini kwa Tanzania Mbunge, Mheshimiwa Tundu Lissu anapigwa risasi, Mkuu wa Mkoa wa Mara anatishiwa kupigwa risasi na polisi; aliyekuwa Waziri wa Habari, Mheshimiwa Nape Nnauye, naye akatishiwa kupigwa bastola, lakini hakuna hatua yoyote ya dhati iliyochukuliwa na Serikali wala tamko lolote. Mambo ya namna hii yanaweza kutokea Tanzania tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko ya Mheshimiwa Tundu Lissu peke yake yalitosha kumwezesha Mkurugenzi wa Mashitaka kuanzisha uchunguzi chini ya Kifungu cha 16 cha Sheria ya Huduma ya Mashitaka na pia angeweza yeye mwenyewe kushiriki kuongoza au kusimamia zoezi la upelegelezi huo lakini hakufanya hata kimojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutohana na mazingira kama hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Mkurugenzi wa Mashitaka ajitafakari kama anatosha kukalia kiti hicho. Aidha, tunataka mamlaka yake ya uteuzi itengue uteuzi wake kwani kwa kutochukua hatua kumeifanya Tanzania ionekane siyo sehemu salama ya kuishi kutohana na kukithiri kwa matukio haya ya utekaji na viongozi kupigwa risasi kizembe na hadharani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania. Tume hii imeanzishwa kwa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria na kufanyiwa marekebiso na Sheria Na. 2 ya mwaka 2018. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 4(1), (2)

na (3) pamoja na marekebisho yake, majukumu ya tume hii ni pamoja na kuchunguza sheria yoyote kwa lengo la kuendeleza, kuiboresha, kupendekeza hatua muhimu za kufanya ili sheria iendane na mazingira ya sasa ya Tanzania na kuondoa kasoro au kufuta sheria zilizopitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tunayo tume ambayo majukumu yake yameainishwa kisheria lakini zipo sheria mbalimbali ambazo hazijafanyiwa marekebisho. Baadhi ya sheria hizo ni kama *Cyber Crimes Act*, Sheria ya Vyama vyta Siasa, Sheria ya Ndoa na sheria nyingine nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inasimamiwa na Ibara ya 59. Moja katika ya majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kuishauri Serikali katika masuala ya mikataba na uandishi wa sheria na kusimamia mikataba tunayoingia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani imegundua upungufu mkubwa katika ofisi hii kwenye utekelezaji wa majukumu yake, jambo linaloweza kuleta mgogoro wa kidiplomasia, kiuchumi na uvunjifu wa amani. Yafuatayo ni baadhi ya maeneo hayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa *Konoike Construction Company* ambao Tanzania inadaiwa kiasi cha shilingi bilioni 130. Katika mkataba huu Serikali ya Tanzania kuitia Wizara iliyokuwa ya ujenzi na uchukuzi ilivunja mkataba wa ujenzi wa barabara ya Singida – Manyoni. Taarifa ambazo Kambi inazo ni kuwa Kampuni hii ipo katika harakati za kushika mali za Serikali ikiwa itafanikiwa katika maombi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba mwengine ni Mkataba wa *Stirling Civil Engineering of Canada* ambao tunadaiwa shilingi bilioni 84. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona wazi kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali hakutekeleza majukumu yake katika kuishauri vizuri Serikali juu ya uingi waji

wa mkataba huu, jambo ambalo limeiingiza Serikali na Taifa katika madeni makubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushindwa kuridhia mkataba wa Afrika kuhusu demokrasia, chaguzi na utawala bora. Hivi sasa ni miaka sita imepita tangu Tanzania ishiriki na kuitisha azimio kuhusu masuala ya demokrasia. Katika hali isiyolewewka, Serikali ya Tanzania mpaka leo hajaridhia na kusaini mkataba huu ambao nchi karibu 35 zimeshasaini na kuridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali haitaki kuridhia mkataba huu kwa kuwa haitekelezi vizuri suala la demokrasia, hakuna uchaguzi ulio huru na haki na sasa dhana ya utawala bora pia imetoweka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo ambalo linashangaza nchi kama Tanzania yenye historia ya aina yake hapa Barani Afrika na duniani kote kushindwa kuridhia mkataba huu unaohusu demokrasia, chaguzi na utawala bora. (*Makofii*)

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa samahani.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imethibitisha pasi na shaka...

MHE. JUMA S. MKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani taarifa ndogo tu.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: ...kwamba kutoridhia mkataba huu kumefanyika kwa hila. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni...

MHE. JUMA S. NKAMIA: Ungesubiri basi ninachotaka kusema.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: ...inataka Serikali kuacha kufedhehesha Taifa kama nchi isiyo ya kistaarabu kwa kuridhia mkataba huu.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba na mambo ya Muungano.

MBUNGE FULANI: Kaa chini bwana. Hiyo hotuba, hotuba ina taarifa!

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya Muungano yameelezwa vizuri katika Ibara ya 3 na 4 ya Katiba na mambo yanayosumbua Muungano ni pamoja na mafuta na gesi, ajira za Wazanzibar katika taasisi za Muungano, uwezo wa Zanzibar kukopa nje, gawio la Zanzibar katika mali za Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na Mfuko wa Pamoja wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suluhisho pekee kulingana na hatua tuliyofikia kikatiba na kisiasa ni muundo wa Shirikisho la Serikali tatu kama ilivyopendekezwa na Tume ya Jaji Nyalali, Tume ya Kisanga, Tume ya Warioba na wananchi wa Tanzania kuititia mchakato wa kukusanya maoni ya wananchi kuhusu rasimu ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani kuititia sera yake ukurasa wa 13 na 14 sura ya 2.4 inaeleza wazi aina ya muundo wa Muungano na kueleza malengo yatakayofikiwa kuwa ni kila mshirika wa Muungano itakuwa ni mamlaka kamili katika kumiliki na kutumia rasilimali na maliasili zake, isipokuwa masuala yote ya msingi na ya jumla kama vile Katiba na Shirikisho la Jamhuri ya Muungano, mambo ya nje na

ushirikiano wa Kimataifa, ulinzi na usalama, uraia, sarafu ya Benki Kuu, mfumo wa elimu na mambo mengine kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; kama ilivyoanishwa katika Ibara ya 129, majukumu ya tume ni kufanya uchunguzi wa mambo yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwajiwa misingi ya utawala bora. Haki za binadamu ambazo tume imepewa mamlaka ya kusimamia ni zile zilizopo katika Ibara ya 12 – 29 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvunjwaji wa haki za binadamu unaoendelea Loliondo; takwimu zinaonyesha kwamba mwaka 2017 ukiukwaji ulikuwa ni mkubwa ikilinganishwa na vitendo vya uvunjwaji wa haki za binadamu kwa mwaka 2016 na 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapema Agosti, 2018, Jeshi la Polisi liliwakamata na kuwatia nguvuni Wenyeviti wanne wa Serikali ya Vijiji huko Loliondo kwa kosa la kuwaongoza wanakijiji wenzao kupigania haki na kupaza sauti dhidi ya uonevu wa kuwaondoa kwa nguvu wanakijiji hao mwishoni mwa mwaka 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio ya uvunjifu wa haki za binadamu na utawala bora yaliripotiwa pia Uvinza Mkoani Kigoma, Jeshi la Polisi waliwaua wananchi katika mchakato wa kuwaondoa katika Kijiji cha Mpeta Wilaya ya Uvinza baada ya kuibuka vurugu kati ya wananchi na Jeshi la Polisi, lakini Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora haijawahi kuchunguza wala kutoa kauli yoyote juu ya uvunjifu huu mkubwa wa haki za binadamu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiukwaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma katika mikataba...

MWENYEKITI: Achana na biashara hiyo. Twende kwenye *Mobile Courts* Ibara ya 35.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Siku ya Sheria Duniani Mahakama ya Tanzania ilizindua kitu kinachoitwa Mahakama Inayotembea. Dhana hii ya Mahakama zinazotembea ni dhana inayomaanisha Mahakama katika ngazi fulani kuhamisha huduma zake na kuzitolea katika sehemu mbalimbali ya mamlaka yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba dhana hii imekuwepo tangu siku za nyuma, lakini kinachoonekana sasa ni dhamira ya kurejeshwa kwa Mahakama hizi ambazo lengo lake lilielezwa kuwa ni kuharakisha mashauri madogo ya madai kwa lengo la kuyamaliza haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia lengo lingine ni kumfuata shahidi kwa sababu ambazo zinatokana na ugonjwa na kuwapunguzia gharama mashahidi au iwapo kielelezo hakihamishiki kirahisi. Kumbukumbu za Kambi Rasmi zinaonyesha kwamba Serikali iliwahi kuleta Muswada wa kuanzisha Mahakama Inayotembea lakini lilikwama kwa kamati husika...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda wetu ndio huo, Mheshimiwa, hitimisha tu.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia njema ya kuwasilisha haya yote, ningependa kuhoji mambo yafuatayo: je,....

MWENYEKITI: Hapana, muda umekwisha.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha. (*Makof*)

**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU
UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2018/2019 PAMOJA NA
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA
KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA
2019/2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, Kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, katika wizara ya katiba na sheria Mheshimiwa Tundu Antipas Lissu (Mb), napenda kuwasilisha maoni ya kambi rasmi ya upinzani Bungeni kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2018/2019 pamoja na makadirio ya mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa fedha 2019/2020.
2. **Mheshimiwa Spika**, kabla sijawasilisha maoni hayo, napenda kuchukua nafasi hili, kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili kuwasilisha maoni hayo. Aidha, napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kutoa pole kwa watanzania wote wanaokumbana na madhira ya uvunjifu wa haki za binadamu nchini huku nikiwashukuru na kuwapongeza watanzania wote ambao ni waumini wa utawala wa sheria hapa nchini. Aidha kipekee kabisa niwape pole viongozi wakuu wa CHADEMA kwa kesi lukuki zenyekila aina na dalili za uonevu zinazowaandama.
3. **Mheshimiwa Spika**, kwa upekee napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa viongozi wetu wa ngazi za Kanda hadi misingi hasa kwa mikoa ya Kanda ya Serengeti, kwa ukomavu wao katika kutambua haki zao za msingi katika kutekeleza majukumu yao ya kisiasa licha ya vitisho vingi wanavyokumbana navyo kutoka kwa watendaji wanaolipwa kwa kodi za wananchi. Naomba niendelee kuwatia moyo kwamba, Tanzania inapita katika kipindi cha mpito kuelekea Demokrasia ya kweli, japokuwa tunarudi nyuma, uvumilivu ni muhimu.

4. **Mheshimiwa Spika**, Mwisho lakini si kwa umuhimu sana naishukuru familia yangu kwa kunivumilia na kunipa moyo katika majukumu yangu haya ya Kibunge na Kisiasa, ambayo kwa namna moja au nyingine naendelea kujifunza. Nasema mmekuwa nguvu yangu na asanteni sana!

[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

6. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Katiba na Sheria ndiyo wizara yenye jukumu la kuhakikisha kuwa Nchi hii inaongozwa kwa kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa na vyombo halali nya maamuzi, Aidha majukumu mengine ya wizara hii yameainishwa katika hati ya mgawanyo wa majukumu kwa mawaziri, kuititia Tangazo la serikali Na. 144A la tarehe 22 April, 2016. Miongoni mwa majukumu hayo ni pamoja na kushughulikia masuala ya kikatiba, kusimamia mfumo wa haki na utoaji haki nchini, uandishi wa Sheria, kuendesha mashataka ya jinai, kushughulikia uendeshaji wa mashauri ya madai na mikataba mbalimbali inayohusu Serikali na utaratibu wa Sheria za kimataifa, kushughulikia masuala ya haki za binadamu na msaada wa kisheria, kurekebisha sheria pamoja na majukumu mengine ambayo sijayataja hapa.

7. **Mheshimiwa Spika**, Hotuba hii inajikita katika kuangazia Je, nikiwa kweli Wizara ya Katiba na Sheria inatekeleza majukumu yake ya kuhakikisha nchi inaongozwa kwa kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni na taratibu zilizowekwa na vyombo mbalimbali nya maamuzi?, katika kufanya hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeonesha kwa kiwango gani majumuku haya yametekelezwa na au kutotekelvezwa, madhara na faida kama zipo na kuishauri Serikali hatua muhimu za kuchukua kulingana na eneo husika.

8. **Mheshimiwa Spika**, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Pamoja na mapungufu yake, ndiyo sheria Mama ambayo watanzania wamekubaliana kwa pamoja misingi ya kuongoza nchi yao ambayo itazingatia uhuru, haki, udugu na amani na wemesistiza katika katiba kuwa Nchi yao itakuwa ya kidemokrasia kwa

kusimamiwa na Bunge lenye wajumbe waliochaguliwa na linalowawakilisha wananchi, na pia nchi yao itakuwa yenye Mahakama huru zinazotekeleza wajibu wa kutoa haki bila woga wala upendeleo wowote, na hivyo kuhakikisha kwamba haki zote za binadamu zinadumishwa na kulindwa, na wajibu wa kila mtu unatekelezwa kwa uaminifu:

[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

11. **Mheshimiwa Spika**, Kauli ya kiongozi wa nchi ndio dira na mtazamo wa serikali anayoingoza hivyo basi, kuweka pembeni mchakato wa Katiba mpya ni kufifisha ndoto za watanzania wote walizokuwa nazo baada ya kutoa maoni yao katika Tume ya Warioba, jambo linaloua ustawi na Dira ya nchi Kiuchumi, siasa na Kijamii. Aidha Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kurejesha haraka mchakato wa Katiba Mpya, ambayo ndiyo matumaini ya watanzania kama ilivyoahidi katika ilani yake ya uchaguzi ya mwaka 2015 – 2020.

[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

b. **Sheria kandamimizi zinazokiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano.**

15. **Mheshimiwa Spika**, Kwa nyakati mbalimbali Bunge lako Tukufu limetunga sheria ambazo katika utekelezwaji wake zinakiuka katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo ni dira ya Taifa letu. Ni katiba hii ambayo sote tumeapa kuilinda na inapotokea kwamba katiba hii inavunjwa huku tukiwa kimya ni sawa na kwenda kinyume na viapo ambavyo sisi wenyewe kwa nyakati mbalimbali tuliapa. Baadhi ya sheria na kanuni ambazo zinakiuka matakwa ya katiba ni pamoja na hizi zifuatazo:

i. **Sheria ya Makosa ya Mtando (The Cyber Crime Act),**

16. **Mheshimiwa spika**, Mapema mwezi April mwaka 2015 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha sheria ya mitandao, ijlikanayo kama "The Cyber Crime Act" hata hivyo sheria hii badala ya kuwa msaada kwa watanzania imegeuka na kuwa fimbo ya watawala dhidi ya wananchi.

Sheria hii imewapa mamlaka Jeshi la Polisi kuingia eneo lolote na kuchukua vifaa vyovyote vya kimawasiliano kama komputa mpakato, simu za mikononi na vifaa vingine, eti wanapoamini kwamba vifaa hivyo vitatumika kama ushahidi dhidi ya kosa linalohisiwa kutendeka. Hata hivyo kifungu cha 16 cha sheria hii kinakiuka "misingi ya kimataifa ya uhuru wa kujieleza (**international standard of freedom of expression**) kifungu hiki siyo tu kinaleta usumbufu kwa wananchi lakini pia ni vigumu kuthibitisha kosa mahakamani kwa kutumia kifungu hiki. Taarifa za Kambi Rasmi ya Upinzani zinaonesha kwamba kwa mwaka 2018 jumla ya mashitaka 12 ambayo tulibahatika kupata taarifa zake, yalipelekwa katika mahakama mbalimbali kuhusiana na kesi za matumizi ya sheria ya mtandao, kati ya mashitaka hayo, shitaka moja ni la kikatiba ambalo liko Mahakama Kuu ya Tanzania kupinga kifungu cha 16 ambacho kinakwenda kinyume na Katiba.

17. Mheshimiwa Spika, Sheria ya mitandao, inakiuka tangazo la Umoja wa Mataifa kuhusu haki za binadamu, Mkataba wa kimataifa kuhusu haki za kijamii na kisiasa, lakini pia Sheria hii haitambui haki ya faragha na ya usalama wa mtu kama inavyotajwa na Ibara ya 16 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sheria hii inaminya uhuru wa kutoa maoni ambao uko katika Ibara ya 18. Kifungu cha 32 cha sheria ya mitandao, kinachomlazimisha mtu kutoa taarifa, Kwa maoni yetu kinaikuka haki ya faragha Kwa mujibu wa Ibara ya 16 ya Katiba. Aidha Kifungu cha 38 cha sheria hii ya mtandao kinakiuka haki ya usawa mbele ya sheria kama ilivyo katika Ibara ya 13 ya katiba, Ni Rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Kwamba, sheria zetu lazima zilenge kuisaidia jamii ya watanzania kuliko dhamira ya kuwakomoa na kuwanyanyasa wananchi na katika muktadha huo, sheria hii ni mionganoni mwa sheria ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuleta mabadiliko marekebisho ya sheria hii.

ii. Sheria ta Takwimu (Statistics Act, 2015)

18. Mheshimiwa Spika, Sheria ya Takwimu ya mwaka 2018 ni mionganoni mwa sheria ambazo zinaweka adhabu kubwa kwa wakosaji na mionganoni mwa sheria kandamizi ambazo zinatakiwa kufanyiwa marekebisho makubwa, Aidha katika

Dunia ya sasa hivi ambayo inategemea matokeo ya tafiti mbalimbali haiwezekani Taifa likawa na chanzo kimoja cha Takwimu. Serikali kupitia sheria hii inajjiwekea mazingira ya kutopingwa kwa takwimu zake hata kama takwimu hizo zinapotoshwa umma. Aidha ni maoni yetu kwamba sheria hii kandamizi na ambayo madahara yake ni makubwa ifanyiwe marekebisho.

iii. Media Service Act, 2016

19. Mheshimiwa spika, tarehe 5 Novemba 2016, Bunge lako tukufu lilitunga Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari inayotumika Tanzania Bara peke yake na kuridhiwa na Mheshimiwa Rais tarehe 16 Novemba, siku 11 baadaye kuwa sheria kamili. Chini ya sheria hii, Waziri mwenye dhamana amepewa mamlaka makubwa na yanatumika kukandamiza vyombo vya habari kwa hisia tu. Kifungu cha 59 kimekuwa kilitumiwa vibaya na waziri mwenye dhamana kufungia vyombo vya habari hasa magazeti. Baadhi ya magazeti kama Gazeti la Mawio, Tanzania Daima na Raia Mwema na Mwanahalisi yalifungiwa chini ya kifungu cha 59 cha sheria hii. Ubatili wa Sheria hii unatokana na hukumu ya Mahakama ya Afrika Mashariki ambayo ilikubaliana na walalamikaji katika shitaka Na. 2 / 2017 kati ya Baraza la Habari Tanzania, (MCT) Kituo Cha Msaada wa Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)na Mtandao wa watetezi wa Haki za Binadamu (THDRC) dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali sasa kuleta marekebisho ya Sheria hii kwa sababu sheria imetangazwa kukiuka misingi ya Katiba ya Nchi na Utawala bora ambayo Tanzania imeridhia katika Mkataba wa Jumuia ya Afrika Mashariki.

iv. (Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa) Access to Information Act

20. Mheshimiwa Spika, sheria hii ilipitishwa tarehe 7 Septemba mwaka 2016 na kuridhiwa na Mheshimiwa Rais kuwa sheria kamili tarehe 23 Septemba 2016, siku kumi na sita baada ya sheria hiyo kupitishwa na Bunge. Sheria hii ambayo inatumika Tanzania Bara peke yake ina baadhi ya vifungu ambavyo vinakiuka haki ya kupata taarifa kama ilivyoainishwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania pamoja na Mikataba mbalimbali ya Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia. Aidha sheria hii pia imeshindwa kuzingatia kwa kiwango kikubwa matakwa ya sera ya Taarifa na Utangazaji ya mwaka 2003 ambao inataka kusiwepo na vizuizi vyta kupata habari. Sheria hii kama ziliyvo kwa sheria mbili tajwa hapo juu, inabakia kuwa tishio kwa watumiaji wa mitandao hapa nchini, dhidi ya uhuru wao wa kutoa maoni. Watumiaji wa mitandao zikiwemo television za mitandaoni,(online tv) na Blogers ni mionganini mwa tabaka ambalo limekumbwa na lungu la Mamlaka ya Mawasiliano Nchini - TCRA baada ya kutungwa kwa sheria hii na kanuni. Kwa mujibu wa ripoti ya CIPESA (2015) kuhusu uhuru wa matumizi ya mtandao Tanzania, Tanzania inatajwa kama Taifa ambalo Serikali yake imetunga sheria za kuminya matumizi ya mitandao na kudidimiza uhuru wa kujieleza mitandaoni. Ni kwa mantiki hii KRUB inaitaka serikali kuleta marekebisho ya sheria hii ili kuondoa changamoto ambazo zimekuwa zikiwakumba watumiaji wa mitandao ya kijamii hapa nchini.

v. **Electronic and Postal Communications Act, na Online Content Regulations, 2018**

21. **Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Kielektroniki na Mawasiliano ya Posta imeanzisha kanuni za maudhui ya kimtandao zinazojulikana kama Online Content Regulations za mwaka 2018, chini ya kifungu cha 103(1) cha sheria hiyo Sura ya 306 ya sheria za Tanzania. Taarifa ya wachambuzi wa masuala ya kimtandao katika uchambuzi wao wa kanuni hizo yaani "**Analysis of the Tanzania Content Regulations**" uchambuzi uliofanywa na Shirika la "*International Centre for Non Profit Law "ICNL"*" unaonesha kwamba kanuni hizo ni mbaya na ni lungu dhidi ya uhuru wa kujieleza ambao unalindwa chini ya Katiba.

vi. **Sheria ya Ndoa ya 1971(The Law of Marriage Act)**

22. **Mheshimiwa Spika**, Sheria hii imekuwa kandamizi na kichocheo cha janga kubwa la ndoa za utotonii, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, tunapongeza uamuzi wa Mahakama Kuu kubatilisha kifungu kilichokwuwa kinaruhusu wasichana

kuolewa kuanzia miaka 15 katika kesi ya Rebeca Giyumi dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hata hivyo serikali haikuridhishwa n maamuzi hayo ya busara na kuamua kukata rufaa ambapo tunaona hila ya wazi ya Serikali na Mahakama kuchelewesha rufaa hiyo kwani tangu 2017 kesi hii haijaitwa kwa ajili ya kusikilizwa wala kufanyiwa maamuzi

23. Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ni sheria ambayo imepitwa na wakati na hivyo inapaswa kufanyiwa marekebisho makubwa sana. Baadhi ya vifungu ambavyo vimetangazwa na Mahakama Kuu ya Tanzania kwamba ni batili ni pamoa na vifungu vinavyomruhusu mtoto wa miaka 14 kuolewa kwa idhini ya wazazi wake. Hata hivyo, hadi sasa serikali haijaleta muswada hapa bungeni wa kubadilisha vifungu hivyo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunajiuliza ikiwa ni dhamira ya serikali kuruhusu watoto wadogo kuendelea kuathiriwa na matakwa ya sheria hili.

24. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaanmini kwamba sheria hizi ni kandamizi na inaitaka serikali kuleta ndani ya Bunge lako tukufu Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, kufanya marekebisho Sheria za Makosa ya Kimtandao, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, Sheria ya Takwimu ya mwaka 2015, Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya mwaka 2016 na sheria zote kandamizi ambazo wadau mbalimbali wa sheria wamekuwa wakizipigia chapua kufanyiwa marekebisho.

25. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali pia kuleta marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (The Criminal Procedure Act)na sheria zote zinazohusu taratibu za kesi mbalimbali ili kuondoa tatizo la watuhumiwa kukaa rumande kwa miaka mingi kwa kisingizio cha kutokamilika kwa upelelezi. Aidha wapo baadhi ya watuhumiwa ambao wako mahabusu kwa miaka mingi kwa sababu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kila mara wanadai mahakamani kwamba upelelezi haujakamilika, kitendo hiki ni kutowatendea haki watuhumiwa na dhana nzima ya utuhumiwa kwa kuwa bado hawajahukumiwa. Sheria kama za utakatishaji wa fedha na sheria ya uhujumu

uchumi zimekuwa kichaka kwa ajili ya kukandamiza watuhumiwa na chanzo cha mapato ya serikali.

TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA

a) **Mheshimiwa Spika;** Tume ya Utumishi wa Mahakama imeundwa kwa mujibu wa Ibara ya 112 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Sheria ya Uendeshwaji wa Mahakama, Sheria Na. 4 ya mwaka 2011. Miongoni mwa majukumu ya Tume ni pamoja na kumshauri Mheshimiwa Rais kuhusu uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, kuteua, kupandisha cheo na kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya watumishi ambao ni mamlaka ya tume.

a. **Kupandishwa vyeo watumishi**

26. **Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria wakati wa kujadili Mpango na Mkadirio ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019, inaonesha Tume ya Utumishi wa Mahakama imepandisha vyeo watumishi katika namna ambayo inaacha maswali mengi yanayohitaji ufanuzi. Kwa mfano, watumishi 255 katika mwaka wa fedha 2014/2015 walipandishwa vyeo na inaonekana majina yao yaliingizwa katika mfumo wa HCMIS lakini watumishi hao hawakurekebishiwa mishahara na katika hali ya kustaajabisha Serikali imeelekeza barua zao zifutwe na badala yake zianzie tarehe 1/11/2017.

27. **Mheshimiwa Spika,** kitendo cha serikali kufuta barua za watumishi hao ambao walikuwa wamepandishwa vyeo kwa kipindi cha miaka 2 ni kinyume na Sheria ya Utumishi wa Umma hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuwalipa watumishi hao madai yao ya miaka miwili ambayo ni malimbikizo kwa nyadhifa zao mpya walizopandishwa na Serikali kushindwa kuwarekebishiwa mishahara.

28. **Mheshimiwa Spika,** utaratibu huu ambao ni uonevu unaonekana pia kwa watumishi 1211 wakiwemo mahakimu 534 walipandishwa vyeo lakini kama ilivyo ada serikali

ikasitisha upandaji wa vyeo na kuelekeza pia barua zao zifutwe na badala yake zianzie tarehe 01/04/2018. Kipindi hiki ni sawa na kuwanyima stahiki zao cha kupandisha madaraja kwa kipindi cha miaka miwili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kufahamu kwanini serikali isiwali pe malimbikizo kwa kipindi chote ambacho hawakurekebishiwa mishahara na badala yake Serikali mnaamua kufuta barua za kupandishwa vyeo?

b). Uteuzi wa Waheshimiwa Majaji.

29. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu Ibara ya 113(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, majukumu ya Tume yatakuwa ni kumshauri Rais kuhusu uteuzi wa majaji wa mahakama kuu. Pamoja na mambo mengine, uteuzi wa waheshimiwa majaji unatarajiwaa kuzingatia uwezo wa mteuliwa na historia ya utumishi uliotukuka. Kwa bahati mbaya zaldi zipo teuzi ambazo zimekuwa zikifanyika na kuacha maswali mengi juu wa weledi wa kitaalumu wa mteuliwa kama ulizingatiwa na au uteuzi ulichochewa na sababu nyingine.

[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

OFISI YA TAIFA YA MASHTAKA:

32. **Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri mapema mwezi Februari 2018, alifanya mabadiliko ya kimuundo katika ya mashitaka (National Prosecution Services) kwa kile kilichoelezwa kuwa lengo la mabadiliko hayo yalikuawa ni kuongeza ufanisi na tija katika uendeshaji wa mashauri ya jinai na kuratibu shughuli za upelelezi zinazofanywa na vyombo vya uchunguzi. Aidha Sheria ya Huduma ya Mashitaka Na. ya 2018 yaani (National Prosecution Service No. 1/ 2018) kifungu cha 16(1)-(3) kinaeleza majukumu ya Mkurugenzi wa mashitaka kuwa ni pamoja na kuratibu shughuli za upelelezi wa vyombo vya uchunguzi. Sambamba na hilo Mkurugenzi wa mashitaka anaweza kutoa maelekezo kwa chombo chunguzi chochote kufanya kufanya upelelezi kuhusu jambo lolote analolisikia au pale kunapokuwepo na malalamiko kwa lengo la

kuhakikisha upelelezi unafanyika kwa kina ili kurahisisha utoaji wa haki.

33. Mheshimiwa Spika Pamoja na kupewa mamlaka hayo yote Ofisi ya Taifa ya mashitaka imeshindwa kutekeleza majukumu yake ama kwa makusudi kutokana na sababu ambazo huenda zinajulikana kwa Mkurugenzi wa Mashitaka mwenyewe, katika kufatilia matukio makubwa na yakutisha yanayolutia doa Taifa letu ndani na nje ya Tanzania.

[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

35. Mheshimiwa Spika, Licha ya kwamba kifungu cha 16 cha Sheria ya Huduma ya Mashitaka kinaeleza wazi kuwa Mkurugenzi wa Mashikata anaweza kutoa maelekezo kwa chombo chochote kufanya upelelezi kuhusu jambo lolote analosikia au pale kunapokuwepo na malalamiko, lakini Mkurugenzi huyu amekuwa akikaa kimya na kutochukua hatua yoyote licha ya malalamiko mengi yanayotolewa na wananchi juu uhalifu ambao unataka kufanywa dhidi yao.

[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

39. Mheshimiwa Spika, kutokana na mazingira kama hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Mkurugenzi wa Mashtaka ajitafakari kama anatosha kukalia kiti hicho. Aidha, tunaitaka mamlaka yake ya uteuzi itengue uteuzi wake kwani kwa kutochukua hatua kumeifanya Tanzania ionekane si sehemu salama ya kuishi kutokana na kukithiri kwa matukio haya ya utekaji, na viongozi kupigwa risasi kizembe na hadhalani bila.

TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA

40. Mheshimiwa Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria imeanzishwa kwa sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria na kufanyiwa marekebisco na sheria namb 2 ya mwaka 2018. aidha kwa mujibu wa kifungu cha 4(1)(2)(4) ambacho kilifanyiwa marekebisco kuititia sheria namba 2 ya mwaka 2018, majukumu ya Tume ni pamoja na kuchunguza sheria

yoyote kwa lengo la kuiendeleza, kuiboresha, kupitia sheria au tawi, kupendekeza hatua muhimu ili kuzifanya sheria ziendane na mazingira ya sasa ya Tanzania, kuondoa kasoro, kufuta sheria zilizopitwa na wakati.

41. Mheshimiwa Spika, Tanzania pamoja na kwamba tunayo tume ambayo majukumu yake yameainishwa kisheria lakini bado ziko sheria mbalimbali ambazo zinakasoro, sheria zisizoendana na mazingira ya sasa ya Tanzania na sheria ambazo zimepitwa na wakati, lakini sheria hizo na wala kupendekezwa kufanyiwa marekebisho. Yamkini sheria hizo hazichunguzwi ili ziboreshwwe kwa kuwa zinatumika kukandamiza jamii ya watawaliwa.

42. Mheshimiwa Spika, Baadhi ya sheria hizo sasa ni pamoja na Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari, 2016, sheria ya makaosa ya mtandao (The Cyber Crime Act) sheria ya vyama vya siasa ya mwaka 2018, sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, ambao mba na hilo ni kupeleka fedha za miradi katika robo ya mwisho ya mwaka, jambo linalopelekea kushindwa kutumika kwa fedha hizo kutokana na utaratibu mzima wa kufuata sheria ya manunuzi ambayo inahitaji kutimizwa kwa masharti. Hivyo kupelekeea fedha hizo kurudishwa Serikali kuu.

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

43. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali inasimamiwa na Ibara ya 59 ya Katiba ya Jamhuri ya Tanzania na sheria ya Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya mwanasheria Mkoo wa Serikali, Sura ya 268 ambayo ilifanyiwa mabadiliko kupitia Tangazo la Serikali Na. 48 ambapo pamoja na mambo menginekazi yake ni kuishauri serikali katika masuala ya Mikataba na uandishi wa sheria, kusimamia wajibu wa kimikataba wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania, kuandaa miswada ya sheria kwa ajili ya kupitishwa na Bunge na kuandaa hati zote za kisheria na maazimio kwa ajili ya kuidhinishwa na Bunge pamoja na majukumu mengine ambayo pia yameaishwa.

44. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya upinzani imegundua mapungufu makubwa katika ofisi hii kwenye utekelezaji wa majukumu yake jambo linaloweza kuleta mgogoro wa Kidiplomasia, mgogoro wa Kiuchumi na uvunjifu wa amani katika nchi. Yafuatayo ni baadhi ya maeneo yenye mapungufu;

a. **KUSHINDWA KUTOA USHAURI WA KISHERIA KWA SERIKALI NA KUISABABISHIA SERIKALI HASARA KUBWA YA FEDHA**

45. **Mheshimiwa Spika**, hivi karibuni kupitia vyanzo mbalimbali imelipotiwa taarifa ya Tanzania kutakiwa kuilipa kampuni ya Kijapani ya Ujenzi ya *Konoike Construction Company* kiasi cha Shilingi Bilioni 130 kufuatia ushindi iliopata katika kesi ilifunguliwa dhidi ya serikali mapema mwaka 2016 kufuatia kitendo cha Serikali ya Tanzania kupitia iliyokuwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kuvunja Mkataba wa Ujenzi wa Barabara Sindida – Manyoni. Taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzni Bungeni inazo ni kwamba Kampuni hii ya Konike sasa ilikuwa katika hatua za kuomba kushika mali za Serikali ya Tanzania na ikiwa itafanikiwa katika maombi yake hayo, kuna uwezekano mkubwa mali za serikali zikakamatwa na Kampuni hiyo nje ya mipaka ya Tanzania katika jitihada za kampuni hiyo kuilazimisha Tanzania kuilipa fedha hizo.

46. **Mheshimiwa spika**, *Konoike Construction Company* walishitaki wizara ya Ujenzi na TANROAD kwa kuvunja mkataba kinyume na matakwa ya mkataba wa ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 150 kwa madai ya kwamba kulikuwa na ucheleweshwaji wa kukamilika kwa mradi. Aidha, hukumu hii inakuja wakati Tanzania ilikuwa katika mchakato wa kulipa kampuni nyingine *Stirling Civil Engineering of Canada* shillingi bilioni 84 baada ya kuvunjwa kwa mkataba wa mradi wa ujenzi wa barabara jijini Dar Es Salaam. Kampuni hii iliwhahi kushikilia ndege aina ya Bombadier iliyokuwa imenunuliwa na Serikali ya Tanzania kufuatia kile kinachoeleza kuwa ni jitihada za kufufua shilika la ndege nchini, hii ndio kesi ambayo ilijulikana baada ya Mbunge wa Singida Mashariki kueleza kwamba ndege iliyokuwa

imenunuliwa ilikuwa ikishikiliwa nchini Canada kutokana na mgogoro huo.

Pamoja na Tanzania kutakiwa kuilipa mabilioni hayo ya fedha, kuna taarifa pia ambazo zinaonesha kuwa makampuni mengine pia ambayo ni *Acacia, Symbion Power and EcoEnergy* wamefungua mashitaka katika mahakama ya usuluhishi wa migogoro ya kimataifa, japokuwa taarifa zinaonesha kesi hizo hazijaanza.

47. Mheshimiwa Spika, Taifa linapata hasara hii kubwa kwa sababu za kuvunjwa mikataba kiholela bila kuzingatia kwanza matakwa ya kimkataba, ni jambo linaloshangaza kwamba, Serikali inaweza kufanya maamuzi ya kuvunja mikataba kwa ushauri wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na bado Taifa likaendelea kupata hasara, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitka Serikali hii kuliambila Taifa ni hatua gani inachukua dhidi ya watendaji wote wa Serikali ambao wamesababisha nchi kupata hasara ya mabilioni ya walipa kodi, kufuatia maamuzi yao ya kuvunja mikataba na makampuni bila kufuata taratibu za kisheria.

Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Wakili wa Mkuu wa Serikali inapaswa kujitathimini juu ya uwezo wake wa kuendesha kesi za kimataifa dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

b. KUSHINDWA KURIDHIA MKATABA WA AFRIKA KUHUSU DEMOKRASIA, CHAGUZI NA UTAWALA BORA.

48. Mheshimiwa Spika, hivi sasa miaka sita imepita tangu Tanzania ishiriki na kuitisha azimio kuhusu masuala ya Demokrasia, chaguzi na utawala bora lilitopitishwa na umoja wa Afrika, ambako Tanzania ni mwanachama. Mkataba huo ulipitishwa na Umoja wa Afrika wakati wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, Januari 30 mwaka 2007. Lengo la mkataba huu ni kuzitaka nchi wanachama kuzingatia na kutekeleza utawala bora, utawala wa sheria na haki za binadamu kama ilivyoiezwa katika ibara ya 3 na 4 ya mkataba huo.

- 49.** **Mheshimiwa spika** katika hali isiyoleweka serikali ya Tanania ni mionganini mwa nchi 19 za Umoja wa Afrika ambazo hazijaridhia na kusaini kataba huo huku jumla ya mataifa 35 wanachama wa Umoja wa Afrika wameshasaini na kuridhia Mkataba huo, hata hivyo serikali haitaki kuridhia mkataba huo kwa kuwa Tanzania haitekelezi vizuri masuala ya Demokrasia, hakuna uchaguzi ulio huru na haki na sasa dhana ya utawala bora pia imetoweza. Mheshimiwa Spika, ni jambo ambao linashangaza kwa Nchi kama Tanzania yenye historia ya aina yake hapa Barani Afrika na Duniani kote kushindwa kuridhia mkataba huu unaohusu demokrasia, chaguzi na utawala bora ili hali Serikali ikijinasibu kwamba inazingatia masuala ya demokrasia na utawala bora.
- 50.** **Mheshimiwa spika**, Serikali imethibitisha pasipo na shaka kwa kushindwa kuridhia mkataba wa Demokrasia, Chaguzi na utawala bora kwamba Tanzania hakuna Demokrasia, kwamba Chaguzi zinazoendeshwa Tanzania siyo huru na haki kwa kukosa Tume huru ya Uchaguzi na pia utawala bora sasa ni jambo lilibaki katika majalada mbalimbali ya ofisi za watawala. Karibuni serikali imeshindwa kuridhia na kusaini mkataba wa Afrika kuhusu Demokrasia, chaguzi na utawala bora
- 51.** **Mheshimiwa Spika**, Mkataba huu, kuhusu Deokrasia, Chaguzi na Utawala bora (**African Charter on Democracy, Elections and Governance**) unaeleza katika Ibara ya 2 malengo ya mkataba huu kuwa ni pamoja na kuhakikisha nchi wanachama wanakuza, kulinda misingi ya demokrasia na haki za binadamu, kulinda na kuzingatia misingi ya utawala bora, kuhakikisha chaguzi huru na haki kwa kuhakikisha taasisi huru za kusimamia uchaguzi, pamoja na uhuru wa mahakama. Haya ni mionganini mwa malengo ambayo leo Serikali ya Tanzania inayaogopa na kuona yanatishia uwepo wao madarakani.
- 52.** **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuacha kulifiedhehesha Taifa kama nchi isiyo ya kistaarabu kwa kuridhia mkataba huu, Tanzania siyo nchi ambayo sasa katika karne hii ya 21 inaogopa

kuridhia mkataba wa Demokrasia, Uchaguzi huru na zenye haki pamoja na utawala bora. Aidha Serikali iache propaganda kwamba Mkataba huu unakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la sivyo waiambie dunia ibara zipi za mkataba huo zinakiuka Katiba ya nchi. Pamoja na hayo hata kama kuna ibara za mkataba zinakiuka katiba, jambo ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaanini siyo kweli, upo utaratibu wa kufanya juu ya Ibara hizo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itekeleze majukumu yake ya Kuishauri serikali kwa maslahi mapana ya Taifa hili.

KATIBA NA MAMBO YA MUUNGANO.

53. Mheshimiwa Spika, Masuala ya muungano, yameelezwa vizuri katika Ibara ya (3) na (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuorodheshwa katika nyongeza ya kwanza ya Katiba. Kumekuwepo na hoja ambazo kwa miaka yote imekuwa ni kilio kutoka upande wa pili wa Muungano (Tanzania Zanziba) na kupelekea kuundwa kwa tume kadhaa ili kujalibu kutatua kero hizo za Muungano. Kero hizo ambazo zimekuwa zinalalamikiwa miaka yote ni;

- Mafuta na Gesi Asilia
- Mambo ya Muungano
- Ajira za Wazanzibari katika Taasisi za Muungano
- Uwezo wa Zanzibar Kukopa Nje
- Gawio la Zanzibar katika Mali za Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki (EACB)
- Mfuko wa Pamoja wa Fedha
- Utozwaji Kodi mara mbili kwa Wafanyabiashara wa Zanzibar

[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

55. Mheshimiwa spika, suluhisho pekee kulingana na hatua tuliyofikia kikatiba na kisiasa ni muundo wa shirkisho la serikali tatu, kama ilivyopendekezwa na Tume ya Jaji Nyalali, Tume ya Kisanga, Tume ya Jaji Warioba na wananchi wa Tanzania kupitia mchakato wa kukusanya maoni ya wananchi kuhusu rasimu ya Katiba Mpya, ndiyo njia pekee ya kutatua matatizo ya muungano huu.

56. Mheshimiwa Spika, Matatizo yanadhihirika katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 hayawezি kutatuliwa kwa Tume za majadiliano. Kwa mfano Ibara ya 26 (1) ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 haimtambui Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama Mkuu wa Nchi ya Zanzibar isipokuwa, Katiba hiyo inatambua Rais wa Zanzibar kuwa Mkuu wa nchi ya Zanzibar, Pili, Ibara ya 123 ya Katiba ya Zanzibar haimtambui Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa ni Amiri Jeshi Mkuu wa Zanzibar bali Katiba hiyo ya Zanzibar inamtambua Rais wa Zanzibar kama Amiri Jeshi Mkuu wa Zanzibar. Kwa mujibu wa Ibara ya 2 ya katiba ya Zanzibar, Zanzibar ni miongoni mwa Nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ibara ya 9 inaongelea Mzanzibar na siyo Mtanzania.

57. Mheshimiwa Spika, katika Mazingira haya, njia pekee ni serikali tatu kama ilivyopendekezwa na Tume mbalimbali, kama hatua za haraka hazitachuliwa, Na namna pekee ya kumaliza matatizo haya ni kurejesha mchakato wa Katiba Mpya ya wananchi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakubaliana na kauli ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika kitabu chake cha uongozi wetu na hatima yetu kwamba huko mbele ni giza tupu.

58. Mheshimiwa Spika, Giza aliloliona Baba wa Taifa linadhihirika kwa kushindikana kupatikana kwa suluhu zaidi ya miongo mitano sasa, ikiwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimefanya vikao vya pamoja visivypungua 80 katika ngazi mbali mbali ili kuzungumzia Kero za Muungano. Aidha Jitihada za Serikali hizi zilipelekea mwaka 1994 kuomba msaada kutoka Shirika la Fedha Duniani, IMF ili kuzishauri kuhusiana na Benki Kuu, mgawano wa Misaada na uhusiano wa kifedha (intergovernmental fiscal relationship). Kama hiyo haitoshi, tarehe 14 Novemba, 2000 wakati Rais Benjamin Mkapa alipokuwa akizundua Bunge aliahidi kuzipatia ufumbuzi Kero za Muungano ndani ya siku 60!! Tokea ahadi ilipotolewa hadi leo ni ni miaka 19 imepita. Serikali zinazoongoza ni zile zile za Chama cha Mapinduzi.

59. Mheshimiwa Spika, Pamoja na hatua zote hizo zilizoambatana na masikitiko ya Viongozi wa juu, manung'unico ya wananchi wa pande zote mbili juu ya uendeshaji wa Muungano na ahadi nzito za viongozi wa juu wa Serikali za kuondoa kasoro za Muungano – lakini bado Kero au Kasoro hizo zipo pale pale na huenda kwa mtazamo wa baadhi ya wananchi, kero za Muungano zimeongezeka. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza hivi kweli CCM inahitaji huu muungano kuendelea kuwepo au ni Muungano kiini macho?

60. Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inazo Ibara maalumu ambazo zinajaribu kutoa utaratibu wa namna ya mambo ya muungano unavyopaswa kuendeshwa, mambo hayo yanaelezwa katika Sura ya Saba ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoeleza masharti kuhusu fedha za Jamhuri ya Muungano. Miongoni mwa mambo hayo ni Tume ya Pamoja ya Fedha (Joint Finance Commission – JFC) asasi ya Muungano iliyoundwa kwa mujibu wa Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (ya mwaka 1977) na Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha Sura 140 ya mwaka 1996). Tume ilizinduliwa rasmi tarehe 5 Juni, 2003, baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuteua Makamishna saba. Aidha Tume ina Sekretarieti ambayo ni chombo kikuu kiutendaji. Tume hii ilikuwa ni njia mojawapo ya kutatua kero za kifedha kati ya zile kero kuu za Muungano lakini kwa masikitiko makubwa hata Tume hiyo ambayo ni chombo cha kiutendaji kimeshindwa kutimiza azma ya uanzishwaji wake.

61. Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Katiba, Tume ya Pamoja ya Fedha ina majukumu ya Kuchambua mapato na matumizi yanayotokana na, au yanayohusu utekelezaji wa Mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali mbili kuhusu mchango na mgao wa kila mojawapo ya Serikali hizo; Kuchunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za fedha wa Jamhuri ya Muungano na pia uhusiano katika mambo ya kifedha kati ya Serikali mbili;

62. Mheshimiwa Spika, Ibara ya 133 ya Katiba inaeleza kuwa; "*Serikali ya Jamhuri ya Muungano itatunza akaunti*

maalum itakayoitwa Akaunti ya Fedha ya Pamoja na ambayo itakuwa ni sehemu ya mfuko mkuu wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambamo kutawekwa fedha yote itakayochangwa na Serikali Mbili kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume ya Pamoja ya Fedha kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge, kwa madhumuni ya shughuli za Jamhuri ya Muungano kwa mambo ya Muungano". Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kupata ufanuzi kutoka kwa Serikali kama matakwa haya yameshatekelezwa na Akaunti ya Pamoja imeishafunguliwa?

63. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani katika kuhitimisha hoja hii ya Katiba na Mambo ya Muungano, inatoa rai kuwa ili matatizo au kero za Muungano ziishe hatuna budi kurejea kwenye mapendekezo yaliyotolewa katika rasimu ya pili ya KATIBA iliyotolewa na Tume ya Marekebisho ya Katiba illyokuwa chini ya Uenyekiti wa Jaji Mstaafu Joseph Sinde Warioba kuhusiana na Muundo wa Muungano. Ibara ya 60(1) ya Rasimu ya Pili ya Katiba ya Muungano inaonesha matakwa ya wananchi kuhusu Muundo wa Muungano wautakao: "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa na Muundo wa shirkisho lenye Serikali tatu ambazo ni; -

- a. Serikali ya Tanganyika
- b. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
- c. Serikali ya Muungano.

64. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani kuitia sera yake uk. 13 &14 sura ya 2.4 inaeleza wazi aina na Muundo wa Muungano na kueleza malengo yatakayofikiwa kuwa ni kila nchi mshirika wa Muungano itakuwa na mamlaka kamili katika kumiliki na kutumia rasilimali na maliasili zake; isipokuwa masuala yote ya msingi ya jumla kama vile Katiba ya Shirikisho la Jamhuri ya Muungano, Mambo ya Nje na Ushirkiano wa Kimataifa, Ulinzi na Usalama, Uraia, Sarafu ya Benki Kuu, Mfumo wa Elimu, Mahakama ya Katiba na Bunge la Shirikisho yatashughulikiwa na Serikali ya Shirikisho.

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

65. **Mheshimiwa Spika**, Kama ilivyoainishwa katika Ibara 129 na ibara ya 130(1) (a) – (h) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ikisomwa pamoja na sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Na.7 ya mwaka 2001, kifungu cha 6 (1) (a) – (o) majukumu ya Tume ni pamoja na kufanya uchunguzi juu ya mambo yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora, kutoa ushauri kwa serikali na vyombo vingine vya umma na vya sekta binafsi kuhusu haki za binadamu na utawala bora na kufungua mashauri mahakamani ili kuzuia vitendo vya uvunjwaji wa haki za binadamu au ukiukwaji wa misingi ya utawala bora.

66. **Mheshimiwa Spika**, Haki za Binadamu na ambazo tume imepewa mamlaka ya kuhamasisha hifadhi yake zimeelezwa katika Katiba ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania, kuanzia Ibara ya 12 – 29 hata hivyo yamekuwepo matukio mengi yanayohusu uvunjifu wa haki za binadamu ambao kwa namna moja au nyingie watanzania walitarajia kuona Tume hii ikitumia mamlaka yake kikataba na kisheria kuzuia uvunjwji wa haki hizo za binadamu, matukio yafuatayo yanathibitisha ukweli huu;

Uvunjwaji wa Haki za Binadamu unaoendelea Loliondo.

67. **Mheshimiwa Spika**, kadiri miaka inavyozidi kusogea mbele vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu vinazidi kuongezeka ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Takwimu zinaonesha kwamba, mwaka 2017 ukiukwaji ulikuwa ni mkubwa ikilinganishwa na vitendo vya uvunjifu wa haki za binadamu kwa mwaka wa fedha 2016, kwa mwaka 2017. Mwaka 2018 kwa mfano Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazotaarifa za uvunjifu wa haki za Binadamu unaoendelea kufanyika dhidi ya wananchi wa Loliondo kufuatia vitendo vya Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na SENAPA kuwaondoa wananchi hao kwa nguvu katika eneo Ardhi yao na kuacha idadi kubwa ya wananchi bila makazi, mali zao zikipotea na pia wakiwa wamejeruhiwa.

68. Mheshimiwa Spika, Mapema mwezi August 2018 Jeshi la Polisi liliwakamata na kuwatia nguvuni Wenyeviti wanne wa serikali za vijiji amba ni Yohana Toroge, Mwenyekiti wa Kijiji cha cha Kirtalo, Kerry Ole Dukuny, ambaye ni Mwenyekiti wa kijiji cha Ololosokwan, Nekitio Ledidi ambaye ni Mwenyekiti wa kijiji cha Olerien na ndugu Kenyata Ole Sikoyo ambaye ni Mwenyekiti wa kijiji cha Arash. Kosa lao kubwa ni kuwaongoza wanakijiji wenzao kupigania haki na kupaza sauti zao dhidi ya uonevu wa kuwaondoa kwa nguvu wanakijiji wa Maasai mwishoni mwa mwaka 2018, Pamoja na vitisho ambavyo wamekuwa wakipata kutoka mamlaka mbalimbali za Serikali.

69. Mheshimiwa Spika, Pamoja na mgogoro huu amba umedumu kwa kipindi kirefu sasa dhidi ya makampuni ya uwindaji huko Loliondo yanayotetewa na Viongozi wa serikali kwa ngazi mbalimbali, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora hajjawahi kuchunguza wala kutoa kauli yoyote ya uvunjifu huu wa haki za wananchi na manyanyaso ambayo wamekuwa wakipata kwa kipindi kirefu. Aidha taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo zinaonesha kwamba viongozi hawa baada ya kuahamasisha wanachi kuchanga fedha na kufanikiwa kufungua kesi Mahakama ya Afrika Mashariki (East Africa Court of Justice) kipinga kuondolewa kwenye ardhi yao, viongozi hao walikamatwa na kufunguliwa mashitaka mbalimbali likiwemo kosa la kuhamasisha wananchi kuchangia fedha kwa ajili ya kufungua kesi katika mahakama ya Afrika Mashariki kwa kile ambacho kinaelezwu kwamba walichangisha fedha hizo bila kibali. Viongozi watatu baada ya kusota rumande kwa muda mrefu waliachiwa kwa dhamana huku Nekitio Ledid akiwa bado gerezani akisubiri maombi ya dhamana yake Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali na Tume ya Haki za Binadamu kutumia madaraka yake ya kikatiba na sheria yake kuhakikisha inatetea na kulinda uvunjifu wa haki za binadamu na ikiwezekana kufungua kesi mahakama kama sheria na katiba vinavyoelekeza.

70. **Mheshimiwa Spika**, Matukio ya uvunjifu wa haki za Binadamu na utawala bora yalilipotiwa pia Uvinza – Mkoani Kigoma, mapema October 16, 2018 ambapo Askari 3 wa Jeshi la Polisi waluuawa na wananchi katika mchakato wa kuwaondoa wakazi wa kitongoji cha Ng'wanduhubantu kijiji cha mpeta katika wilaya ya uvinza mkoani Kigoma baada ya kuibuka kwa vurugu kati ya wananchi na Jeshi la Polisi. Taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo ni pamoja na uvunjifu wa haki za binadamu lakini Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora haijawahi kuchunguza uvunjifu huu wa haki

71. **Mheshimiwa Spika**, Yapo matukio mbalimbali yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu ikiwemo haki ya kuishi, ambapo hivi karibuni kuliibuka sintofahamu baada ya kuripotiwa kwa mauaji ya watoto mkoani Njombe, ambapo hadi sasa ninaposoma ripoti hakuna ripoti maalumu iliyotolewa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Matukio ya Jeshi la Polisi kuua raia pia yameongezeka, vitendo hivi ni kinyume na haki ya kuishi, Ibara ya 14,

72. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia Jeshi la Polisi kwanza linachunguza mauaji yote ya Watoto hao wasio na hatia na kuwafikisha mbele ya vyombo vya sheria lakini pia Jeshi la Polisi lijitahimini dhidi ya Mauaji ya Raia waiokuwa na hatia ambao wamefariki wakiwa mikononi mwa Jeshi la Polisi na kuwachukulia hatua wahusika wote. Hata hivyo, Serikali itoe maelezo kuhusu sababu za kutoteuliwa kwa Mwenyekiti wa Tume pamoja na wajumbe wake kwa mujibu wa Ibara ya 129 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

[MANENO HAYA YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

MAHAKAMA INAYOTEMBEA (MOBILE COURT)

75. **Mheshimiwa Spika**, Siku ya Sheria Duniani, Mahakama ya Tanzania ilizindua kile kinachoitwa Mahakama zinazotembea. Dhana hii ya mahakama zinazotembea ni dhana inayomaanisha mahakama katika ngazi fulani kuhamisha huduma zake na kuzitolea katika sehemu

mbalimbali ndani ya mamlaka yake. Kwa mfano Mahakama ya ngazi fulani inapoamua kuhamishia shughuli zake kutoka eneo moja kwenda eneo lingine ndani ya mamlaka yake.

76. Mheshimiwa Spika, Pamoja na kwamba dhana hii imekuwepo toka siku za nyuma kwa historia yake lakini kinachoonekana kwa sasa ni dhamira ya kurejeshwa kwa Mahakam hizi ambazo lengo lake lilielezwa kuwa ni kuharakisha mashauri madogo ya madai kwa lengo la kuyamaliza haraka. Aidha kuna sababu pia zinazosemekana kwamba mionganoni mwa msukumo wa kuanzishwa kwa Mahakama hii inayotembea ni kumfuata shahidi kwa sababu ambazo zinatokana na ugonjwa au kuwapunguzia gherama mashahidi au iwapo kielelezo hakihamishiki kirahisi.

77. Mheshimiwa Spika, Kumbukumbu za Kambi Rasmi za Upinzani Bungeni zinaonesha kwamba, Serikali iliwahi kuleta muswada wa kuanzisha mahakama inayotembea lakini likakwama kwa ngazi ya kamati husika iliyochambua muswada huo baada ya Serikali kushindwa kuijengea hoja. Sasa Serikali kwa kupitia mahakama imeanzisha mahakama hiyo ambayo ilizinduliwa siku ya sheria duniani, kitendo hiki kimefanyika baada ya jitihada za kupita Bungeni kushindikana. Pamoja na nia njema ya kuwasaidia wananchi kupata huduma kwa karibu sababu ambayo inatajwa kuwa nyuma ya agenda hii, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda Serikali kutoa ufanuzi kuhusu mambo yafuatayo:

i. Je, Mfumo huu wa mahakama zinazotembea umezingatia kwa kiwango haki ya uwakilishi kwa wadaawa? Wadawa watakao kuwa na nia ya kuweka waheshimiwa mawakili wa kujitegemea na kutakiwa kuwasafirisha kutoka waliko hadi eneo ambalo mahakama hiyo itakuwa limezingatiwa kwa kiwango gani?

ii. Pili, madai ya kwamba lengo ni kusikiliza mashauri na kuyamaliza linamanisha nini, haki za kukataa rufaa kwa upande ambao haujaridhika inaelezwaje na ikiwa mashauri haya yatakuwa yanakatiwa rufaa uhakika wa kukamilishwa mashauri haya unatoka wapi?

iii. Gharama ya kununua gari moja na kulifanya huduma yaani service ni kiasi gani likiwa na kila kitu ndani yake dhidi ya gharama za kujenga Jengo moja la mahakama ambalo litadumu kwa miaka yote?

iv. Je, sababu ambazo zilielezwa kwenye Kamati za Bunge wakati serikali ikileta muswada ni zippi kwa kuzitaja na kila moja imetekeliezwa kwa kiwango gani.

v. Mwisho Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuleleza Bunge hili Tukufu ikiwa Serikali ilikamilisha sababu zilizotolewa na Kamati wakati ilipowasilisha mswaada huo, kwanini Serikali sasa haikurejesha mswaada huo Bungeni kama ilivyodhamiria awali?

79. Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha

.....
Salome Wycliffe Makamba (Mb)
**KNY. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI**
KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA
17 Aprili, 2019

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Salome Makamba, umesoma vizuri na umezingatia maelekezo ya Kiti. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, nirudie tangazo nillolitoa mapema, kuna mkanganyiko kidogo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa anaomba niwatangazie Wabunge wote kutakuwa na mhadhara kwa Umma kuhusu Mwelekeo wa Upatikanaji wa Chakula, Kukuza Mnyororo wa Thamani ya Uzalishaji wa Bidhaa Zinazotokana na Kilimo Duniani, saa 8.00 mchana, wote, siyo kwamba ni Wanakamati. Hii itakuwa ukumbi wa Pius Msekwa saa 8.00

mchana. Mgeni rasmi atakuwa Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa taarifa hapa, nanyi mnifundishe Kiswahili, nitamtaja baadaye aliyeleta *note* hii. Anasema hivi, katika taarifa aliyokuwa anasoma Mheshimiwa Salome kwa niaba ya Kambi, "amesema viongozi wamepigwa risasi kizembe." Kiswahili fasaha ni kwamba, hawa hawakupigwa vizuri. Sasa Mheshimiwa Nkamia haya, mimi nadhani mtaendelea kujifunza Kiswahili, lakini hiyo ndivyo alivyoisoma taarifa. (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walingumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Watakaoanza kuchangia...

Waheshimiwa tusikilizane tu. Watakaoanza kuchangia mchana kwa sababu ya muda wa leo, tutaanza na Mheshimiwa Upendo Peneza dakika tano na Mheshimiwa Peter Lijualikali naye dakika tano, *then* tutajipanga na wengine.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni leo.

(Saa 7.05 Bunge lilitishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae. Mchana wakati naahirisha Bunge nilikuwa nimewataja wachangiaji wetu wa kwanza jioni hii. Mheshimiwa Upendo Peneza.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia na ningependa zaidi kujikita katika suala la mrundikano wa mahabusu ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu ambazo zipo ndani ya nchi yetu, kwa hali ya magereza ni kwamba katika watu wote ambao wapo magereza/mahabusu ni asilimia 53.3. Pamoja na hayo pia tuna sheria ndani ya nchi hii ambazo ni kandamizi na zenyewe pia zinachangia kuongeza idadi ya mahabusu hao ndani ya magereza yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni Sheria ya *Money Laundering* na hizi za Uhujumu Uchumi ambazo zimebekwa na hazimpatii mtuhumiwa dhamana anapokuwa amekwisheshtakiwa. Sasa suala linalokuja ni kwamba, sheria hii sasa inatumika kuweza kuwaonea na kukandamiza watu na inawezekana hata baadaye ikatumika hata kuwaumiza watu kisiasa kwa sababu namna bora ya kuwaondoa watu katika maeneo ya nchi yao na kuwa huru ni kumpa mtu kesi ya *money laundering*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mfano wa kesi ambazo zinaendelea, kesi inaendelea kwa miaka minne, miaka mitano hakuna usikilizwaji wa msingi unaoendelea hata upelelezi wenyewe haujamilika. Sasa umempeleka mtu mahakamani kwa sababu gani kama upelelezi haujamilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba tunahitaji kuwa na utashi wa kisiasa kati ya Ofisi ya DPP, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mahakama zetu ili hatimaye kuweza kuondoaa hili tatizo. Kwa hilo, naiomba Serikali sasa iweze kuleta mabadiliko ndani ya Bunge hili, tuweze kubadilisha sheria hizo za *Money Laundering* ili tuache kuwaonea Watanzania, tuache kuwaonea watu ambao wanafanya kazi zao ndani ya nchi hii, kama mtu ana kesi, basi tutafute namna bora ya lawama hizi zisiweze kuendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna bora ambayo nadhani inaweza ikasaidia ni pamoja na kuwa na muda maalum wa kesi hizi kufanyika, hakuna muda ambao umewekwa kisheria. Tuwe na mfano, kama sheria zile za uchaguzi ambazo zina muda maalum kwamba kesi hii iishe

ndani ya muda Fulani. Kwa hiyo kama kesi humpi mtu dhamana, angalau basi uweke kwamba itakwisha ndani ya miaka miwili au mitatu, huyo mtu awe ameshaondoka na tatizo hilo liishe, kama mtu anafungwa ama kama mtu huyo anaachiwa huru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niweze kuchangia katika suala linalotuhusu sisi Wabunge wa Viti Maalum. Wabunge wa Viti Maalum tupo ndani ya Bunge kulingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 66. Hata hivyo, kuna kitu kibaya ambacho kinaendelea ndani ya nchi hii, kilianza ndani ya Bunge hili Tukufu lakini na viongozi wengi wanaokaa ndani ya Meza wamekuwa ni watu ambao wanakemea tabia hiyo ya kipuuzi, naomba niite hivyo, lakini sasa tabia hiyo inaendelea huko nje ambapo Mheshimiwa Humphrey Polepole, Katibu Mwenezi wa CCM, amesimama na kusema Wabunge wa Viti Maalum wa CHADEMA wanapatikana mpaka wapitiwe na Mwenyekiti wao. Sasa ifike mahali tutambue kwamba huo ni udhalilishaji ambao hauruhusiwi hata na sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Polepole amekuwa anafanya kazi kwenye asasi za Kiserikali kwa muda mrefu, sasa kama hatambui haki hizo za kimsingi ambazo zinatolewa hata na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni aibu kwa Chama cha Mapinduzi kuwa na Mwenezi anayedhalilisha wanawake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hilo naiomba...

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo...

MWENYEKITI: Ehe, hebu subiri, taarifa Mheshimiwa.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba amesema Katibu Mwenezi wa Chama, Humphrey Polepole ametamka kwamba Wabunge wa Viti Maalum wa CHADEMA wanapitiwa na Mwenyekiti wao. Sasa neno kupitiwa hatujaelewa labda atoe ufanuzi.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho naomba niseme ni kwamba ifike mahali nafasi za watu na vyeo walivyonyavyo viheshimiwe. Ni aibu kwa kiongozi wa nchi hii kusimama na kusema kwamba mafanikio ya mwanamke ya kisiasa yanatokana na shughuli za kingono. Tunawajengea watoto wetu fikra mbaya ndani ya vichwa vyao kwamba hakuna tena jitihada, jibu pekee ni waende wakalalane na watu huko watapata nafasi. Sasa hatuwezi tukaruhusu kuwa na viongozi wa namna hiyo. Kitu ninachokiomba sasa ifike mahali tulombe Wizara na Serikali utaratibu halisi wa upatikanaji wa Viti Maalum ujulikane. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, huu uchungu unaokuja sasa unajengeka na matusi ya namna hii...

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MHE. UPENDO F. PENEZA: ...ifahamike kwamba sasa tunahitaji mabadiliko ya Katiba kwa ajili tu...

MBUNGE FULANI: Taarifa ya ufanuzi.

MWENYEKITI: Sitaki taarifa sasa.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba tunahitaji pia mabadiliko ya Katiba ya nchi hii kwa ajili pia ya heshima ya mwanamke. Sasa ifike wakati Katiba iandike kwamba wanawake wakagombee, hata kama ni viti vya wanawake.

Mfano nchini Uganda, kuna viti vya wanawake lakini wanapigiwa kura na wananchi, inayotoa hata nafasi ya *accountability*, wananchi kuweza kumwajibisha Mbunge ambaye analipwa kwa kodi zao na Mfuko wa Jimbo wanapewa lakini... (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, dakika tano hizo. Mheshimiwa Lijualikali atafuatiwa na Mheshimiwa Ngonyani.

MHE. PETER A. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 4 Machi, 2019, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa ikulu alizungumza sakata la Mo Dewji na akasema anashangazwa na namna ambavyo polisi wameshughulikia. Pia akasema kabisa Watanzania sio wajinga, picha iliyochezwa haiingii akilini; ni maneno ya Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa *IGP* akasema ndani ya siku nne atatoa taarifa, atasema kinagaubaga nini kilichotokea, leo ni siku ya 42, *IGP* kachuna, kakaa kimya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azory Gwanda amepotea, ama amepotezwa hatufahamu, hayupo duniani ama sijui yupo wapi hatujui. Mheshimiwa Lissu kapigwa risasi mchana kweupe, Ben Saanane mpaka leo hajulikani yupo wapi. Watu wameokotwa kwenye mifuko ya sandarusi kwenye fukwe za bahari ya nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia maneno ya Rais aliyomwambia *IGP* na akasema Watanzania sio wajinga, kwenye kitu ambacho kilikuwa wazi, ambacho hakijajificha cha Mo Dewji, Rais akasema hapa haiko sawa na *IGP* akasema kwamba hili ndani ya siku nne nitalishughulikia, hivi kama hivi imefanyika kwa Mo Dewji, jambo lipo wazi kiasi hiki, hawa akina Mheshimiwa Lissu, hali ikoje, akina Ben Saanane, watu wa kawaida hali ikoje? Ni mambo mangapi yanafanyika katika nchi hii kwa taswira hii ambayo watu hawapo *accountable* kwa hayo mambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza jambo hili ni fedheha, kitendo cha *IGP* kutamka hadharani atatoa majibu ndani ya siku nne halafu mpaka leo amekaa kimya na Serikali wamekaa kimya, jambo zito kama hili, hii inamaanisha kabisa kwamba nchi yetu haina utawala wa kisheria. Hii inamaanisha kabisa kwamba Serikali ya CCM hawajibiki kulinda raia wa Tanzania; ni mfano wa dhahiri kabisa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hivyo ndivyo jinsi ilivyo, naomba iundwe tume maalum ya kufuatilia mambo yote haya na tume hii iwe na hadhi ya kimahakama. Kama Rais anaweza akatoa jambo na akasema Watanzania wana akili, wameona kuna matatizo na *GP* akasema ni kweli ndani ya siku nne nitatoa maelezo, leo siku ya 42 amekaa kimya, maana yake kuna mambo mengi katika nchi hii hayapo sawa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa tume ikiundwa yenye nguvu ya kimahakama, ipitie mambo yote; ipitie jambo la Ben Saanane, Azory Gwanda, Akwilina na Mheshimiwa Lissu. Mambo yote haya yaje na ikiwezekana hii tume ije iripoti Bungeni ili Wabunge tuweze kusema *way forward* nini kifanyike kwenye nchi yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Sheria ya Uhujumu Uchumi na Utakatishaji wa Fedha. Hii sheria inawezekana kabisa iliundwa kwa nia njema kabisa lakini kwa jinsi ambavyo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, dakika tano hizo.

MBUNGE FULANI: Mbona tatu.

MWENYEKITI: Haya wewe endelea kujiaminisha hivyo. Tunaendelea, nilimtaja Mheshimiwa *Engineer Ngonyani*

dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Musukuma, dakika tano.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Dkt. Augustine Mahiga, baba yangu na kwa kweli nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi kubwa wanazozifanya. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuridhia kuanzisha zile taasisi mbili zinazojitegemea, moja Kurugenzi ya Mashtaka na Ofisi ya *Solicitor General*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa sababu sasa tunaamini mambo ya haki yatafanyika vizuri zaidi kuliko ilivyokuwa katika mfumo wa zamani. Nimeona bajeti imeongezeka kwa sababu tumeanzisha taasisi tofauti na bajeti yake sasa hivili mekuwa kubwa na mnakumbuka kipindii cha nyuma aliyekuwa Mwanasheria Mkuu alikuwa analalamika sana kuhusu bajeti, lakini nina uhakika sasa huyu Mwanasheria Mkuu wa sasa amepata bahati kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni dakika tano tu, naomba niongelee kitu kimoja tu kidogo cha kuhusiana na matumizi ya Mfuko wa Mahakama. Nimwombe sana Mheshimiwa Dkt. Augustine Mahiga, Waziri wa Katiba na Sheria atusaidie sisi Wananaamtumbo, tuna idara ya mahakama pale ngazi ya wilaya inafanya kazi vizuri sana, lakini mazingira walijonayo sio mazuri. Wamekaa katika majengo ambayo ni ya kuazima na kwa bahati mbaya sasa hivi wamezungukwa na Kituo cha Afya cha Namtumbo. Nimwombe aingize katika bajeti ya mwaka huu Wilaya ya Namtumbo kujengewa Mahakama ya Wilaya ili pale walipo sasa waweze kupisha shughuli za Kituo cha Afya kipyaa kabisa cha Namtumbo kiweze kufanya kazi vizuri zaidi kuliko kuchanganya haya mambo mawili katika eneo moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa fursa, nilitaka niliongelee hilo jambo moja, dakika tano sio

muda mrefu, ni kwa sababu tu unapoanza kuongea moja kwa moja unaanza kwenye hoja, lakini ukianza kuogelea maeneo mengine unajikuta muda umeisha, hoja uliyotaka kuongea unaikosa na ni kitu ambacho wenzetu inabidi wajifunze ili tuweze kwenda vizuri katika kuwatumikia wananchi wetu majimboni kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kauli hiyo, naomba nisisitize Mahakama ya Wilaya ya Namtumbo ipate fursa ya kujengwa... (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer Ngonyani*.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Niseme tu kiukweli Mheshimiwa Waziri na Serikali ni vizuri wakaangalia uwezekano wa kurekebisha sheria, hasa kwenye makosa madogo madogo ambayo ndiyo yamepelekea magereza yetu mengi yamejaa mahabusu kwa kesi ambazo kiukweli zingine zinastahili tu hata makofi mtu anaenda nyumbani. Kwa hiyo, nashauri sana, hizi sheria zilitungwa Watanzania tukiwa milioni 20, leo tupo milioni 55 bado mtu anawekwa mahabusu wiki mbili kwa kesi ya kuiba kuku. Ni vitu ambavyo kiukweli lazima tufikirie adhabu ambazo zitawenza kupunguza mrundikano wa mahabusu kule ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; nimeona kwenye taarifa ya Waziri katika mahakama zilizojengwa zimo na ya

Geita, Chato na Bukombe na mimi natokea Geita ambako kumejengwa mahakama hiyo. Nimwombe tu Mheshimiwa Waziri, aongeze msukumo mahakama ile iweze kukamilika. Sio kweli kwamba imekamilika kama alivyoandika kwenye kitabu chake na tunaona kesi kubwa zinakwenda kufanya kwenye vyumba vya Wakuu wa Wilaya, sio haki. Ni vizuri tukayakamilisha yale majengo ili yaweze kutoa haki kwa wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilikuwa nasoma kwenye Kitabu cha Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusiana na uteuzi wa Majaji pamoja na kwamba yameondolewa lakini ukiangalia kwenye Katiba, Ibara ya 109(7) na (8) pale inampa mamlaka Mheshimiwa Rais kuteua na anakuwa na jopo ambalo linamshauri. Ningewashauri tu wenzangu, ni vizuri tukamuachia Rais madaraka yake, akafanya kazi kwa mujibu wa Katiba yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho; nimeongea hapa nasikia rafiki yangu Mheshimiwa Sugu ananiita mboyoyo, nakubali, sawa, lakini Watanzania wanajua kati yangu mimi na wewe mboyoyo ni nani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; dada yangu, Mheshimiwa Upendo nilikuwa namuuliza tu kwa nia nzuri, amesema Humphrey Polepole amesema uteuzi wa wanawake wa CHADEMA unapatikana mpaka wapitiwe na Mwenyekiti. Mimi sikuelewa Kiswahili ndiyo maana nikauliza kwa sababu ninavyofahamu Humphrey yupo sawa; yule ni Mwenyekiti wa chama lazima apitie majina ya watu wake, kuna tatizo gani analolalamika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa namna ya pekee naomba nipongeze mhimili wa Mahakama kwa kufanya kazi vizuri. Hata huo mrundikano wa kesi tunaouona ni kwa sababu watu

wana imani kubwa na mahakama na ndiyo maana wanakwenda kupeleka mashauri yao. Hapa nimeona complain kubwa katika Kitabu cha Hotuba ya Kambi ya Upinzani wanasema mahakama haina uhuru, yaani kama mahakama inaingiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhuru wa mahakama umeanzia kwenye Katiba ibara ya 107B, ambayo inasema: *"Katika kutekeleza mamlaka ya utoaji wa haki, mahakama zote zitakuwa huru na zitalazimika kuzingatia tu masharti ya Katiba na yale ya sheria ya nchi."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuipa mahakama uhuru wake umeanzia kwenye Katiba, lakini wenzetu wanashindwa kutofautisha kati ya Mahakama za Hakimu Mkazi, wanawapongeza Majaji kama sio sehemu ya mahakama. Utaratibu wa maamuzi ya mahakama ya chini kupelekwa katika Mahakama ya Rufaa ni utaratibu wa kimahakama; uwe umeshinda au umeshindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wao hawaziamini mahakama za chini lakini wanawapongeza Majaji, hawajui Majaji na wenyewe ni sehemu ya mahakama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, limeongelewa suala la Katiba. Kupanga ni kuchagua. Hata baba anapopata hela nyumbani matatizo yapo mengi anaamua na ndiyo maana hata wao hela ya ruzuku inapopatikana wanaamua kukopeshana Wabunge kununua magari; japokuwa hawana ofisi wanashindwa kujenga ofisi, wanakopeshana Wabunge kununua magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuendelea kudumisha utawala wa sheria na Katiba pamoja na kuboresha sheria mbalimbali. Tumeshuhudia Sheria ya Madini imefanyiwa marekebisho, sheria ambayo ilikuwa kandamizi. Pia Sheria ya Vyama vya Siasa ambayo ilikuwa kandamizi ambapo ilikuwa inatoa mianya ya baadhi ya Wenyeviti ruzuku inapopatikana wanaolea mke wa pili na watatu badala ya kufanya vitu vingine vya vyama. Sheria

za Mitandao, sisi viongozi ni waathirika wakubwa sana wa sheria mbovu za mitandao ya kijami. Tulikuwa tunashuhudia Wabunge, wanamziki na watu maarufu wanazalilishwa. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kuweka sheria kali za mitando ili kukomesha tabia hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya *Statistics*, jana hapa tulishuhudia Mheshimiwa Mbunge akisema Mkoa wa Tabora peke yake wanafunzi waliopewa mimba kwa mwaka mmoja ni 70,000. Takwimu hizi zinaenda kwa watu huko, watu wengi hawasomi wengi wanapata *data* kutokana na kusikiliza. Sasa sheria zikiwa mbovu watu watakuwa wanapata taarifa ambazo siyo sahihi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Vyombo vyा Habari, vyombo vyा habari zimekuwa nguzo kubwa ya kuzalilisha watu na kutoa taarifa za uongo. Kwa hiyo, hata sheria kali zilizowekwa sitasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa upotoshaji mkubwa ambao unafanywa na vyombo vyा habari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ia mwisho, Mheshimiwa Mbunge mmoja ameomba uwekwe utaratibu katika Katiba Maalum juu ya upatikanaji wa Viti Maalumu vyा Wanawake. Navyofahamu mimi kila chama kimepewa mamlaka ya kuteua Wabunge wa Viti Maalum. Kwa mfano, CCM kuna makundi ya wanawake mikoani wanachaguana wenyewe mikoani, vyuo vikuu, vijana na walemaru. Kwa hiyo, kila kundi limeweka utaratibu wake wa kuwapata kwa kupigwa kura. Sasa wenzetu wana utaratibu wao ambapo wameachia watu wachache wanafanya huo uchaguzi na ndiyo maana umeona analalamika kuwa Mheshimiwa Polepole amewasema vibaya lakini hao hao wanalalamika kwa Katiba haijasema wanapatikanaje.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Mussa Mbarouk dakika kumi atafuatiwa na

Mheshimiwa Zito Kabwe dakika kumi ajiandae Mheshimiwa Bulembo dakika tano.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia kukutana katika kikao chetu hiki tukaweza kuzungumzia masuala mbalimbali ya nchi yetu. Sitaacha kuwakumbuka na kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Tanga Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko katika kuitisha bajeti ya Wizara ya Sheria na Katiba. Kwanza nianze kwa masikitiko kidogo kwa sababu sheria nyingi Tanzania bado ziko katika utaratibu ule ule wa kikoloni labda niseme kwa sababu zinaandikwa katika lugha ambayo kwa Watanzania siyo lugha mama kwao. Matokeo yake wengi hawaelewi na wanapata kigugumizi na wakati mwingine wanafanya makosa kwa sababu sheria hawazitambui na hawazifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kutoa ushauri kwa Serikali, sheria zetu ziandikwe katika lugha zote mbili iwe lugha ya Kingereza lakini pia katika lugha ya Kiswahili ambayo *our mother tongue*.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu nimeshudua kwa sababu mara nyingi...

MWENYEKITI: Eeh, umesemaje? Hebu rudia tena.
(Kicheko)

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi nimeshudua sheria zetu hizi kutokana na kuandikwa Kingereza matokeo yake wengine wanakuwa hawazifahamu. Kwa hiyo, niseme tu kwamba kama tunavyotayarisha vipeperushi mbalimbali hasa kwa wenzetu wa vijiji au kuzifanya ziende katika makala mbalimbali za

magazeti kuwe na kurasa ambazo zinatafsiriwa sheria mbalimbali ili wananchi waweze kusoma na kuzielewa. Kwa sababu lugha inayozungumzwa katika Mahakama zetu unakuta wananchi ama washtakiwa au washitaki wengine hawaelewi na mwingine anakuwa hana Wakili wa kumuwakilisha katika kesi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulipitisha sheria hapa kuwapatia Watanzania usaidizi wa kisheria kwa maana kuwapata Mawakili wa Serikali. Labda Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atueleze ni kesi ngapi Watanzania wamepatiwa hawa Mawakili wa Serikali kuwasaidia kuwatetea katika kesi hizo? Kwa sababu mpaka leo bado kuna tatizo kubwa la uwakili na wananchi wetu asilimia kubwa hawana uwezo gharama za uwakili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojua kesi ni gharama na Mawakili wana gharama kubwa. Labda niipongeze Serikali kwa ile azma nzuri ya kutoa usaidizi wa kisheria kwa wananchi lakini mpaka leo hakuna taarifa yoyote iliyotolewa kwamba wananchi kadhaa kesi zao zimesimamiwa na Mawakili wa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri na kuweka msisitizo kwamba Serikali itumie fedha na iongeze bajeti kuhakikisha sheria zinatafsiriwa katika lugha ya Kiswahili. Pia hizo tafsiri ziwe katika vipeperushi au majarida mbalimbali ili ziende mpaka kwa wananchi. Kwa sababu wakati mwingine mtu hana usaidizi lakini amefanya kosa na utetezi hauwezi na katika sheria tunaambiwa *ignorance of law is not a defense*, hii ndiyo kubwa inayofanyika lakini watu wanaendelea kufungwa, kuwekwa mahabusu na wanaendelea kufanya makosa kwa sababu hawaelewi tafsiri ya kisheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuna sehemu imesemwa hapa kwamba Tanzania tumeridhia Mkataba wa Afrika kuhusu suala la demokrasia lakini leo ni mwaka wa sita sisi bado hatujaweka saini. Naomba Waziri atakapokuja hapa aelete ni kwa sababu zipi mpaka leo sisi hatujasaini lakini tulishiriki katika kuridhia mkataba huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu hiki kuna kipengele kinasema kwamba hivi sasa miaka sita imepita tangu Tanzania ishiriki na kuitisha Azimio kuhusu masuala ya demokrasia, chaguzi na utawala bora liliopitishwa na Umoja wa Afrika ambapo Tanzania ni mwanachama. Mkataba huo ulipitishwa na Umoja wa Afrika wakati wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Serikali za Umoja wa Afrika 30 Januari, 2007. Lengo la mkataba huu ni kuzitaka nchi wanachama kuzingatia na kutekeleza utawala bora utawala wa sheria na haki za binadamu kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 3 na 4 ya mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu hili suala linatutia aibu kama Tanzania. Tanzania kama tunavyosema sisi ni kisiwa cha amani na Tanzania katika mambo mengi ndiyo mfano wa kuigwa vipi tuna kigugumizi katika suala hili la kutia salini huu Mkataba wa Demokrasia, Utawala Bora pamoja na Haki za Binadamu? Hili ni jambo kubwa na zito katika Afrika na dunia kwa ujumla, sasa Waziri atuleleze kwa nini mpaka leo miaka sita imepita bado hatujasaini mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala hili la kupiga marufuku mikutano na maandamano. Jambo hili lipi katika sheria ya nchi sasa inakuwaje tunapiga marufuku mikutano, maandamano hali ya kuwa ni jambo ambalo limo ndani ya sharia? Inakuwaje wananchi wakose haki yao ya kikatiba kwa sababu Katiba ndiyo sheria mama na ndiyo iliyotoa ruhusa hiyo kwa nini tuzuie mikutano ya hadhara, maandamano hali ya kuwa tunaona katika nchi za wenzetu kupitia maandamano na mikutano hata inapokuwa wananchi hawamkubali Rais anajiondoa. Kwa mfano, Rais wa Algeria, wananchi, Jeshi na wanafunzi wamefanya maandamano na hapakuwa na umwagaji damu kumetokea mapinduzi baridi Rais yule ameondoka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika baadhi ya nchi wananchi wanapokuwa hawaridhishwi basi wanapoandamana wanakuwa wamepeleka ujumbe wa jambo fulani. Kwa mfano, baadhi ya nchi bei ya mkate inapoongezeka au fedha yao kupungua thamani au

mfumuko wa bei kuzidi wanafanya maandamano ya amani ambapo hauliwi hata sisimizi na matokeo yake Serikali inakubali na inafanya marekebisho na mambo yanakwenda vizuri. Kwa hiyo, mimi niseme suala hili la kuzuia mikutano ya hadhara na maandamano tujitanzame upya ili tuweze kutoa ruhusa na ukiangalia tunaelekea katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Mimi napenda Tanzania ionekane ni mfano wa kuigwa katika mambo mengi hasa haya ya demokrasia pamoja na utunzaji wa haki za binadamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni dhamana. Katika Bunge liliopita niliwahi kuzungumza hapa nikaiomba Serikali, tena nilimwomba Mheshimiwa Rais kupitia kwa huyu Mkurugenzi wa Mashtaka (*DPP*) kumtaka kwamba wale Wabunge wenzetu...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika kumi tayari?

MWENYEKITI: Ndiyo.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Naona umeweka tano.

MWENYEKITI: Hapana, ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Zitto Kabwe dakika kumi, Mheshimiwa Abdallah Bulembo atafuatiwa Mheshimiwa Mchengerwa, dakika kumi.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kupata nafasi ya kuchangia mafungu mbalimbali katika Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mzee wangu Mheshimiwa Balozi Mahiga kwa uteuzi wake wa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Naamini kwamba uzoefu wake katika Mambo ya Nje utaweza kusaidia kwa kiwango

kikubwa kazi kubwa iliyoko katika Wizara hii. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Mahiga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitoe shukrani za dhati kwa Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanikisha ufunguzi wa Mahakama Kuu, Kanda ya Kigoma. Mahakama hiyo itaweza kutusaidia sana watu wa Kigoma kuweza kupunguza mwendo wa kwenda Tabora kwa ajili ya kufuatilia kesi mbalimbali. Kwa hiyo, naomba salamu zangu kwa Jaji Mkuu ziweze kufika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mawili tu ambayo ningependa kuya-*address*. Jambo la kwanza linahusiana na mashauri mbalimbali ambayo Serikali yetu inakabiliwa nayo katika Mahakama mbalimbali za Kimataifa na namna gani bora ya kuweza kuhakikisha kwamba maslahi ya Taifa kwa maana ya *public interest* yanazingatiwa katika kukamilisha mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara kadhaa siku za nyuma nimekuwa nikishauriana kwanza Waziri, Mheshimiwa Kabudi na baadaye Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba kuna baadhi ya kesi ambazo sisi tumeshtakiwa lakini tuna vithibitisho vya kuhakikisha kwamba sisi tusishitakiwe katika kesi kama zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi mojawapo ni ambayo inafanyika sasa na imeshaamuliwa kati ya Tanzania na Benki ya *Standard Chartered* ya Hong Kong ambayo mwaka jana ilikuwa ni *audit query* kwenye Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na mwaka huu nimeona Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameweuka Jedwali la Utekelezaji na ameeleza kwamba *TANESCO* kwa kushirikiana na Serikali iko katika mchakato wa kutekeleza *Deed of Indemnity* iliyotumiwa na Bwana Harbinder Singh Sethi kwa niaba ya *IPTL* na Benki ya Tanzania kwa ajili ya Serikali ya Tanzania kutatua madai yanayotarajiwa na *Standard Chartered Bank - Hong Kong* ikiwa *TANESCO* itashindwa. Hii ni kesi ya zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 148.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala ambalo napenda Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Serikali nzima iweze kulieleza kwamba *public interest* yetu hapa ni fedha ambazo zilichotwa kutoka Benki Kuu kurejeshwa. Ndiyo *public interest* yetu hapa, *public interest* siyo kuwaweka watu ndani na fedha zile zikosekane. Sasa kwa sababu tuna *Deed of Indemnity* na tayari mazungumzo yanaendelea, Serikali inaweza kulifahamisha Bunge ni hatua gani inazichukua ili watu ambao wamewaweka ndani waweze kushirikiana na Serikali, *Deed of Indemnity* ifanye kazi tuondokane na haya madai ambayo sisi tunadaiwa. Kwa hiyo, naomba hili Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wenzake waweze kutupatia majibu kwa sababu ni jambo ambalo linaweza kuokoa mabilioni ya fedha iwapo tutalifanya kwa maarifa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kesi ambayo sitaki kuizungumzia kwa undani, ya *Standard Bank* ya Mzee Kitilya ya zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 6. Wote tunafahamu kwamba kuna Benki ya Kimataifa ambayo iwapo raia wetu wangetumika kama mashahidi nchi yetu tungeweza kukwepa mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 600 ambao sisi tunaamini kwamba ulipatikana kwa njia za rushwa. Hata hivyo, Serikali yetu badala ya kufanya kazi na raia wake inawaweka ndani raia wake, inarefusha kesi wakati kuna deni hapa ambalo kila mwaka tunalipa riba na thamani ya shilingi inaporomoka na gharama ya deni inaongezeka. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashindwa kuelewa Serikali hapa hekima yake ni ipi? Hekima yake ni kuhangaika na Dola milioni 6 na kuwaweka watu ndani au hekima ni kuokoa mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 600 ambao kama tuki-prove kwamba ulipatikana kwa rushwa mkopo ule nchi yetu haitaweza kuulipa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nipate maelezo ya Serikali inatumia hekima gani katika hili? Au inaona raha tu kumweka Kitilya ndani au inataka kumkomoa Kitilya na wenzake? Kwa nini hatufanyi maamuzi ambayo

public interest ni kubwa zaidi kuliko kuumiza watu kama ambavyo tunafanya? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni jambo ambalo nililzungumza kwenye bajeti ya mzee wangu Mheshimiwa Mkuchika, suala la Ofisi ya DPP. Majibu ambayo Mheshimiwa Mkuchika aliyatoa pamoja na kwamba aliongea kwa busara sana lakini sikuridhika nayo kwa sababu mateso ambayo wananchi wanapata kutokana na ubambikiwaji wa kesi na majadiliano ya pembeni ambayo hayafuati sheria kwa sababu hatuna sheria ya *pre-bargain* tunawaonea raia wetu sana. Naomba Serikali iweze kutazama na ni jambo rahisi sana.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Kuhusu utaratibu, Kanuni gani?

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Niambie Kanuni kwanza.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64.

MWENYEKITI: Nitajie Kanuni kwanza nijiridhishe.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu ya Kanuni ya 64, Kuhusu Utaratibu, Mheshimiwa anayezungumza.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

WABUNGE FULANI: Kanuni ya 64(1)(c).

MWENYEKITI: Haya endelea.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji anayezungumza anazungumza vizuri lakini utaratibu ni kwamba kesi ikishakuwa iko Mahakamani haitakiwi kuzungumziwa humu ndani Bungeni. Kwa hiyo, mzungumzaji anavunja Kanuni za Bunge.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto, nilikuvumilia tu kwa sababu huendi kwa undani, hitimisha tu ile *point* yako. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachokiona ni kwamba mfumo wetu wa jinai (*criminal justice system*) ni mfumo ambao umejaa uonevu, unaweka mazingira ambapo tunawatesa raia wetu na unapaswa kufumuliwa. Ili mfumo huu ufumuliwe sawasawa lazima tuanze na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka (*DPP*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachokiomba na nitatumia Kanuni ya 120(2)(a) ya Kanuni za Bunge kwamba mara baada ya mjadala huu kukamilika, nitatoa taarifa kwamba Bunge liunde Kamati Teule kwa ajili ya kuchunguza, kufanya *probe* ya makubaliano ambayo Ofisi ya *DPP* inafanya na watu ambao walikuwa watuhumiwa na kutoa fedha, kwa sababu fedha zingine zinatolewa pembedni, wanazungumza unaambiwa mpelekee mtu fulani, malalamiko mtaani ni makubwa sana. Ukiyasikia malalamiko hayo unaumia, mtu yoyote anayependa *justice* anaumia. Haiwezekani mfumo wetu wa mashtaka ndiyo ukawa mfumo wa kukomoa watu, ikawa kama ni *Kangaroo Court* ikawa watu wanaonewa, unakamatwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana muda umekwisha. Mheshimiwa Bulembo dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa dakika kumi.

MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kabla ya

yote nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Katibu Mkuu na Majaji wote wanaotoa haki katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianzie hapa, Mheshimiwa Balozi kabla hujateuliwa kuwa Waziri katika eneo hilo alikuwepo Waziri mmoja anaitwa Mheshimiwa Kabudi. Mheshimiwa Kabudi nilimuuliza kuhusu Mahakama ya Wilaya ya Misenyi. Wilaya ya Misenyi ina miaka zaidi ya 25, ipo *boarder* na ina kesi nydingi, nikaambiwa bajeti inayokuja Misenyi itakuwepo, kitabu chako hakina Misenyi. Mahakama ya Wilaya haionekani ndani ya kitabu hiki. Sitaki kusema sana Mwanasheria na Waziri tukitoka tuongee kidogo ili mjue utaratibu mtaufanyaje wa Mahakama ya Wilaya ya Misenyi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu Mahakimu wetu wa Mahakama za Mwanzo. Ni kweli tunajenga Mahakama za Mwanzo, tunarekebisha na kadhalika lakini haki inaanza chini, hawa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo maisha yao mnayajua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu Mahakimu wetu wa Mahakama za Mwanzo. Ni kweli tunajenga Mahakama za Mwanzo, tunarekebisha, tunafanya nini, lakini haki inaanza chini. Hawa Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo maisha yao mnayajua; ambao wanaanza na kesi ili mtu akate rufaa mpaka Mahakama Kuu, mazingira waliyonayo mnayaona?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu, hebu nafasi, wapeni haki ili haki itendeke na watu waweweze kuona kwamba haki inaonekana. Maisha yao jamani yanatisha. Sitaki kuingia sana kwa undani lakini naomba Mheshimiwa Waziri pale alipo, hebu akakae na Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo aone wanaishije na wanafananaje ili haki ipatikane. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni wasaidizi wa Majaji. Hawa nao wana haki sawa na Mahakimu. Hivi hawa stahili zao ni zipi jamani? Ndio wanamsaidia Jaji kuandaa, kuandika

na kadhalika. Hali zao ni dhofulhali, samahani nitumie kauli hiyo. Hebu wapeni *value* na wao, maana wakitoka pale mnawateua kuwapa nafasi za juu, lakini kazi zao ni ngumu na maisha yao ni magumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kitabu cha bajeti humu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika bajeti ya maendeleo haina hata shilingi, lakini ofisi hii ndiyo inafanya kesi zote za nje, ndiyo inasafiri, tunaenda kushindwa. Kuna nini hapa? Kesi za Kimataifa ziko kwenye ofisi yake, hamkumpa hela ya maendeleo hata shilingi moja, atafanyaje kazi? Au tumemaliza kesi za Kimataifa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kuna Mahakama kama za rafiki zangu akina Mheshimiwa Bashe hawa. Wamejenga wenyewe, wamejenga maboma, wanatakiwa kumaliziwa, kwa nini msingekuwa mnaenda kwa hawa watu ambao wameshatarahisishia kazi ili wakapata huduma hiyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nampongeza Mheshimiwa Waziri, najua ameingia hivi karibuni bado ana siku chache, lakini hayo machache yanamtosha. Mwakani tutakuwa na mengi sana ya kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Mchengerwa.

MHE. MOHAMED O. MCHENERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba amani na utulivu wa Taifa letu ni misingi iliyooachwa na Waasisi wa Taifa hili katika kuimarisha Serikali, Bunge kusimamia Serikali na Mahakama kuachwa kuwa huru katika kuamua mashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere miaka ya themanini aliwahi kusema kwamba zipo kazi ambazo kila

Mtanzania anaweza kufanya, lakini mionganoni mwa kazi hizo, siyo kuwa Hakimu au kuwa Jaji. Mwalimu Nyerere alizingatia kwamba Katiba yetu ya mwaka 1977 lakini nyakati za upatikanaji wa uhuru, yako mambo mengi ambayo Watanzania pengine wangependa kuwa nayo. Nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ameendelea kufanya uteuzi wa Majaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi kifupi kilichopita, tume pata Waheshimiwa Majaji vijana kabisa na tunaipongeza Serikali kwa sababu Waheshimiwa Majaji hawa wataweza kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 20 na kupata uzoefu mrefu zaidi kuliko kuteua mtu ambaye amekuwa mtu mzima na anashindwa kufanya kazi vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, Msemaji ame-*challenge* mamlaka ya Mheshimiwa Rais kuteua Majaji akiishutumu Tume ya Utumishi wa Mahakama aki-*cite* Ibara ya 113 kwamba inashindwa kumshauri vyema Mheshimiwa Rais. Naomba nimkumbushe msemaji kwamba ajiongoze katika Ibara ya 109, ibara ndogo ya (7) pamoja na ibara ndogo ya (8). Mheshimiwa Rais hafungwi na masharti katika uteuzi wa Waheshimiwa Majaji. Mheshimiwa Rais ana uwezo wa kumteua Jaji ye yeyote, kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa katika ibara ndogo ya (7) au vile atakavyoona yeye mwenyewe inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa katika taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu demokrasia. Msemaji katika ukurasa wa 15 amesema kwamba Tanzania haifuati misingi ya demokrasia iliyoainishwa katika *chapter* mbalimbali za Umoja wa Mataifa pamoja na Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimkumbushe Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba demokrasia siyo *Coca Cola*. Niseme haya kwa kuwakumbusha Watanzania wote kwamba hotuba iliyotolewa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Baba wa Taifa, kwenye Mkutano Mkuu Maalum wa Chama cha Mapinduzi, hotuba hii ilitolewa

tarehe 18 mwezi Februari, 1992 naomba ninukuu baadhi ya maneno ambayo Mwalimu Nyerere aliwahi kuyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere alisema kwa sauti yake kwamba "Utaratibu wa kidemokrasia uliobora kwa nchi yoyote, yaani utaratibu utakaofaa kwa nchi hiyo utatofautiana wakati wowote kati ya nchi moja na nchi nyiningine na hata kati ya nchi moja, utaratibu utakaofaa utatofautiana kipindi kwa kipindi. Demokrasia si bidhaa kama Coca Cola ambayo nchi moja inaweza kuagiza kwa fedha za kigeni kutoka nchi nyiningine na nchi zote duniani zikawa zinakunywa Coca Cola ile ile; na ole wake nchi yoyote ambayo haina fedha za kigeni." (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni maneno ya Julius Kambarage Nyerere aliyowahi kuyasema wakati huo. Naomba niwakumbushe tu wenzangu kwamba demokrasia zinatofautiana, nami napenda niishauri Serikali kutoridhia mikataba ya namna hiyo kwa sababu hatuvezi kufanana. Demokrasia iliyopo Tanzania haiwezi kufanana na demokrasia iliyopo Misri pamoa na nchi nyiningine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nitoe ushauri. Tanzania kuna Wilaya zaidi ya 169, lakini kati ya Wilaya hizo, Wilaya 27 tu pekee ndiyo zenye Mahakama za Wilaya ambazo ziko katika mamlaka ya usikilizwaji wa mashauri katika wilaya hizo. Wilaya zaidi ya 87 zinaazima majengo mbalimbali katika maeneo husika. Pia Wilaya zaidi ya 23 wanategemea kutoka kwenye mamlaka ya wilaya za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali, kwa kuwa mamlaka ya uanzishwaji wa mikoa na wilaya ni mamlaka ya Serikali, naiomba Serikali, wakati inaandaa mpango mkakati wa kuanzishwa wilaya, basi pengine wafikirie ni namna gani wanawezza kuisaidia Mahakama kwa kuanzisha majengo ya Mahakama, lakini wakati fulani inakuwa ni aibu kwa Mahakama kwenda kununua ardhi au kutafuta ardhi ya kujenga Mahakama za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali wakati inafikiria kwenda kuanzisha Mamlaka za Wilaya na Mikoa, izingatie pia kwamba ipo Mahakama ambayo imetamkwa kwenye Ibara ya 107 kwamba ni muhimu kuwepo kwa Mahakama katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kushauri ambalo nimejaribu kulieleza katika taarifa yangu, ni marekebisho ya sheria Na. 2 ya mwaka 2018 ambayo yamempa mamlaka makubwa Mkurugenzi wa Mashtaka. Naiomba sana Serikali, namwomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuona uwezekano wa kuleta marekebisho ili Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, basi iweze kupata *proceeds* ya kiasi cha fedha ambayo inaokoa wakati wa uendeshwaji wa mashauri yale ya uhujumu uchumi na mashauri mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili nimelizungumza vizuri sana kwenye taarifa yangu na naomba nisisitiza kwa Serikali, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuona uwezekano wa kuleta marekebisho ya sheria au kwa kutumia kanuni ili mwongezea mamlaka Mkurugenzi wa Mashtaka kuweza kupata kiasi cha fedha kidogo ambacho kinaweza kusaidia. Eneo hili, siyo tu kwa Mkurugenzi wa Mashtaka, hata vyombo vingine vinanufaika na maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kusisitiza ni kuhusu mlundikano wa mahabusu. Wiki kadhaa zilizopita tulimsikia Mheshimiwa Rais akitoa maelekezo kuhusu moja ya kesi za jinai ambazo mtu mmoja alishitakiwa kwa kosa la mauaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, lakini pia tuiombe sana Mahakama. Sheria Na. 2 ya mwaka 2018 imetoa maelekezo fasaha kabisa kuhusu jukwaa la haki jinai. Nami niseme kwamba Mahakama imepata bahati kubwa sana kwa kumpata Jaji Kiongozi ambaye aliwahi kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka, ana ufahamu mzuri sana kwenye eneo hili. Sheria hii imeelezea utaratibu wa haki jinai. Tumwombe Mkurugenzi

wa Mashtaka atumie jukwaa hili ili kupunguza mlundikano wa mahabusu Magerezani na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia imezungumzwa kuhusu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mchengerwa kwa mchango wako.

MBUNGE FULANI Mwongozo, mwongozo wa Spika.

MHE. MOHAMED O. MCHENERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, msinichezee nikiwa nimekalia kitii hiki. (*Kicheko*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbozi lenye vijiji 63 na kata 11 lina Mahakama mbili tu za Mwanzo. Naomba kwa niaba ya Wananchi wa Mbozi Serikali iweze kukarabati jengo la Kijiji cha Igamba, Jimbo la Mbozi ili lianze kutumika. Miaka ya nyuma jengo hili lilitumika kama Mahakama ya Mwanzo, Igamba. Jengo hili likikarabatiwa litafanya Jimbo la Mbozi kuwa na Mahakama tatu za Mwanzo za Itaka, Mlowo na Igamba. Hivyo, ni vema Serikali ikawasaidia wananchi wa Igamba ili kuwaepusha na safari ndefu ya kwenda kutafuta huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Mahakama ya Mwanzo Itaka licha ya kwamba inatumika lakini imechakaa sana hivyo, Serikali ichukue hatua za haraka ili kulinusuru jengo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Wilaya Mbozi iliyopo Mji wa Vwawa ipo katika hali mbaya sana. Ukumbi wa Mahakama ni mdogo sana na miundombinu mbalimbali kama vile vyoo vipo katika hali mbaya sana. Mahakama ya Wilaya ya Mbozi kwa sasa ndiyo Mahakama ya Mkao wa Songwe. Naishauri Serikali ikarabati Mahakama hiiili iweze kuwashudumia wananchi wa Mkao wa Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Mahakimu waongezwe mishahara ili wafanye kazi wakiwa na ari nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nkasi ina umri wa miaka 40 lakini Makao Makuu ya Wilaya Namanyere haina jengo la Mahakama ya Wilaya wala Mahakama ya Mwanzo. Cha ajabu sana kila mwaka hotuba ya Waziri utakuta Namanyere watajenga jengo la Mahakama lakini mwaka huu hakuna kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ajabu sana Makao Makuu ya Wilaya hakuna jengo la Mahakama ya Mwanzo wala ya Wilaya wakati wilaya mpya zimepewa fedha za majengo ya Mahakama ya Wilaya, hii si haki kwa Wilaya ya Nkasi. Wilaya ya Nkazi tunahitaji jengo la Mahakama kama Wizara iliyoadidi kwenye bajeti ya mwaka 2017/2018 na 2018/2019.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara ya Katiba na Sheria na hasa Mahakama kwa kusimamia sheria na haki za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri Serikali, kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Bajeti, kuhakikisha fedha zilizotengwa kwa maendeleo zipelekwe ili kukamilisha miradi ya maendeleo. Maeneo mengi yakiwemo mijii na mijii midogo haina Mahakama au miundombinu imechakaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji Mdogo wa Mbalizi hauna jengo la Mahakama badala yake shughuli za Mahakama zinafanyika kwenye jengo lililopo katika soko kwenye

msongamano mkubwa. Napendekeza na kusositiza Wizara iharakishe ujenzi wa Mahakama ya Mbalizi kwa usalama wa watumishi wa Mahakama na hata watuhumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza kuunga mkono hoja hii. Wilaya ya Nyang'hwale haina Mahakama ya Wilaya na jengo la Mahakama, wananchi wanafuata huduma hiyo Geita umbali wa kilomita 180 kwenda na kurudi. Kwa hiyo, ni gharama kubwa hadi kesi kuisha na wengine kushindwa kumudu gharama za kwenda mara kwa mara Mahakamani hadi kufutwa kwa kesi na kukosa haki zao. Je, ni lini Serikali itaanzisha Mahakama ya Wilaya ya Nyang'hwale? Je, ni lini Serikali itaanzisha ujenzi wa jengo la Mahakama Wilaya ya Nyang'hwale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani iliyosomwa na Mheshimiwa Salome Makamba kwa niaba ya Mheshimiwa Lissu Antiphas.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mlimba lenye Kata 16, Serikali imeanza ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo, Kata ya Mlimba na jengo limefika juu (boma). Ingawa boma limeisha mwanzoni mwa Machi 2019 lakini vibarua wa ujenzi ambao ni wakazi wa Mlimba ambao idadi yao yapata 19 hivi hawajalipwa. Je, huyo mkandarasi hajalipwa hadi ashindwe kulipa waliofanya kazi? Naomba mkandarasi huyo afuatiliwe na awalipe vijana hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ilete marekebisho ya Sheria ya Polisi kukamata watuhumiwa walioachiwa na Makahama na hapo hapo Askari Polisi kuwakamata kwa kutumia kifungu 225. Kifungu hicho

kimepitwa na wakati kwani kinasababisha mlundikano wa mahabusu kwenye magereza na vituo vy'a polisi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri viongozi wa Wizara hii watembelee magereza nchini na magereza zote zaMkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwepo muda maalum wa kuchunguza kesi za jinai nchini kwa kuwa magerezani kumekuwa na wananchi wengi na wanakaa muda mrefu hadi miaka 10 mahabusu kusubiri kukamilika kwa upelelezi. Upo ushahidi usio na shaka kwa mahabusu wengi kusota maregeza muda mrefu kwa kuwa hawana msaada wa kisheria na pesa za kutoa rushwa kwa wapelelezi. Nashauri mttembelee magereza na kuongea na mahabusu ili mpate taarifa muhimu zinazohusu rushwa.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri lakini niwapongeze Katibu Mkuu na viongozi wote wa Wizara hii.

Mheshiimiwa Mwenyekiti, nipongeze Serikali kwa jithihada kubwa za uamuvi wa kujenga Mahakama Kuu na Mahakama za Wilaya maeneo ambayo hayakuwa na Mahakama. Napenda kujua ni lini Mahakama ya Wilaya ya Kilindi itakamilika maana toka msingi ukamilike, mkandarasi ameondoka *site*. Napata maswali mengi kwa wananchi wa Kilindi kwamba ni lini Mahakama hiyo itakamilika? Wameisubiri Mahakama hii kwamuda mrefu sana. Natumai Mheshimiwa Waziri nitapata majibu ya swali hili ili nikawajibu wananchi wa Kilindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni ushauri kwa Wizara hii, tumeshuhudia baadhi ya miradi imesimama mfano Shirika la *NHC*, wakandarasi wapo *site* na gharama zinaendelea kuongezeka. Ili Serikali isije kuingia kwenye migogoro na kulipa gharama za kumweka mkandarasi *site* kwanini Wizara isifuatilie miradi yote ambayo siku za usoni inaweza kuileta Serikali hasara zisizokuwa za lazima kwa kuangilia mikataba

yote ambayo hajakaa sawa? Tumeshudia haya kwenye maeneo ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ndiyo yenyeye kusimamia haki na utawala wa sheria zilizowekwa na vyombo mbalimbali vya maamuzi. Katiba ndiyo Sheria Mama na hivyo ni muhimu mno Wizara hii kutekeleza majukumu yake kwa weledi na bila ubaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi katika kipindi hiki tunashuhudia jinsi Katiba yetu na sheria halali zinavyo kiu kwa. Mfano, tumeona na kusikia matamko yasiyofuata kabisa Katiba, Sheria na Kanuni yakinolewa hadharani tena bila woga, kama vile zuio la mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa wakati Sheria ya Vyama vya Siasa inaruhusu nakutokulipa watumishi wa Serikali *annual increments* na ama nyongeza ya mishahara ilio kisheria eti kwa kigezo fedha zinaenda kwenye miradi mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendo vya ukiukwaji washeria siyo tu vinakomoa wapinzani bali kutia doa nchi yetu ambayo ilionekana kama nchi yenyeye amani na utulivu na nchi ya kipekee (*unique*). Ileleweke kwamba bila haki hakuna amani wala upendo. Hivyo basi, tuna kila sababu ya kusimamia haki, Katiba nasheria ili nchi yetu iwe na amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matukio mbalimbali yanayoashiria Ofisi ya Taifa ya Mashtaka haifanyi kazi zake vizuri ama kwa makusudi ama kwa hofu. Baadhi ya mambo tunayoyalalamikia ni pamoja na kutekwa kwa mfanyaabiashara maarufu Mohamed Dewji, kupotea kwa Ben Saanane, Azory, kupigwa risasi kwa Mbunge Mheshimiwa Tundu Lissu na kupotea kwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kibondo na kadhalika. Pamoja na matukio haya na mengine mengi Ofisi hii ya Mashtaka na Mkurugenzi wake amekuwa kimya kwa kutochukua hatua licha ya malalamiko mengi ya ndugu, jamaa na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa hakuna anayeweza kutengua uteuzi wa Mheshimiwa Rais ila yeye mwenyewe, hasa tukijua ni suala la kikatiba lakini pale inapoonekana waziwazi kuwa kuna mazingira yanayoonesha teuzi zinakuwa fadhila kwa jambo lililofanyika, tuna kila sababu ya kushauri. Wote tunajua Viongozi wa Kambi ya Upinzani akiwemo Mheshimiwa Mbowe wako kwenye Shauri Na.112 la 2018. Shauri hili linadhaminika lakini Hakimu wa Mahakama ya Kisutu aliwanyang'anya dhamana na kupelekwa mahabusu Segerea kwa siku 104 (zaidi ya miezi mitatu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichonishangaza ni Hakimu huyu kupandishwa cheo na kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Hata kama alikuwa amefikia kupandishwa cheo mtu yejote ataamini ni fadhila kwa kuwa muda ulikuwa mfupi mno. Hata hivyo, rufaa ya Mahakama ya Rufaa na Mahakama Kuu ilidhihirisha kuwa Hakimu huyo alikiuka utaratibu na hivyo dhamana ikawa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki kucheleweshwa ni haki kunyimwa. Wote tunajua wananchi wengi hawajui sheria lakini pia kesi nyingi zinachukua muda mrefu huku mahabusu wakiendelea kusota rumande. Mfano, kuna watu wamekaa rumande kwa miaka hadi sita bila kuhukumiwa na kwa sheria zetu hata mtuhumiwa akihukumiwa, ule muda aliokaa rumande hauhesabiki. Huu ni unyama na ukatili. Tunaishauri Serikali iliangalie suala hili ili watuhumiwa wasikae mahabusu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naiomba Serikali ijenge Mahakama za Mwanzo na za Wilaya ili haki ziweze kupatikana kwa wakati na kuwaondolea wananchi usumbufu wa kwenda mbali kutafuta haki zao.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia kuhusu watu kuteswa wanapokamatwa na na Polisi kabla Mahakama hajasema kama mtu huyo ana kesi ya kujibu au la. Je, nikifungu gani cha sheria kinachompa

Askari Polisi haki ya kumpiga mtuhumiwa na kumtesa kabla ya Mahakama kuamua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la kubambikiziwa kesi. Hivi sasa kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa wanabambikiziwa kesi na hawapelekwi Mahakamani kwa wakati. Je, kwa kufanya hivi siyo kuvunja sheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna changamoto kubwa katika ujenzi wa Mahakama katika Wilaya mbalimbali nchini. Jambo hili linapelekea wananchi wengi kuanza kutumikia kifungo kabla ya kufikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki ya kupata taarifa. Sheria iliyotungwa imepelekea maumivu makali kwa Watanzania. Kupata habari/taarifa ni hakli yao ya msingi wakati wote watakaohitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndoa za utotoni. Sheria inayoruhusu ndoa za utotoni imekuwa kandamizi kwa wananchi wa Tanzania kwani kwa kiasi kikubwa kwa sasa inatumika vibaya kukandamiza watoto wa kike na kuzima ndoto zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni juu ya mikataba mibovu tunayoingia. Suala hili la kuingia mikataba mibovu inapelekea Taifa kuingia kwenye hasara kubwa na kupelekeea umaskini kwa uzembe kwa kutopitia mikataba hii vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi wa Mahakimu kuanzia Mahakama ya Mwanzo. Kulingana na kazi wanazofanya za kuhukumu watu ni vyema jambo hili likaangaliwa upya kwani watu hawa wanahitaji ulinzi wakiwa kazini na nje ya kazi.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nataka kuweka mkazo kwa mchango wangu kuhusu umuhimu wa utawala wa sheria na haki, utaratibu wa kukamata watu kwa tuhuma ambazo *DPP*

hana ushahidi si sawa kabisa. Kuwaweka watu rumande kwa muda mrefu halafu mchezo wa "uchunguzi haujakamilika" si sawa kabisa, ni uonevu, hakika. Kama mtu anatuhumiwa kutenda kosa uchunguzi ufanyike na sheria ichukue mkondo wake lakini mtindo mpya wa kubambikiziwa mtu kesi au *charge* ambazo hazina dhamana kusudi asote rumande miaka nenda, miaka rudi, si haki, si sawa na ni kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magereza zimejaa watu ambaao wametuhumiwa makosa ya kawaida mfano, *traffic case* lakini wamenyimwa dhamana wako jela miezi hata miaka. Katika Gereza la Muleba nimeshuhudia wanawake waliokekwa mahabusu ili wapishe waume zao kuuza mashamba ya familia. Nimeshuhudia watu walio mahabusu muda mrefu kwa sababu ya ugomvi. Hata kesi za mauaji inabidi ziwekewe mkazo na uchunguzi ufanyike na *Nolle prosequi* zitoke kwa muda muafaka na zisipotoka basi kesi zisikilizwe kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mhimili wa Mahakama uko huru na ni muhimu sana uhuru huo udumishwe. Mhimili wa Mahakama sharti ujitathimini. Tunashuhudia baadhi ya Mahakimu hasa ngazi za Mahakimu wa Mwanzo na Wilaya wakila rushwa za waziwazi, unakuta Hakimu Mkazi anafanya mtandao na viongozi wenyeji wenye uwemo kuwanyanyasa wananchi kwa kubuni kesi ambazo zinahukumiwa na mtu anashindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nililalamikia Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ya Mubunda huko Muleba, Ndugu Omar Musa kwa tabia yake mbaya kutoa hukumu kwa dhuluma. Hakimu huyu alipokuwa Mahakama ya Mwanzo, Kashasha, Wilayani Muleba alisababisha mtoto kumfunga mama yake mzazi katika mgogoro wa shamba. Nililazimika kulipa faini aliyokosa huyo mama iliatoke mahabusu lakini huyo mama alikuwa siku mbili baadaye kwa huzuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hakimu huyo alipohamishiwa Mubunda akajingiza katika kesi za Diwani

wa Kata ya Kashurunga, Ndugu Khalid Swalehe na kuwafunga Mwalimu Mkuu wa Shule huko Kimeyo na mke wake na baadaye Mwenyekiti wa Kijiji cha Nkomero katika mgogoro wa eneo la ardhi ya shule. Diwani anataka kupora eneo la shule na mwalimu na mke wake na Mwenyekiti wanatetea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa juhudzi zangu kutetea suala hili hadi leo zimeshindwa. Nimeambulia kutolewa tamko la Chama cha Majaji na Mahakimu Tanzania (*JMAT*) juu ya matamshi ya Mbunge wa Muleba Kusini dhidi ya Mahakama isiyo na tarehe lakini iliyosainiwa na Rais wa chama hicho, Jaji Wilberforce Samson Luhwago. Ni tamko la *pages* saba linanilaani mimi kwa kulalamikia Mhimili wa Mahakama mara kwa mara na hatimaye kulalamika katika mkutano wa hadhara mbele ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naambatisha tamko hilo ili liwe sehemu ya *Hansard* ya mchango wangu. Yaani mimi mtu wa kawaida ninatolewa tamko na Chama cha Mahakimu na Majaji kwa kufanya kazi yangu ya Ubunge ambayo ni kutetea wananchi na kuijulisha Serikali na Mhimili wa Mahakama juu ya mapungufu waliiyonayo ili wayafanyie kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo juu ya suala hili na hatma yangu nikiwa na kesi Mahakamani nani ataisikiliza kwani tamko hilo liidaiwa ni la Majaji na Mahakimu wote. Kwa dharau kabisa hadi leo Hakimu Omar Musa bado hajahamishwa kutoka Mubunda hivyo kunipa kazi ya ziada kuwatuliza wananchi wenye hasira wasifanye fujo. Naomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali alitolee ufanuzi jambo hili na kunielekeza juu ya utaratibu wa kusikiliza kesi zangu zinapokuwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba Mhimili huu katika kujitathmini waangalie mtindo mpya wa baadhi ya Mahakimu wasio waadilifu kufanya kazi na Mawakili wasio waadilifu. Kwa hiyo, mtuhumiwa unaelekezwa naHakimu

kama unataka kushinda kesi kamlete *advocate* fulani. Mhimili huu ujitathmini kwani changamoto za rushwa zinawaumiza watu ambao *niinnocent*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na watendaji wote kwa kuleta hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika eneo la urejeshwaji wa wahalifu wa kimataifa katika makosa ya jinai (P.36). Tanzania inapakanana nchi za jirani za Maziwa Makuu. Kwa mfano, Mkoa wa Kigoma umepakana na nchi jirani za Congo DRC, Rwanda na Burundi. Kuna matukio mengi ya kihalifu yanayohusishwa na raia wananchi jirani kuvuka mipaka kuingia Tanzania na kufanya uhalifu kwa kupora mali za wananchi, kuteka, kubaka na wakati mwagine kufanya mauaji. Matukio kama haya yanatokea Kakonko, Kobondo na Kasulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwagine nashawishika kuamini kwamba wahalifu hao wa kigeni wanao wenyeji wanaowawezesha kuingia na kutoka nchini bila kutiwa nguvuni. Je, Wizara inazo taarifa za wahalifu wa kigeni (wakiwemo wakimbizi) katika Mkoa wa Kigoma ambao wamerejeshwa nchini ili wajibu mashtaka? Katika eneo hili, naishauri Wizara kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani hususan Polisi na Uhamiaji ili kudhibiti wimbi la uhalifu unaoaminika kutekelezwa na wenyeji kwa kushirikiana na wageni ambao inasemekana wakishavuka mipaka kwenda kwao hawapatikani kwa urahisi kuja kujibu mashataka yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Muumba wa Ulimwengu na vilivyomo ndani yake tukiwemo sisi wanadamu. Aidha, napenda tujue kwamba Allah ana sheria zake ambazo tunapaswa tuzitii na kuzifuata. Vilevile

na sisi binadamu tumeandaa sheria zetu na kanuni ili kuzifuata na kuzitii ambazo ni sheria za nchi husika zinazotutaka kila raia kuzifuata na hakuna mtu aliye juu ya sheria. Kwa maana nyiningine, ndiyo tukatengeneza Katiba ambayo ni Sheria Mama ya nchi yetu Tanzania. Ndiyo maana Bunge na Wabunge wako hapa kuilinda Katiba na hata Kiongozi wa nchi naye huapa kuilinda Katiba hii hii, kwa kuwa hakuna aliye juu ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria ndiyo Wizara nyeti na Wizara ambayo husimamia majukumu ya Katiba, Sheria, Kanuni na utaratibu zilizowekwa na vyombo halali vyta maamuzi. Baada ya kutoa ufanuzi huo, ama utangulizi huu napenda kutoa maoni yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na upotoshaji na uvunjifu wa Sheria na Katiba yetu kwa wananchi na viongozi wa nchi na kuwa juu ya sheria, jambo ambalo siyo zuri na ni baya sana na litapelekecha uchafuzi wa demokrasia na amani ya nchi, kwa sababu kuna ambao wako juu ya sheria na kuna ambao wako chini ya sheria; jambo ambalo ni baya sana na nalipinga kwa nguvu zote na naomba Bunge lako lipinge na Wizara husika itoe kauli na kupinga vikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi ambacho Taifa hili linapitia katika changamoto na ugumu mkubwa ni kipindi hiki. Kumekuwa na changamoto ya kutoheshimu utawala bora wa sheria; ni kipindi ambacho Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Sheria mbalimbali za nchi na Kanuni zote hazifuatwi, badala yake kuvunjwa sheria kwa makusudi. Kwa hiyo, Wizara ya Katiba na Sheria ndiyo Wizara yenye jukumu la kuhakikisha kuwa nchi hii inaongozwa kwa kuzingatia Katiba ya nchi hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na msisitizo huu kuwekwa kwenye maneno ya utangulizi (*Preamble*) ya Katiba yetu, tangu mwishoni mwa mwaka 2014 mpaka leo, ninapotoa maoni yangu, nchi yetu imekuwa ikipitia katika kipindi kigumu cha janga la Kikatiba ambapo Serikali ya CCM haisimamii misingi ya Katiba ya mwaka 1977 wala haina

mpango wowote madhubuti wa kurejesha mchakato wa Katiba pendekewza ya Jaji Warioba ya mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inathibitishwa na kauli ya Mheshimiwa Rais kuwa hajawahi kuahidi kuhusu Katiba Mpya na wala haikuwa sehemu ya ahadi zake za Kampeni kauli inayokinzana na llani ya uchaguzi ya CCM ambayo katika ukurasa wake wa 206 – 207 kipengele cha 145(e) inasema " Ili kuendeleza utawala bora, demokrasia na uwajikaji katika kipindi cha miaka mitano ijayo 2015 – 2020, CCM itahakikisha kuwa Serikali inatekeleza yafuatayo: (e) Kukamilisha mchakato wa kutunga Katiba Mpya na kuanza kuitekeleza kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba." Mwisho wa kunukuu. Kwa hiyo leo hii Serikali ya Chama cha Mapinduzi inakana llani yake iliyoinadi kwenye uchaguzi na badala yake inaikanyaga Katiba kupitia viongozi wake. Huko ni kuvunja uaminifu na maadili ya Chama na Serikali yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwa na uvunjifu wa sheria na ukiukaji wa Katiba na Utawala Bora kwa mambo ambayo yanaendelea kujitokeza katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Tano ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli. Kuna ushahidi wa kimazingira unayoonesha baadhi ya uteuzi kufanya kwa fadhila baada ya wahusika kufanya vitendo vyta kuwanyima haki watu wengine kwa lengo la kutekeleza matakwa ya utawala. Mfano, uteuzi wa Hakimu mmoja kutoka Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa Jaji wa Mahakama ya Tanzania, ni mionganini mwa teuzi ambazo zinaonesha ushahidi wa kimazingira kwamba ni fadhila kwake baada ya Hakimu huyo kufuta dhamana ya Kiongozi Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman A. Mbewe, pamoja na Mbunge wa Tarime Mjini Mheshimiwa Esther Matiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi wa Jaji ulikuwa ni fadhila kwake baada ya kutekeleza hila au kile ambacho alielekezwa na mamlaka zilizomtuma ama kujipendekeza. Hali hii haikubaliki kwenye nchi ambayo inasimamia vizuri Demokrasia, Sheria, Kanuni na Utaratibu tuliojiwekea katika Katiba ambayo tuliahidi kuilinda na kuifuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, narudia kuwa hakuna mtu aliye juu ya sheria. Kwa hiyo, ni wakati wa kutenda haki na kusimamia Utawala Bora wa Sheria na kutimiza ahadi zetu tulizoweka mbele ya Mungu kwa kiapo.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja hii kwa kuanza na Mahakama. Mahakama nyingi zimechoka hapa nchini hasa Mahakama zilizoko vijiji, hazina vyoo, vitendea kazi, samani na vinginevyo. Hata Mahakimu wakitoa hukumu, upatikanaji wa hati unakuwa mgumu kwa kuwa ni vigumu kupata hati au hukumu ya kesi iliyochapisha kwa kukosa vifaa. Nashauri Serikali izingatie hilo hasa katika mkoa wangu wa Iringa kwa zile Mahakama za ngazi ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba za Mahakimu ni chache, hili inahatarisha usalama wao, kwani wengi wao wanaishi uraiani, mitaani na wamepata usumbufu. Serikali ihakikishe inajenga nyumba za Mahakimu. Mahakama nyingi hazina mahabusu na kunapotokea wahusika kupelekwa Mahakamani inakuwa ni gharama pia kwa kuwa hawana sehemu ya kuhifadhi mahabusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mishahara ya Mahakimu na posho kama vile posho ya nyumba lakini waendesha mashtaka wanapewa posho, hivyo na Mahakimu wapewe pia posho. Mfumo wa mashtaka ni mbovu, wananchi wengi wanaonewa sana, haki haitendeki. Nashauri mfumo huu ufumuliwe na uundwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia uchunguzi unachukua muda mrefu sana.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jimbo la Mikumi lina Kata 15 na katika Kata hizo zinapata taabu sana ya kutokuwa na Mahakama na zile zenye Mahakama zinachangamoto zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama nyingi hazijapimwa au kurasimishwa na kusababisha wananchi

kuingilia na kufanya shughuli mbalimbali za kibinadamu kwenye maeneo ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni uchakavu mkubwa wa majengo ya Mahakama za Jimbo la Mikumi. Mahakama nyingi zimechakaa sana na hazina umeme wala vyoo kitu kinacholeta usumbufu kwa watumiaji wa Mahakama zetu na watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni ofisi kutokuwa na nembo ya Taifa na Bendera. Mahakama zetu za Jimbo la Mikumi, mfano Kata ya Mikumi na Kata ya Malolo hazina nembo ya Taifa na kupunguza heshima ya Mahakama zetu. Mahakama zetu hazina samani za ofisi, mfano *computer*, mashine za kurudufu hukumu, makabati ya kuhifadhi nyaraka mbalimbali muhimu. Hii inasababisha malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi maana wanakosa haki yao ya kupata hukumu ya kesi na kuambiwa waje siku nyingine hata kama hukumu imeshatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linginei ni mahabusu. Mahakama nyingi ziko mbali na vituo vya Polisi au Magereza na kusababisha Mahakama kupata shida ya kuwahifadhi watuhumiwa, mfano Mahakama ya Kata ya Malolo ipo zaidi ya kilomita 200 kutoka Kituo cha Polisi na kusababisha usumbufu mkubwa wa kusafirisha wafungwa. Inabidi mtuhumiwa atoe shilingi 60,000/= kwa nauli wakati ni wajibu wa Serikali na ikishindwa inabidi hakimu alipe hela yake ya mfukoni inakuwa ngumu sana. Tunaomba Polisi waje kuwachukua wafungwa ili kupunguza mzigo kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nichangie kuhusu upungufu wa watumishi wa Mahakama. Kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mishahara ya Mahakimu na watumishi wa Mahakama ni midogo. Vile vile posho za nyumba; Mahakimu ni watu muhimu sana kutokana na aina ya kazi zai wanazofanya wanastahili sana kupata posho za nyumba kama wanayopata waendesha mashtaka, maana

mahakimu wengi wanaishi mbali sana na maeneo ya Mahakama ambapo hawajapewa na Serikali nyumba za kulishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokakana na kazi yao ya kutoa haki sawa na kuhukumu, Mahakimu wanastahili sana wapewe ulinzi wa kutosha maana kutokana na kazi yao watuhumiwa wengi wanaokutwa na hatia wanawatisha sana Mahakimu wetu na kutishia usalama wao hasa kwa kuzingatia Mahakimu wengi wanaishi mitaani bila ulinzi wa uhakika na usalama wao na kuhtarisha maisha yao. Ahsante sana.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hadi sasa Tanzania haina Tume Huru ya Uchaguzi, naomba Serikali kuunda Tume Huru ya Uchaguzi ili kutenda haki na kudumisha demokrasia ya kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Katiba ya sasa ina upungufu mwingi, mfano muundo mzima wa kupata uongozi unaondoa uhalali wa Katiba hiyo. Hivyo, naomba Serikali iendeleze mchakato wa kupata Katiba mpya maana Kipengele kilichobaki ni kupiga kura kwa Katiba hiyo mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na kutokutenda haki kwa Mahakama zetu nchini. Mahakimu wengi wamekuwa wakifuata maelekezo ya Serikali katika kutoa haki badala ya kusimama kama mhimili unaojitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna malalamiko ya wananchi kuhusu uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masuala ya haki za wanawake, watoto na walemauvu; nashauri Serikali ijipange

kuyachunguza maeneo haya ili uvunjifu huu uishe. Wanawake wananyanyasika sana, hususan katika jamii na Magerezani. Ni kwa nini Serikali hii ya Awamu ya Tano imeshindwa kumaliza malalamiko haya ambayo kila siku yanaongezeka kuititia vituoni, Polisi na Mahakamani? Hii inasababisha kuteseka kwa wanawake na watoto ambao kimsingi ni kundi kubw. Hivyo Serikali iondoe malalamiko haya mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mlundikano wa mahabusu Magerezani na Vituo vya Polisi, mamlaka inayoshughulikia masuala haya imeshindwa kumaliza jambo hili. Gereza la Kalika, Nkulunkulu lililopo Mpanda mpaka leo mahabusu na wafungwa wanafanyiwa vitendo viovu na Askari Magereza na hawana sehemu ya kulalamika wakihofia maisha yao, kwa sababu hawa Askari wanaishi nao. Wanapoumwa hawashughulikiwi vya kutosha na kusababisha afya zao kuwa duni na ukizingatia wanalandikana katika Magereza hayo ambayo kiafya inakiuka haki za kimsingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, Serikali imeshindwa kutatua kwa sababu malalamiko bado yanaongezeka. Je, Serikali haionti kwa kushindwa mambo haya inafanya makusudi kupoteza nguvukazi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni vita dhidi ya rushwa. Matatizo ya kiuhalifu yataendelea kuongezeka kwa sababu baadhi ya Askari wasio waaminifu wamekuwa wakipokea rushwa na kuwaacha walalamikaji wakiishi katika maisha ya wasiwasi. Mahakama na Polisi ikishindwa kudhibiti mianya ya rushwa na tunaamini katika vyombo vya sheria ndiyo sehemu pekee inayoweza kutafsiri makosa, hii inaleta tafsiri mbaya katika jamii na wananchi wataamua kujichukulia hatua mkononi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni ukarabati wa majengo ya Mahakama za Wilaya na Miko. Bado hali ni mbaya na hairidhishi katika Mahakama zetu. Uhifadhi wa mafaili ya kesi hypotea; hii inaleta picha mbaya kwamba

na Mahakama zetu zinashindwa kulipa kipaumbele jambo hili.

MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la haki za binadamu kwa nchi yetu ya Tanzania ni wimbo wa mdomo, lakini kiutekelezaji hakuna kabisa. Ni miaka 58 tangu nchi yetu ipate uhuru, lakini katika maeneo ya mahabusu, Vituo vyta Polisi na Magereza nchi nzima haki za binadamu hakuna kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia suala la haki za binadamu, tunagusa mambo mengi ikiwemo kusikilizwa, kutibiwa, malazi na sehemu ya kujisitiri kiafya. Hadi leo wanajisaidia mahali pa wazi huku wengine wanamwona. Isitoshe sehemu wanayojisaidia na chakula wanalia hapo hapo na kulala hapo hapo. Kutenda kosa kunamwondolea mtu kuwa siyo binadamu. Naomba Mheshimiwa Waziri anapohitimisha hoja hii atoe majibu, ni lini sasa suala hili litakoma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikitika kuwa hotuba ya Katiba na Sheria katika kipindi ambacho Taifa linapitia katika changamoto ya kutoheshimu utawala wa sheria, ni kipindi ambacho Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na sheria mbalimbali za nchi na kanuni zake hazifuatwi; ni kipindi ambacho matamko yasiyozingatia tena Katiba, sheria na kanuni yanatolewa hadharani kwenye majukwaa ya siasa na wakati mwingine hutolewa kwa waraka bila woga wowote; ni kipindi ambacho dira ya ofisi nydingi za Serikali imejielekeza inafanya nini ili mtu afurahi zaidi. Kwa maneno mengine, dira ni kumfurahisha mtu zaidi kuliko kuzingatia matakwa makuu ya katiba na sheria za nchi yetu.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umuhimu wa marekebisho ya Katiba kwa ajili ya kupata Tume Huru ya Uchaguzi, kwa nini wanasiasa wanatakiwa kuwa Wakurugenzi wakati ni *returning officer* wa chaguzi za Jimbo? Mfano, Mhagama aliyekuwa Katibu wa CCM Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mlundikano wa maabusu wakati kesi zao zinadhaminika ilihali wanatumia fedha za Umma katika kuwa-*sustain*, kumekuwepo na ucheleweshwaji mkubwa wa kesi kunakosababishwa na Ofisi ya Taifa ya DPP, Mwendesha Mashtaka, kwani maelezo ya Polisi mara zote yamekuwa, *file* bado liko kwa DPP.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kurejeshwa haraka kwa mchakato wa Katiba mpya, ufanyike mara moja kwani Katiba zilizopo zinaonesha upungufu mkubwa na imeendelea kupigwa kelele. Vile vile sheria ya maudhui ya mtandao inaonesha nia mbaya ya Serikali ya Awamu ya Tano katika kutoa maoni na uhuru wa kujieleza licha ya kuwa na vifungu vinavyo kiuuka mikataba ya Kitaifa. Hivyo ifutwe mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Serikali kujikita kwenye *sensorship* ya vyombo vyya habari hasa magazeti kuititia Msemaji Mkuu wa Serikali, hii ni kilitia aibu Taifa na kuonesha ubeberu wa kiutawala.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa hatua mbalimbali katika kuhakikisha haki na utu wa kila Mtanzania unathaminiwa kwa kuimarisha Wizara hii muhimu katika kusimamia usawa na upatikanaji wa Hakimu katika kutafasiri katiba na sheria mbalimbali.

Hata hivyo, nawapongeza pia wateule wote walioko chini ya Wizara hii wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri Augustine Mahiga bila kuwasahau watumishi wote walioko katika Wizara hii.

Mmheshimiwa Mwenyekiti, ni Sera ya Taifa kuwa kila kata nchini iwe na huduma ya Mahakama ya Mwanzo na kila Wilaya kuwa na Mahakama za Wilaya, lakini katika Wilaya la Liwale pamoja na kuwa ni Wilaya ya siku nydingi, tangu mwaka 1975 Wilaya hii ina Kata 20 lakini ina Mahakama mbili tu ya mwanzo, yaani ile ya Liwale mjini na ya kata ya Kibutuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wilaya ya Liwale hadi leo haina jengo la Mahakama ya Wilaya. Jengo linalotumiwa ni lle liliokuwa la Mahakama ya Mwanzo ya Liwale Mjini. Upo uhitaji mkubwa sana wa jengo la Mahakama Wilayani Liwale, sambamba na uwepo wa watumishi wa kutosha. Wilaya pia inahitaji kuwa na Mahakama ya Mwanzo kwenye Kata za Lilombe na Miruwi kwa kuwa kata hizo zina shughuli mbalimbali za uchumi ikiwepo uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa watumishi wa Idara ya Sheria ni mdogo sana jambo linalosababisha Halmashauri zetu kuingia mikataba isiyo na tija na kuzisababishia Halmashauri kuingia kwenye migogoro ya kisheria mara kwa mara. Pia watumishi hawatoshi, kuwepo kwa mwanasheria mmoja kwenye Idara ya Sheria kunapunguza ufanisi kwenye Idara ya Sheria na Halmashauri zetu. Mfano Wilaya ya Liwale ina mtumishi mmoja tu kwenye idara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Kurekebisha Sheria ni bora ikafanya mapitio ya sheria mbalimbali mara kwa mara kwani zipo sheria nyingi zinazohitaji kufanyiwa mapitio. Ili zifanyiwe marekebiso ziendane na wakati uliopo kwani kuwepo kwa sheria zilizopitwa na wakati ni kuwapora haki wananchi. Mfano sheria inayoruhusu Serikali kumkamata tena mtuhumiwa aliyefutiwa mashtaka na Hakimu baada ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kushindwa kupeleka mashahidi Mahakamani, ni sheria inayojaza mahabusu kwenye Magereza zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria nyingine ni ile ya maliasili kuhusu kifuta machozi kwa waathirika wa kushambuliwa au mashamba kuliwa na wanyama waharibifu. Ni bora sasa wakapewa fidia badala ya hicho kinachoitwa kifuta machozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Mwendesha Mashitaka Mkuu imekuwa ni sababu kubwa ya kulundikana kwa mahabusu nyingi; imekuwa ikitindwa kupeleka majalada mbalimbali Mahakamani, hapa ndipo hadi sasa

pana rushwa kali sana. Ili jalada lifike Mahakamani, ni lazima mhusika atoe chochote hasa zile kesi kubwa kubwa. Ofisi hii pamoja na changamoto za kifedha, bado kuna utendaji usiozingatia misingi ya Utumishi wa Umma. Ndiyo sababu ya Mahakimu kufuta mashitaka na Mwanasheria Mkuu kuwakamata tena kwa sheria niliyoitaja hapo juu. Wapo mahabusu wengi kwenye Magereza nchini wakisubiri majalada toka kwa *DPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ni vyema ikawa na Wanasheria waliobobea kwenye fani ya sheria na wanaoijua jamii ya Watanzania na mazingira halisi ya nchi yetu, kwani Miswada mingi inayoletwa Bungeni kwa ajili ya kutungiwa sheria na mengine kukosa kabisa uhalisia kiasi cha kudhani watu wanaoanda Miswada hiyo sio watu wanaotoka katika jamii yetu; kiasi cha kufanya Miswada inayoletwa na Serikali kufanyiwa marekebisho na Bunge pengine ni kwa asilimia zaidi ya 80. Hili huchangia kulifanya Bunge kutunga sheria inayodumu kwa muda mfupi.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupoteza muda napenda kuongelea kuhusu taratibu za kisheria. Moja, wananchi wapewe elimu kuhusu sheria mbalimbali, mfano, anakamatwa mwizi aidha anapigwa au anachomwa moto hadi kufa kabisa. Wananchi wanajichukulia sheria mikononi mwao, wananchi waeleweshwe umuhimu wa kulitumia Jeshi la Polisi kwa tatizo lolote linalotokea ikiwa mitaani, maofisini au kwenye mikusanyiko yoyote ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Jeshi la Polisi litoe mafunzo kwa Askari wake ambao wanamhukumu mtuhumiwa kabla hata kosa liliomtuhumu halijajulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama nyingi ni chakavu sana kiasi kwamba nyingine zinavuja au wakati mwingine mafaili yanakosa mahali pa kuhifadhiwa. Tunaiomba Serikali ikarabati mahakama ambazo zimechakaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazee wa Baraza wengine ni wala rushwa sana wala hawashughulikii kuleta haki katika kesi zinazopelekwa kwao, Serikali iangalie kuwaweka wazee wenye weledi katika mahakama ili haki itendeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makosa ya jinai, kuna wanaoshtakiwa kwa makosa mbalimbali ya jinai, lakini baadhi walipelekwa mahakamani kesi imezungushwa kiasi mwisho wake mtuhumiwa anaachiwa huru. Serikali ione umuhimu wa kudhibiti wenye makosa ya jinai, wachukuliwe hatua zinazostahiki na kuwaachia huru wale wenye tuhuma ambazo ni za kubambikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. SHAABANI D. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hoja ya Katiba na Sheria kwa asilimia mia moja. Pia nampongeza Waziri Mheshimiwa Balozi Dkt. Mahiga na timu yake yote kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Lushoto ina Majimbo matatu na Halmashauri mbili, na jiografia yake ni ya milima milima na mahakama zilizopo ni chache mno ambazo hazikidhi huduma kwa wananchi. Kwa hiyo, niiombe Serikali yangu Tukufu itujengee Mahakama za Mwanzo hasa katika maeneo ya Malibwi na Ngwelo. Pamoja na maeneo hayo ambayo hayana mahakama, kuna mahakama ambazo zinahitaji ukarabati. Mfano, Mahakama ya Gare na Mahakama ya Mlola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Gare pamoja na kuomba kukarabatiwa, pia haina watumishi, wakati Mahakama ya Gare ilikuwa inafanya kazi, lakini nilishangaa mahakama ile imefungwa, kuuliza sababu nikaambiwa hakuna watumishi. Mahakama ile inasaidia zaidi ya kata nne, yaani Kata ya Kwemashai, Gare, Migambo, Kwai, Kata jirani ya Baga na Malibwi. Kwa hiyo, kufungwa kwa mahakama hii imesababisha usumbufo mkubwa sana kwa wananchi hao. Naiomba Serikali irudishe huduma hii

haraka pamoja na ukarabati wa haraka ili wananchi wasipate usumbufu wa kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo. Pia niiombe Serikali yangu Tukufu itoe ajira kwa watumishi katika mhimili huu wa mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, mahakama hizi zote mbili hazina vifaa kama *photocopy machine, computer* kwa ajili ya kurudufu nakala za hukumu na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Wilaya ya Lushoto ni ya zamani sana, kwa hiyo, niiombe Serikali yangu kama siyo kukarabati basi kujengewa mahakama nydingine ili na sisi wananchi wa Lushoto tuwe na mahakama ya kisasa na inayoendana na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wananchi wa Wilaya ya Lushoto tuna bahati ya kuwa na Chuo cha Mahakama Lushoto (*IJA*), lakini wananchi walio wengi hasa wa vijiji wanadhlumiwa haki zao na kutohana na wananchi hawa kutojua sheria. Sasa basi niiombe Serikali yangu Tukufu kwa kuwa tuna Chuo cha Mahakama, niiombe Serikali yangu wakati wanafunzi wanakwenda *field* basi waende vijiji hasa katika Vijii vya Lushoto ili wananchi wa Lushoto waweze kufaidika na fursa ya kuwa na Chuo cha *IJA*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo pia kuwe na dawati la kutoa elimu ya sheria kwa wananchi wa Lushoto na elimu hiyo itolewe na Uongozi wa Chuo cha Mahakama (*IJA*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Mungu ibariki Tanzania, Mungu mbariki Rais wetu Dkt. John Joseph Magufuli.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti nampongeza Mheshimiwa Dkt. Augustine Mahiga, Waziri wa Katiba na Sheria kwa kupata fursa ya

kuiongoza Wizara hii ya *learned friends*. Aidha, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri ahakikishe Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka 2019/2020 unatumika vilevile kujenga Mahakama ya Wilaya ya Namtumbo pamoja na Mahakama za Mwanzo ambazo wamechukua viwanja nya kujenga kwa muda mrefu na hawajaanza kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Namtumbo wa maeneo waliyochukua na kuweka vibao nya kuonyesha kama maeneo ya Mahakama wanashangaa hakuna kinachoendelea. Maeneo hayo ni pamoja na Kijiji cha Mawa. Naomba sana Wizara itenye fedha za Mfuko wa Mahakama tunazozipitisha kuanza kujenga Mahakama ya Wilaya ya Namtumbo na ikiwezekana na ujenzi wa Mahakama za Mwanzo walizozipanga kuanza kujenga katika Wilaya ya Namtumbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja ya Waziri wa Katiba na Sheria kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya Mwenyekiti wa Mahakama ya Ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru; kumekuwa na ucheleweshwaji wa kazi za ardhi na migogoro kutokana na kutokuwepo kwa Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi. Tunaomba Tunduru tupatiwe Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi ili kupunguza migogoro ya ardhi inayozidi kuongezeka siku hadi siku katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa majengo ya Mahakama; kuna upungufu mkubwa wa majengo ya Mahakama. Katika Jimbo la Tunduru Kusini, hivyo shughuli nyingi za Mahakama kufanyika katika maeneo yaliyofanana

na Mahakama. Pamoja na kutokuwepo kwa nyumba za Mahakimu wengi na Mahakimu wanakaa katika nyumba za kukodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa Mahakama; kumekuwa na upungufu mkubwa wa Mahakama. Jimbo la Tunduru Kusini lina Tarafa tatu, Nalasi, Hukumbule na Namasakata na Kata 15, lakini Mahakama zinazofanya kazi hazizidi tatu, moja kila Tarafa, hivyo tunaomba angalau kila Kata kungekuwa na Mahakama ya mwanzo ili kupunguza migogoro ya wananchi wetu huko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu mkubwa wa Mahakimu; Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ina upungufu mkubwa wa watumishi wa Mahakama (Mahakimu) pamoja na Makarani wa Mahakama, hivyo tunaomba tuongezewe Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ili kurahisisha kusikiliza kesi mbalimbali. Mahakama zilizopo hazina Mahakimu na kufanya Mahakimu waliokuwepo kuwa na mzigo mkubwa wa kusikiliza madai mbalimbali ya wateja hivyo kufanya Mahakimu kufanya mzunguko kupita kusikiliza kesi katika Mahakama zilizopo vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa vitendeakazi; Mahakama zilizopo Tunduru zina changamoto kubwa ya vitendeakazi hasa magari na pipipiki. Mahakimu waliopo hawana hata vyombo vya kusafiria ili kwenda kusikiliza kesi vijijini, hivyo kufanya kesi kuahirishwa mara kwa mara kutokana na kutokufika kwa Hakimu kusikiliza kesi hizo kwa kukosekana usafiri.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mchango wangu wa shukrani za dhati kwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama na watendaji wake kwa kuridhia na kuanzisha ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Mtae - Mlalo, Lushoto. Hii ni hatua muhimu kwa ujenzi na utoaji wa haki katika Mhimili huu. Nafarijika sana kuona jambo hili limekamilika na sasa ujenzi upo katika hatua za upauzi na usafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahakama hii itahudumia kata sita za Tarafa ya Mtae na kata za jirani na itapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la wananchi kujichukulia sheria mkononi kwa kukosa sehemu sahihi za kutafsiri haki katika ngazi hii ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kutoka katika Idara ya Mahakama kupitia Chuo cha Sheria Lushoto tuweze kupata msaada wa kisheria katika maeneo yetu ya uwakilishi. Tunaamini hili litasaidia sana katika kuwapa uwezo vijana wetu wanaosoma katika chuo hiki, lakini pia kuwasaidia wananchi kwenye mashauri mbalimbali katika maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Law School*; kumekuwa na uhitaji mkubwa wa wanafunzi waliomaliza katika vyuo mbalimbali vya hapa nchini katika Shahada ya Sheria, hata hivyo, linapokuja suala la kupata ujuzi wa elimu ya Uwakili Chuo pekee kinachotoa taaluma hii ni *University of Dar es Salaam*. Tunaomba Mtendaji Mkuu wa Mahakama kuona namna bora ya kuweza kupanua wigo ili Taaluma hii ya Uwakili iweze kupatikana katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho la ushauri ni kuhusu azma ya mahakama kutaka kujenga mahakama kila kata ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba kushauri jambo hili lipitiwe upya na lifanyiwe utafii wa kina kwani kwa maoni yangu kushusha mhimili wa Mahakama katika ngazi ya kata itakuwa ni mzigo na gharama kubwa kwa mhimili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, napendekeza kwamba ni bora mahakama hizi zikaishia katika ngazi ya tarafa. Yapo maeneo ikiwemo Lushoto eneo la tarafa ni rafiki kufikika kwa urahisi hivyo kutokwa na uhitaji wa kuweka mahakama katika ngazi ya kila kata. Tunazo tarafa tano zinazounda Halmashauri ya Lushoto, hivyo ni vyema angalau kila tarafa ikapata Mahakama ya Mwanzo ili kuleta ufanisi katika kutafsiri sheria na kutoa haki. Katika Halmashauri ya

Bumbuli, Lushoto kwenyewe zipo tarafa tatu lakini kuna Mahakama ya Soni na Bumbuli pekee, Tarafa ya Tamota na Mgwashizi hazina mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kupongeza mhimili huu wa Mahakama lakini pia Viongozi Watendaji Wakuu wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa utendaji wao na kuipa heshima Wizara hii, hasa katika eneo hili la usimamizi na utoaji wa haki. Nawasilisha.

MHE. ZAINAB M. AMIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nipongeze kazi kubwa inayofanywa na Wizara hii chini ya Waziri Mheshimiwa Dkt. Augustine Philip Mahiga, naishauri Serikali iwajengee nyumba maalum Majaji na Mahakimu kutokana na kazi zao za kusimamia sheria na maslahi mbalimbali na waweze kuwa na ulinzi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara hii ikamilishe upelelezi wa kesi kwa wakati ili kupunguza msongamano wa watuhumiwa magerezani na mahabusu. Fedha zinazotolewa za bajeti zipelekwe kwa wakati ili kutekeleza na kukamilisha miradi ya maendeleo kwa wakati. Pia naishauri Serikali ikarabati Mahakama za Mwanzo hadi Wilaya, mfano, Mahakama ya Mwanzo ya Temeke Dar es Salaam ni chakavu na ndogo haikidhi mahitaji; Serikali iongeze vyuo vya mafunzo ya Mahakama ili kuweza kupata wataalamu wa sheria wa kutosha.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja na ningependa kuchangia suala moja muhimu. Jimbo la Muheza halina jengo la Mahakama ya Wilaya, bajeti iliyopita ilikuwa limepangwa kwenye mpango wa ujenzi na likaondolewa katika hatua za mwisho, mwaka huu katika bajeti hii limeondolewa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Muheza tulikwishatayarisha kiwanja muda mrefu, jengo linalotumika halina hadhi ya kimahakama, hivyo tunaomba tufikiriwe katika mpango wa ujenzi wa kisasa. Nakushukuru.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa hii na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri na hotuba yenyewe kusheheni mambo mazuri kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake mzuri wa kujenga Mahakama Kuu katika Mikoa ya Mara na Kigoma. Uamuzi huu kwa busara unaenda kutatua kero ya muda mrefu iliyopelekea wananchi wa mikoa hii kusafiri masafa marefu ili kupata huduma hii muhimu. Ombi langu kwa Serikali ni kuziwezesha Mahakama hizi kuwa na bajeti ya kutosha ili kuziwezesha kufanya kazi zake kwa ubora na ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mafia yenyewe vijiji 23 ina mahakama moja tu ya mwanzo, hali hii inapelekeea utoaji wa huduma za kisheria kuwa mbali na wananchi. Ombi langu kwa Serikali ni kwamba, itujengee Mahakama moja ya mwanzo katika Tarafa ya Kusini kwani wananchi katika maeneo haya wengi wanatoka katika Visiwa Vidogo Vidogo vya Juani, Chole na Jibondo, wanasaifiri masafa marefu na wanatumia gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya adhabu na faini mbalimbali nyingi zimepitwa na wakati kulingana na mazingira ya sasa, hivyo niiombe Serikali yangu sikivu kufanya mapitio upya ya viwango vya faini na adhabu zilizopitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa nyumba ya Jaji Mkuu katika Jiji la Dodoma umekuwa ni ahadi ya siku nyingi, kiongozi wa mhimili ni vema akawa na makazi yenyewe hadhi sawa na wadhifa wake. Nakushukuru na naunga mkono hoja.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Balozi Dkt. Mahiga, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri na kuweza kuwasilisha hotuba yake hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo masuala ambayo naomba kupatiwa ufanuzi, ambayo ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, sheria zilizopitwa na wakati; kumekuwa na malalmiko mengi kuhusiana na Sheria nyingi kuitwa na wakati na kusababisha wananchi kutotendewa haki. Je, kuna utaratibu au mkakati gani ili kuhakikisha kuwa zile sheria zilizopitwa na wakati, Miswada inaletwa Bungeni ili kuzifanya marekebisho au kuhuishwa.

Pili, hukumu kuandikwa katika lugha ya Kiingereza; naomba kujua ni kwa nini Serikali hajaweza kuweka utaratibu wa hukumu kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili na kutenda haki kwa mshtakiwa kukata rufaa? Kwa sababu nilipotembelea gereza kuu Mkoa wa Iringa changamoto mojawapo ya wafungwa ilikuwa wameshindwa kukata rufaa kutokana na kutoelewa lugha iliyoandikwa na hasa kama huna Mwanasheria wa kukusaidia. Je, Serikali haioni kama hawatendi haki kwa wasiojua lugha ya Kiingereza? Naomba kujua mkakati wa Serikali kuhusiana na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wa mashtaka; naomba kujua umri wa mashtaka kwa sababu ipo kesi ya waliokuwa wafanyakazi wa kilichokuwa Kiwanda cha Kukata Almasi (*Tancut Diamond Iringa*), kiwanda kilifungwa mwaka 1995 kwa kuingia mufilisi, hivyo wafanyakazi hawajalipwa na toka wakati huo walifungua kesi dhidi ya Serikali lakini matokeo yake mpaka leo bado wanaendelea kuhudhuria mahakamani. Naomba ufanuzi juu ya suala hilo kwa sababu linachukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa kutoa tamko la kumaliza mashtaka yanayohusu wanawake na watoto ndani ya miezi sita. Kwa hili napongeza sana, sababu katika Mkoa wetu wa Iringa kumekuwa na kesi nyingi za ubakaji watoto ambao zimechukua muda mrefu sana kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Tunaendelea. Sasa namwita Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali aanze kuchangia hoja hii. Utakuwa na dakika zako zisizozidi dakika 15.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika kuhitimisha hoja iliyopo mezani. Nami nitajitahidi kupitia masuala kadhaa na hasa nitajikita kwa yale yaliyoibuliwa katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, imezungumzwa juu ya sheria zinazodaiwa zinakiuka katiba, mifano imetolewa; *Cybercrimes Act*, *Media Services Act*, *Accesses to Information Act* na nyinginezo na kwamba hizi zinaingilia uhuru wa kujieleza na uhuru wa kupata habari na haki nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema tu ni kwamba masuala ya haki na uhuru yana mipaka na hii imeelezwa vizuri sana katika Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 30. Hata tukienda katika zile sheria za Kimataifa, kama ile *International Covenants on Civil and Political Rights*, tunaona Ibara ya 19 inazungumzia juu ya uwepo wa mipaka katika haki mbalimbali zilizoelezwa katika sheria hiyo. Kwa hiyo, ninachotaka kusema hapa tu ni kwamba, sheria hizi zinakuwepo, haki na uhuru viro katika katiba lakini haki na uhuru huo una mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, linamhusu Mkurugenzi wa Mashtaka (*DPP*) kwamba anayo mamlaka ya kutoa maelekezo ya kufanya upelelezi anapoona jambo fulani limetokea na kwamba analaumiwa hapa kwamba hajachukua hatua yoyote kwenye matukio kadhaa yaliyotokea, kwamba hakutoa maelekezo kwamba upelelezi ufanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba Mkurugenzi huyu wa Mashtaka, huwa anatoa maelekezo pafanyike upelelezi kama anaona upelelezi huo haujafanywa na chombo chochote kinachopaswa kufanya

uchunguzi. Kama kuna vyombo kadhaa; kimoja au viwili au vitatu vinavyofanya uchunguzi katika jambo hilo, hana haja ya kutoa maelekezo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu lilikuwa linahusu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika majukumu yake ya kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu masuala ya mikataba na kwamba pengine ofisi hii haijafanya vema katika jukumu hilo. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kweli imekuwa na changamoto za hapa na pale, lakini kwa sasa hivi maboresho makubwa yamefanyika katika ofisi ile hasa katika eneo hili la uchunguzi wa mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulilizungumza hili hata mwaka jana kwamba tumeweka hata masuala ya ubobezi katika uangalizi wa mikataba. Kwa hiyo, sasa hivi wanasheria wetu wako *specialized*. Kama ni mikataba ya mambo ya ujenzi, kama ni mikataba ya rasilimali, kama ni mikataba ya *financing*, kama ni mikataba ya manunuzi na kadhalika sasa tumeweka *specializations* katika ofisi ile na nafikiri ofisi inafanyakazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia imeanzishwa idara maalum ambayo inahusika na kutoa ushauri pia. Kwa hiyo, kama kuna upungufu wa *capacity* kule kwenye idara inayohusika na mikataba hii idara nydingine inayohusika na ushauri kwa ujumla inasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne liliolelezwa katika taarifa hiyo ni kushindwa kutoa ushauri sahihi kwenye kesi mbalimbali na hasa zilizofunguliwa nje ya nchi na hadi kupelekea Serikali kupata hasara kubwa na mifano hapa imetolewa Kesi ya Konoike, kesi ya *Sterling* iliyokuwa inahusiana na zile ndege zetu, kesi iliyofunguliwa na ACAC/As, kesi iliyofunguliwa na *Symbion*, *Eco energy* pengine na nydingezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kutoa taarifa kwa zile kesi mbili za kwanza, kesi ya Konoike na kesi ya *Sterling*, *actually* mashauri haya yameshamalizika, kwa

sababu pia palikuwa na mazungumzo kati ya hawa wadai pamoja na Serikali. Niseme tu hapa kwamba hata fedha zilizolipwa katika mashauri haya ni ndogo sana sana sana kuliko zile ambazo zinaelezwa au zilioneshwa katika zile hukumu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika kesi ya Konoike inasemwa ilikuwa ni shilingi bilioni 80, lakini iliyolipwa ni kidogo kabisa. Kwenye kesi ya *Sterling* nayo ilisemwa ni zaidi ya shilingi bilioni 80 lakini iliyolipwa ni chini ya hata ya theluthi moja ya kiasi hicho kinachotajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi zile nyingine za *ACACIAS*, *Symbion*, *EKOenergy* zinaendelea, kwa hiyo, hatuwezi kuzzungumzia sana. Hata hivyo, hawa wahusika waliotushitaki katika kesi hizo, wao wenyewe ndio wamekuwa wa kwanza kuomba pawe na mazungumzo kati yao na Serikali. Serikali imepokea wito huo na kwa hiyo, mazungumzo yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ilikuwa ni kuhusu mkataba wa Afrika kuhusu mambo ya demokrasia, chaguzi na utawala, yaani *African Charter on Democracy Elections and Governance* na kwamba Tanzania haijatia saini mkataba huo; na kwamba Mataifa 35 yameshatia saini mkataba huo na kufanya sheria ya nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hapa kwenye hii idadi siyo sahihi. Mataifa ambayo yametia saini na kuufanya huo mkataba kuwa sehemu ya sheria za nchi zao, yaani *ratification* hayajazidi 11 hadi sasa hivi. Napenda tu kusema kwa haraka haraka kwamba kuna mambo kadhaa ambayo bado yanajadiliwa na yanaonekana bado ni kikwazo kwa nchi nyingi kuweza kutia saini mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawili makubwa, kuna suala la *unconstitutional change of government* halijatafsiriwa vizuri na kuelezwu vizuri; na masuala yanayohusu uangalizi wa uchaguzi (*election monitoring*). Sasa nchi nyingi bado zina mashaka, nini hasa majukumu ya

waangalizi wa uchaguzi na kadhalika. Kwa hiyo, siyo Tanzania peke yake na kila mara tunashauriwa kwamba nchi ichukue tahadhari ya kutosha kabla ya kuingia tu kwenye mkataba wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine liliobiuliwa katika taarifa hiyo ni suala la Katiba na linaingiza masuala ya Muungano. Taarifa hii kwa namna moja au nyingine inaijadili au inaizungumza Katiba ya Zanzibar na inahoji katika maeneo fulani fulani kwamba kwa nini katiba ya Zanzibar kwa mfano inamsimamo huu, haimtambui Rais kuwa ndiyo Mkuu wa nchi yote kwa Jamhuri ya Muungano, pamoja na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili niliweke vizuri kabisa. Bunge hili lina mamlaka na uwezo wa kuzungumzia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katiba ya Zanzibar ni ya Zanzibar na hata anayeweza kuizungumzia kwa kweli kwa mamlaka kama ninavyoweza kuizungumzia hapa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ni Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar ndio anayeweza kuizungumzia *authoritatively* Katiba ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana hata likitokea shauri lolote linalogusa Katiba ya Zanzibar, shauri hilo haliwezi likafika katika Mahakama ya Rufaa ambayo ni Mahakama ya Muungano, shauri hilo litakomea katika Mahakama Kuu ya Zanzibar na huo ndio utaratibu na misingi ya Kikatiba tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo ya Muungano, tunazungumza kwamba tuna changamoto. haya yote yaliyoelezwa katika ile taarifa ni changamoto za Muungano. Mpaka sasa hakuna jambo la kikatiba ambalo limebishaniwa rasmi kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ipo Ibara katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni vema tuwe tunaisoma kila wakati, inayosema: "kama kutakuwa na jambo linalobishaniwa kati ya Serikali hizi mbili, itaundwa Mahakama Maalum ya Katiba." Kwa kumbukumbu zilizopo Mahakama hii haijawahi kuundwa kwa sababu hakujatokea

jambo linalobishaniwa; na kwa hiyo, yaliyopo haya yote ni changamoto za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumezungumzwa pia juu ya mashauri mbalimbali yaliyoko nje ya nchi, nadhani huu ni mchango wa Mheshimiwa Zitto, akazungumza juu ya kuangalia *public interest* katika mashauri hayo na akatolea mfano wa kesi ya *Standard Chartered Hong Kong*; na akaeleza kuna kitu kinaitwa *indemnity* ambayo iliwekwa na wahahusika wa ile kampuni ya *IPTL* na kwamba kwa nini wasitolewe mahabusu kwa sababu waliweka ile *indemnity*? Sasa hapa nahitaji kueleza kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumezungumzwa pia juu ya mashauri mbalimbali yaliyoko nje ya nchi, nadhani huu ni mchango wa Mheshimiwa Zitto. Amezungumza juu ya kuangalia *public interest* katika mashauri hayo na akatolea mfano wa kesi ya *Standard Chartered Hong Kong*na akaeleza kuna kitu kinaitwa *indemnity* ambayo iliwekwa na wahusika wa ile kampuni ya *IPTL* na kwamba kwa nini wasitolewe mahabusu kwa sababu waliweka ile *indemnity*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa nahitaji kueleza kidogo. Ni kweli kabisa kwamba wale watu waliopo mahabusu kuhusiana na *Escrow Account* katika ile kampuni ya *IPTL* waliweka *indemnity*. Hata hivyo, *indemnity* ile ilikuwa ni kuipa kinga Serikali iwapo litatokea shauri lolote na kutakuwa na hasara fulani au malipo fulani yanayotakiwa kufanyika, *indemnity* hiyo ita-cover ama hasara hiyo au malipo hayo au mahitaji yoyote yale. Kwa hiyo kimsingi *indemnity* inagusa masuala ya madai, ni mashauri ya madai, inagusa kwenye madai, kwamba unanipa kinga ikija kutokea shauri lolote linaibuka hapa wewe utanilipa gharama pengine za kesi, wewe utanilipa gharama pengine za kesi, wewe utalipa gharama fulani, wewe utalipa chochote nitakachotakiwa nilipe, ikiwa ni pamoja na yale ambayo mahakama mbalimbali za kimataifa zimeamuru *Standard Chartered Hong Kong* walipwe kimsingi wanatakiwa kulipwa kutoka kwenye *indemnity* hii lakini...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Muda wetu...

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekeiti, dakika moja;

MWENYEKITI: Haya, endelea.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekeiti, ahsante sana, dakika moja tu nimalizie hapo, kwa sababu ni suala la muhimu kidogo. *Indemnity* hii haigusi masuala ya jinai, sasa wahusika hawa aliowatatajaa Mheshimiwa Zitto wana kesi, wapo ndani au mahabusu kwa sababu ya kesi za jinai. Nadhani kuna mashtaka kadhaa yanayowahusu kwenye jinai hilo.

Mheshimiwa Mwenyekeiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mwanasheria Mkoo wa Serikali kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Profesa Kabudi Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, muda ujisizozidi dakika kumi na tano.

WAZIRI WA MAMBO NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA

MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekeiti, awali ya yote nianze kuunga hoja mkono iliyoletwa mbele yetu na Dkt. Augustine Maiga, Waziri wa Katiba na Sheria ambaye amewasilisha hii hoja kwa umahiri mkubwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekeiti, ningependa kuchangia katika maeneo machache ya hoja iliyoletwa kwetu na Balozi Dkt. Maiga. Kwanza kuhusu mashauri ya nje; kama alivyoakeza Mwanasheria Mkoo wa Serikali toka kuundwa kwa Ofisi ya Wakili Mkoo wa Serikali mafanikio yetu yamekuwa makubwa. Ndani wiki mbili zilizopita na waliosoma gazeti la *Citizen* juzi tumeweza kushinda kesi ya *Valambhia* ambaao

walikuwa wanaidai mabilioni ya fedha Benki ya Tanzania. Sasa kama alivyoeleza Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kesi ya *Sterling Construction*, kwanza kampuni hii sio ya Kanada kama ilivyoandikwa kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani. Kampuni hii ni ya Uingereza na kabla ya hapo ilikuwa kampuni ya Italy ambapo deni lake lilinunuliwa na kampuni ya Uingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa tumefanya maelewano yote, wao wenyewe kampuni ya *Sterling Construction Company* waliomba *the Supreme Court of Quebec* kiwango cha fedha walicholipwa na ile hukumu iwe siri. Kwa hiyo, maagizo ya kwamba hukumu na kiasi cha fedha kilicholipwa iwe siri, hayakuwa maombi ya Tanzania, yalikuwa maombi ya kampuni ya *Sterling Construction* ya Uingereza na ilikubaliwa na *the Supreme Court of Quebec* na sisi kuyaweka hadharani itakuwa ni *contempt of court*, lakini pia itakuwa ni kuvunja uungwana wa maelewano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia walitueleza wazi kwamba mnafanya makosa makubwa sana mara nyininge mnapoyaweka mambo haya wazi kwa sababu mna kesi na watu wengine na si ajabu wakijua kiwango ambacho ninyi mmetupa na wao wanaweza wakakidai au kikaleta maswali mengi. Kwa hiyo suala hilo ni wazi ni maombi ya *Sterling* na uzuri hukumu wa Jaji wa Canada ambaye kwanza alianza kwa kutupa pole ya askari wetu kule Congo kuuawa alieleza wazi. Kwa hiyo sio Serikali ya Tanzania ni *Sterling Quebec* lakini kiwango kilicholipwa siku wakikubali taarifa hiyo iwe wazi, ni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uteuzi wa Majaji, ningependa suala hili nieleze kabisa, Majaji wote walitoteuwa, wameteuliwa na Mheshimiwa Rais kwa ushauri wa *Judicial Service Commision*. Nami nichukuke nafasi hii kukupongeza sana wewe ulipokuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali mwaka 2000 na mwaka 2005 uliletta mabadiliko ndani ya Bunge hili ambayo moja yalipanua na kuongeza *divest* ya wajumbe wa *Judicial Service Commision*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakumbuka kabla ya wewe kuleta hayo mabadiliko ya Katiba, *Judicial Service Commision* ilikuwa na watu wachache na wote walikuwa kwenye mhimili wa Mahakama lakini ni wewe mwaka 2000 mara ya kwanza na 2005 mara pili uliyefanya mabadiliko makubwa kuishauri Serikali kufanya hivyo, ikiwa ni pamoja na kuboresha haki za binadamu, wewe ukiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ulileta mabadiliko hapa Bungeni ambayo yaliondoa *clawback clauses* zote. Sisi ndio Katiba pekee katika Bara la Afrika inapokuja kwenye haki za binadamu haina *clawback clauses*, someni ya Kenya, Uganda, Zambia, Zimbambwe na nchi nyingi, lakini kazi hiyo alifanya Mheshimiwa Andrew John Chenge mwaka 2005 akiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ndio maana daima nabeba Katiba hii mwisho hapa A. J. Chenge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndio aliingiza haya mabadiliko. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watu wa umri mdogo humu wanapapukia mambo wasiyoyajua, wangejua tulipotoka wangejua tulipofika. Kwa hiyo ni jukumu letu hawa walio wadogo tuwakumbushe tulikotoka na ndio maana Katiba hii Mheshimiwa Chenge wewe ni mionganini mwa watu walioisaidia *Judicial Service Commision*. Kwa sababu hiyo basi, uteuzi wa Majaji umebadilika; leo hii Majaji hawatoki katika mhimili wa mahakama tu, wanatoka kwenye vyuo vikuu, wanatoka kwenye Mawakili binafsi na huo upanuzi wa aina ya Majaji wanaoingia, imeongeza ubora wa hukumu lakini pia imeongeza ubora wa utendaji katika Mahakama zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kwa kutumia mamlaka ndani ya ibara 109(7) na (8) hatoi fadhila, anateua watu wenye sifa na sababu za kuwa Majaji baada ya kuwa amependekerezewa na Tume ya Mahakama. Kwa hiyo, nataka nisisitize, Rais hatoi zawadi katika kuteua Majaji. Nami narudia tena kwa ndugu zangu, hakuna kazi ambayo naiogopa na tuwaombee sana Majaji na mkitaka kujua ugumu wa kazi ya kuwa Jaji, kaisomeni Zaburi ya 15 na baada ya hapo muisome Zaburi 51 na Zaburi ya 32. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakishazisoma Zaburi hizo tatu za toba katika kipindi hiki cha kwaresma watawaombe sana Majaji. Si kazi ya kukurupukia ni kazi ya kumwombea mtu huyo aliyopewa kwa sababu amechukua kazi ambayo ni ya Mwenyezi Mungu mwenyewe, ye ye pekee ndiye Hakimu wa kweli wengine wote wanajitahidi kufanya hivyo.

Kwa hiyo si kazi kuendelea kuwabeza na ndio maana naunga mkono nchi nyininge ambazo mambo ya mahakama hayajadiliwa kabisa katika Bunge. Sisi tumeruhusu kuyajadili mambo hayo, lakini tuyajadili kwa hekima, kwa kiasi, kwa saburi, lakini kwa unyenyekevu mkubwa maana hatupo katika viatu vya watu hawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la Sheria ya Ndoa, sio kweli kwamba Sheria ya Ndoa ya Tanzania ya mwaka 1971 ni sheria kandamizi, ni sheria ya kimapinduzi. Narudia tena Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ni sheria ya kimapinduzi na nchi nyininge mpaka leo zimeshindwa kutunga sheria ya aina hii. Kwa hiyo tusichukulie suala moja tu la umri wa mtu kuo au kuolewa likawa ndio kigezo cha kusema sheria hii ni kandamizi. Hata hilo suala la mtu kuo au kuolewa, mtu akikisoma kwa makini kifungu hicho hakizungumzii msichana tu bali pia kinamzungumzia mvulana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ndani sheria zetu wapo wavulana wanaoweza kuona chini umri ya mdogo, soma kile kifungu vizuri, kinasema *either parties or one of them*. Sheria hii ni sheria ya kimapinduzi kwa sababu ndio sheria kwanza mwaka 1971 iliyowakomboa wanawake wa Kitanzania hasa wenyewe ajira sasa kuweza kwenda kufanya kazi eneo lolote na Tanzania na kupanda vyeo. Kwa sababu kabla ya hapo sheria tulioachiwa na Waingereza ilikuwa mwanamke lazima akae mahali alipo mumewe na hilo liliwanyima wanawake fursa kama akina Dkt. Christine Ishengoma asingeweza kuwa Mkuu wa Mkoa Iringa akamwacha Profesa Morogoro, ilikuwa lazima akae Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisimtoolee mfano yeye tu, nitolee mfano sasa mwagine, kwa sababu sheria kabla ya mwaka 1971 *Cohabitation* maana yake ilikuwa lazima siku zote mlale katika chumba kimoja, lakini leo chini ya sheria hii kwa hiyo *habitation* pamoja na *whatsApp* pamoja na simu. Hilo limewakomboa wanawake wa Tanzania kuweza kwenda kufanya kazi maeneo mbalimbali ya nchi. Ni makosa kuita sheria ya namna hiyo ni sheria kandamizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, katika umiliki wa mali hii ndio sheria ya kwanza katika Bara la Afrika iliyotambua kwamba mwanamke aliyolewa anaweza akamiliki mali kwa jina lake, someni sheria za nchi zingine, hata Uingereza, hata Ujerumani imewachukua miaka mingi mwanamke ndani ya ndoa kuruhusiwa kumiliki mali kwa jina lake. Alimiliki mali kwa jina la mumewe au kwa jina la baba yake. Sisi tuliosoma nje tulishangaa kwamba mwanafunzi wa kike Ujerumani hawezি kupanga chumba mpaka baba yake atie saini ya ile *form*, hapa wanasaini tu. Hapo tulishangaa kwa kujua wanawake wa Ulaya, wenyе sifa sawa na kazi sawa wanalipwa mshahara kidogo kuliko wanaume eti tu ndani ya mwezi kuna siku ambazo henzieleweki kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja kama hiyo huwezi kuileta hapa, kwamba kuna siku ambazo mwanamke haeleweki na hiyo alipwe mshahara mdogo. Mpaka leo ipo katika nchi Ulaya. Kwa hiyo kuna mambo sheria hii imefanya makubwa ambayo ni vizuri tuyaelewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umri wa mtoto kuolewam, hili suala ni suala *very sensitive*, tukitaka tulibue tutagombana humu. Uingereza yenyewe mpaka leo umri wa mtoto wa kike kuolewa ni miaka 16, lakini leo wasichana wengi Uingereza hawaolewi kwa sababu ya fursa mbalimbali za elimu na mwamko lakini n I mpaka leo. Ukienda kwenye Sheria ya Kanisa Katoliki kwenye *Canon Law*, *Canon* namba 1083 inasema wazi kabisa umri wa msichana kuolewa ni miaka 14, kwa mvulana kuoa ni miaka 16 na hii sio mimi, ni *Canon Law* ya Kanisa Katoliki ambayo ndani ya vitabu ipo wazi.

Kwa hiyo kwa kanisa katoliki binti anaweza kuolewa na miaka 14 mvulana 16, ingawa mamlaka za kidunia zilipo zimeruhusiwa kubadili, lakini mpaka leo *Canon Law* hajabashwa kifungu cha 1068 na kifungu 1071 ambacho kilitolewa na baba Mtakatifu Paul wa Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sitaki kwenda kwenye mifano ambayo daima tunapenda kuitoa kwenye dini ya Kiislam, lakini hata huko kwa madhehebu ya *Shafii* ni miaka 15; kwa madhehebu ya *Hanbali* miaka 15 kwa madhehebu *Maliki* ni miaka 17; kwa madhehebu ya *Hanafi* ni miaka 12 kwa mvulana, miaka tisa kwa msichana na kwa madhehebu ya *Ja'fari*, hawa *Shia* ni miaka 15 na tisa. Tusiende kwenye majadala huo, tuache sheria ilivyo na busara itawale, kwenda kwenye haya tutaingia kwenye mambo ambayo si vizuri kuyaingia kwa sasa. Hata hivyo, nirudie kueleza, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 tofauti na ilivyoelezwa ni sheria ya kimapinduzi, iliyokuja kwa wakati muafaka na unaostahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa pia nieleze kuhusu haki za binadamu kwa kifupi. Tumetoka kwenye Baraza la Umoja wa Kimataifa la Haki za Binadamu, Geneva mwezi Februari, tumetoa maelezo kule na baada ya maelezo ya Tanzania, Kamishna wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa kwa kinywa chake ametupongeza kwa utekelezaji mkubwa wa haki za binadamu katika eneo la elimu, eneo la afya, eneo la maji. (*Makofii*)

WABUNGE FULANI: Aaaaaaa.

MWENYEKITI: Nakuongeza muda kidogo Profesa. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MAMBO NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA
MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja na tuliungwa mkono na nchi zote za Afrika, sisi ndio tunaongoza kwa idadi kubwa ya magazeti ambayo yanatoka kila siku ya aina zote na tunamshukuru Mungu kwamba sio sisi tuliyoyabeba magazeti haya kuyapeleka Geneva, tulikuta Umoja wa

Kimataifa wanayo magazeti hayo. Walishangaa kabisa uhuru mkubwa tulionao wa haki za magazeti ya risasi yaani wanaojimwaga, yapo, kwa sababu ni *diversity*, ya muziki yapo na magazeti ambayo ni *very critical*, yapo. Hata hivyo, pia sisi ndio nchi ya kwanza ambayo magazeti mengi ni magazeti binafsi, magazeti ya Serikali ni mawili tu *Dalynews* na Habari leolakini magazeti mengine yapo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vituo vya redio sisi ndio tuna vituo vingi kuliko vyote, vituo vya redio vingi na kwenye vituo vya redio huingilii. Vingi vinaeleza mambo ya nchini.

Kwa hiyo Umoja wa Matifa umetuondoa katika tuhuma hizo ambao watu walizipigia kelele, tumechukuliwa ni nchi ya mfano kwa sababu katika *Universal Declaration of Human Rights*, *haijapanga haki, civil and political rights, economic and social rights* zipo sawa na sisi tunaongoza katika *economic and social rights*. Sio tu Afrika lakini pia katika Bara la Afrika na Asia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo ya kufanyiwa kazi na haya maeneo ya kufanyiwa kazi yanafanyiwa kazi na mahakama. Mwaka huu na mwaka uliopita Mahakama za Tanzania zimetoa *land mark decision* moja on private investment, judgment ya Court of Appeal/kuhusu kesi ya *Tigo* ambayo watu wengi hawajaisoma ambapo Mahakama ya Rufaa tena, hukumu ya Jaji Mkuu Juma ime-reaffirm the right to private property na kesi hii haikuwa dhidi ya Serikali, ilikuwa kesi ya mfanyabiashara mmoja tapeli aliyetaka kuidhulamu *Tigo shares* zake, mwaka jana Mahakama ya Rufaa imetoe hukumu muhimu sana inayoeleza uwazi kabisa mipaka ya DPP katika kutekeleza majukumu yake na kumpa mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu Mahakama Kuu imetoe mwongozo katika utoaji wa *bail*. Sasa mara nydingi watu tunataka majibu ya mkato, badala ya kutaka process ya mahakama iende na baada ya hapo mahakama itoe mwongozo.

Baada ya kumweleza Kamishna wa Umoja wa Mataifa kuhusu mambo hayo na kumkabidhi zile *judgment*, alisema zile *judgments* zinatazwa dunia zima jinsi ambavyo Mahakama za Tanzania zipo mbali katika kufafanua na kusimamia haki za binadamu...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

WAZIRI WA MAMBO NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Profesa Kabudi kwa mchango wako mzuri, umeelimisha na kuwasaidia Wabunge lakini pia na Watanzania.

Sasa namwita mto hoja, ahitimishe hoja yake kwa muda usiozidi dakika 30, Mheshimiwa Balozi Dkt. Maiga.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii ili niweze kutoa majibu ya hoja mbalimbali kutoka kwa Wabunge waliochangia kwa mdomo na maandishi katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Katiba na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko mengi kuhusiana na sheria nyingi kuitwa na wakati na kusababisha wananchi kutotendewa haki, je, ni utaratibu au mkakati gani umeweka ili kuhakikisha kuwa sheria zilizopitwa na wakati zinaandikwa kitaalam na kulingana na wakati? Hili ni swali ambalo limeulizwa na Mheshimiwa Ritta Kabati. Jibu ni kwamba, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na sheria zinazokidhi mahitaji ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hali hii imepelekea kuanzisha kwa Tume ya Kurekebisha Sheria mwaka 1980 kama chombo mahususi cha kupitia sheria zote ili ziweze kwenda na wakati katika kuandika na kuleta maendeleo na haki katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Kurekebisha Sheria katika muda wote imekuwa ikipitia sheria mara kwa mara na kutoa taarifa Serikalini juu ya maeneo ya sheria yanayohitaji maboresho. Serikali imekuwa ikitumia taarifa hizo katika kufuta sheria zilizopitwa na wakati, kurekebisha sheria zenye kasoro na kutunga sheria mpya katika maeneo mapya ambayo hayana sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nytingine imetolewa na Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa Mafia. Anasema adhabu na faini mbalimbali zilizoko kwenye sheria zimepitwa na wakati kulingana na mazingira ya sasa. Anashauri Serikali ifanye upya mapitio ya vifungu vya faini na adhabu zinazotolewa. Majibu yanafanana na lile swali ambalo limeulizwa na Mheshimiwa Ritta kwamba kuna jitihada za kila aina ili kuhakikisha kwamba sheria zilizopitwa na wakati pamoja na adhabu mbalimbali zinarekebishiwa na Tume ya Sheria inafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nytingine ni ya Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale. Anasema Tume ya Kurekebisha Sheria ifanye mapitio ya sheria mara kwa mara. Nalo hili majibu yanafanana na kama kutakuwa na ziada ya yale ambayo tumeshayatoa, tutaweza kuyajibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Pauline Gekul ameuliza kuhusu fidia ya wananchi ambaao maeneo yao yalichukuliwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Mahakama ya Mkoa na ya Wilaya ya Babati watalipwa lini? Jibu ni kwamba ni kweli Mahakama ilipatiwa eneo na Halmashauri ya Mji wa Babati kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama eneo ambalo lilikuwa bado halijatolewa fidia. Aidha, kati ya viwanja vinne viliviyotolewa viwanja vitatu vilishalipwa fidia. Mahakama inaendelea kuwasiliana na Halmashauri ya Mji kuhakiki kiasi halisi cha fidia inayodaiwa ili kuwalipa wananchi wanaohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Pauline Gekul pia amesema posho ya Wazee wa Baraza Mahakama ya

Babati hawajalipwa miaka miwili iliyopita, je, wazee hawa wametapeliwa, ni lini watapewa lini fedha zao. Madeni ya Wazee wa Baraza wa Babati ni shilingi laki mia saba sitini elfu na deni hili ni sehemu ya madeni ya Wazee wa Baraza ambapo fedha imetengwa na malipo yatafanyika kabla ya Juni, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maswali yanayofanana ambayo yameulizwa na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mheshimiwa Joseph Haule, Mheshimiwa Ally Keisy, Mheshimiwa Pascal Haonga, Mheshimiwa Aida Khenani, Mheshimiwa Edwin Amandus Ngonyani, Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mheshimiwa Hamoud Jumaa Kibaha na Mheshimiwa Susan Lyimo. Swali ni ni upungufu wa majengo ya Mahakama katika Jimbo la Tunduru, Mafia, Nkasi, Namtumbo na Liwale. Majibu ni haya yafuatayo, Mahakama ina upungufu mkubwa wa majengo ya Mahakama nchini katika ngazi zote. Mahakama inao mpango wa miaka mitano wa kujenga na kukarabati majengo katika ngazi zote. Mpango huu unaendelea kutekelezwa kama ilivyosemwa kwenye hotuba yangu aya ya 30 kwa kuanzia ujenzi katika makao makuu ya tarafa na baadaye kwenye kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maswali yaliyoulizwa na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate na Mheshimiwa Joseph Haule na hili ni fupi tu linahusu upungufu wa vitendea kazi hasa magari na pikipiki. Jibu ni kwamba tunaendelea kununua vitendea kazi vya ofisi kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha za Serikali na kutumia zile zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna swali limeulizwa na Mheshimiwa Hamoud Jumaa, Mbunge wa Kibaha ambalo ni kulalamikiwa kwa maamuzi ya mashauri yanayohusu migogoro ya wakulima na wafanyakazi Kibaha Vijijini. Jibu ni kwamba mfumo wa utoaji haki wa masuala ya ardhi umegawanyika katika maeneo matatu, Mabaraza ya Kata ambayo yako chini ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Mabaraza ya Wilaya, Ardhi na Nyumba ambayo yako chini ya Wizara ya Ardhi; na Mahakama Kuu ambayo inapokea

rufaa kutoka kwenye mabaraza mengine. Kazi ya Wizara yangu ni kuratibu shughuli za upatikanaji haki ikishirikiana na Mahakama na Wizara ya Ardhi na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati na kwa weledi. Pale ambapo wadai hawaridhiki na uamuzi washauriwe/washawishiwe kufuata utaratibu wa rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lucia Mlowe, alizungumzia kuhusu Mahakama kutotenda haki na kufuata maelekezo ya Serikali. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua uhuru wa Mahakama katika usikilizaji na utaoji wa maamuzi mbalimbali. Aidha, mfumo wa rufaa unamtaka mtu ambaye hajaridhishwa na maamuzi ya Mahakama ya chini kukata rufaa katika Mahakama ya juu. Hivyo, kama kuna mtu yejote ambaye hajaridhika na maamuzi yoyote ya Mahakama afuate utaratibu wa kukata rufaa kwenda Mahakama ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Joseph Leonard Haule Mikumi anauliza kuhusu mishahara midogo kwa Watumishi na mikataba mibovu tunayoingia inapelekea Taifa kuingia kwenye hasara kubwa na kupelekea umaskini kwa uzembe wa kutopitia mikataba vizuri. Hili ni swali ambalo litafuata baada ya kujibu hili. Kwa sasa Serikali chini ya Bodi ya Mishahara na Maslahi ya Watumishi wanaendelea kufanya kazi suala hili ili kurekebisha hali iliyopo sasa hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna swali linalohusu Mahakimu kupewa ulinzi. Serikali inathamini kazi ya Mahakimu wa ngazi zote za Mahakama. Hata hivyo, kwa sasa tumewahimiza Mahakimu kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa. Aidha, tunawashauri wananchi kushirikiana na Mahakimu ili kuondoa dosari zozote zinazoweza kuhatarisha usalama wao. Hatujapata matishio makubwa ya kuweza kuweka walinzi kwa Mahakimu wote zaidi ya 1,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie swali hili la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Viti Maalum,

CHADEMA ambapo anasema mikataba mibovu tunayoingia inapelekea Taifa kuingia kwenye hasara kubwa na kupelekea umaskini kwa uzembe wa kutopitia mikataba hii vizuri. Jibu ni kwamba uwezo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa kuititia mikataba umeimarika baada ya kuanzishwa Idara Maalum inayopitia mikataba na kutoa ushauri. Pili, marekebisho ya Sheria ya Manunuzi, Kanuni ya 59 ya Kanuni za Manunuzi ya mwaka 2013 na marekebisho yake ya 2016 ambayo imeongezewa wigo hadi shilingi bilioni moja na zaidi hali iliyopelekea kupungua kwa idadi ya mikataba sambasamba na kuimarika kwa mapato. Tatu, raslimali watu inaendelea kuongezwa na kusababisha Wakili wa Serikali kupata muda wa kutosha kuititia mikataba mbalimbali kwa kina tofauti na ilivyokuwa siku za nyuma, hivyo uwezekano wa kuwa na mikataba mibovu kwa sasa umepungua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka anasema Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ina wanasheria waliobobea kwenye fani ya sheria na wanaojua jamii ya Watanzania, ni kwa nini Miswada mingi inayoletwa Bungeni kwa ajili ya kutungiwa sheria na Bunge huletw ikiwa na mapungufu mengi ya kisheria na mengine kukosa kabisa uhalisia kiasi cha kudhani watu wanaoandaa Miswada hiyo si watu wanaotoka katika jamii yetu? Jambo hili hufanya Miswada inayoletwa Serikalini kufanyiwa marekebisho na Bunge wakati mwingine kwa asilimia 80. Hii inachangia kulifanya Bunge kutunga sheria inayodumu kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ni kwamba Miswada inayowasilishwa Bungeni na Serikali ni mapendekezo na maoni ya Serikali kuhusu kutungwa kwa sharia. Miswada hii kama ilivyopendekezwa inawasilishwa ili Bunge litekeleze jukumu lake la kufanya uchambuzi, kujadili na hatimaye kupitisha. Mchakato wa kutunga sheria au kuchambua Miswada unajumuisha maoni ya wadau wengi ambayo yanazingatiwa katika maboresho ya Miswada hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yamekuwa mengi na mengi ya hayo yatajibowiwa kwa maandishi na kutumwa

kwa Waheshimiwa wanaohusika. Nakuomba nitumie nafasi na muda uliobakia kwa unyenyekevu mkubwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuniwezesha leo asubuhi kuwasilisha Mpango wa Makadirio ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa namna ya pekee namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwezesha Waheshimiwa Wabunge kushiriki na kuchangia hotuba ya Wizara yangu. Kwa namna ya pekee pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi Mwenyekiti kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hotuba yangu na kwa umahiri wako katika uendeshaji wa vikao vya leo katika Bunge hili na kwa kusimamia mjadala huu kitaalamu na vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Profesa Adelardus Lubango Kilangi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano ambao ananipa katika utekelezaji wa majukumu yangu na kipekee kwa kuungana nami katika kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala wa hotuba yangu. Nichukue nafasi hii pia kumshukuru sana Profesa Kabudi ambaye alikuwa Waziri kabla yangu kwa mchango wake mkubwa sana katika masuala mbalimbali ambayo yaliguswa na hotuba yangu na ameonesha ujuzi, utaalamu na ufanisi wake na nadhani mchango wake ni mkubwa na utakumbukwa sana katika kikao cha Bunge hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa maoni na ushauri ambao wanaipatia Wizara na taasisi zake katika kutekeleza majukumu yetu vizuri. Napenda nikuhakikishie wewe binafsi, Kamati yako na Waheshimiwa Wabunge wote kuwa tumepokea kwa unyenyekevu na shukrani maoni, hoja na ushauri mliotupa wakati wa mjadala wa bajeti yetu. Kwa niaba ya Wizara, tunaahidi kufanyia kazi masuala yote yallyojitokeza katika mjadala huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani kwa wadau wa maendeleo waliochangia utekelezaji wa

majukumu ya Wizara yangu. Wizara yangu inatambua na kuthamini mahusiano hayo. Wadau hao ni Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake (*UN Women*), Jumuiya ya Ulaya (*EU*)...

WABUNGE FULANI: Mabeberu.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza (*DfID*), Shirika la Maendeleo la Denmark (*DANIDA*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (*UNEP*) na Shirika la Misaada ya Kimataifa la Watu wa Marekani (*USAID*). (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Mabeberu.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Wengine ni Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kushughulikia Dawa za Kulevyia na Uhalifu, Mfuko wa Kimataifa wa Kuhudumia Wanyamapori, Shirika la Maendeleo la Ujeruman, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Shirika la Udhibiti wa Usafirishaji Haramu wa Wanyamapori na Misitu, *Bloomberg DHI* na Shirika la Maendeleo la Italia (*AICS*). (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Mabeberu.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mjadala wa hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu na katika mjadala wa hotuba ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Waheshimiwa Wabunge walitoa hoja mbalimbali ambazo kwa namna moja au nyingine ziligusa Wizara yangu na sekta ya sheria kwa ujumla. Tumezipokea hoja zote zilizotolewa na tunaahidi kuzifanya kazi na kuleta mrejesho hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuongea na wale waliochangia kwa maandishi na kuchambua Bajeti yetu kwa kina. Michango yenu ni nyenzo muhimu ya

kuboresha utendaji kazi wa Wizara na taasisi zake ili Sekta ya Sheria ikidhi matarajio ya Watanzania na iwe na mchango chanya katika maendeleo yao ya jamii, kisiasa na kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Wabunge waliochangia hotuba yetu, Wabunge 17 wamechangia kwa maandishi na Wabunge nane (8) wamechangia kwa kuzungumza. Kati ya wale waliozungumza mchana huu walitoa hoja nzuri na kubwa tutayajibu kwa maandishi ili tuwe na ufasaha zaidi katika kujibu maswali yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa uniruhusu nianze kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa. Nadhani hapa maandishi yamekorofisha.

MWENYEKITI: Eeh, umalizie. Malizia kwa kutoa hoja tu. (*Makofi/Kicheko*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndyo maana nimesema naomba rasilimaliwaitu tuiboreshe, lakini ninawashukuru wafanyakazi walionisaidia kujibu maswali haya kwa muda mfupi ambayo mmeyauliza na nina hakika majibu ambayo mtayapata kwa maandishi yatakuwa ni sahihi zaidi kuliko ambayo mmeyapata hapa kutoka kwangu. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, toa hoja.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Hoja imetolewa na imeungwa mkono na Bunge zima. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa hitimisho lako. Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA- KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 41- Wizara ya Katiba na Sheria

Kif.1001- *Administration and HR Mgt.*..... Sh. 6,191,384,000/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nina majina yaliyoletwa kwenye meza nitajitahidi, lakini kwa sababu ya muda tunaanza na Mheshimiwa Zungu.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais na Serikali kwa kuzindua Mahakama (*Mobile Court*), lakini nachukua nafasi hii vilevile kwanza kumpongeza sana *DPP* kwa zoezi ambalo amelianza sasa hivi la kwenda kwenye Mahabusu na Magereza na kupunguza msongamano kwenye Magereza yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatumia takribani *one billion* kwa mwezi kulisha mahabusu ambao kesi zao wengine ni ndogo ndogo tu. Ili kuokoa pesa hizi, swali langu ni hili: Serikali sasa ina mkakati gani wa kufanya zoezi hili liwe endelevu na kumsaidia *DPP* kwa kumpa *funding* za kwenda kufanya kazi hizi kwa uhakika ili Magereza haya yapungukiwe na hawa mahabusu na Serikali iweze kuokoa pesa zake kwa kulisha watu ambao wanawenza kuwa wananchi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina lengo la kushika shilingi ya Waziri. Nakushukuru. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Zungu. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna hili tatizo la mlundikano

wa mahabusu na ni kweli kwamba ziko hatua kadhaa ambazo zimeanza kuchukuliwa, mojawapo ikiwepo ile hatua ambayo *DPP* amefanya ziara katika mahabusu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema tu kwamba sio *DPP* peke yake, hata Wizara ya Katiba na Sheria imekuwa inashiriki katika ziara hizo, hata Majaji ikiwa ni pamoja na Majaji Wafawidhi katika maeneo mbalimbali Mahakimu, Wanasheria na Mawakili wa Serikali nao pia wamekuwa wanashiriki katika ziara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme kwamba ziara hizo zimekuwa zina manufaa makubwa kwa sababu mojawapo ya mambo ambayo wameyagundua ni kwamba watu wengine wanakuwa wako mahabusu kwa sababu hajajui tu wafanye nini ili waweze kupata dhamana na makosa yao ni madogo madogo na kwa kweli kesi hizi nyingi zinaanzia hasa kwenye Mahakama ya Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri mbali na kuongeza zaidi hizi ziara kadri Mheshimiwa Mbunge anavyoshauri, pia nafikiri itaambatana na kutoa elimu zaidi kwa hawa mahabusu namna gani waweze kuomba dhamana na wasilazimike kuwa mahabusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria inao mpango wake kwa sababu ile sheria ya kuhusu msaada wa sheria ilishatungwa na Bunge lako Tukufu na sasa uko mpango wa kutekeleza utoaji wa msaada wa sheria na mojawapo ya walengwa katika msaada wa sheria itakuwa ni mahabusu, wajue namna nzuri ya kuomba dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea Mheshimiwa Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Langu ni moja tu ambalo nilikuwa nahitaji uafanuzi wa Mheshimiwa Waziri kuhusu suala ambalo

Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati wamelizungumzia katika kitabu chao ukurasa wa 15 juu ya wazee wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa muda mrefu sasa wazee wa Mahakama wamekuwa wakifanya kazi na Mahakimu katika Mahakama zetu za mwanzo, lakini hawapati posho zao kwa wakati posho. Kwa bahati mbaya wanalipwa shilingi 5,000/= kwa kesi baada ya kesi kuhukumiwa. Nina kesi za wazee 14, naamini hili pia liko kwa maeneo mengine katika Mji wa Babati, ambapo tangu mwaka 2017 hawajalipwa fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifahamu, pamoja na hili la Kamati kushauri hao wazee waondolewe, kwa kuwa sasa tuna Mahakimu ambao wanazingatia sheria zaidi; wakati mnafanya mchakato huo, ni lini mtawalipa madai yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina sababu ya kuondoa shilingi lakini nahitaji *commitment* ya Serikali, maana hao wazee kwa kweli wanatia huruma na wengine wamefariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba ziko changamoto zinazohusiana na malipo ya Wazee wa Mahakama na kwa kweli zinatokana na upungufu wa fedha, ingawa zimekuwepo juhudzi za kuongeza bajeti ya kuwalipa wazee hawa kila mwaka. Kwa hiyo, kila mwaka zinafanya kila juhudzi za kuongeza kidogo bajeti hiyo na ili itumike pia kulipa madeni yaliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mjadala na mazungumzo wa namna nzuri zaidi ya kuweza kuwalipa wazee hawa kwa sababu nafikiri kwa sasa hivi wanalipwa kwa kesi mpaka itakapokamilika. Nadhani hiyo nayo

inachangia katika kupunguza kile kipato wanachokipata. Yapo majadiliano ya kutafuta mfumo mzuri zaidi wa kuwalipa labda iwe inahesabiwa kwa siku au kwa namna nyingine yoyote itakayofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile lingine la kuhusu kama iko haja ya kuendelea kuwa na wazee hawa wa Mahakama, ni pendekezo zuri, jema lenye nia nzuri na ninafikiri kwa upande wa Serikali litachukuliwa, lakini linahitaji mjadala mpana na mashauriano, kwa sababu palikuwa na sababu mpango huu wa kuwa na Wazee wa Mahakama ulipowekwa katika mfumo wa sheria zetu. Nafikiri mojawapo ya wazo lililokuwa linafikiriwa, hawa wana-reflectmsimamo au *thinking* ya jamii katika suala lile husika. Kwa hiyo, kama nilivyosema. nadhani ni wazo zuri, litachukuliwa, litaingizwa katika mchakato wa kuchujwa na kuangaliwa ili kusudi mwisho wa siku tuwe na kitu ambacho wadau wote tunaridhika nacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Hussein Bashe.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilitaka nipate *commitment* kutoka Serikalini kwamba utoaji wa haki ni *mirror muhimu* sana katika maendeleo ya nchi yoyote duniani. Mahakama kama *pillar* ni moja ya taasisi muhimu katika maendeleo ya Taifa lolote; na pale ambapo Mahakama inakuwa *not efficient and effective* kwa sababu ya kukosa *resources*, inatia doa dhamira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango wa Maendeleo wa Mahakama na walivyokuja kwenye Kamati ya Bajeti, Mahakama iliomba kiasi cha shilingi bilioni 3.6 na ukiangalia katika mafungu mbalimbali Ofisi ya *Attorney General*/haijatengewa hata shilingi za *development*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka nipate *commitment* ya Serikali kwamba wakati tunapitisha mafungu haya watauongezea Mfuko wa Mahakama fedha kwa ajili

ya kuweza kusaidia Ofisi ya *Attorney General* na kuisaidia Mahakama kukamilisha miradi mikubwa miwili ya uanzishwaji wa *High Court* Mara na katika Mkoa wa Kigoma? Naomba *commitment* kutoka Serikalini katika hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mbunge kwa kutambua umuhimu wa mhimili wa Mahakama. Huu ni mmoja wa mhimili mitatu ambayo lazima iwe na *resources* ipewe kipaumbele ili Serikali iweze kukamilika. Kati ya vipimo vyta Serikali bora inayokubalika ni mfumo mzima wa sheria na haki kwa rala zake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani katika hotuba nilioitoa, maboresho mageuzi, uandishi wa sera mpya, zoezi ambalo linaendelea, madhumuni yake ni kuipa uzito mhimili huu wa haki na kuuboresha ili ukamiliike na wananchi waweze kutambua kwamba wanapata haki na kwa wakati. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kamati ya Bajeti, nawashukuru sana washiriki wote ambao mlisema kwa hoja zenye nguvu umuhimu wa kuongeza bajeti ya Mahakama. Hata Mheshimiwa Waziri wa Fedha alikuwepo na kamati nzima hatimaye tulikuja kutambua kwamba kwa hali ilivyo sasa hivi, hatuwezi kuvuka kikomo cha bajeti, lakini ndani ya Wizara na ndani ya Mahakama kuna uwezekano wa kurekebisha vifungu Fulani fulani ambavyo vitapelekwa kwenye maeneo muhimu na ambayo ni kipaumbele kama vile ulivyoeleza Mheshimiwa Mbunge hasa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hilo linaendelea na *commitment* ambayo mimi kama Waziri wa Wizara hii naweza kuitoa ni kwamba zoezi la kutazama kasma mbalimbali ndani ya Wizara litafanyika ili pale ambapo ninyi

wenyewe Wabunge mlisema panahitajika kuongeza pesa tuweze kuzipeleka huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa hukusema kwamba unataka kutoa shilingi. Kwa hiyo, tunaendelea. Mheshimiwa Kingu.

MHE. ELIBARIKI E. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, langu ni dogo. Nilikuwa nataka nipate ufanuzi wa Serikali namna ya upatikanaji wa ma-*advocate* wetu ambao wanasaidia tafsiri za sheria katika Mahakama zetu Tanzania. Kwa uhalisia inaonekana kwamba *concentration* yote ya kuwapata ma-*advocate* wanafunzi wanapomaliza elimu zao za *degree* ya kwanza katika vyuo mbalimbali lazima waendele *Law School* pale Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nipate ufanuzi wa Serikali; nchi yetu hii ni kubwa na watoto wa kimasikini wa Kitanzania wanapotoka vyuo mbalimbali; Mbeya, Arusha, Mwanza na baadhi ya mikoa ambapo kuna vyuo vikuu, kwa nini Serikali isianzishe mikakati maalum ya kuhakikisha kwamba sehemu ambapo kuna vyuo vinavyotoa *degree* ya kwanza ya sheria, vijana wa Kitanzania waweze kupata fursa ya kufanya *Law School* katika mikoa yao kuliko kwenda Dar es Salaam?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imekuwa ikiwasababisha Watanzania wengi, watoto wa kimasikini kuingia gharama kubwa. Jambo hili nafikiri siyo sahihi, nilikuwa nataka nipate ufanuzi wa Serikali, nini mipango ya Serikali? Kama sitapata majibu mazuri kwa kweli nitaomba kushika shilingi na kama Bunge litaridhia tuweze kujadili na kupata mustakabali wa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Kingu, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tunayo *Law School of Tanzania*, yaani shule ya mafunzo ya mafunzo kwa vitendo kwa ajili ya kuandaa Wanasheria wetu kwa ajili ya kufanya kazi za Mawakili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kwa sasa hivi shule hiyo au chuo hicho kiko Dar es Salaam peke yake na ni kweli kwamba nchi yetu ni kubwa, viko vyuo vingi ambavyo vinatoa mafunzo ya sheria katika ngazi ya *degree*; na ni kweli kadri anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna hizi changamoto kwamba vyuo ni vingi, wanafunzi ni wengi na kwa hiyo pengine ingekuwepo haja ya kuwa na mkakati maalum wa kuona namna gani ya kulifanya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze kwa kusema kwamba, hata kuwa na hiki chuo kimoja Dar es Salaam ilikuwa ni hatua moja kubwa, pamekuwa na historia ndefu na mchakato mrefu na mazungumzo marefu ya namna gani ya kuwajengea uwezo wanasheria wetu wanapotoka katika vitivo vyta sheria kabla ya kwenda kwenye *practice*, wapitie mahali fulani ambapo wataweza kunolewa na kutayarishwa vizuri kwa ajili ya kuwa mawakili wazuri. Katika mkakati huo ambao nadhani ulikuwa sehemu ya *Legal Sector Reform Program* na kulikuwa na *firm map project* na kadhalika, vilifikiria kuanzisha chuo hiki kimoja. Kwa hiyo, hii ilikuwa ni hatua ya kwanza. Ni mafanikio kuwa na shule hii moja hapo ilipo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yaliyotokea baadaye nafikiri ni matokeo ya mafanikio kwamba, sasa elimu imeongezwa zaidi, wigo umepanuliwa zaidi, kwa hiyo changamoto hii imejitokeza. Nipende tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, jambo hili tayari limeshafikiriwa na kwa kweli ilishaanza mijadala ya kufikiria ni namna gani ya hii huduma ya *Law School of Tanzania* inaweza ikasambazwa katika maeneo mbalimbali. Hiyo sasa inawahitaji kuwaleta pamoja wadau mbalimbali ambao ni watumiaji wa hizi huduma, vyuo vinavyotoa elimu ya *degree*,

mahakama na kadhalika. Nimhakikishie kwamba mjadala huo unaendelea na nafikiri siku za usoni tutapata suluhisho juu ya nini kifanyike. Naomba kuwasilisha hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu. Mheshimiwa Kingu.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nashukuru kwa maelezo mazuri ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakin basi tu niongeze kwa kuweka msisitizo kwamba, Serikali ione haja ya kupeleka huduma hii ya Shule ya Sheria mikoani ili kuwapunguzia adha ya mzigo mzito wanayoipata watoto wa Kitanzania katika masuala mazima yanayohusiana na kuandaa ma-*advocate*. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Acha tui patie Serikali muda waliangalie kwa umakini. Mheshimiwa Salome Makamba.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kama sitapata majibu mazuri ya Serikali nina nia ya kushika shilingi ya Waziri. Sote tunafahamu kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo dira na ndiyo inayotoa mwongozo na mtazamo wa Utanzania na Tanzania ni nini. Mwaka 2014, Watanzania waliona kwamba Katiba tuliyonayo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina vifungu ambavyo vimepitwa na wakati na kama haitoshi inatakiwa ifanyiwe marekebisho. Likakaa Bunge Maalum la Katiba wakaanza mchakato wa kutafuta Katiba Mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tumemsikia Mheshimiwa Rais akisema kwamba, suala la Katiba Mpya siyo kipaumbele chake na haimo kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi. Kama nilivyosema kwenye hotuba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, ukurasa wa 206 mpaka 207 wa llani ya Chama cha Mapinduzi unasema wazi: Ili kuendeleza utawala bora, demokrasia na uwajibikaji katika kipindi cha miaka mitano ijayo CCM itahakikisha kuwa Serikali inatekeleza yafuatayo:-

(g) Kukamilisha mchakato wa kutunga Katiba mpya na kuanza kuitekeleza kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini *commitment* ya Serikali kutimiza ahadi waliyowahadaa wananchi wa Tanzania kwamba wataleta Katiba mpya, nataka *commitment* ya Serikali, la sivyo, nitashika shilingi ya Waziri. *(Makof)*

MWENYEKITI: Ahsante. Kwani Mheshimiwa Makamba, kwani llani ya Chama chochote cha Siasa ukiiandika na kuitoa kwa wananchi lazima chochote kila kitu kilichomo mle kitekelezwe?

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba Katiba ni dira, Katiba ndiyo Utanzania, Katiba ndiyo mwongozo wa kila kitu na halafu ikafika muda fulani ikaonekana kwamba iko haja ya kurekebisha baadhi ya vifungu vya Katiba. Katiba hii ina historia, tena historia yake ni ndefu katika nchi yetu na kwamba tumekuwa tunaendelea kuiishi hii Katiba kama sehemu ya maisha yetu. Hata sasa hivi tunaendelea kuiishi kama sehemu ya maisha yetu.

Sasa kulikuwa na zile ahadi kwamba itakamilishwa, huu mchakato utaangaliwa upya, hiyo *commitment* bado iko pale pale kwa sababu Katiba tunayo, Katiba tunaiishi, Katiba ni maisha yetu, Katiba siyo kitu kilichoandikwa tu hapa, Katiba ni mambo yote ambayo Serikali inayafanya, Katiba ni mambo yote ambayo jamii inayafanya, hiyo ndiyo Katiba katika ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mchakato wa Katiba *commitment* ya Serikali ni hiyo kwamba, mchakato

wa katiba utaendelea kwa kadri mazingira na mahitaji yatakavyoruhusu. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Salome Makamba, maelezo yametosheleza!

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu wa Serikali analishauri Bunge kwamba suala la Katiba ni tunaliishi, tunaliishi, tutalifikia. Sijaridhishwa na majibu ya Serikali kwa sababu suala hili siyo la masihara, naomba niwaombe Wabunge wenzangu waweweze kuchangia tushauriane namna ambavyo tutapata *commitment* ya Serikali juu ya mchakato wa Katiba mpya. Naomba kutoa hoja.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Haijaungwa mkono eeh?

WABUNGE FULANI: Aaaa, imeungwa mkono.

MWENYEKITI: Haya, hoja imeungwa mkono, wanaotaka kuichangia tuone, tuchukue majina! Waheshimiwa tuna Mafungu mengi tunazingatia hilo. Mheshimiwa Komu.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nianze kwa kusema Katiba ni mkataba kati ya wananchi na wale wanaotawala. Kwa hiyo kama tunataka katika nchi hii tuendelee kuwa nchi ambayo ina amani, nchi yenye utulivu, nchi ambayo ni mahali pazuri pa kuishi ni lazima hili jambo liishe haraka kwa kadri inavyowezekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata jana Waziri mmoja hapa akihitimisha alisema kwenye Mataifa mengine ambayo yana *stability* kuna mambo ambayo tayari walishatulia na hawayasemi tena, ni kwa sababu Katiba zao walishakaa wakafika *consensus*. Kwa hiyo tunahitaji *consensus* katika hii nchi. Ndiyo maana kilio hiki cha muda mrefu kilisikilizwa na

Serikali ya Awamu ya Nne na walioandika hii llani nafikiri walifanya uchambuzi wakaona kwamba mambo machache ya muhimu ya kufanya ni pamoja na mchakato wa Katiba na wakasema kabisa watalikamilisha. Jambo hili limechukua gharama kubwa ya fedha za Watanzania, sasa ni kwa nini halikamilishwi? Lilikuwa limeshafika hatua za mwisho, kwa hiyo kero na vilio bado viro. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo hapa la mfumo wa uchaguzi katika nchi yetu ambao una utata mkubwa, tuna tatizo la Muundo wa Tume ya Uchaguzi ambayo siyo huru katika nchi hii, tuna kero nyingi za Muungano. Kama tunataka amani katika nchi hii na tunaenda kwenye uchaguzi, tunahitaji Katiba mpya kuliko kitu kingine...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Komu. Mheshimwa Waitara.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Bahati nzuri hakuna kiongozi wa Serikali yeoyote ambaye amewahi kusema kuwa Katiba siyo muhimu, kwa hiyo Katiba ni muhimu sana. Jambo la pili tuna viporo vingi katika nchi hii na kupanga ni kuchagua. Tunayo maeneo ambayo tunaweza tukaunganisha lami katika mkoa na mkoa, hiki ni kiporo na Katiba ni kiporo, tumalize kwanza lami. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna maeneo ambayo tuna shida ya maji katika Taifa hili, tuweke maji watoto wapate maji, tusubiri Katiba. Tuna watu wanahitaji kujenga maeneo mbalimbali, Mahakama zinadaiwa hapa zijengwe, tujenge kwanza majengo ya Mahakama, tusubiri Katiba. Hiki kiporo kitasubiri mpaka Serikali itakapopata fedha ya kutosha kuweza kukamilisha mchakato wa Katiba mpya. Hakuna mtu ambaye amesema usipomaliza Katiba utakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Makamba ni Mbunge Viti Maalum, Mkoa wa Shinyanga, yale malalamiko watu wanahitaji maji ya kunya safi na salama, tuwapelekee maji kwanza! Yale madarasa, tujenge madarasa, vyuo vikuu na vitu chungu nzima. Jambo hili ni muhimu lakini kwa wakati wake litatekelezwa kadri ya uwezo wa Serikali. Ahsante. (Makof)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Haji.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Bahati nzuri nami nilikuwa ni mmoja kati ya Wajumbe wa Bunge la Katiba lililopita. Hili jambo kiudhati lilifikia mwisho na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi walioanza sherehe ndani ya Bunge hili kwa kuitisha Katiba Mpya, haikutosha wakaenda uwanja wa Jamhuri kusherehekea kuitisha Katiba Mpya. Wako viongozi ambao wamewapa nishani kwa ajili ya kuitisha Katiba Mpya, akiwemo Makamu wa Rais, Mheshimiwa mama Samia, wana nishani ambazo wameziweka kwa sababu walikubali kuitisha Katiba Mpya. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wanaomba kura Watanzania, walikuwa wanajua kama Watanzania wanahitaji maji, wanahitaji afya, wanahitaji maendeleo yote, lakini la Katiba bado wakaona umuhimu wake na ndiyo maana waliliweka kwenye llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Kwa hiyo, nawaomba wawe waungwana, wawe wakweli, Watanzania wamewaahidi na Watanzania waliwapa kura mojawapo ikiwa ni kwa sababu waliwaahidi kuwaletea Katiba Mpya ndani ya nchi. *Nawaomba msilambe matapishi yenu*, simameni katika uungwana na ukweli, Watanzania wanahitaji Katiba Mpya na si kwa njia nyingine... (Makof) [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Haji, hebu tumia lugha ya kibunge tu futa haya maneno kulamba matapishi yenu, futa tu.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafuta hiyo kauli.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimesikitishwa sana na maneno ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, nami nilikuwa mmoja katika Wajumbe wa Bunge la Katiba. *Stages* zote zilishapita, tulishapitisha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, tulishakuwa na Tume ya Warioba, lilibaki jambo moja tu la kura ya maoni. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi Wabunge wa CCM wananihangaza, walisema kabisa kwenye llani yao na llani ni jambo ambalo wanalitekeleza. Hata juzi Bashiru anasema ye ye anapita sehemu mbalimbali za nchi kwa sababu wao ndio Chama Tawala na ndio wanatekeleza llani na moja ya mahitaji yaliyokuwepo kwenye llani yao ni suala la Katiba.

Sasa watuambie, walikuwa wanawalaghai wananchi au maana yao ni nini? Yaani siku zote wamekuwa wakicheza humu ndani wanafurahia kupitishwa kwa Katiba, leo Mwanasheria Mkuu anasema kwamba mahitaji bado, tunaishi Katiba, Katiba ipi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani kwa kweli tuna kila sababu, kwa sababu katika hiyo Katiba Mpya tungekuwa na Tume, lakini siyo hiyo tu, wanawake wa Bunge tungekuwa sasa *fifty fifty*, hatungekuwa na sababu ya Viti Maalum... (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Lyimo. Mheshimiwa Msukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana. Nami naomba nichangie tu kwamba namshukuru mjomba wangu Salome anajua vizuri kuisoma llani ya Chama cha Mapinduzi. Ilani ya Chama cha Mapinduzi si kuisoma tu, ni vizuri aungerudi huku ili tukawa tunamweleza na mambo mengine ambayo tumeyapanga kama chama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala linaonekana linataka kuwa la haraka sana kwa upande wa wenzetu, lakini naijiliza kwani llani tu, yaani suala hili tu ndiyo limekuwa la umuhimu sana. Hebu naomba niwarudishe nyuma, miaka iliyopita wakati sisi hatujaingia Bungeni, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ililandika kusomesha bure haikutekeleza, tulikuwa na mradi wa *Stiegler's Gorge* hatukutekeleza, hatukuwa na reli ya mwendo kasi, hatukutekeleza, tulikuwa na kuhamia Dodoma, hatukutekeleza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mjomba wangu na kwa kuwa yeye tunatoka sehemu moja na shida zetu anazijua, maji, hiyo reli na vitu vingine na watu wa Shinyanga wanamwangalia Wasukuma, kweli anakuja kuomba Ilani anaacha kuomba matatizo ya maji na upungufu wa madarasa na mambo ya wanafunzi. Namwomba mjomba wangu, aachane na hizo kelele huko, arudishe shilingi tuendelee kutekeleza miradi ambayo ni ya msingi na... (*Makof!*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Msukuma. Mheshimiwa Simbachawene.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli leo nimesikitika na nimesikitika kwa sababu ni hawa hawa ndugu zetu wa upande wa Upinzani wakati sisi tumemaliza zoezi la Katiba na sasa tunayo Katiba pendekewa na ni kweli tulikutana uwanja wa Jamhuri,

wenyewe walikuwa wanatembea nchi nzima kупinga hiyo Katiba pendekezwa. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu walikuwa wanaipinga, sasa leo watujibu maswali yafuatayo:- Kwamba, je, tukirudisha zoezi Katiba mpya watapiga kura ya ndiyo? Pia kwa nini wakati ule walipinga na leo wanasesma wanaitaka, ni ile ile au nyine? Swali la tatu, je, yale ambayo walikuwa wanayakataa sasa yamo? Au waliyokuwa wanayataka sasa wameona yamo? Hawa hawana msimamo na kwa sababu hawana msimamo, watuache tuliopewa dhamana ya kuongoza nchi hii tuendelee na kazi yetu ya kuwatafutia wananchi maji, barabara na mahitaji muhimu kwa ajili ya maendeleo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Mtanzania anayeweza kufa kwa sababu ya kukosa Katiba. Katiba hii tulionayo imefanya mambo makubwa, imeijenga hii nchi katika misingi unayoiona leo, nchi hii ina amani, ina uhuru, imetulia na iko vizuri kwa sababu ya Katiba hii. Tuienzi Katiba hii, hawa hawana tatizo la Katiba wana matatizo yao binafsi... (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Simbachawene. Mheshimiwa Joseph Mbilinyi.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwanza nimwambie Mheshimiwa Simbachawene, ile Katiba haikuwa Katiba pendekezwa ilikuwa Katiba chakachuliwa. Tulikataa ile Katiba yenu pendekezwa kwa sababu mllichakachua matakwa ya wananchi yaliyotolewa kwenye Tume ya Warioba. Mimi nataka niwaulize, kwa nini hawa watu wanaogopa sana Katiba Mpya? Mchakato ule ulianza vizuri, Mzee Kikwete alitaka kuacha *legacy*, baadaye hawa jamaa wakaona Mheshimiwa Dkt. Kikwete anaondoka wakaingia woga. Wakavuruga ule mchakato, sasa tunasema muda basi wa

Katiba unaweza ukawa umekwisha, hata tume huru pia hamtaki, mnafaidika nini na kitu ambacho kila mwananchi anakilalamikia suala la kutaka Katiba mpya, suala la kutaka tume huru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tume hii kama tutashindwa Katiba, basi tuifumue hii tume narudia tena, maana hii tume ni ile ambayo Rais amewaambia watendaji wake kwamba, iwapo watachagua wagombea au washindi kutoka Upinzani watafanya nini, atawafukuza kazi. Hawajamaa wanaogopa njaa, wanaogopa kufukuzwa kazi, matokeo yake wataenda kusababisha maafa kwa sababu wataenda kusimamia vitu ambavyo hata wao wenyeche hawaviamini. Mwanasheria Mkuu... (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mbilinyi.

(Hapa Mhe. Joseph O. Mbilinyi aliendelea kuzungumza)

MWENYEKITI: Ahsante, hamna hiyo, muda wako umekwisha.

(Hapa Mhe. Joseph O. Mbilinyi aliendelea kuzungumza)

MWENYEKITI: Mheshimiwa! Mheshimiwa Kakunda.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja tu sijamaliza, dakika moja tu.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi namsifu sana Mheshimiwa Makamba, siyo Mheshimiwa Makamba wa kwetu, Mheshimiwa Salome Makamba wa Upinzani amesoma Ilani ya Uchaguzi. Sasa mimi nataka nimfafanulie kwamba Ilani ya Uchaguzi aisome vizuri ina Ibara 189, maelekezo mahsus kwa sekta 507 na yamepangwa kwa *priority*, nimsomee *priority* 12 za kwanza, kwama ifuatavyo: Elimu, maelekezo 43; ardhi, maelekezo 38; afya maelekezo 36; uwezeshaji

maelekezo 36; maji maelekezo 29; uchukuzi maelekezo 28; usafiri na usafirishaji maelekezo 26; kilimo maelekezo 25; nishati maelekezo 24; sekta ya fedha maelekezo 19; madini maelekezo 19 na mifugo maelekezo 17. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo ndiyo *priority* za juu kwenye llani ya Uchaguzi, naomba asome vizuri. Hiyo ndiyo Rais anayetuongoza sisi ametuelekeza tujielekeze kwenye kutekeleza zile *priority* za juu ambapo hilo eneo lake analolizungumizia halipo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka tu nimwambie aisome vizuri llani ya Uchaguzi ye ye mwenyewe atajua *priority* zetu ni zipi. Kama ye ye anaona ni *priority* kuingizwa kwenye uchaguzi wa mwaka ujao waingize kwenye llani yao haina shida. Ahsante sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Makamba, hitimisha.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashukuru Mheshimiwa Rais anaona aina ya Mawaziri aliorachagua kumsaidia kusimamia Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri hawa hawa wanapita wanasema llani hii imetekelozwa kwa asilimia 100, hawa hawa, leo wamegeuka wanasema wanavyo vipaumbele na Katiba pendeketzwa ya Warioba siyo kipaumbele cha Serikali ya CCM. Watanzania watawahukumu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Serikali iache kuchezea pesa za Watanzania. Bunge la Katiba limetumia zaidi ya shilingi bilioni 60 kukaa na kujadili mchakato wa Katiba Mpya leo jambo limefika mwisho kwenye hatua ya kura ya maoni Serikali ya CCM inafika hapa na kuwakana Watanzania baada ya kuteketeza pesa zao na kusema suala la Katiba Mpya siyo kipaumbele chao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimetekeleza wajibu wangu kama Mbunge kuikumbusha Serikali kwamba suala la Katiba ya wananchi, Katiba iliyopo inampa mamlaka makubwa sana Mheshimiwa Rais, haina Tume huru ya Uchaguzi, inakandamiza uhuru wa Wanzibar na inasababisha mauaji na hakuna mwenye nguvu ya kuhoji. Waheshimiwa Wabunge, leo nitaingia kwenye historia kwa kupigania haki ya Taifa letu na niwaruhusu kura ipigwe hapa ya kuamua kwamba tunataka...

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa tutafanya uamuzi kuhusu hoja ya Mheshimiwa Salome Makamba.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja ilihamuliwa na Kukataliwa)*

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i>	Sh.152,064,000/=
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning Division</i>	Sh.367,696,000/=
Kif. 1004 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh.84,820,000/=
Kif. 1005 - <i>Government Communication Unit</i>	Sh.80,138,000/=
Kif. 1006 – <i>Procurement Management Unit</i>	Sh.121,057,000/=
Kif. 1007 – <i>Information and Communication Technology Unit</i>	Sh.242,155,000/=
Kif. 2001 – <i>Human Rights Division</i>	Sh.315,440,000/=
Kif. 2004 – <i>Public Legal Services Division</i>	Sh.264,247,000/=
Kif. 2005 – <i>Natural Wealth and Resources Observatory Unit</i>	Sh.150,217,000/=
Kif. 4001 – <i>Constitutional and Justice Monitoring Division</i>	Sh. 364,378,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama

Kif. 1001 - <i>Administration and HR Management</i>	Sh.984,620,000/=
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i>	Sh.57,350,000/=
Kif. 1003 – <i>Procurement Management Unit</i>	Sh.22,950,000/=
Kif. 1004 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh.10,020,000/=
Kif. 1005 – <i>Recruitment, Appointment and Confirmation Unit</i>	Sh.210,322,000/=
Kif. 1006 – <i>Ethics and Discipline Section</i>	Sh.19,700,000/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kif. 1001 – <i>Administration and HR Management</i>	Sh.1,895,189,000/=
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i>	Sh.345,053,000/=
Kif. 1003 – <i>Planning Division</i>	Sh.433,047,000/=
Kif. 1004 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh.185,02,000/=
Kif. 1005 – <i>Government Communication Unit</i>	Sh.116,630,000/=
Kif. 1006 – <i>Legal Registry Unit</i>	Sh.0
Kif. 1007 – <i>Procurement Management Unit</i>	Sh.164,348,000/=
Kif. 1008 – <i>Research and Library Service Unit</i> ... Sh.	80,078,000/=
Kif. 1009 – <i>Information and Communication Technology Unit</i>	Sh.204,707,000/=
Kif. 2001 – <i>Coordination and Advisory Services</i>	Sh.991,526,000/=
Kif. 2003 – <i>Legislative Drafting</i>	Sh.1,078,829,000/=
Kif. 3001 – <i>Civil Litigation and Arbitration Division</i>	Sh.0
Kif. 3001 – <i>Treaties and Contracts Division</i> ..Sh.1,137,974,000/=	
Kif. 4001 – <i>Constitutional Affairs and Human Rights</i>	Sh. 0

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 19 – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

Kif. 1001 – *Administration and HR*

Management Sh.2,797,370/=

Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit* Sh.99,200,000/=

Kif. 1003 – *Planning Division* Sh.111,106,000/=

Kif. 1004 – *Internal Audit Unit* Sh.80,315,000/=

Kif. 1005 – *Procurement Management Unit* Sh.69,640,000/=

Kif. 1006 – *Information and Communication*

Technology Unit Sh.69,640,000/=

Kif. 1007 – *Government Communication*

Unit Sh.53,475,000/=

Kif. 1008 – *Library Services and Research Unit* Sh.84,446,000/=

Kif. 1009 – *Legal Registry Unit* Sh.75,085,000/=

Kif. 2001 – *Case Management and Quality*

Assurance Sh.328,418,000/=

Kif. 2001 – *Arbitration Division* Sh.2,604,119,000/=

Kif. 2003 – *Litigation Division* Sh.667,050,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

Kif. 3001 – *Fraud, Money Laundering and*

Corruption Offence Sh.702,486,000/=

Kif. 3002 – *Assets Forfeiture Transnational &*

Specialized Crimes Sh.760,395,000/=

Kif. 3003 – *Case Management, Coordination of*

Criminal Cases Sh.661,404,000/=

Kif. 1001 – *Administration and HR*

Management Sh.2,155,197,000/=

Kif. 1002 – *Finance and Accounts*

Unit Sh.364,775,000/=

Kif. 1003 – *Planning Division* Sh.286,833,000/=

Kif. 1004 – *Internal Audit Unit* Sh.115,833,000/=

Kif. 1005 – *Procurement Management*

Unit Sh.125,700,000/=

Kif. 1006 – *ICT and Information Unit* Sh.118,052,000/=

Kif. 1007 – *Government Communication Unit* Sh.63,306,000/=
Kif. 1008 – *Research and Library Services Unit* Sh.81,906,000/=
Kif. 1009 – *Legal Registry Unit* Sh.147,265,000/=
Kif. 2002 – *Civilization and Prosecutions* Sh.761,701,000/=
Kif. 2004 – *Regional Office Arusha* Sh.912,383,000/=
Kif. 2005 – *Regional Office Dodoma* Sh.421,439,000/=
Kif. 2006 – *Regional Office Dar es Salaam* Sh.2,058,436,000/=
Kif. 2007 – *Regional Office Iringa* Sh.351,577,000/=
Kif. 2008 – *Regional Office Moshi* Sh.446,003,000/=
Kif. 2009 – *Regional Office Kagera* Sh.341,090,000/=
Kif. 2010 – *Regional Office Mbeya* Sh.546,400,000/=
Kif. 2011 – *Regional Office Mtwara* Sh.374,064,000/=
Kif. 2012 – *Regional Office Mwanza* Sh.898,136,000/=
Kif. 2013 – *Regional Office Ruvuma* Sh.286,814,000/=
Kif. 2014 – *Regional Office Sumbawanga* Sh.279,123,000/=
Kif. 2015 – *Regional Office Tabora* Sh.556,442,000/=
Kif. 2016 – *Regional Office Tanga* Sh.451,383,000/=
Kif. 2017 – *Regional Office Shinyanga* Sh.403,240,000/=
Kif. 2018 – *Regional Office Singida* Sh.313,878,000/=
Kif. 2019 – *Regional Office Lindi* Sh.234,281,000/=
Kif. 2020 – *Regional Office Mara* Sh.335,040,000/=
Kif. 2021 – *Regional Office Manyara* Sh.155,064,000/=
Kif. 2022 – *Regional Office Kigoma* Sh.254,509,000/=
Kif. 2023 – *Regional Office Pwani* Sh.341,803,000/=
Kif. 2024 – *Regional Office Njombe* Sh.304,048,000/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wajumbe, naongeza muda usiozidi dakika thelasini ili tukamilishe kazi iliyo mbele yetu. Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

Kif. 2025 – *Regional Office Morogoro* Sh.310,745,000/=
Kif. 2026 – *Regional Office Geita* Sh.290,563,000/=
Kif. 2027 – *Regional Office Simiyu* Sh.196,316,000/=

Kif. 2028 – Regional Office Katavi Sh. 212,111,000/=
Kif. 2029 – Regional Office Songwe Sh. 84,417,000/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama

Kif. 1001 – Administration and HR

Management Sh.68,816,922,532/=

Kif. 1002 - Finance and Accounts Unit ... Sh.182,349,995/=

Kif. 1003 – *Planning and Monitoring Division..Sh.639,960,000/=*

Kif. 1004 – Internal Audit Unit Sh.205,592,950/=

Kif. 1005 – *Information, Communication and*

Technology Unit Sh.256,054,000/-

Kif. 1007 – Procurement Management Unit...Sh.299,000,000/=

Kif. 1008 – Estates Management Unit Sh.208,521,500/=

Kif. 1009 – Records Management Unit . . . Sh.326,745,550/=

Kif. 1010 - *Library Services Unit* Sh.275,492,000/=

Kif. 1011 - Legal Services Unit Sh.49,114,800/=

Kif. 2001 – High Court Main Registry... Sh.1,743,841,000/=

Kif. 2002 - Court of Appeal Dar es Salaam..Sh.1,450,403,000/=
KIS 2002-1116-7 Sh. 7/24/2014 (20/)

Kif. 2003 - High Court Zones Sh. 7,846,271,600/-
Kif. 2004 - High Court Districts Sh. 8,579,810,000/-

Kif. 2004 - High Court Divisions..... Sh. 3,578,912,000/-
Kif. 2005 - Resident Magistrate Courts..... Sh. 5,224,500,000/-

K.R. 2005 - Resident Magistrate Courts Sh. 5,324,500,000/-
K.R. 2006 - District Courts Sh. 6,110,300,000/-

Kif. 2007 Primary Courts \$b F 030-030-073 /

Kif. 2008 - Case Management Division \$b 216,170,000 /

Kif. 2000 - Judicial Inspection, Supervision &

RRI: 2009 - Judicial Inspection, Supervision & Ethics Sh 125,965,000/-

f. 2010 – Judiciary Delivery Unit Sh.265,520,000.

Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 55 - Iume ya Hakī za Bihārī

Administration and HR

KII. 1001 - Administration and HR
Management Sbs. 1 700 E40 E08 /

Kif. 1003 – <i>Internal Audit Unit</i>	Shs. 96,857,602/=
Kif. 1004 – <i>Legal Services Unit</i>	Shs. 294,670,000/=
Kif. 1005 – <i>Procurement Management Unit</i>	Sh. 61,086,000/=
Kif. 1006 – <i>Management Information System Unit</i>	Sh. 75,992,900/=
Kif. 1007 – <i>Planning, Monitoring and Evaluation Unit</i>	Sh. 122,440,000/=
Kif.2001 – <i>Complaints and Investigation Division</i>	Sh. 1,037,038,900/=
Kif. 2002 – <i>Human Rights</i>	Sh. 0
Kif. 2003 – <i>Public Ed., Comm. Research & Documentation</i>	Sh. 347,888,800/=
Kif. 2004 – <i>Public Education and Training</i>	Sh. 0
Kif.3001 – <i>Zanzibar Office</i>	Sh. 179,015,200/=
Kif.3002 – <i>Mwanza Office</i>	Sh. 145,712,000/=
Kif.3003 – <i>Lindi Office</i>	Sh. 58,705,000/=
Kif.3004 – <i>Pemba Office</i>	Sh. 18,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria

Kif. 1001 – <i>Administration and HR Management</i>	Sh. 864,293,000/=
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i>	Sh. 192,813,000/=
Kif. 1003 – <i>Planning and Coordination Unit</i>	Sh. 49,125,000/=
Kif. 1004 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 96,646,000/=
Kif. 1005 – <i>Procurement Management Unit</i>	Sh. 72,057,000/=
Kif. 1006 – <i>Public Legal Awareness Unit</i>	Sh. 218,474,000/=
Kif. 1007 – <i>Law Review Unit</i>	Sh. 242,399,000/=
Kif. 1008 – <i>Law Research Unit</i>	Sh. 249,968,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kif. 1003 – *Planning Division*.....Sh. 0

(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 19 - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

Kif. 2001 – *Case Management & Quality Assurance*.....Sh. 248,363,000/=

(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

Kif.3001 – *Fraud, Money Laundering & Corruption Offence*Sh. 0

(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Fungu 40 - Mfuko wa Mahakama

Kif. 1001 – *Administration and HR Management*.....Sh. 0

(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1003 – *Planning and Monitoring Division*.....Sh. 15,075,900,756/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lyimo.

Waheshimiwa ukurasa wa 72, vote 40, Mfuko wa Mahakama, tatizo liko wapi? Tuko kitabu cha maendeleo, siyo cha matumizi ya kawaida, tumeshahama huko.

NDG. BAKARI KISHOMA - KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti narudia.

MWENYEKITI: Rudia.

Kif. 1001 – *Administration and HR Management*Sh. 0

(Kifungu kilivyo tajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1003 – *Planning and Monitoring*
Division.....Sh. 15,075,900,756/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye *sub-vote 6310 - Construction and Rehabilitation of District Court Buildings*. Hoja yangu ni kwamba mwaka 2018 utaona zilitengwa shilingi bilioni 10 na bado kumekuwa na malalamiko makubwa sana kwamba hakuna Mahakama nydingi za Wilaya, lakini mwaka huu tunaona zimepungua kwa takribani shilingi bilioni tano, kwa sababu imetengwa shilingi bilioni tano tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua, kutokana na upungufu mkubwa wa Mahakama na siku zote tunasema kwamba haki ikicheleweshwa ni haki imenyimwa, nataka kujua, kwa fedha hizi kidogo zilizotengwa, wanategemea kujenga Mahakama ngapi ili wananchi waweze kupata haki yao kwa sababu wananchi kwa kweli wanateseka, wanatembea mbali? Naomba maelezo ya Serikali.

MWENYEKITI: Ahsante, maelezo ya Serikali, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, kwa kifupi tu.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2018 kulikuwa na matumizi ya ziada ambayo yameshakamilika na kwa mpango wa bajeti ya mwaka huu kulingana na fedha zilizokuwepo na ukipunguza

mahitaji ambayo yalishakidhi mwaka uliopita, ndiyo maana kumekuwa na upungufu.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1005 – *Information, Comm. & Technology Unit* Sh. 0
Kif. 1008 – *Estates Management Unit* Sh. 0
Kif. 2001 – *High Court Main Registry*.....Sh. 0
Kif. 2010 – *Judiciary Delivery Unit*Sh. 7,082,000,000/=

(Vifungu viliwyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria

Kif. 1003 – *Policy and Planning Division*.....Sh. 5,075,853,500/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Kif. 1004 – *Legal Services Unit*.....Sh. 0
Kif. 1007 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*..... Sh. 2,567,381,802/=
Kif. 2002 – *Human Rights*.....Sh. 0

(Vifungu viliwyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

NDG. BAKARI KISHOMA -KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge lilitrudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Taarifa, Mtoa Hoja. (*Makof*)

TAARIFA

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante, hoja imetolewa na imeungwa mkono karibu na Bunge zima. (*Makof*)

Sasa nitawahoji kuhusiana na taarifa hiyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Makadirio na Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Katiba na Sheria, yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha, 2019/2020 sasa yamepitishwa rasmi na Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii niwashukuruni sana kwa kazi mliyofanya leo kwenye mafungu yote haya yaliyo chini ya Wizara hii, hasa yale ambayo mmeyasemea sana upande wa Mahakama.

Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa hoja yake hii ambayo imehitimishwa sasa hivi. Amefanya kazi nzuri. Vile vile namshukuru sana Waziri wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Profesa Kabudi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maelezo ya kina waliyotoa katika kufafanua hoja za Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Katika hatua hii tuitakie Wizara hii na taasisi zake kila lililo na heri katika mwaka ujao wa fedha. Naelewa rasilimali fedha hii bado ni chache lakini hata hicho tujaribuni kutumia vizuri ili tuweze kufanyikisha malengo yetu. Kilio ni kikubwa, lakini Wizara hii ndiyo tegemeo kubwa sana kwa Watanzania katika suala zima la haki.

Mimi leo najisikia vizuri sana kubahatika kuongoza shughuli za Bunge kwenye kujadili makadirio au maombi ya fedha kwa sekta hli muhimu ambayo nillbahatika kuhudumu kwa kipindi kirefu. Kwa hiyo, sina la ziada, bali kuwatachia kila lililo la heri. (*Makofi*)

(Hapa Mhe. Kabwe Z. R. Zitto alismama kuomba Kiti kimpe na nafasi ya kuongea)

MWENYEKITI: Mheshimiwa ngoja kidogo, tuna taratibu zetu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa sidhani kama kuna mtu anataka kusaliti ndoa yake, lakini nina pete mbili hapa za harusi zimeletwa kwangu. Zimeokotwa upande wangu wa kulia huku. Yawezekana ni kwa bahati mbaya, lakini wajue kwamba ziko salama salimini. Mheshimiwa Zitto. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 120(2)(a) na nitaomba kuisoma. "Baada ya Hoja iliyokuwa ikijadiliwa na kuamuliwa, Mbunge yeoyote mwenye nia ya kutoa hoja chini ya kanuni hii, anaweza kusimama mahala pake na kutoa taarifa ya mdomo, kwamba anakusudia kutoa hoja ya kuunda Kamati Teule. (b) inaelezea masharti yanayopaswa kufuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa ya mdomo, kwamba nakusudia kuleta hoja ya kuunda Kamati Teule kwa ajili ya kuchunguza mwenendo wa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini katika kumaliza mashauri ya jinai na watuhumiwa bila kuwepo kwa sheria inayowezesha hilo na pia kuchunguza malalamiko ya wananchi juu ya rushwa katika kumaliza mashauri hayo ya jinai na tatu kupendekeza namna bora ya kumaliza mashauri haya kwa mujibu wa sheria. Naomba kutoa taarifa hiyo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Zitto kaisoma Kanuni ya 120 vizuri. Katika hatua hii yeye anatoa tu kusudio lake kwa maana ya kutoa taarifa kwa mdomo bila maandishi; na kwamba anakusudia kutoa hoja ya kutaka kuunda Kamati Teule. Kitakachofuata sasa ni kwenye (b), ni mchakato sasa. Aende kwenye hilo kusudio lake ambalo amelitolea taarifa la kuleta hoja ya kuunda Kamati Teule, iwe kwa maandishi na iwasilishwe kwa Katibu wa Bunge. Kama itafuzu, itabidi sasa kama ilivyo kawaida ipangwe kwenye Shughuli za Bunge kuititia *Order Paper*. Imekuja vizuri.

Katika hatua hii, hakuna cha kuunga mkono, ni kutoa tu kusudio lake, amefanya hivyo na lazima ije kwa mujibu wa Kanuni ya 120(1) iwe ni kwa hoja mahususi, lakini itokane na hoja iliyokuwa mbele ya Bunge. Hoja iliyokuwa mbele ya Bunge ni Hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria. Kwa hiyo, mtiririko huo umekaa vizuri, nikutakie kila la kheri katika hatua zinazofuata. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, sina la ziada. Kwa maana hiyo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho, siku ya Alhamisi, tarehe 18 Aprili, saa 3.00 asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge, narudia tena. Upande huu kuna tatizo gani? Nawaaga tena. (*Kicheko*)

*(Saa 1.58 Usiku Bunge lilahirishwa hadi siku ya Alhamisi,
Tarehe 18 Aprili, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*